**WILAYA ZILIZO JUMUISHWA**

1. **NAIROBI SCHOOLS**
2. **STAREHE BOYS CENTER**
3. **MANGU HIGH SCHOOL**
4. **ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL**
5. **HOMABAY**
6. **RACHUONYO**
7. **MIGORI**
8. **UGENYA/UGUNJA**
9. **KISUMU WEST**
10. **MATUNGU**
11. **BUTERE**
12. **KAKAMEGA EAST**
13. **NYATIKE**
14. **KHWISERO**
15. **TRANS NZOIA WEST**
16. **TRANSMARA**
17. **KAKAMEGA NORTH**
18. **MUMIAS**

# MADA ZILIZOMO



| | Ukurasa |
|---|---|
| **KARATASI YA KWANZA 102/1** | |
| **Insha za Kiuamilifu** | **3** |
| **Insha za kawaida** | **4** |
| **KARATASI YA PILI 102/2** | 5 |
| **Ufahamu** | **5** |
| **Ufupisho** | **20** |
| **Matumizi ya lugha** | **30** |
| **Isimu Jamii** | **40** |
| **KARATASI YA TATU (102/3)** | 43 |
| **Riwaya: UTENGANO: S.A. MOHAMMED** | **43** |
| **Tamthilia: KIFO KISIMANI: KITHAKA WA MBERIA** | **44** |
| **Ushairi** | **46** |
| **Fasihi Simulizi** | **59** |
| **Hadithi Fupi : K. WAMITILA:**<br>**MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINEZO** | **62** |
| **Mwongozo wa kusahihisha** | **62-152** |

**Mkusanyiko huu umegawanywa katika sehemu tatu kuu kulingana na karatasi ya Kiswahili.**

# Karatasi ya kwanza 102/1

## Insha za kiuamilifu

1. Andika mahojiano baina ya mkuu wa wilaya na mwandishi wa habari kuhusu utovu wa usalama wilayani mwako.

2. Hali ya usalama imekuwa ikizorota katika lokesheni yako. Andika barua kwa chifu wa eneo lenu ukionyesha visa vya ukosefu wa usalama na upendekeze njia za kukabiliana na hali hiyo.

3. Umealikwa katika ofisi ya mkuu wa wilaya kupendekeza njia za kukomesha uadui unaotokana na ukabila nchini. Andika mazungumzo jinsi yalivyoendelea.

4. Wewe ni kiranja anaye husika na masomo shuleni mwako. Mwandikie kiranja anayehusika na masomo katika shule jirani ukiwaalika wanafunzi wake katika mjadala shuleni mwako. Ambatanisha ratiba itakayofuata siku hiyo.

5. Kitengo kinachohusika na usalama barabarani kimekuchagua wewe kama mwanajopo kati ya wanachama watano. Mmetakiwa kuchunguza kinachosababisha ajali nyingi nchini na kutoa mapendekezo yenu jinsi ya kurekebisha hali hiyo. Andaa ripoti yenu.

6. Umehudhuria mkutano wa vijana kujadili njia za kuboresha maisha ya vijana katika jamii. Andika kumbukumbu za mkutano huo.

7. Umefikishwa hospitalini ukiugua. Andika mahojiano kati yako na daktari

8. Wewe ni Afisa Mkuu wa Polisi wilayani mwenu; Andika kumbukumbu za mkutano wa kamati ya usalama uliofanyika hivi karibuni kuhusu mikakati ya kuimarisha usalama wilayani humo.

9 Suala la ufisadi limekuwa tatizo sugu katika jamii ya Kenya. Andika mahojiano kati ya mwenyekiti pamoja na Afisa wa Sheria katika Tume ya Kupambana na Ufisadi nchini na mwandishi wa habari juu ya mbinu za kupambana na ufisadi.

10. Mkuu wa mkoa wa Tuinuane ameongoza mkutano wa viongozi mkoani uliojadili kuhusu amani na maridhiano baada ya vita vya kikabila mkoani humo. Andika kumbukumbu za mkutano huo

11. Matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne yametangazwa. Imesadifu kwamba wewe ndiye mwanafunzi bora katika Mkoa wa Magharibi. Mwanahabari wa Gazeti la Tujivune amekutembelea nyumbani kwenu. Andika mahojiano yenu.

12. Wewe ni Katibu wa kamati ya chama cha wazazi na walimu shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika hivi karibuni.

13. Kumetokea mzozo wa kisiasa nchini mwako. Mmealika msuluhishi kutoka nchi jirani. Andika mahojiano baina ya msuluhishi huyo na mwanasiasa.

14. Shule yenu ilishiriki hivi majuzi katika mashindano ya riadha ya shule za Sekondari wilayani. Ulikuwa mmojawapo wa washiriki. Andika ripoti kuhusu mashindano hayo.

15. Mhariri wa gazeti la **Jicho Pevu** ametangazia wasomaji katika toleo la Jumatano kutuma makala yao ili kuchangia katika kuandika tahariri itakayohusu mabadiliko ya hali ya anga na athari zake

katika toleo la Jumapili. Andika makala yako.

## Insha za kawaida

1. Andika insha itakayotamatika na ....kweli dunia ni mwendo wa ngisi, ina masalata wengi.
2. Elimu bila malipo nchini Kenya ina changamoto zake. Jadili
3. Eleza namna katiba mpya inavyofaa kutetea nafasi na hadhi ya jinsia ya kike.
4. Ajira ya watoto ina madhara mengi. Fafanua.
5. Zigo la kuliwa halilemei.
6. Andika insha itakayomalizikia kwa :
   ….mkuu wa askari aliwaeleza kuwa ikiwa njia hizo zingetumika, uhalifu ungezikwa kwenye kaburi la sahau
7. Mwenye kovu sidhani kapoa.
8. Elimu ya bure inayotolewa na serikali katika shule za msingi za umma humu nchini, imekuwa na athari mbalimbali. Jadili.
9. Andika insha itakayomalizikia maneno yafuatayo:-
   ....aliyakumbuka mashauri ya mamake ambayo aliyakaidi. Machozi yalimbubujika alipojiona kadhoofika kiafya jinsi ile; mguu mmoja duniani, mwingine kaburini.
10. Uhaba wa kazi ni tatizo sugu katika nchi zinazoendelea. Jadili.
11. Andika kisa kinachodhihirisha ukweli wa methali: "**subira huvuta heri**"
12. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya:- ...........nilipiga magoti chini na kumshukuru Maulana kwa kuyanusuru maisha yangu.
13. Kumekuwa na kilio kila uchao. Pendekeza njia mbalimbali za kutokomezea mbali umaskini katika jamii yako. Fahali wawili wapiganapo, nyasi huumia.
14. Andika insha itakayoishia kwa maneno yafuatayo:-
15. ....hapo ndipo nilipoapa kwamba sitawahi kumfungulia mtu yeyote yule mlango usiku.
16. Asifuye mvua imemnyea.Thibitisha ukweli wa methali hii kwa kisa.
17. Utovu wa nidhamu shuleni umesababishwa na mabadiliko katika sekta ya Elimu. Jadili.
18. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno ...ama kweli dunia ni mti mkavu; ukiuegemea utaanguka. Nilikuja kutambua kwamba ni heri uwe maskini wa mali na tajiri wa fadhili kuliko tajiri wa mali na fukara wa utu.
19. Licha ya kufaulu kiasi, utoaji wa elimu ya bure katika shule za msingi na upili umekumbana na matatizo si haba. Jadili
20. Mchuma janga, hula na wa kwao.
21. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya………… moyo ulinidunda nilipoona gari letu likibingiria kuelekea ufuo wa bahari, machozi yakanitoka kwa wingi nikakumbuka yote niliyokuwa nimetenda ulimwenguni, nikayafunga macho yangu.
22. Udongo uwahi/upatilize ungali maji.
23. Kuavya mimba ni uovu usioweza kuvumiliwa , jadili.
24. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya:
   ................ndipo nilipogundua kuwa mtu ambaye siku yake imefika hana budi kufa hata akafanyiwa dawa za aina gani.
25. Wewe kama Mwalimu ambaye amehitimu katika chuo kikuu cha Kenyatta, kuna nafasi ya kufundisha katika shule ya upili ya Angeko. Andika wasifu-kazi utakaoandamana na barua yako.
26. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji.
27. Vizingiti \Vikwazo vya kuundwa na kupatikana kwa katiba mpya nchini Kenya sio wanasiasa pekee.Fafanua.
28. Andika insha itakayomalizikia kwa: **. . .** Na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho, Hidaya akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge wa eneo bunge la Kubali.
29. Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo
30 Uavyaji wa mimba ni suala sugu hapa nchini Kenya. Jadili
31. Ilikuwa mara ya kwanza kufikishwa mahakamani…………….. endeleza
31. Kisa cha mwanafunzi kilingane na chanzo hiki na aonyeshe ubunifu na matumizi mazuri ya lugha
32. Eleza jinsi haki za watoto zinavyokiukwa katika jamii huku ukipendekeza suluhu.
33. Cha Mchama huchama, cha Mgura hugura.

34. Rais Julius Kabarage Nyerere ni mtu anayejulikana katika taifa la Afrika kusini na Mataifa mengine. Alipozaliwa..........................................................................
35. Shughuli ya kuavya mimba iharamishwe. Jadili
36. Ganga ganga ya mganga humlaza mgonjwa na matumaini.
37. Andika insha itakayomalizikia kwa: Baadaye niligundua kuwa kutotii wazazi kunaweza kuwa na madhara ya muda mrefu sana.
38. Bandu bandu huisha gogo.
39. Suluhu kwa matatizo yanayoikabili nchi yetu ni katiba mpya. Jadili,
40. Kamilisha mtungo wako kwa kifungu kifuatacho.
   ……………………………………………. Ni uso wa nani usiotahayuri kwa kisa kama hiki?
41 Mchumia juani hulia kivulini.
42. Uhalifu umekithiri sana humu nchini. Jadili sababu zinazochangia hali hii na upendekeze njia za kukabiliana nao.
43. Andika insha itakayomalizikia maneno haya----------------------niliketi nikishika tama. Iliyokuwa nyumba yangu ikawa jivu tu! Sikuyazuia machozi yalionibubujika.
44. Andika Mtungo unaothibitisha ukweli wa methali: Jitihada haiondoi kudura.
45. Simu za rununu zina madhara mengi kuliko manufaa . Jadili.
46. Andika insha itakayoisha kwa maneno yafuatayo: .............nilipogutuka niliangaza macho huku na kule. Aah! kumbe nilikuwa nikiota!
47. Fafanua njia mbalimbali za kukabiliana na umaskini nchini mwetu.
48. Samaki mkunje angali mbichi.
49. Hauchi hauchi unakucha. Naam, siku njema niliyosubiri kwa hamu na ghamu iliwadia. Nilifurahi ghaya ya kufurahi……. (endeleza insha hii).

## <u>Karatasi ya pili 102/2</u>

### <u>UFAHAMU</u>

**1.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Panografia ni tendo, maandishi, picha au michoro inaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, tovuti na kanda za kunasia picha na sauti.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea kote ulimwenguni mithili ya moto mbugani wakati wa kiangazi. Kuenea kwake kumechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi ukiwa umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbalimbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la kuvuruga madili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu.Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Kwa mfano, baadhi ya wanamuziki hutumia **<u>ponografia</u>** kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji wa ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushaihidi kuonyesha kuwa wale wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kwamba kinachoonekana kwa jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kisasi ikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama vile masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera, huyaiga wanayoyaona na kuyasikia. Hii ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Hivyo basi wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni ukahaba, utendaji

mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa huku wengine wakiambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza kuwaletea mauti.

Yasemekana kuwa akili za binadamu hunasa zaidi mambo yanayowalishwa kwa picha na hivyo basi matusi haya yaweza kudumishwa katika kumbukumbu zao. Tabia mbaya kama vie ushoga, ubasha na usagaji huwa matokeo yake na hata matokeo ya vijana hugeuka wanapoanza kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, lugha, ishara na miondoko inayohusiana nanmgono huibuka. Yote haya yanakinzana na desturi za mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kuchapo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama vile unywaji pombe na matumizi ya vileo ambavyo huchochea uchu wa ngono na kuibua tabia za kinyama.

Kuendelea kuzitazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, huondoa makali kiasi kwamba hata katika uzima mtu hupoteza mhemko na kugeuswa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mjini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na malezi haya yasiyo na kizuizi.

Kuuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi, watu wazima kuwajibika kwa kuwalinda na kuwahimiza vijana kuhusu maovu haya na wale wenye midahilishi, video na sinema kutowaruhusu vijana kutazama uchafu huu kunaweza kuwa maana ya kuyakinga au hata kuyaepuka madhara ya ponografia. Ni sharti pia sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na uenezaji wa upungufu huu. Bila shaka, sheria na hatua kali za ziweze kuchukulia dhidi ya waivunjao. Hali kadhalika, wazazi wasijipweteke tu bali wawaelekeze watoto wao ipasavyo na ila mtu alitekeleze jukumu lake.

**Maswali**

(a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka
(b) Toa sababu za kusambaa kwa uchafu unazozungumziwa katika taarifa
(c) '**Bendera hufuata upepo**'. Thibitisha ukweli wa usemi huu kulingana na makala
(d) Ni kwa nini ni muhimu kuwakanya vijana dhidi ya uchafu huu?
(e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya aina ya uozo unaozungumziwa na mwandishi?
(f) Fafanua msamiati huu kimuktadha
(i) **uchu** …………………………………………………………………
(ii) **wasijipweteke** ……………………………………………………….
(iii) **nishai** …………………………………………………………………

**2.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ilikuwa Jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya Habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za kiinua mgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki.

Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa Kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baaada ya taarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukua mara moja.. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kilimo nilitenga ekari kumu za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikakati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nilipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya

kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo 'amonia.' Gharama yake ikawa shilingi1,300 kila gunia. Hivyo, nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano..

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siwanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanis wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa 'Usikate majani, mnyama hajauawa.'

Bila taarifa wala tahadhari mvua ikatoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makasio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi.

Lakini 'Muumba ndiye Muumbua.' Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha. Muda is muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tukio lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafhuku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba nikaona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudi hali yake tena, kisha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii ikawa shilingi 5,000. Kuvuna, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa: 'MAHINDI GUNIA 900/=.' Niligutuka usingizini.

**Maswali:**

a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari.

b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika?

c) Taja matatizo **matatu** yaliyotisha mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi.

**d) Eleza maana ya methali zifuatazo:**

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa.

e) Eleza mambo **mawili** yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia.

f) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu?

**g) Eleza maana ya:**

(i) kiinua mgongo.

(ii) manyakanga wa kilimo.

3. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Mtoto anapozaliwa huwa ni malaika wa Mungu. Hutaraji kuongozwa kwa kila njia ili awe mwana mwelekea. Jukumu la kulea mtoto huanzia nyumbani. Wako baadhi ya watu ambao wanaamini kuwa jukumu hili muhimu hutekeleezwa bora na mama; wengine husema kuwa ni jukumu la baba. Ni kweli kwamba mtoto huwa na mama yake kwa muda mrefu zaidi ya baba lakini kivuli cha baba hakikosi kumwandama na **kumwathiri** maisha yake.

Uongozi wa mama huanzia siku ya mwanawe kuingia ulimwenguni. Kwa hivyo, mama zaidi ya baba huwa ndiye **chanzo cha chemichemi** ya maisha ya mwanawe. Mtoto kwa kawaida ana tabia ya kuiga kila jambo analoliona na kusikia na mambo ya awali ajifunzayo hutokana na mamaye.

Je; mtoto huiga kutokana na mama pekee? Kila utamaduni hasa huku kwetu Afrika, una taratibu zake zilizopangwa kuhusu malezi ya watoto. Kwa mfano; akina baba wengine wanaoishi maisha ya kijadi huonelea kwamba ni jukumu lao kuwalea watoto wa kiume. Kwa hivyo mvulana anayekulia katika mazingira haya **akishachuchuka** kiasi cha kujua lipi zuri lipi baya huanzia kuwa mtoto wa baba zaidi ya kuwa wa mama. Baba humuathiri mtoto wake kwa kumshauri kuhusu maneno ya kiada ya wanaume. Hupenda kukaa naye katika uga wake kwa kumshauri kuhusu maneno ya kiada ya wanaume huku akimkataza kukaa jikoni na kumsisitizia kuwa wanawake ni tofauti naye. Aidha, humfunza sifa kama vile ushujaa na uvumilivu kwa namna ambayo huona kuwa ni ya kiume. Pindi mtoto anapoonyesha tabia za kikekike, baba hujiandaa kuzitadaruki kwa kumkaripia. Baba hutaka kujiona mwenyewe katika hulka ya mwanawe.

Baba kama huyu humpa nafasi ndogo sana mkewe ya kumwongoza mtoto wake wa kiume kwa jambo lolote hata kama wakati mwingine ni la heri. Kwa upande mwngine baba huyu huwa na machache ya kuzungumza na bintiye kwa kuwa huona kuwa si stahili yake kufanya hivyo. Mtoto wa kike huachiwa mamake. Lakini kutokeapo jambo la kulipima mama huona linampita kimo, humwita baba kuingilia kati na aghalabu baba naye humwagiza dadake aje atoe suluhisho mwafaka.

Ulezi kama huu una nafasi yake katika jamii, lakini ni lazima tukiri kuwa pia unaendeleza maisha ya fawaishi na kuanzisha **taasubi** ambayo hatima yake ni mwanamke kukandamizwa na mwanaume. Wazazi walio na mwelekeo huu katika malezi yao hufikiri kuwa wataishi na watoto wao katika mazingira finyu na kwa hivyo waendelee kuwapulizia pumzi za kuhilikisha. Lakini ni sharti wakumbuke kuwa wao sio walezi peke yao na wala mtoto hawezi kuishi peke yake na kuwa na tabia ya kipekee. Leo ataishi kwao lakini kesho itambidi atoke aone ulimwengu. Kila atakapotia mguu ataona mambo mapya yatakayompa tajriba mpya na mawazo mapya ambayo aghalabu yataendelea kuiathiri **hulka** yake. Iwapo tabia alizozipata kwa wazazi wake hapo awali zilikuwa na misingi isiyokuwa madhubuti na mielekeo finyu, zinaweza kuwa pingamizi katika maingiliano yake na watu wengine. Mambo haya yanatuelekeza katika kufikiri kwamba maisha ya siku hizi hayaruhusu ugawaji wa kazi ya malezi ya namna ya baba na mama wa kijadi. Baba na mama ni walezi wa kwanza ambao kwa pamoja wanapaswa kuwaelekeza watoto wao katika maisha ya ulimwengu uliojaa bughudha na ghururi. Ni lazima wazazi watambue tangu awali kuwa katika malezi hakuna cha ubaguzi. Hakuna, mambo ajifunzayo mtoto wa kiume ambayo hayamhusu mtoto wa kike. Uvumilivu, bidii, utiifu na kadhalika ni sifa zinazomwajibikia kila mtoto kama vile upishi, ukulima na usafi. Mwanamke tangu azali ameumbwa kuwa mama na haipasi kulazimishwa kuchagua baina ya mtoto wa kike na kiume. Mapenzi na wajibu wa wazazi yapaswa yasiwe na mipaka bali yawe maridhawa kwa watoto wote.

**Maswali**

(a) Toa kichwa mwafaka cha makala haya

(b) Kulingana na kifungu hiki, taja mambo **mawili** ambayo yanaweza kuwa hatari kwa malezi ya watoto

(c) Kwa nini baba humpa nafasi ndogo sana mkewe ya kumwongoza mtoto wa kiume katika jambo lolote hata kama wakati mwingine ni la heri

(d) Eleza mambo **mawili** ambayo ni ya manufaa katika ulezi jadi

(e) Kulingana na makala haya, ushahidi gani unaonyesha kwamba kuna kutegemeana katika ulezi jadi?

(f) Taja sifa **mbili** ambazo baba humfundisha mwana wa kiume

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kaktika kifungu hiki:

(i) **Chanzo cha chemichemi**...

(ii) **Akishachuchuka**...

(iii) **Hulka**.

4. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Habari kuwa watoto chini ya miaka mitatu 'huwindwa' kitandani na kuraushwa na wazazi wao waende shuleni mwendo wa saa kumi na moja asubuhi ni za kusikitisha.

Kwa mujibu wa ripoti za wataalamu wa elimu ya watoto wachanga (ECD), watoto hao hutakikana kuwa darasani kabla ya saa kumi na mbili asubuhi.

Wanapowasili wao huanza kufukuza ratiba ya masomo ambayo huwapatia muda mfupi mno wa kula, kucheza, kupumzika na hata kuchunguza afya na usalama wao.

Badala ya kuondoka mapema kuelekea nyumbani, wengi wao hufika saa za usiku pamoja na wazazi wao wakitoka kazini. Wanapowasili nyumbani wanapaswa kuoga na kupata chakula cha jioni kwa pupa ili wafanye mazoezi waliyopewa na walimu wao.

Mazoezi hayo huwa ya masomo yote matano huku kila somo likiwa na zaidi ya maswali thelathini. Badala ya kupumzika mwishoni mwa juma, watoto hao huhitjika kuhudhuria shule siku nzima ya Jumamosi. Jumapili wanatakiwa Kanisani na hali hii hujirudia mpaka muhula umalizike. Ikiwa ulidhani watapewa nafasi ya kupumzika wakati wa likizo , umekosea kwa sababu watoto hao huhitajika kuhudhuria shule. Hili limekuwa likiendelea hata baada ya Wizara ya Elimu kupiga marufuku kusomesha wakati wa likizo.

Wazazi-hasa wale wanaofanya kazi mijini- wamekuwa wakiunga mkono mtindo huu kwa sababu unawaondolea mzigo wa malezi na gharama ya kuwaajiri walezi.
Wataalamu wanasema matokeo ya hali hii ni watoto **wakembe** wenye afya na **maadili** mabaya kutokana na kuchanganyishwa akili na walimu wanaowataka wajue kila kitu wakiwa na umri mdogo.

**Kuwashinikiza** watoto wakembe wahudhurie shule na zaidi ya hayo wajue kila kitu kuna madhara mengi. Kwanza kabisa, kuraushwa kwa watoto macheo waende shule kunawanyima fursa ya kulala na kupumzika. Utafiti unaonyesha kuwa watoto wanahitaji kulala na kupumzika kwa zaidi ya saa 12 kwa siku. Hii ina maana kuwa mbali na muda mfupi wanaolala na kupumzika mchana kutwa, watoto wanapaswa kutumia usiku mzima kwa usingizi.

Hii huwasaidia kukua wakiwa na afya nzuri hasa kiakili. Matokeo ya kuwarausha watoto hao waende shule saa hizo huwafanya wakose furaha mbali na kuwafanya wachanganyikiwe kiakili.

Pili, kuwalazimisha watoto wakae darasani kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni huwa kunawanyima fursa ya kucheza na kutangamana. Wataalamu wa afya ya watoto wanapendekeza kuwa watoto wachanga wanapaswa kucheza ili viungo vya miili yao kama moyo, akili, mapafu na kadhalika vifanye kazi vizuri.

Kinyume na watu wazima ambao hufanya kazi nzito nzito na kuwawezesha kufanya mazoezi, watoto huwa hawafanyi kazi hizo. Wazazi na walimu wanapaswa kufahamu kuwa kazi ya watoto ni mchezo na wana kila haki ya kupewa furaha ya kucheza wakiwa shuleni na hata nyumbani.

Tatu, wazazi wengi ambao hufurahia kuwaachia walimu jukumu la kuwalea watoto wao huku wao wakiwa kazini huwa wanasahau kuwa sio kila mwalimu ana maadili yanayopaswa kuigwa na mwanawe. Ingawa tunawatarajia walimu wawe mifano bora ambayo inaweza kuigwa na kila mtu, ukweli ni kwamba baadhi ya walimu hawajui maana wala hawana maadili. Hatari ni kwamba watoto **wakembe** husoma kwa kuiga wakubwa wao na ikiwa walimu wanaoshinda nao shule wamepotoka kimaadili, kuna uwezekano mkubwa wa watoto hao kupotoka pia. Hii ndiyo sababu wazazi wengi wamekuwa wakilalamika kuwa wanawao tabia mbaya ambazo hawaelewi zilipotoka.

Kila mzazi anayejali maisha ya mwanawe anapaswa kutekeleza jukumu lake la kumlea na kumwelekeza jinsi anavyotaka akue. Ni kinaya kuwa wanawatarajia wanawao wawe na tabia na maadili kama yao ilhali hawachukui muda wa kukaa nao na kuwaelekeza.

Nne, kuwawinda, kuwaamsha, kuwaosha na kuwalazimisha watoto waende shule kila siku hata ingawa hawataki huwa kunawafanya wawe wategemezi wasioweza kujipangia na kutekeleza mambo kivyao.

***(TAIFA LEO, IJUMAA, FEBRUARI 5, 2010)***

**MASWALI.**

(a) Ipe taarifa anwani mwafaka
(b) Mwandishi anatoa maoni gani kuhusu ratiba ya masomo?
(c) Eleza athari za mfumo wa elimu unaoangaziwa hapa
(d) Ni ushauri upi unaotolewa kwa wazazi ?

(e)Taja mbinu zozote **mbili** za lugha alizotumia mwandishi

(f) Eleza **maana** ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa.

(i) '**huwindwa' kitandani**

(ii) **Maadili**

(iii) **Kuwashinikiza**…

(iv) **Wakembe**…

5. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma.

Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho n.k. kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini.

Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharibu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyi kazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vyaafya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umaa wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, whandisi, mawakili, walimu na mahesibu ambao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi.. Wengine wasio wataalam huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwinginehulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza hudumia jamii.

Ufisadi **umekita mizizi** na **kushamiri** katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyikazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyikazi wasiohitimu na wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyikazi wenye biddi hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishaia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimeteuliwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya Kuchunguzavisa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni ya shilingi) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupikea malalamiko kutoka kwa wananchi **waliohasiriwa** na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa wakalipa, au wakilipwa kuwatetea mahakamani wanakwepa jukumu hilo ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

1. Eleza aina **nne** za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma
2. Kulingana na kifungu ulichosoma, ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani?
3. Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi?
4. Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini?
5. Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa
6. Eleza mana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni;
   (a) Majukumu
   (b) Kashfa
   (c) Shamiri
   (d) wakilia ngoa
   (e) Waliohasiriwa
   (f) Kita mizizi

6. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea. Wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama. Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka, wakiwemo viongozi na watu mashuhuri.

Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani ni pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya uchukuzi na mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vithibiti mwendo vilivyowekwa hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawa peleki magari yao kwa ukaguzi mara kwa mara kama inavyopaswa kutekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani. Fauka ya hao, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya kama vile miraa na bangi, hutumiwa sana na watu hawa, na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini utapata kuwa barabara nchini Kenya haziko katika hali nzuri . Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbi mithili ya machimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa za lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame.Kinachohitajika ni serikali kuzifanyia ukarabati ili kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo tayari yamejaaa kupita kiasi. Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi sana kuliko ile ya kilomita 80 kwa saa iliyokubaliwa.

Inafahamika kuwa maafisa wa uslama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita dhidi ya ufisadi na ajali za barabarni, ni mwananchi mwenyewe ambaye alawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wapelekwe kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na wachukuliwe hatua kali, matatizo haya yataisha.

Lakini kabla kufika hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza ya kukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

**Maswali**

1. (a) Mbali na ajali za barabarani, taja, tatizo lingine sugu ambalo linakumba nchi ya Kenya
   (b) Ajali za barabarani zinasababishwa na nini?
   (c) Mwandishi anapendekeza hatua zipi zichukuliwe na serikali ili suluhisho la kudumu lipatikane?
   (d) Taja hatua ambazo serikali imechukua ili kuimarisha uchukuzi

(e) Ni kitu gani ambacho kinaonyesha kuwa serikali imeshindwa kukabiliana na ajali barabarani?

(f) Eleza maana ya maneno haya:-

(i) Tatizo sugu.
(ii) Vithibiti mwendo.
(iii) Machimbo.
(iv) Ukarabati.
(v) Hongo.
(vi) Kuhamasisha..

7. ***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali</u>***

Nchini Kenya, pamoja na kuwa mwanamke amepewa hadhi kubwa ikilinganishwa na hapo awali, kumetokea visa vingi vya unyanyasajiwa wanawake. Visa hivi haviwakati wengi maini, bali ni vyombo vya kuwazindua viongozi kuona kwamba hali haijafika kiwango cha kuridhisha. Visa vya ubakaji wa watoto wa kike na wazee, na wakati mwingine baba zao, vimetokea katika miaka ya hivi karibuni. Isitoshe, akina mama wengi wamekuwa wahasiriwa wa mivua ya makonde kutoka kwa waume zao, hata kwa makosa madogo madogo. Hivi majuzi mmoja wa wanawake hawa, ambao maisha kwao ni shairi tu, alichomwa vibaya na mumewe, kisa na maanaamejitia kujua kuwa kuna siku ya wapenzi, yaani Valentine day. Mwanamke huyu, baada ya kutoa mashambani kuja kujumuika na mumewe kusherehekea siku ya wapenzi, alipata sherehe za kuchoma moto huku mumewe akilalamika kuingiliwa uhuruwake. Mama huyu bado anauguza majeraha ya mwili na moyo!

Mwanamke aliyesoma na kupewa fursa ya kufanya kazi na ajira ofisini naye amekabiliwa na changamoto nyingi. Huyu lazima atekeleze majukumu yake kama mama, mke na mfayikazi. Wengi wa wanawake wanaofanya kazi mjini hulalamika wanafanya kazi maradufu ya wanaume. Mwanamke kama huyu, kama alivyolalamika mmoja wao ambaye ni afisa wa utawala wa mikoa, huanza siku yake alfajiri na mapema kuitayarishia familia staftahi, kisha kuelekea ofisisni ambapo anakabiliwa na migogoro mingi ya kusuluhisha. Arejeapo nyumbani jioni, hali huwa hiyo hiyo, kutayarisha chajio, kushughulikia kazi za shule za watoto na kuichangamsha familia. Maisha yake huwa hivyo, siku nenda siku rudi. Utashangaa mja huyu atayabeba mangapi?

Hali huwa mbaya zaidi kwa wanawake ambao wameingia siasa. Hawa mikasa yao haihesabiki. Mara watupiwe mabezo ya kila aina na wanasiasa wenzao, mara washutumiwe na kutiwa midomoni na wanajamii kwa kuonekana wakichapa kazi na kuwa na uhusiano wa karibu na wazalendo wenzao wa kiume. Maisha yake hupigwa darubini hata nyakati ambazo hayahitaji kuangazwa.

Mwanamke amekuwa kinyago cha kufanyiwa mzaha. Juzi karibu mbingu zianguke alipojitokeza mwana vitimbi mmoja aliyejitia kufanyia utani yasiyohitaji. Alimwasiri mwanamke kama aliyechangia kukosewa heshima kwake kwa kule kutamani kufanywa hivyo. Ingawa wanawake walimshinikiza mhusika huyu kuomba msamaha, upayukaji wake haupaswi kuchukuliwa kama mzaha. Ni ishara ya hisia ya ndani za watu wengi kuhusu mwanamke; kwamba ingawa wakenya wamejitahidi kupigania haki za wanawake; baadhi yetu bado wana zile fikira za kijadi kuhusu wanawake.

Uchumi wa nchi kamwe hauwezi kuendelea bila kumhusisha kila mtu. Nchini humu, baada ya kutambua haya, mwanamke amepewa nyadhifa mbalimbali katika serikali. Ingawa kuna baadhi ya wanawake waliohusika na kashfa mbalimbali za kifisadi, Kuna wale ambao wametumia nyadhifa zao kuhifadhi nchi. Mmoja wa wanawake amejaribu kwa jino na ukucha kuyalinda mazingira dhidi ya mapapa. Nani asiyekumbuka matusi na mabezo aliyopata mwanamke huyu anayejitoa mhanga kuikinga sehemu Fulani ya burudani dhidi ya kunyakuliwa na wanaostahili? Hakuyajutia yaliyompata. Aliowatisha walijaribu kummeza mzimamzima lakini mwishowe walisalimu amri na kuliacha eneo hilo. Hiki kilikuwa kitendo cha ujasiri na uzalendo mkubwa. Matunda yake yamewafaidi wengi, vijana kwa wazee. Kila mwisho wa wiki huwaona watu wakimiminika kwenye eneo hili kujipumbaza. Hii si fahari kwake tu, bali kwa nchi kwa jumla. Wale waliompinga na kumwita punguani wakati huo wamebaki kuinamisha nyuso tu; bila shaka wamefunzwa mengi.

Wanawake sasa wana haki ya kumiliki mali mathalani shamba. Kutokana na hili tumeshuhudia ongezeko kubwa la uzalishaji wa chakula mashambani na kwa hivyo kupunguza njaa na umaskini.

Biashara ndogondogo zinazoendelezwa sokoni na mitaani, kwa kiasi kikubwa, huhusisha wanawake. Biashara hizi huchangia pakubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi kwani hutoa ajira ya kibinafsi kwa maelfu ya watu. Ushuru na leseni zinazokatiwa biashara hizi huongezea serikali pato la ndani.

Mgala muuwe na haki umpe. Ni ukweli kwamba tumekuwa na visa vya hapa na pale vya ukiukaji wa haki za wanawake. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba nchi hii imejitahidi mno kuendelea kumkwamua mwanamke kwayo. Hata mashirika ambayo hapo awali hayakupenda kuwaajiri wanawake, sasa yanawapa nafasi sawa na wanaume. Vyuo vikuu vya kibinafsi vimeanzishwa kuwasajili wanawake. Jijini humu, mna chuo kikuu cha sayansi cha wanawake. Aidha kumeanzishwa kituo (shule) cha kuwasajili wasichana kutoka familia maskini kujiunga na kidato cha kwanza. Wasichana hawa watapata wadhamini kutoka mashrika na watu mbalimbali ili kujiendeleza kimasomo.

Kumheshimu mwanamke ni miongoni mwa haki za kibinadamu ambazo shart zitekelezwe. Hata hivyo, wanawake wakumbuke kwamba hata wanapopuliza siwa kuhusu pupewa haki, lazima wao pia wawajibike. Wao ndio walimu wa kwanza wa wanao; ikiwa basi wataonekana kwenye vyombo vya habari wakining'inia juu ya magari ya wachunga magereza kwa kuzitafutia pesa za mayatima maumizi bora, watakuwa wanapotosha watoto wao. Wawe watu wa vitendo zaidi ya upayukaji.

Maswali

a) Kwa mujibu wa taarifa, ni mambo yapi yanayoonyesha ukiukaji wa haki za wanawake

b) Fafanua jinsi mwanamke aliyesoma huteseka maradufu zaidi ya mwanamme

c) Ni faida gani ambazo zimepatikana kutokana na wanawake kupigania haki zao?

d) Hatimaye wanawake wanahimizwa kufanya nini?

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao jinsi ulivyotumiwa katika nakala

Kinyago…

Mabezo

f) Andika mfano wa mbalagha na uhuishi uliotumiwa katika makala haya

i) Mbalagha…………

ii) Uhuishi…………

8. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:-***

Uundaji wa istilahi – hasa za lugha ya Kiswahili ni shughuli nyeti na nzito hivi kwamba, haipaswi kupapiwa na mtu yeyote. Hii ni shughuli inayohitaji umakinifu zaidi kwa wanaoshiriki katika mchakato wa uundaji istilahi za kutufaa katika mawasiliano na kukuza Kiswahili kwa jumla. Ufanisi wa watu binafsi, vyombo vya habari kama vile Shirika la Habari la Kenya (KBC), Taifa Leo na mashirika mengineyo katika ukuzaji wa lugha hutegemea mno sera na utayarishaji wa serikali katika kugharamia shughuli hii. Aidha, shughuli za kukuza lugha hukwama kwa sababu ya ukosefu wa fedha pamoja na sera maalum ya serikali kuhusu lugha.

Hata hivyo, katika kuyakwepa matatizo haya, pamekuwepo na hatua za kimataifa za kujaribu kusawazisha shughuli ya uundaji wa maneno. Hatua hii ilichochea kubuniwa kwa shirikisho la kimataifa la vyama vya usanifishaji istilahi mnamo 1936. Lengo la kitengo hiki lilikuwa ni kufafanua msingi madhubuti ya uundaji wa istilahi duniani. Kwa hakika, shirikisho hilo limesaidia mno katika kuweka misingi ya shughuli za ukuzaji wa istilahi. Misingi hiyo ni ya jumla na haihusu taaluma yoyote mahususi. Katika makala hii, tunapiga darubini baadhi ya misingi hiyo pamoja na mapendekezo yake.

Mosi, uundaji istilahi unafaa uanzie kwenye dhana na wala sio neno. Hii ina maana kwamba, kwanza pawepo na dhana au hali ambayo inahitaji itafutiwe neno au istilahi ya kuielezea. Inasikitisha sana kwamba pana wataalamu ambao wanaukaidi au kuukiuka msingi huu. Wanataaluma hawa hufanya mambo kinyume kwa kujibunia maneno yao na kuyahifadhi kwenye

mikoba yao – halafu wakasubiri dhana izuke ndiposa waipachike istilahi yao. Pili, dhana zinabuniwa au kutolea istilahi au maneo ni muhimu zielezwe kwa ukamilifu na uwazi. Istilahi zinazoundwa zinafaa ziwe fupi iwezekanavyo na ziwe na uwezo wa kuelezea dhana kwa njia inayoeleweka bila utata. Tatu, maneno yanayoundwa sharti yawe na uhusiano wa aina fulani na dhana zinazowakilishwa na maneno hayo.

Uhusiano huo unaweza kuwa ama ni wa kimaumbile au wa kiutendaji. kwa mfano, Mzee Sheikh Nanhany wa Mombasa alipobuni istilahi 'uka' kwa maana ya 'ray'. Neno hili latokana na kupambauka au (kupambazuka kwa lafudhi ya kiamu. Neno 'image' ni jazanda kwa Kiswahili. 'Mirage' kwa Kiswahili ni 'mangati' (kutoka kwa mang'aanti) – yaani kung'aa kwa nchi. Mtaalamu mwingine aliyewazia uendajikazi wa kifaa na kubuni istilahi inayokubalika mpaka sasa ni Prof. Rocha Chimerah ambaye alibuni istilahi 'tarakilishi'. Pengine Prof. Chimerah alifikiria kazi ni kifaa husika na kuunda neno la Kiswahili linaloakisi kazi hiyo. Tunajua kwamba kompyuta hufanya kazi inayohusu tarakimu kwa haraka kama umeme. Labda Chimerah ameegemea sifa hii kuibuka na istilahi hii.

Maneno mengine ambayo yamebuniwa kufuatana na msingi huu ni ya Mzee Nabhany-mathalan 'barua pepe' (e-mail), na wavuti (website). Tukiegemea maumbile, neno 'kifaru' lina maana ya vita ilihali tuna zana ya vita iliyopewa jina hilo kwa sababu ya labda kuwa na maumbile sawa na kifarumnyama. Nne, istilahi zinaweza kukopwa kutoka lugha nyingine. Yamkini hakuna lugha hata moja ulimwenguni-zikiwemo lugha duniani kama vile kiingereza zinazoweza kujitosheleza. Takriban asilimia 80 ya maneno katika kiingereza ni ya kukopwa. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili inapokopa, hali hiyo haipaswi kuchukuliwa kuwa ni lugha dhaifu.

Hata hivyo, istilahi zinazokopwa zi-nafaa zichukuliwe zilivyo katika umbo lao asili. Umbo hili linaweza kufanyiwa marekebisho machache tu, kulingana na sarufi na matumizi ya lugha kopaji. Mifano ya istilahi kama hizi ni 'televisheni' (television), kopmpyuta (computer), kioski (kutokana na jina 'kiosk' la Kijerumani) na redio (radio), Tano, pale istilahi haiwezi kukopwa, lugha husika ijaribu kubuni msamiati ufaao, kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba, lugha inastawi. Lakini tahadhari inapaswa kuchukuliwa hivi kwamba, Kiswahili kisikope maneno kiasi cha kupoteza upekee wake. Mwisho, uundaji wa istilahi uzingatie mofolojia ya kawaida ya lugha. Istilahi zinazoundwa kwa kuzingatia mofolojia huwa rahisi kuiua maneno yenye uhusiano wa istilahi asili kwa njia ya mnyambuliko.

**Maswali**

(i) Taja mambo ambayo huchnagia ukuaji na ufanisi wa jumla wa lugha ya Kiswahili
(ii) "Lugha ya Kiswahili ni dhaifu na isiyotosheleza" Je, mwandishi wa makala haya ana msimamo upi kuhusu kauli hii?
(iii) Tahadhari zipi zinazofaa kuchukuliwa kabla ya kukopa istilahi kutoka lugha zingine?
(iv) Yape makala haya anwani mwafaka
(v) Eleza maana ya maneno yafuatayo:
(a) Dhana-
(b) Takribani –
(c) Istilahi – .
(d) Mofolojia –... .

9. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:-***

Kitabu kinaeleza Mungu kamuumba mwanamke kutokana na ubavu tu wa mwanamume. Na hapa bila shaka ndipo linapojisalimishia shina lisilokuwa na mzizi thabiti la ubinafsi wa kiume – mwanamume akijijadilia kimoyomoyo. Ikiwa huyu mwanamke alitokana na ubavu wangu, yeye awe nani kwangu? Hakuna shaka ni wangu, mali yangu. Kwa sababu hii, miaka nenda miaka rudi mwanamke amekuwa akiugua na kuguna chini ya uonevu wa mwanamume.

Swala la kitabu kumleta duniani mwanamke kupitia ubavu wa mwanamume laweza kueleweka katika muktadha wa kile ambacho kimekuja kujulikana kama taasubi ya kiume. Na ili tuelewane barabara kuhusu maoni haya, tujisitishe kidogo katika kunusa tumbako huku tukijiuliza: ni nani au ni kina nani walihusika katika kubuni au kuandika hadithi ya asili ya mwanamke kitabuni? Ni kawaida ya binadamu kutazama na kueleza jambo kibinafsi. Asili ya

mwanamke ilivyoelezwa kitabuni katika mkururo wa fikra hii yaweza kutambulikana kama uzushi tu.

Kiutamaduni, hasa wa Kiafrika, huku akiwa yuakua, mtoto wa kike husombezewa kasumba ya mawazo akilini, na kwa bahati mbaya sana, aghalabu na mamake au nyanyake, kuhusu namna anavyotarajiwa kutabasamu, kujinyenyekeza, na jumla kujidunisha mbele ya mvulana. Ni mwiko kwake_kudhihirisha tabia za kimabavu, sitaji kujitetea, ili asije **akatiwa mdomoni** mitaani! Msichana atacharazwa na wazazi wake kwa ujasiri licha ya kuthubutu kupigana na mvulana. Na hapo ndipo ilipojificha siri ya kuwa anapoolewa na akosane na mumewe, daima yeye hutolewa makosa na kupatikana na hatia mbele ya wazee.

Wavulana kwa upande wao ni wanaume na lazima afanye mambo kiume. Si ajabu kuwa kinyume cha yale yanayowafika wasichana, wavulana wengi **huonyeshwa mbovu** na baba zao kwa sababu wamepigwa na wenzao. Ni vibaya baba kusikia mtoto (mvulana) wake amepigwa.

Nyumbani msichana hutarajiwa kujilindia heshima kimwili hasa kwa kuhifadhi ubikira mpaka aolewe. Anapotembea na wanaume huitwa Malaya. Ni ajabu kuwa hakuna bikira wala Malaya mwanaume. Mvulana ambaye hajajuana kimwili na mwanamke kabla ya ndoa huchukuliwa kuwa zuzu; ilhali anayetembea ovyo na wanawake ndiye dume.

Fauka ya hayo, inasikitisha kabisa kuwa mwanamke hana mahali pa kutua kikamilifu duniani. Kabla hajaolewa nyumbani, huchukuliwa kuwa mpita njia tu. Na anapoolewa ni poa kaolewa. Isitoshe mwanamke huolewa, haoi wala yeye na mume hawaoani. Mwanamke mahali pake ni jikoni pia anaonekana tu; ni hatia kwake kujaribu kusikika.

Mkutano kuhusu mwongo wa wanawake uliofanyika miaka miwili iliyopita jijini Nairobi ilinuiwa kupalilia vizuri mwamko juu ya ukweli kuwa binadamu ni binadamu na hakuna haja ya wao kubaguana. Tofauti za kimaumbile haziwezi kuwa hoja. Tusiupigie makelele ubaguzi wa rangi huko Afrika kusini ilhali kwetu tuna ubaguzi wa kimaumbile. Tusipozingatia ushauri huu daima tutakuwa kwenye kile kinaya cha kuchekwa katika muktadha wa methali kuwa **nyani haoni ngokoye**.

Ni kweli kosa lilifanyika tangu awali ambapo kufumba na kufumbua, mwanamke akapigwa jeki na kuachwa akilewalewa katika hali ambayo hangeweza kujitetea hivyo basi akachukuliwa kuwa kiumbe duni. Lakini haidhuru, **yaliyopita si ndwele**, tugange yajayo. Kinachohitajika ni wanawake kuwa na nia na msimamo imara. Ni lazima wajifunge kibwebwe na kujitoa mhanga na kupambana dhidi ya taasubi ya kiume.

**Maswali**

(a) Andika kichwa kinachofaa kutokana na taarifa uliyoisoma
(b) Taasubi ya kiume ilianzaje?
(c) Katika utamaduni wa mwafrika ni kasumba gani anayosombezewa mtoto wa kike anapokua?
(d) "**Wavulana walidekezwa na utamaduni".** Eleza
(e) Taja kwa ufupi mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika mkutano wa mwongo wa wanawake mjini Nairobi
(f) ***Eleza maana ya semi zifuatazo kama zilivyotumiwa katika taarifa uliyosoma:-***
(i) Nyani haoni ngokoye .
(ii) Akatiwa midomoni
(iii) Huonyeshwa mbovu
(iv) Wajifunge kibwebwe
(v) Yaliyopita si ndwele ganga yajayo

**10.** ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Asifuye mvua imemnyea. Huu ni msemo wenye hakika isiopingika, na kutilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande wa magharibi badala ya mashariki. Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo, na kama halipo li njiani. Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini alishangaza

umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya Ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa Ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina **kirefu cha kutamauka** na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mojawapo ya mafunzo ya kidini ambayo Padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja wetu ni kushukuru tu. Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

**Ima fa ima**, na waswahili husema, "mlaumu nunda na kuku pia". Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kulala nje. Huenda alikosana na ndugu zake kwa kuepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia **kufidia makosa yake**. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na Ukimwi, raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa jumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili ni kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto ni adhabu inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya P.N. inafafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka. Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la ndoa bila haya. Huu upotofu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P.N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu huo wake.

**Maswali**

1.Taja kichwa kwa makala haya

2. Katika aya mbili za kwanza, mwandishi anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani?
   Eleza chanzo cha tabia za P.N

4. Mwandishi wa taarifa hii anataka P.N achukuliwe hatua gani? Kwa nini?

5. Barua ya P.N. bila shaka imeonyesha uvumbuzi mpya. Utaje

6. Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumiwa katika taarifa:
   (a) Kina kirefu cha kutamauka
   (b) Ima fa ima
   (c) Kufidia makosa yake

11. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

**CHIMBUKO LA USHAIRI**

Ushairi ni fani kongwe kama mwanadamu mwenyewe alivyo mkongwe duniani. Na mashairi yamekuwepo kitambo sana hata kabla ya lugha ya Kiswahili bado haijanawiri na kushamiri kama ilivyo hivi leo. Ndipo tunasikia kuna mashiri ya kipemba, mashairi ya kimvita, mashairi ya kivumba, mashairi ya kipate, mashairi ya kiyunani, ya kirumi na kadhalika,. Almradi kila jamii na kila kabila lilikuwa na mashairi yake.

Katika utafiti na kongomano zao, wataalam wa arudhi za Kiswahili asili wamechambua na kufafanua kwamba mashairi ya Kiswahili asili yake ni nyimbo za jadi zilizokuwa zikiimbwa na manju, wangoi au waimbaji stadi wa tangu na tangu walipojumuika katika matukio na hafla mbalimbali kama za jando, arusi, matanga, ngoma na shangwe zao za maishani.

Nyimbo hizi zilitumiwa na watangulizi wetu, kidhamira hazikuhitalafiana hata kidogo na mashairi ya Kiswahili tunayohimiza wakati huu. Farka iko katika lugha na umbo kwani kila jamii ilitumia lugha yake na lahaja ya mazingira yake. Na kwa upande wa umbo, tungo hizo za awali kabisa hazikuwa na sanaa kwa maana ya ushauri tunauona leo. Bali tungo hizo zilijengeka katika nguzo mbili kuu. Kwanza ni uzito wa mawazo maadilifu ambayo yalitaamaniwa sana. Na pili ni

mizani ya sauti ya manju kulingana na lahani, pumzi zake pamoja na madoido katika uimbaji ambao ulikuwa burudani naathari katika noyo za wasikilizaji wake.

Kwa kifupi ni kwamba, nyimbo hizo ziliuhifaid umma kwa njia mbili, mawaidha kwa mapana na taathira au jadhba kutokana na sauti tamu ya manju.

Kama utakubalika, basi huo ndio ushairi wa awali kabisa ullioambatana na nyimbo zetu za kienyeji. Kila kabila katika nchi zetu lilikuwa na ushauri wake au nyimbo zake zenye undani uliolenga sababu maalum na tukio maalum katika jamii.

Nyimbo kama hizo kwa jina la sasa tunaweza kuita mashairi ndizo zile zilizoitwa 'mwali' na wakamba; gichandi kwa 'wakikuyu'; 'gigia gi sigele' kwa waluo na 'wagashe' kwa wasukuma zilikuwa na undani wa kipekee tena uliodidimia ambao si bure kutolewa hadharani.

Aina za mashairi ya watu wa mwambao ni kama lelemama, misemele, gungu, nyiso, kongozi n.k.

***(Walla Bin Walla – Malenga wa Ziwa Kuu , E.A.E.P)***

1. Ni nini haswa chimbuko la ushairi?
2. Kulingana na kifungu hiki, ni nini umuhimu wa ushairi ?
3. Ni maswala gani yaliyowapendeza wasikilizaji wa tungo hizo za zama ?
4. Tofauti kati ya nyimbo za zama na ushairi wa leo upo kwenye vipengele gani viwili ?
5. Kifungu : '**haijanawiri na kushamiri'** ina maana gani katika lugha nyepesi ?
6. **Eleza maana ya :**
   (a) Kongamano …
   (b) Jadhiba
   (c) Farka
   (d) Awali..

12. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Chamkosi alipiga goti huku machozi yakimdondoka njia nne nne. Mbele yake, palikuwa na makaburi mawili. Waliokuwa wamelala mle hawakuwa na habari juu ya kihoro na simanzi ya aliyepiga magoti pale. La kwanza, lilikuwa kongwe kiasi na lilikuwa limemea vichaka na magugu. La pili lilionyesha upya kwani shada za maua zilizowekwa na waombolezaji zilikuwa bado kukauka. La kwanza, ndimo babake mzazi alipolala. Nalo la pili, ndimo mamake alimolazwa kiasi cha siku mbili zilizopita.

Kwa Chamkosi, maisha hayakuwa na maana tena. Alikuwa mwanafunzi wa miaka kumi na miwili. Hakuwa amehitimu kujitegemea na kukimu mahitaji yake. Aliokuwa akiwategemea sasa wamemwacha akiwa yatima. Hakuna yeyote ambaye angejaza pengo la wazazi wake wawili kwa kipindi cha mwaka mmoja. Haya yalikuwa kama donda sugu lisilopona.

Kwa sasa, Chamkosi anayakumbuka mengi. Anakumbuka maisha ya babake. Alikuwa jibaba nene, zito lenye sura jamala na sifa nzuri. Baba mtu alikuwa na chake na alijiweza kiuchumi. Wengi pale mjini walimheshimu na kumstahi kutokana na uwezo wake wa kiuchumi. alitunza familia yake vizuri. Chamkosi hakumbuki siku moja aliyokosa chochote alichohitaji kutoka kwa babake. Alikuwa na bidii kazini mwake pia.

Walakini, kama mja asiyekamilika, baba mtu alikuwa na dosari moja. Aliyapenda maisha ya anasa na kufukuzia wasichana wadogo pale mtaani. Mamake Chamkosi aliyajua haya. Alijaribu kuzozana na mumewe ili aachane na tiabia hizi lakini kila akitaka ushauri, mama mtu alikemewa na kufokewa kuwa aache upuzi wa wanawake. Akafikia kufyata ulimi na kumwachia Mungu aongoze maisha ya bwanake.

Hata hivyo hakuna marefu yasiyo na kikomo. Baada ya kuponda raha na vimada si haba, baba mtu alianza kuugua. Maradhi yake yakawa ni msururu. Mara, alipata mafua yasiyopona, mara kuendesha, mara maradhi ya ngozi. Haya yalimtia wasiwasi. Baada ya kukaguliwa na daktari, alipatikana kuwa *ameumwa na mbuzi.* Hakuamini haya. Baba aliyekuwa bashasha na mcheshi aliingiwa na upweke na kutotaka kutangamana na yeyote hata jamaa zake.

Waliosema kuwa hakuna msiba usiokuwa na mwenzake, hawakukosea. Maradhi ya baba mtu yaliifilisi jamaa huku waking'ang'ania kumtafutia tiba. Wakaenda kwa waganga si haba. Waganga nao wakafaidi tamu.

Muda si mrefu, mama mtu naye akaanza kuugua. Baada ya uchunguzi, alipatikana kuwa na maradhi yayo hayo ya bwanake. Ikawa ni kama mji umelogwa. Baada ya muda mfupi baba

mtu aliaga dunia, mama naye hakukawia. Naye akasalimu amri na kumfuata bwanake kaburini. Familia ikawa kama inaangamia. Chamkosi kijana mdogo akaachwa pweke.

Kama kawaida, mja hakosi neno. Wengi walisikika wakisema hili na lile kuhusu vifo hivi. Wengi walieneza uvumi. Lakini, Chamkosi alijua ukweli wa vifo vya wazazi wake.

Sasa hapa alipo aliyatambulia macho makaburi ya wazazi wake, anasononeka. Anaomboleza zaidi kifo cha mamake ambaye alimwona hana hatia na hakupaswa kufa kwa maradhi yale. Anaukumbuka vizuri wema wa mamake usio na kifani. anakumbuka alivyojitunza kama mke na mzazi.

Anakumbuka jinsi mamake alivyomshughulikia babake katika siku zake za mwisho licha ya baba mtu kuungama maisha yake maovu. Chamkosi alishindwa kujua kwa nini mamake akawa msamehevu kiasi hicho. Hakukosa kukumbuka wasia wa mama yake. Haya yalimfariji. Faraja hizi zilimpa nguvu mpya za kuyakabili maisha.

Chamkosi aliwaza juu ya maisha yake. Akaona kuwa, kama yatima atawategemea wafadhili miongoni mwa jamaa na marafiki wenye huruma iwapo wapo. Aliwaza jinsi anasa za babake zilivyowaathiri watu wengi.Alitambua kuwa Ukimwi haumwathiri aliyeupata tu, bali na wengine wengi. Kweli, mtego wa Panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo. Lakini akiwatazama watu, hakuelewa kwa nini walidhamiria kuishi ujingani. Aliwaona baadhi ya vimada wa babake wakishikana viuno na vijana wadogo. Akawasikitikia. Akabaki na swali kwa nini watu wengine wanafikiria kuwa virusi hivi haviwezi kuwapata. Kwani wanafikiria kuwa vinabagua na kuwa wao hawahatarishi maisha yao? Alishindwa kufahamu watu watabadili vipi mienendo yao miovu na waweze kukabili janga hili lini?

Kwa wakati huu, Chamkosi alikata shauri kusomea Taaluma ya Uelekezi na Ushauri kutokana na vifo vya wazazi wake. Alitaka kupata ujuzi utakaomwezesha kuwashauri na kuwaelekeza vijana wenzake ambao wanahatarisha maisha yao. Kama mshauri, alinuia kuhamasisha na kuzindua jamii juu ya hatari za Ukimwi.

Alitaka kuhakikisha kuwa hatua zimechukuliwa na kila mtu katika jamii kukabili janga hili n kuliangamiza

Chamkosi aliomba dua fupi. Akainuka na kuondoka huku akiwa na faraja na matumaini moyoni kutokana na azimio lake lile.

(a) Toa kichwa mwafaka kwa makala haya
(b) Eleza madhara mawili ya ugonjwa sugu uliotajwa katika makala haya
(c) Taja mifano ya tabia zinazoweza kumfanya mtu aathiriwe na ugonjwa wa Ukimwi
(d) Tofautisha tabia za baba na mama wa Chamkosi
(e) Chamkosi baada ya kufikwa na madhila hayo yote aliamua kufanya nini? Toa maoni
(f) ***Eleza maana ya:***
(i) Tumbulia macho ..........................................................................................................
(ii) Ameumwa na mbuzi.......................................................................................................

13. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Licha ya kuwa na historia ya kiasi, maisha ya binadamu ni kioja kikubwa. Hebu jiulize jinsi uhai wako wewe mwenyewe ulivyoanza sembuse unavyoweza kupumua na kuishi siku nenda siku rudi.

Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Muumba. Hata hivyo muumba hutumia mume na mke kutuanzishia maisha yetu humu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la mwanamke muda mfupi tu baada ya mume na mke kushirikiana katika tendo la kujamiana. Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanamume, hudunga na kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo mtu huwa na mama akawa mjamzito. Hatua ya kwanza ya uhai!

Wanasayansi wametuthibitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanamume ina kromosomu ishirini na tatu (23) nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya kromosomu. Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini na sita (46).

Kromosomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu kwa kukadiria mambo mbalimbali adhimu. Kwa mfano, kukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu mweusi, mwerevu au wa wakia chache, mwenye nywele za singa au za kipilipili, atakuwa na damu ya namna gani, michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za usoni.

Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga juu ya yaliyokwisha kuanzilishwa na kromosomu katika yai lililorutubishwa tumboni.

Haihalisi kabisa kufikiria kwamba huwa katika **hali ya ukupe**. La hasha! Yeye hujitegemea kwa vyovyote na ana upekee wake. **Hatangamani na mama yake**. Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa na ya mama yake, humtembea na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyomdhibiti katika **himaya** yake ndogo.

Amini usiamini, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa kimaumbile na mwingine na wala hatakuweko. Hata watoto pacha kutoka yai moja la mama hawawi sawa, lazima watofautiane. Si nadra kusikia mtu amepata ajali akahitaji msaada wa damu, na pakakosekana kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kimwauni. Basi ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni.

**Maswali-**

1. Ipe taarifa uliosoma anwani mwafaka
2. Mwandishi ana maana gani anaposema '**ngono yenye ufanisi**'?
3. Uchunguzi wa sayansi umekita mizizi imani gani ya kidini?
4. Taja majukumu yoyote **matano** yanayotekelezwa na kromosomu
5. Katika makala, elimu kutoka kwa jamii na mazingira yaelekea kuwa bure ghali. Kwa nini?
6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala:-
   (i) huwa katika hali ya ukupe…
   (ii) himaya
   (iii) hatangamani na mama yake

14. ***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali***

Kwa zaidi ya mwongo mmoja uliopita, ulimwengu mzima uliathiriwa na masaibu ya kifua kikuu kwa kiwango cha kuogofya kiasi kwamba katika mwaka wa 1993, shirika la afya duniani (WHO) lilitangaza ugonjwa huu kuwa swala dharura la kimataifa.

Ongezeko kubwa la visa vya kifua kikuu lililotokana na kuchipuka kwa **viini** vinavyosababisha maradhi hatari ya Ukimwi na magonjwa yaliyohusiana na punde baadaye ilibainika kuwa bara la Afrika lilikuwa ndilo lililoathiriwa zaidi na Ukimwi pamoja na maradhi ya kifua kikuu. Hii ndiyo hali inayotawala sasa ulimwenguni. Afrika likiwa bara linaloongoza kwa wagonjwa walioambukizwa viini vya Ukimwi lilikuwa likishuhudia visa vya maradhi ya kifua kikuu.

Viini vya Ukimwi vinapunguza uwezo wa mwili wa mgonjwa kupigana na vijidudu vya maambukizi. Swala linalowafanya wagonjwa hawa kutodhibiti maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Katika hali ya kawaida mwili wa mtu kama huyo unaweza kujikinga dhidi ya viini kama hivyo. Maambukizi kama haya kawaida hujitokeza kukiwa na nafasi duni ya kinga mwilini. Katika baadhi ya mataifa kama vile Kenya, maambukizi ya kifua kikuu hufanyika mapema katika umri mchanga maishani.

Kwa kawaida, viini hivyo huwa havisababishi ugonjwa wenyewe. Badala yake, kinga katika mwili wa aliyeambukizwa unaweza **kusitiri** maambukizi hayo bila mhusika kuwa mgonjwa kutokana na sababu mbalimbali. Viini hivyo baadaye vinaweza kuwa hai tena na kumfanya mgonjwa kukumbwa na ugonjwa. Swala hili kwa kawaida hujitokeza wakati mgonjwa anapoambukizwa virusi vya Ukimwi. Virusi hivyo pia huongeza hatari ya ugonjwa kujitokeza baada ya maambukizi au pengine kujitokeza tena baada ya mgonjwa kupokea tiba ya kwanza.

Kulingana na utafiti, inakadiriwa kwamba mmoja kati ya wagonjwa wawili au watu wenye virusi vya Ukimwi watapata kifua kikuu wakati mmoja katika maisha yao. Inakadiriwa kwamba karibu asilimia 50 hadi 60 ya wagonjwa wenye maradhi ya kifua kikuu nchini Kenya pia wameambukizwa viini vya Ukimwi. Kwa upande mwingine, maradhi ya kifua kikuu hujitokeza

kama kawaida kwa wagonjwa wenye virusi vya ukimwi. Kwa hivyo, wakati wa kushughulikia wagonjwa ni lazima pia wafanyiwe uchunguzi wa kubaini ikiwa wameambukizwa kifua kikuu.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma kichwa mwafaka
(b) Ni nini hasa kilichochangia kuongezeka sana kwa maradhi ya kifua kikuu?
(c) Kwa kifupi, eleza ni kwa nini ugonjwa wa Ukimwi ni hatari mwilini
(d) Ukimwi na kifua kikuu una uhusiano mkubwa, eleza uhusiano huu kulingnana na taarifa uliyoisoma
(e) Andika urefu wa neno 'Ukimwi"
(f) Eleza mambo mawili ambayo yametokana na utafiti
(g) Ni jambo lipi ambalo ni la kushangaza kuhusiana na kifua kikuu
(h) Andika maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu hiki
 (i) Kusitiri
 (ii)Mwongo
 (iii) Swala la dharura.
 (iv)Viini

15. ***Soma makala yafuatayo kisha kisha ujibu maswali:-***

Waajiri wengi wanazilaumu taasisi za elimu kwa kukosa kutoa wafanya kazi wenye ujuzi tosha, hasa wa kiteknolojia za kisasa kama kutumia kompyuta kutenda kazi mbalimbali. Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha sana.

Ujuzi wa kuweza kutumia Kompyuta unaweza kumfaa mwanafunzi hata anapokosa nafasi ya kujiunga na chuo kikuu kwa vile anaweza kuendelea na elimu yake kupitia kwa elimu mtandao. Pia anaweza kufanya utafiti wa kina kupitia intaneti na kwa njia hii akaimarisha elimu yake.

Mojawapo ya njia ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia ni kuanzishwa kwa mikakati mipya ya kufunza. Somo la Kompyuta laweza kuimarika mashuleni endapo kwanza walimu watahamasishwa juu ya faida za ujuzi huu.

Kwa kutumia Kompyuta kufunza, walimu wanaweza kufunza madarasa kadhaa katika kipindi kimoja bila kulazimika kuyahudhuria. Hii itapunguza kiwango cha kazi kwa walimu kwa vile watapata muda wa kufanya utafiti mpana. Aidha, watapata habari na ufahamu zaidi wa mambo kwa kutumia mitambo ya Kompyuta kutoka kwenye intaneti, kupitia tovuti.

Hata hivyo mipango hii inakabiliwa na changamoto kama vile bei za juu za mitambo na vifaa vya Kompyuta, ukosefu wa miundo msingi itakayowezesha utumiaji wa mitambo hii na ukosefu wa walimu waliohitimu somo la Kompyuta.

Pia, kuna tatizo la ukosefu wa nguvu za umeme hasa maeneo ya mashambani; vile vile, katika maeneo yaya haya, wanafunzi na wazazi wengi huvichukulia somo la Kompyuta kuwa gumu na linalofaa wakaazi na wanafunzi kutoka maeneo ya mijini na linalofaa wakaazi muhimu kwao mashambani.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma anwani inayoifaa
(b) "Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha." Ni hali gani inayozungumziwa katika aya ya 1?
(c) Ujuzi wa kutumia Kompyuta unaweza kumfaidi vipi mwanafunzi?
(d) Mikakati mipya ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia inakabiliwa na vizingiti vipi?
(e) Taja manufaa **mawili** ambayo mwalimu anaweza kupata kutokana na ujuzi wa teknolojia ya Kompyuta
(f) Andika msamiati mwafaka zaidi kwa maneno yafuatayo:
 (i) **Kompyuta**
 (ii) **Intaneti**

# Ufupisho

1. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Umaskini ni tatizo sugu katika jamii. Binadamu wengi hujikuta katika hali hii kwa sababu hawakubahatika kusoma. Baadhi yao huenda walijaribu kusoma wakashindwa mapema kujipandisha kielimu. Ukosaji wa elimu huchangia sana katika kukuza ukata. Elimu huweza mtu kupata tonge kwa kujipatia kazi za kumwezesha kuyakidhi mahitaji ya maisha. Hali kadhalika, elimu humsaidia binadamu kupata maarifa mengi ya kutendea shughuli zake za kimaendeleo. Kwa mfano, kama ni wakulima wanaweza kutumia **<u>pembejeo</u>** zifaazo ili kuboresha uzalishaji wa mazao. Wakulima wenye elimu hawatapendelea njia duni za kuendeleza kilimo kama vile kutumia visagilima na mbinu nyingine za kijadi. Badala yake watatumia njia za kisasa za kuvunia mazao yao.

Umaskini mwingine huwa mwiba wa kujichoma. Baadhi ya watu ni mikunguni. Kulaza damu kwao kunawafanya kuwa wategemezi katika familia na jamii kwa jumla. Kwa vile hawajazoea kuinamia cha mvunguni, hata wakifunzwa kuchakura hawawezi. Ili kujaribu kuutibu uwele wao na ufukara baadhi yao hutafuta njia za mkato kama vile upwekuzi wa vitu vya wale waliojitahidi. Wakifanikiwa huweza **<u>kufurisha vibindo vyao.</u>** Hata hivyo mkono mrefu wa walinda usalama ukiwakumbatia wao hubakia kusagika kwa dhiki isiyomithilika ndani ya magereza.

Majanga ya kimaumbile kama vile mitetemeko ya ardhi, mikurupuko ya maradhi hatari, moto, ukame na mafuriko huchangia na kuzidisha umaskini. Matukio hayo yakiandama kidindia watu wengi huhasirika. Licha ya mali nyingi kupotea, manusura huachwa wakiwa maskini hohehahe. Matumizi yao hupotea kwani wengi huhitajika kuanza maisha upya.

Vijana ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Endapo watajiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya, wataathirika wao wenyewe na jamii kwa jumla. Pamoja na kuwa vijana hawa hufuja pesa nyingi katika ununuzi wa dawa hizi, dawa zenyewe huwadhoofisha na kuwapoka nguvu za kushiriki katika uzalishaji mali. Kutokana na hali hii,umaskini hupaliliwa na kushamiri zaidi.

Umaskini huzua matatizo mbalimbali katika jamii. Ufukara huchachawiza juhudi za serikali za kuwapa raia wake mahitaji ya kimsingi kama vile huduma za afya. Pia umaskini husababisha maovu mbalimbali ya kijamii kama vile mauaji na ukahaba.

Baadhi ya wanajamii huona kwamba njia ya kipekee ya kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na hali ya ulitima ni kupitia kwa biashara haramu. Hali hii huchochea zaidi kudorora kwa maadili ya kijamii.

Mataifa mbalimbali ulimwenguni yamezua mikakati mahsusi ya kukabiliana na umaskini. Baadhi ya mataifa yamebuni utaratibu maalum wa kupunguza mwanya mkubwa uliopo kati ya matajiri na maskini. Mojawapo ya mipango hiyo ni kupandisha viwango vya kodi inayotozwa wenye mishahara minono na wafanyibiashara wenye pato kubwa. Aidha huduma za burudani hutozwa kodi ya kiwango cha juu. Kupitia kwa kodi hizo, na njia nyinginezo, serikali za nchi hizo hupata pesa za kuwahudumia maskini.

Mataifa yanayoendelea yanaweza kuwakwamua wananchi kiuchumi kwa kuwapa wahitaji mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Mifano ya miradi hiyo ni viwanda vya ‘Jua kali’, ususi wa vikapu na uchongaji wa vinyago. Hali kadhalika, serikali inaweza kuwatafutia masoko ya nje wafanyi biashara wadogo wadogo. Aidha, serikali inaweza kupunguza ushuru kwa bidhaa zinazoagizwa na masoko ya nje wafanyibiashara wa aina hiyo. Mathalan, ushuru unaotozwa nguo kuukuu zinazoingizwa nchini ukipunguzwa, wauzaji wa nguo hizi watafaidika zaidi na hali ya umaskini itaendelea kupungua.

Sehemu za mashambani ni mhimili mkubwa wa uchumi. Ingawa kumekuwa na juhudi za kuzistawisha sehemu hizi kwa kusambaza huduma za umeme na maji kwa gharama nafuu, bado hali haijawa ya kuridhirisha. Ili kuimarisha sehemu hizi na kukabiliana vilivyo na tatizo la umaskini, hatuna budi kusambaza huduma hizi hasa katika sehemu kame. Sehemu hizi zikipata maji, kilimo chenye natija kitaendelezwa na umaskini utakuwa karibu kuzikwa katika kaburi la

sahau. Ikiwa tutazitekeleza sehemu hizi, vijana wanaoweza kusistawisha watahamia mjini kutafuta maisha 'bora'. Hali hii itazidisha msongomano wa watu mjini.

Umaskini ni nduli ambaye lazima aangamizwe ima fa ima. Vijana hawana budi kubadili mtazamo wao hasa kuhusu kazi za mashambani na kujitahidi kuimarisha kilimo. Fauka ya hayo, mifumo mwafaka ya elimu ibuniwe ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya taifa. Badala ya kuhimiza elimu ya kinadharia, elimu tekelezi isisitizwe zaidi ili wale wanaokosa kazi za kiafisi waweze kujiajiri katika kazi za kiufundi. Ukusanyaji wa ushuru uimarishwe zaidi. Hali ya usalama iendelee kustawishwa ili kuzidi kuwavutia wawekezaji, na hivyo kubuni nafasi zaidi za kazi.

**Maswali**

(a)Kulingana na kifungu '**umasikini ni hali inayoletwa na udhaifu wa mtu binafsi'**. Jadili (maneno 30-40)

(b)Jamii ina uwezo wa kukabiliana na hali ya umaskini inayowakumba raia wake. Thibitisha kwa mujibu wa kifungu (maneno 40-50)

2. **MENO YA BINADAMU**

Kila mara tunapokula, meno yetu huuma, kutafuna na kusaga chakula tunachokula. Meno yanatuwezesha kukivunja chakula ili kuwezesha mwili wetu kukitumia. Ili mwili uweze kukitumia chakula hicho, pana vitu fulani vinavyokifanyia chakula hicho kazi mpaka kikaweza kuingia kwenye mwili wenyewe. Hivi hujulikana kama vimeng'enya. Binadamu ana meno ya aina nne kuu. Kwanza, kuna meno ya mbele au makato ambayo kazi yake ni kuuma au kukata chakula. Haya yanasaidiana na mengine yanayojulikana kama michonge; yanakata pia lakini yako sehemu ya nyuma. Michonge hufuatwa na meno mengine yanayosaga chakula na ambayo hujulikana kama masagego. Masagego hufanya kazi na meno mengine yajulikanayo kama magego. Kazi ya aina hizi mbili za meno ni kutafuna na kusaga chakula kabisa kabla ya kukimeza. Idadi ya meno ya mtu mzima ni thelathini na mbili. Bila ya kuwa na meno mazuri, binadamu hukabiliwa na matatizo makubwa wakati wa kula. Meno huweza kuharibika kwa sababu ya kutopigwa mswaki vizuri mara kwa mara. Ili kuhakikisha kuwa meno yetu ni mazuri, pana umuhimu wa kudumisha afya nzuri ya meno. Kila baada ya kulala, lazima tuhakikishe tumeyapiga mswaki vizuri bila ya papara ili kuondoa mabaki ya chakula yanayoweza kuwa chanzo cha viini vinavyoharibu meno. Pili, lazima tuhakikishe kuwa hatuharibu ufizi wa meno, yaani ile nyama inayoshikilia meno hasa kwa vijiti katikati ya meno baada ya kula. Afya ya meno ni muhimu ili kuhakikisha kuwa meno yetu yanadumu na kuendelea kutufaidi katika uhai wetu.

. (a) Kwa nini ni muhimu kudumisha usafi wa meno?
(Tumia maneno yasiyozidi 25)

(b) Fupisha taarifa uliyosoma. (Tumia maneno yasiyozidi 80).

**3.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu huathirika na biashara ya kimataifa.Biashara hiyo inaweza kuwa inafanya kwa uagizaji ama uuzaji wa bidhaa za nchi nyingine.

Biashara ya kimataifa ina umuhimu mkubwa. Kwanza, inawezesha nchi kupata bidhaa ambazo haitengenezi mbali na kusaidia kuwepo na uhusiano kati ya nchi mbalimbali. Uhusiano huu huiwezesha nchi kupata bidhaa kwa bei rahisi kuliko ambavyo ingekuwa kama zingetengenezwa kwao, hasa ikiwa nchi inayohusika haina malighafi yanayohusika katika utengenezaji wa bidhaa hizo. Pia husaidia wakati nchi imekumbwa na dharura au majanga kwani itaauniwa na nchi nyingine ingawa hali kama hii haihakikishwi, ushirikiano huu vile vile huchochea upatikanaji wa nafasi za kazi kwa wengi.

Kwa sababu za kushughulikia utengenezaji wa bidhaa na utoaji huduma nyingine kutokana na uzoefu wa muda na kuwepo raslimali, nchi huwa na uzoefu fulani. Ni kwa sababu hii nchi inawezeshwa kupata pesa za kigeni na kuuza bidhaa za ziada.

Hata hivyo kuna matatizo yanayozikumba nchi za kiafrika katika biashara hii. Kwanza, biashara ya aina hii hutatiza viwanda vichanga katika nchi zinazoendelea kwa ushindani usio sawa. Ajabu ni kwamba nchi zilizoendelea zimetumia bishara hii 'kutupa' bidhaa za hali ya chini

ama zenye athari kwa hali za kijamii.Urafiki haukosi. Ikiwa nchi inategemea uagizaji wa bidhaa, haitaweza kuikosea ama kuhitilifiana na nchi ambayo inategemea, hivyo kuathiri uhuru wa nchi kama hiyo.

Hata hivyo, nchi mbalimbali zimeweka mikakati ya kulinda viwanda kutokana na athari ya biashara kama hii. Baadhi zimeweka ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa utoka nje kwa wasio washirika wa kibiashara. Licha ya hayo, baadhi ya bidhaa zinazonuiwa kwa nje kwa matumizi ya kielimu, utafiti wa kisayansi nabidhaa za maonyesho huagizwa bila ushuru huo. Wakati mwingine ni benki kuu ndiyo hutoa leseni kwa niaba ya serikali kama njia ya kudhibiti bidhaa kutoka nje. Njia nyingine ya kuvisaidia viwanda nchini ni kuuza bidhaa kwa njia ya kuvipunguzia ushuru, usafirishaji nafuu na kuvipa ushuru.

Serikali nyingine huhakikisha kuwa ni bidhaa kiasi fulani tu ambazo zinaweza kuagizwa kwa kipindi fulani. Kwa mfano, kuna idadi fulani ya magari kutoka nje yanayoweza kuagizwa kuja Kenya kwa mwaka mmoja. Hata hivyo, wakati mwingine, serikali husitisha uagizaji wa bidhaa kama vile dawa, sinema, maandishi ya kisiasa na vitabu kutoka nje; bidhaa ambazo zinachukuliwa kuwa hatari kwa nchi. Licha ya matatizo haya, biashara imekuwepo na inaendelea kujiimarisha.

**Maswali**

(a) Kwa mujibu wa mwandihsi wa makal haya, bishara ya kimataifa itaendelea kujiimarisha. Eleza (al. 6) (maneno 40-50)

(b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya mbili za mwisho. (maneno 40-50)

4. ***Soma taarifa inayofuata kisha ujibu maswali yaliyoulizwa***

Usafiri ni upelekezi wa watu na bidhaa au mizigo kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine. Tuseme kutoka kituo A na kuenda kituo B.

Katika ulimwengu wa leo, watu na bidhaa husafirishwa barabarani kwa mabasi au motokaa za kila aina au kwa kutumia magari moshi yanayopita juu ya reli, au meli zinazopita majini, kadhalika, usafiri unaweza kufanyiwa hewani.

Hivyo, hali haikuwa hivyo zamani. Usafiri uliojulikana sana kale ni usafiri kwa miguu. Watu waliposafiri kutoka eneo moja hadi jingine walilazimika kufanya hivyo kwa miguu. Kadhalika, watu waliposafirisha mizigo mizito kutoka eneo moja hadi nyingine, iliwabidi kuibeba mizigo hiyo wao wenyewe. Mpaka leo usafiri huu upo.

Wanyama vilevile walitumiwa kama njia moja ya usafirishaji. Huku Afrika ya mashariki kulitumika wanyama wengine kama vile punda. Punda ni mnyama anayependwa sana kwa sababu anaweza kuenda mwendo mrefu pasipo na kunywa maji. Mpaka leo, mnyama huyo hutumika sana na wamaasai, wagala, warendile na wengine.

Mnyama mwingine aliyetumika sana, na mpaka leo anaendelea kutumika ni ngamia. Ngamia anafaa sana katika usafiri wa jangwani. Kwato za ngamia huweza kusafiri kwa urahisi jangwani ama popote penye mchanga mwingi kwa sababu kwato zake hazizami kwenye mchanga. Isitoshe ngamia wanaweza kwenda mwendo mrefu bila maji au chakula huku wakitegemea mafuta yaliyohifadhiwa kwenye nundu zao.

Katika ulimwengu wa kisasa, binadamu amepiga hatua kubwa sana katika masuala ya usafiri. Baadhi ya maendeleo hayo ni ya kustaajabisha. Kwa mfano, binandamu anaweza kuruka kwa kutumia vyombo vya angani kwenda kwenye anga za mbali. Katika karne iliyopita binadamu anaweza kuruka kwa kutumia vyombo vya angani kwenda kwenye anga za mbali. Katika karne iliyopita binadamu amefika mwezini kwa kutumia vyombo hivyo. Kuna tetesi kwamba sasa anajaribu kuzizuru sayari zilizoko mbali na ardhi.

Ama kwa hakika, usafiri bora in kipimo kimojawapo cha maendeleo ya nchi yoyote katika ulimwengu wa sasa. Bila njia ya kisasa za usafiri, baadhi ya mambo yanayofanyika katika nchi zetu hayangefanyika.

(a) Katika habari hii, punda na ngamia wana sifa gani muhimu zinazowawezesha kutumiwa

kwa usafirishaji? (maneno 30-40) (ala. 6, 1 mtiririko))

(b) Kwa mujibu wa taarifa, usafiri wa zamani unatofautiana vipi na ule wa siku hizi? (maneno 40-50) (al. 7, 1 mtiririko)

5. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii na kwa dhati ya mioyo yetu uweze kupata ufanisi na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu. Tukumbuke, "Ajizi ni nyumba ya njaa". Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo chini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu.Tunahitaji taifa la watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeka. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni Wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wake. Wengi ni wale wenye mawazo kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wageni .

Mafunzo tunayopata nyumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwana Kenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu wazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja, "Utengano ni uvundo". Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu ,wakati tunapokosea na kufanya masahihisho mara moja kwani, :Usipoziba ufa, utajenga ukuta. "Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashtumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa tuwe na nidhamu shuleni na nyumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo; lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo, basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kwa utajiri wake. Kwa hivyo basi, tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba au ya utajiri.

a) Dokeza mambo muhimu yaliyomo katika aya ya kwanza. (Maneno 65 – 70)

b) Fupisha aya ya mwisho kwa kuzingatia mambo muhimu yanayowapasa vijana kufanya (Maneno (maneno 35 – 45)

6. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:***

Usawa wa wanadamu upo kimaumbile – maumbile ya mtu kamwe hayatakosewa na yale ya mnyama wa mwituni. Lakini fikira, tabia, kimo, uwezo na mahitaji huwa tofauti kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Kwa mintarafu hii yapasa wakufunzi na wazazi kuwapa watoto wao widhaa mapema ili wachague kwa wakati unaofaa kazi watakayoifanya maishani.

Watoto wanapopelekwa chuoni, wazazi wao huukilia kuwasomesha hadi kiwango fulani cha masomo kisha wajitafutie kazi ambayo itawapa masurufu na pesa za shughuli zingine maishani.

Katika nchi yetu tangu tupate uhuru mtindo wa kutoa kazi umekuwa ni ule wa kuchukua watu waliofaulu mitihani ya viwango fulani na kuwapa kazi moja kwa moja. Mwenendo huu wa kuajiri watu kazi umeendelea muda mrefu lakini sasa yamkinika utasitishwa na njia mpya kufuatwa. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa nafasi za kazi zimekuwa finyu sana. Kabla na punde

baada ya uhuru nafasi hizo zilipatikana kila mahali. Nyingi ya hizo ziliachwa wazi na wageni walioihama nchi hii tulipojitawala. Siku hizi wanafunzi wanaokomea darasa la saba, kidato cha pili na hata cha nne huwa hawazioni ahadi za kupata kazi za madaraka fauka ya kazi yoyote. Wanaoiona tabasamu ya kazi mbele yao ni wale wanaotasawari masomoni wakifuata taaluma fulani.

Tatizo la kazi laeleweka vema kwa serikali na ni kwa ajili hii serikali imemtasulia kila mwananchi kuwa wakati wa kuania kazi za utanashati umetimiuka. Wakati uliopo ni wakati wa kujifunga vibwebwe kisaki na kuchapa kazi zile ambazo hadi sasa zafikiriwa kazi chafu na zisizofaa wasomi. Dhana kama hiyo ni ya kibwanyenye, na ubwanyenye hauji ila kwa sulubu. Usemapo kuna kazi nzuri na mbaya huwa unazusha maswali mengi. Utatakiwa ueleze kinaganaga kazi nzuri au mbaya kwa nini? Kazi huwa nzuri kwa upande wa tija au kwa upande wa wepesi wake? Kujibu maswali ya namna hii kutahitaji wekevu mwingi, waima mtesi ataonekana dufu.

Zipo kazi aina mbili. Ipo kazi ya kuajiriwa na ya kujiajiri. Kazi ya kujiajiri kwa kulinganishwa huonekana ngumu na yenye matatizo mengi mwanzoni. Lakini itakubalika pato lake ni kubwa zaidi ikishapata msingi imara. Msingi imara huwekwa kwa juhudi za mwanzoni zikiambatana na ujasiri. Mtu asiyejasiri kutenda tendo lolote maishani ni sawa na yule asiyejua atokako na kule aendako; yuaishi kungozwa. Ardhi ni thawabu, tena thawabu tunu. Ukiwa na kipande cha ardhi ifaayo kwa kilimo ufakiri ukikutawala ni wewe mwenyewe kupenda: la sivyo ufa umo ubongoni unaohitaji bwana mganga

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza na ya pili. maneno 60-70)

(b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho. Eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi. (maneno (50-60)

7. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ufupishe taarifa hii kulingana na maswali yanayofuata:-***

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, tumeshuhudia mabadiliko na maendeleo makubwa kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hapo awali, redio ndicho chombo cha habari cha kipekee kilichotamalaki kote nchini. Familia nyingi ziliweza kumiliki chombo hiki. Runinga ilikuwa miliki ya wachache, hasa mabwenyenye. Sasa hivi, hata akina yahe nchini na mashambani wanamiliki chombo hiki.

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasilianao kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundisha. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkem kwa mtu wa kila rika. Hali kadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji ya kufundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo wa vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia , kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanayowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa wanafamilia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa na kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalan, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya madawa ya kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaoutumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya waelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

**<u>Maswali</u>**

(a) Ukitumia maneno 50-60, fupisha manufaa ya runinga

(b) Fupisha hasara za runinga ukitumia maneno 70-80

**8.** ***Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.***

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kutoka kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza ubongo hunasa jambo kisha huliihifadhi. Baadaye huanzisha mfumo wa kutoa kilicho hifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yeyote katika moja wapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitajika mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini), bidhaaa za soya, matunda, maziwa, ,bidhaa za ngano, samaki, pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madina haya ni mboga za kijani, mawele, ndengu, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini. Kwa hivyo, vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisicho hatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni

kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kumvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na pia namna ya kukitoa.

Halikadhalika, mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa na mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na taratibu ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya hayo, mazoezi ya kiakili, kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitenzi ndimi ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo kuyakumbuka mambo ni ya jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

**Maswali:**

a) Kwa maneno 60 – 65 fupisha mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.

b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 80 – 90

9. ***Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.***

Faragha ni muhimu kwa binadamu kwani huwa ndio wakati ambapo mtu atakuwa akitulia pekee mahali na huku akijiuliza ni mema mangapi ameyatenda siku hiyo, maovu mangapi ameyafanya, na kama siku hiyo ilikuwa ya manufaa au la.

Si binadamu wote ambalo wanapendelea kutumia wakati wao wa faragha kwa kupiga domo, nyumbani, kustawisha mabustani yao ya maua au mimea, au hata kuchukua kitabu au magazeti ya kusoma na kujifunza. Watu kama hawa huwa na fikira na mawazo mbalimbali juu ya umuhimu wa thamani ya wakati wa faragha. Watu kama hao utawakuta wakikusanyika katika makundi kwa matarajio ya kujinufaisha kwa mapato fulani au kujiingiza katika upigaji wa kamari. Wengine hunufaika wakasifu mafanikio yao ya siku ya mkusanyiko na baadhi yao ambapo hufanya mhanga wa michezo hii huibuka huku wakilaani na kuapiza bahati zao mbaya.

Kuna kundi jingine ambao hustahabu vilabu vya usiku kwa kujiliwaza au kujitumbuiza ili wapate kujituliza mawazo yao, wakayatafuta makali na kileo. Mwanzo wa ushirika kama huu huwa mzuri, watu huongea na kutoleana mawaidha yenye muafaka kiungwana kabisa. Lakini mara tu baada ya kuyakata makali haya kwa muda hivi, washiriki wake hupumbazwa na huanza kuyakata matindi mithili ya komba mpaka kiasi cha kubwata maneno ovyo ovyo na hatimaye kupoteza mbali fahamu. Ndipo kuruka kwa akili na kuanza zahama zenye kuonyesha utoto badala ya utu uzima. Kadiri makali hayo yanavyosiliwa kwa kuiva kwake, ndivyo wafuasi na mashabiki wake huyatumia kwa wingi na hata kuyaabudu, huyaabufu; huyabugia bila kujali uzito.

Na iwapo ndio kwanza wapokee mabunda yao, hakuna la kutia kikomo tafrija hizo ila uzito wa matendo ya ubadhirifu hujitokeza baada ya kurudi nyumbani, kulala fofofo na wazindukanapo siku ya pili yake ndipo wagundue walivyo taabani.

Mtindo wa matumizi ya faragha hutokea tangu mwanzo wa mazingira ya mtu; hivyo tangu utoto wake; tabia njema na zipasazo huhitajiwa kufunzwa. Sehemu kubwa ya mafunzo haya muhimu hutokana na malezi ya nyumbani chini ya uongozi wa mama na baba. Kama wasemavyo wahenga, mtoto akuavyo ndivyo alivyolelewa. Na mama mtu awe nyoka, hapana budi kuwa mwanawe naye atainuka kustahabu unyoke" wa mama yake. Hivyo ni wajibu wa wazazi kujenga mazingira yanayofaa kwa vizazi vya kesho kwa kuelekezwa namna yake. Ingewezekana himizo kubwa lingesisitizwa katika marekebisho ya tabia za wazazi kuwezesha manufaa yake. Ingewezekana, himizo kubwa lingesisitizwa katika marekebisho ya tabia za wazazi kuwezesha watoto kuiga mtindo au mitindo ya maisha yanayofaa. Kielezo chema ni kuwa na mzazi mwenye tabia njema kwa mtoto wake, rafiki zake na kwa jamii yake.

(a) Ni nini umuhimu wa faragha kwa binadamu kwa mujibu wa aya ya kwanza?(maneno 20)

(b) Eleza jinsi watu wengine wanavyoharibu wakati wao wa faragha kwamambo ya upotovu kwa kurejelea aya ya pili na ya tatu (maneno 30) (al. 5 al. 1ya utiriko)

(c) Eleza mchango wa mzazi kwa mwanwe kuhusu matumizi bora ya wakati wa faragha.
Zingatia aya ya mwisho

**10.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo***

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia huletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng’ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

(a) Fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 50 -55)
b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho (Maneno 55-60)
Utiririko ni alama 3

**11.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Kwa hali nyingine , tunaweza kusema kuwa uchafuzi wa mazingira ni uharibifu wa vile vitu vinavyowazunguka binadamu na wanyama maishani mwao. Kuna uchafuzi wa aina mbalimbali na kila uchafuzi humhusu binadamu kwa njia fulani.

Maendeleo ya viwanda duniani ni sababu mojawapo ya uchafuzi wa hewa. Mitambo katika karakana huwa inatoa moshi mwingi wakati bidhaa zinapotengenezwa. Moshi husambaa eneo kubwa na kuchanganyika na hewa inayovutwa na binadamu. Uchafu hutupwa ovyo ovyo na kuwa hatari kwa afya ya binadamu. Maji machafu huweza kutiririkia mtoni, maziwani na hata baharini. Yale yanayotiririka mitoni na maziwani huchafua maji ambayo hutumiwa na watu wa eneo hilo kwa kunywa, kupika na kunywesha mifugo wao. Yale yanayotiririka baharini huwa ni hatari kwa samaki wanaotegemewa na binadamu kuwa kitoweo muruwa.

Ongezeko la watu pia ni hali nyingine ya uchafuzi wa mazingira. Halaiki ya watu hufanya uharibifu wa misitu ya asili. Hii ni kwa sababu ya kutaka kuongeza ekari za mashamba. Hili husababisha mmomonyoko wa udongo ; hivyo basi kuiacha ardhi bila rutuba yoyote. Katika hali

hii, kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa nchi nyingi duniani huzoroteshwa. ''Maisha ya binadamu hutegemea kilimo kwa kila hali kwa hivyo kilimo kinapozoroteka hata uchumi nao huathirika. Kila uchao tunasikia kwamba nchi fulani imekabiliwa na njaa.

Ufugaji wa wanyama wengi bila mpango maalum pia huharibu mazingira ya asili kama nyasi na vichaka. Watu wengi hufuga ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kwa kuwa hawana mahali maalum pa kuwalisha, huzunguka nao huku na huko kutafuta nyasi na majani ya kuwalisha. Wanyama wanaotangishwatangishwa namna hiyo humaliza majani na nyasi zote na kuacha ardhi tupu ambayo hatimaye huyabisika kwa jua. Ardhi ya namna hii haishiki maji mvua inyeshapo. Nchi iliyoneemeka huweza kuwa jangwa lililo na chungu ya mchanga.

Watu wanapoongezeka huko mashambani huwabidi wakate misitu ili waanzishe maskani mapyapamoja na mashamba yao. Miti hukatwa bila hadhari na mabiwi ya matawi pamoja na majani huchomwa moto. Jambo la kusikitisha ni kwamba miti hiyo inapokatwa hakuna mingine inayopandwa kuchukua mahali pake.

Mahitaji ya binadamu ya kuendeleza njia za mawasiliano pia huzusha balaa nyingine. Barabara zinazidi kuongezeka na pia watu wanaozidi kuongezeka pamoja na mazao yao. Kwanza, barabara zinapotengenezwa misitu hukatwa mahali zinapopitia. Pili, wingi wa magari huzidi na baadhi ya hayo hutoa moshi unaoharibu hewa.

Njia kadha wa kadha za kuzuia uharibifu wa mazingira zimependekezwa. Ingawa suluhisho timamuhalijafikiwa, Serikali nyingi duniani zimo katika harakati za kutafuta suluhisho la uchafuzi huo.

Njia mojawapo ni kukomesha ujenzi wa viwanda katika miji mikuu na mahali palipo na watu wengi.Wenye viwanda pia wanahimizwa kufikiria jinsi ya kutupa takataka na maji machafu bila kudhuru afya ya binadamu.

Watu wakizingatia suala la upangaji wa uzazi na kuwa na familia ndogo ndogo, idadi ya watu haitaongezeka kwa kasi kwa hivyo itakuwa hakuna haja ya kuanzisha makao mapya mara kwa mara.

Serikali nyingi zimechukua jukumu la kuwaelimisha raia juu ya madhara yanayotokana na uharibifuwa mazingira. Raia wanahimizwa kupanda miti kwa wingi.

Jitihada zinazofanywa kuzuia uchafuzi wa mazingira hukumbana na matatizo. Tatizo kubwa ni fedha za kuendeleza miradi inayopendekezwa. Shida nyingine ni kwamba juhudi zingine huwa zinamwingilia binadamu na mali yake.

**Maswali.**

(a) Fupisha aya za kwanza sita za taarifa uliyosoma (maneno 50-60)

(b) Fupisha aya za mwisho tano kwa maneno 40-45

12. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Vijana wa siku hizi hujifikiria kuwa wao ni bora kuliko wazee wao. Wao hujifikiria kuwa wameelimika zaidi, wana busara zaidi, wanauelewa ulimwengu vizuri zaidi na wanaweza kujiamulia hatima yao bila uongozi wa wazazi wao. Wazee kwa upande wao, hawakubali kabisa madai ya aina hiyo. Kwao ni maasi tu. Wanachojua wazee kwa hakika ni kuwa vijana wa siku hizi hawaajibiki kwa lolote, wamedekezwa mno na wanapenda sana nafsi zao. Kwa sababu hiyo, vijana wanahitaji uongozi na ushauri wa wazeee.

Je, kuishi kwingi ni kuona mengi? Ingawa wazee wanafikiria wanajua mengi kwa sababu ya umri wao, vijana hupenda sana kukosoa fikira za wazee wao. Hawakubali imani na itikadi za wazee wao. Kwa mfano; vijana hupendelea mitindo ya mywele ambayo wazee wao hufikiria kuwa kichaa tu.

Wazee husifiwa sana enzi zao. Husifia jinsi walivyolelewa kwa kuchapwa na kufanyishwa kazi zinazohitaji uvumilivu mkubwa kama vile kuchanja kuni, kufyeka misitu, kutayarisha mashamba, kuwinda na kadhalika. Kwa sababu ya malezi hayo, wazee husema wao walirithi nidhamu nzuri na ushujaa. Vijabna kwa upande wao hawaoni chochote cha kujivunia katika zama za wazee wao; wao hufikiria kuwa wazee wao walilelewa kwa ukatili kwa sababu zama zao zilikuwa enzi za giza, kabla ya majilio ya uungwana na ustaarabu wa kisasa.

Wazee husifia kuwakumbusha vijana ule msemo mashuhuri wa wahenga usemao kuwa 'mwacha mila ni mtumwa.' Kwa maoni ya wazee, vijana wengi wamekuwa watumwa kwa sababu wao huonyesha kwa vitendo kuwa hawadhamini desturi za wazee wao. Ka mfano; vijana hawafuati miiko ya jadi, hawapendi kuhudhuria sherehe za kienyeji, kwa mfano sherehe za kutoa makafara. Vijana pia hawapendi ngoma za kitamaduni, na isitoshe vijana hawazionei fahari koo zao. Vijana hawakubali kuwa wao ni watumwa wa mtu yeyote. Mila wanazosifia wazeee wao si vitu vyenye umuhimu wowote kwa vijana. Kwa mfano; baadhi ya miiko ni kisayansi. Kuhusu ukoo, si vijana wengi wanaona umuhimu wake. Ukoo na kabila zilikuwa muhimu zamani wakati ambapo kulikuwa hakuna serikali, bima na hata kazi ya mtu binafsi. Mambo haya sasa ni kama masalia ya zamani ambayo yamepitwa na wakati.

Je, vijana hupenda sana burudani na anasa tu kama wanavyodai wazee! Wazee wengi hufikiria kuwa vijana hupoteza muda wao mwingi kujitafutia anasa na burudani kwa mfano vijana wengi hurandaranda barabarani au mitaani wakisingizia kupunga hewa. Wengine huenda sinema na kuhudhuria dansi na karamu zisizo na manufaa. Vijana kwa upande wao hawaoni kinachowawasha wazee wao; pilipili wasioila yawashia nini?

1. Katika makala haya wazee wana malalamiko yapi kuhusu vijana? (maneno 50-60)
2. Msemo unaosema "Mwacha mila ni mtumwa" unathibitishwa vipi katika maoni ya wazee katika makala haya? (maneno 15- 25)

13. ***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali</u>***

Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo itokeapo amali, shughuli na harakati zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima kwa serikali au dola kama ulinzi, sheria na mpangilio wa jamii huwa huria kwa watu binafsi. Msingi wa soko huria, sifa kuu ya utandawazi, ni kuibua na kudumisha mazingira na hali zinazochochea na kumruhusu mtu yeyote kuongozwa na hawaa, au matamanio ya kibiashara anayoyaona sawa pasi na hofu ya kuingilia na udhibiti wa serikali.

Mazingira hayo yanawapa watu satua ya kufanya maamuzi kuhusu hatima yao ya kiuchumi, uamuzi kuhusu suala la ajira yao, matumizi ya mtaji kipato na harija zake, na uwekezaji mzima. Suala mojawapo linaloibuka kuhusiana na mfano wa soko huria ni kuweka mipaka bainifu na wazi baina ya amali na shughuli zinazohusishwa na serikali na zile ambazo huachwa huria kwa watu. Kwa mfano, inaaminiwa kuwa haki ya kuishi na kulindwa dhidi ya shambulizi, liwe la kijambazi au la kigaidi, ni ya kimsingi ambayo haiwezi kuhusishwa na uwezo wa kiuchumi wa mtu binafsi. Aidha huduma za kimsingi za afya nazo zinaingia katika kumbo hili. Ikiwa huduma hizi zitaachwa huria pana uwezekano mkubwa kuwa zitaishia kuwa istihaki ya wenye mtaji na kipato cha juu tu.

Licha ya kuwepo kwa sheria au kanuni huria kutoka nyanja maalum, hutokea hali ambapo adhibiti wa kiserikali ni lazima. Hii hutokea pale ambapo ipo haja ya kuyalinda mazingira hasa kutokana na uchafuzi wa viwanda au tasnia. Aidha udhibiti huo ni lazima pale ambapo haki za watu wengine zinahusika: yaani ikiwa uhuru wa hata mtu mmoja unaadhirika kutokana na sera hizo pana haja ya kuingilia ili kuisawazisha hali yenyewe.

(a) Andika kwa muhtasari maana ya uchumi wa soko huria kulingana na taarifa hii.
(maneno 25-30) (al. 5, 1mtiririko)
(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya pili na ya tatu.
(maneno 70-75) (al. 10,3 za mtiririko)

**14.** **<u>WAJIBU</u>**

Sisi vijana ni wa taifa. Hatuna budi kutumikia umma kwa moyo wetu wote.Hakuna haja ya kulaza damu ikiwa taifa linatuhitaji. Ni lazima tuwe shupavu kwa mambo yote. Tuwe wenye busara, adabu njema na ari ya kutenda kazi kwa moyo wa utu. Ni muhimu kabisa kulinda, kutumikia na kuendeleza taifa hili changa katika mbinu zake na mipango yake yote kuhusu zaraa, elimu, uchumi, ulinzi na mipango yote ya maendeleo ya ustawi wa nchi na jamii. Inatupasa tuelewe

ujamaa wetu na jinsi ya kupambana na ubepari, ukabila, ukupe, unyonyaji na ukoloni mamboleo. Hii itaondoa kabisa jasho letu. Inatubidi sisi vijana tujifunze jinsi na namna ya kuwa watu bora.

Elimu tuipatayo kutoka nyumbani, shuleni na katika jamii, lazima igeuze fikira zetu. Elimu hiyo lazima tuitumie ili itupatie uwezo wa kuelewa mema na mabaya maishani mwetu. Ni bora tujue wajibu wetu katika kufikiri, kusema na hata kutenda kufuatana na wajibu huo kwa mioyo na dhamiri safi. Tuwe vielezo kwa wengine. Hasa tujitayarishe kuwa wazazi na viongozi bora wa kesho. Mno mno tuwe wazalendo na raia wema wa taifa hili changa. Tuhimize na kuendeleza utamaduni wetu wa lugha yetu ya taifa. Hatimaye tutambue usawa wa kila binadamu, popote alipo bila kujali taifa, kabila, rangi na hata dhehebu yake.

Tujifunze kujishutumu. Pia tukubali kusahihishwa makosa yetu na watu wengine. Hasa tuwe nguzo, kinga na ngao ya nchi yetu inapopigwa adharusi.
Acha nirudie kusema tena kuwa ni shabaha yetu sisi vijana kuwa na nidhamu njema. Nidhamu njema ni chanzo cha asili cha siha ya ujamaa na kujitegemea. Kwa hivyo, uongozi bora na bidii, ushirikiano mzuri na kujishughulisha. Uchaguzi bora wa viongozi na mifano mizuri ni kurunzi ya maendeleo ya ustawi wetu.

(i) Ni nguzo zipi ambazo kifungu hiki kimezipa kipaombele kwamba zitasimamisha ustawi na maendeleo ya nchi kutokana na vijana? Jadili kwa maneno thelathini
(ii) Vijana wameshauriwa wafanye mambo mengi mema. Jadili kinyume cha ushauri huu ukitumia maneno yako mwenyewe

# Matumizi ya lugha

1. (a) **Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi "O"**
Mtoto anayelia huchapwa
(b) **Andika kinyume**
Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.
(c) **Andika sentensi tatu ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii:-**
Kule ndimo alipoingia
(d) **Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi iuatayo**
Mama <u>amewahi</u> <u>kupika</u> jikoni
(e) **Eleza maana ya misemo ifuatayo** :-
(i) Giza la ukata…
(ii) Meza mate machungu
(f) **Unda vitenzi kutokana na :-**
(i) Mkufunzi
(ii) Maeneo
(g) **Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, taja aina za sentensi za kiswahili**
(h) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale**
Mwalimu huyu mzuri anafundisha darasani.
(i) **Eleza maana mbili za sentensi :-**
Mama alimlimia mwanawe shamba
(j) **Akifisha sentensi ifuatayo:-**
ah huu ndio upuuzi aliotuitia mmoja wao akaropoka.
(k) **Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano**
(l) **Andika sentensi ifuatayo katika msemo halisi :-**
Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa umetangulia.
(m) **Pambanua viungo vya kisarufi katika kitenzi kifuatacho**
Tuliwalimia
(n) **Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:**
Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (**kanusha kwa umoja**)
(o) **Tunga sentensi ukitumia neno "Vile" kama:**

(i) Kiwakilishi
(ii) Kivumishi
(iii) Kielezi

(p) **Bainisha matumizi viambishi "ku" na "Ji" katika sentensi zifuatazo**:-
(i) Mwanafunzi hukusoma kwa bidii
(ii) Atakupiga
(iii) Amejikata
(iv) Mchezaji huyu ni hodari

(q) **Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha**
Kijibwa changu ni kikali sana

2. (a) **Jaza mapengo**:-

| **Kutenda** | **Kutendesha** |
|---|---|
| (i) Chota | |
| (ii) Lewa | |

(b) **Taja sauti moja ya;**
(i) King'ong'o
(ii) Kiyeyusho

(c) **Tumia neno "*shujaa*" katika sentensi kama**:-
(i) Kivumishi
(ii) Kielezi...

(d) **Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:-**
Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi .

(e) **Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa**:-
Kichinjio hiki kilikarabatiwa kwa pesa nyingi

(f) **Eleza maana zinazojitokeza katika vifungu vifuatavyo**:-
(i) Jambazi kutoka dukani liliiba.
(ii) Liliiba jambazi kutoka dukani.
(iii) Kutoka dukani jambazi liliiba.
(iv) Jambazi liliiba kutoka dukani.

(g) **Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi:-**
(i) Vile vitu **ulivyovichanganya** itakubidi
(ii) Bomba hili l**imeziba** mwite fundi aweze

(h) **Unganisha sentensi hii kwa kutumia *'O'* rejeshi :-**
Wavu umekatika. Wavu ni wao

(i) **Eleza matumizi mawili ya "*ka*" na utunge sentensi kwa kila mojawapo**

(j) **Yakinisha sentensi hii**:
Sijafahamu kwa nini hawamkaribishi mpwa wao.

(k) **Andika katika usemi halisi:-**
Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(l) **Akifisha sentensi ifuatayo**:-
Sijaona kitabu kizuri kama mayai waziri wa maradhi, utaniazima siku ngapi bashiri alimwuliza rita

(m) **Changnanua kwa njia ya mishale**
Mama anapika na baba akisoma gazeti

(n) **Tunga sentensi moja na uonyeshe kwa mstari**;
(i) Shamirisho kipozi
(ii) Shamirisho kitondo
(iii) Shamirisho ala/kitumizi

(o) **Tungia vitenzi vifuatavyo sentensi katika hali zilizobanwa**:-
(i) Fa(**mazoea**)
(ii) La**(kutendeka)**
(iii) Pa (**kutendea**)

(p) **Tambulisha kishazi tegemezi na kishazi huru**

Wanafunzi walifoanya vyema walituzwa jana

(q) **Pambanua viambishi mbalimbali katika sentensi ifuatayo**
Waliwapendezea

3. a) **Onyesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani:-**
i) Unamjua vyema kweli?
(ii) Hicho wanachokitaka hakipo

(b) **Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi**:-
(i) Minghairi ya
(ii) Wala

(c) **Yakinisha sentensi ifuatayo**:-
Chakula hakipikiki vizuri

(d) **Jibu kulingana na maagizo kwenye mabano:-**
(i) Hatujui ambako alitorokea (**tumia 'O' rejeshi**)
(ii) Angekuwa na pete, angekupatia (**ibadilishe katika wingi kisha uikanishe**)

(e) **Bainisha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo:-**
Maksuudi alimjengea Tamima Kasri kwa matofali mazuri

(f) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale/mistari:-**
Watoto wote wameamka mapema na wazazi wanatayarisha staftahi

(g) **Unda nomino moja moja kwa kila kitenzi**
Shuku
Vumilia
shona
lia

(h) **Eleza maana ya <u>'jinsi'</u> kama inavyojitokeza katika sentensi zifuatazo**
(i) Naomba unionyeshe jinsi ya kuendesha gari
(ii) Wakenya hawapendezwi na jinsi viongozi wanavyoendeleza ufisadi

(i) **Bainisha aina za nomino zilizopigiwa mistari katika sentensi hii:-**
<u>Uhodari</u> wa <u>wanariadha</u> wa <u>Kenya</u> unahitajika kote duniani

(j) **Tunga sentensi ukitumia mzizi – choyo kama** :-
(i) nomino
(ii) Kivumishi
(iii) Kiwakilishi

(k) **Eleza matumizi <u>mawili</u> ya kila mojawapo wa alama za uakifishaji zifuatazo**:-
(i) msitari
(ii) Parandesi

(l) **Geuza zentensi zifuatazo katika kauli kwenye mabano**:-
(i) Fundi ameharibu saa (**kutendea)**
(ii) Umemwona mgeni? (**kutendewa**)

(m) **Andika kwa udogo:-**
Gari la Mzee Maritu limegonga ng'ombe wa jirani wake

4. (a) ***Andika sifa bainifu za sauti***
(i) e:-
(ii) n:- .

(b) ***Eleza maana ya :-***
(i) Kiimbo:.
(ii) Shadda…

(c) ***Tunga sentensi moja moja kudhihirisha ngeli zifuatazo***:-
(i) U-U
(ii) Pokomo /Pa-ku-mu

(d) ***Unda kitenzi kimoja kutokana na nomino*** '**Mtubia**"

(c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi '***ku***'

(f) Tunga sentensi ya maneno manne ambayo ina sehemu zifuatazo. Kielezi cha namna,

kivumishi,kitenzi na jina

(g) ***Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi***:-

Ng'ombe aliyeletwa juzi ameuzwa leo jioni.

(h) ***Onyesha matumizi mawili mawili ya alama zifuatazo:-***

(a) Alama ya mshangao

(b) Mshazari

(i) **Tunga sentensi sahihi ukitumia –*wa*- katika kauli ya kutendeana**

(j) ***Andika udogo wa sentensi:-***

Ndama wa ng'ombe yule ameuzwa.

(k) ***Onyesha tofauti ya vitate vifuatavyo kwakuvitungia sentensi***

(i) Dhamani

(ii) Thamani

(l) ***Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi***

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari

(m) ***Ainisha shamirisho /yambwa katika sentensi ifuatayo***:-

Mchezaji alimpigia mwenzake mpira kwa mguu wa kushoto.

(n) Huku ukitumia mifano mwafaka, eleza tofauti ya sentensi sahili na ambatano

(o) ***Onyesha aina za viambishi katika sentensi hii***:

Nitajisomea

(p) ***Andika katika usemi wa taarifa:-***

Tutaanza mashindano kesho, Mwalimu alimwambia mwanafunzi.

(q) ***Eleza maana mbili ya sentensi***:-

Tumetengeneza barabara

(e) ***Tumia mifano mwafaka kueleza aina za mofimu***

5. a) Unda nomino za/lm,k, dhahania kutokana na maneno yafuatayo :-

i) Kwea .

ii) Himarisha …

b) Huku ukitoa mifano eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili

c) Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi: 'umba'

d) Andika katika

Meza ii hii ndiyo aliyotumia kulia

e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendewa

i) cha …

ii) nywa

f) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo:

atakuajiri

g) Sisi tunajua sheria ingawa tu wafisadi

Anza: Japo………….

h) Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo:-

i) Wanafunzi wote wameingia darasani

ii) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani

i) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia njia ya matawi**:-

Amekuja kuwatembelea manusura waliopata ajali ya ndege

j) Taja sifa mbalimbali za sauti zifuatazo:

**/Z/**

**/K/**

k) Huku ukitumia mifano ya sentensi eleza matumizi **mawili** ya kiambishi, **'ji'**

l) **Andika udogo wa:**

Magari yote yaliyobakia yatauzwa na mzee yule mwembamba

m**) Sahihisha:**

i) Kila mwanafunzi alipewa ndazi na mayai moja

ii) Nipee huo mkoba nitoemo vitabu zangu

n) **Tumia – 'ako' katika sentensi kama**:

i) Kivumishi
ii) Kiwakilishi
iii) Kitenzi

o) Bainisha aina **mbili** za vishazi katika sentensi hii :-
Shamba lile kubwa litauzwa kesho

p) **Andika katika usemi wa taarifa** :
"Karibu Rahma, tafadhali kaa," Musa akasema . Ahsante, je, habari za hapa?' Rahma aliuliza

q) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi tofauti ya neno: '**somo'**

**6.** (a) Taja sauti **mbili** ambazo hutamkwa nyuma ya ulimi kati ya hizi
/h/,/o/,/y/,/u/,/kh/,/g/,

(b) Ng'oa kisiki hiki haraka askari akaamrisha mahabusu
(**Andika kwa msemo halisi**)

(c) **Badili sentensi zifuatazo katika kauli iliyoonyeshwa kwenye mabano**
(i) Si vizuri mwanafunzi kumwibia mwenzake pesa (**Kutendeana**)
(ii) Mpishi aliharibu mchuzi huu kwa kuongeza chumvi nyingi. (**tendeka**)

(d) **Bainisha matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo**:-
Alipowasili alionyeshwa walipo.

(e) **Andika kwa usemi wa taarifa:-**
"Wasichana wakielimishwa wataweza kuwa bora kuliko wavulana," Naibu wa Chansela wa chuo Kikuu aliwaambia mahafala.

(f) **Tunga sentensi ambayo ina aina za maneno uliyopewa:-**
N + V + V + T

(g) **Tumia ''O'' rejeshi ya kati**
Lisemwalo silo liwalo

(h) 'Msipokuwa wenye bidii hamtayapata mafanikio maishani.' Yakinisha katika umoja

(i) **Changanua kwa kutumia mishale**
'Mimi sikumwona wala Mwenda hakumwona'

(j) **Tunga sentensi ukitumia maneno haya katika kinyume**.:-
(a) afikiana
(b) sifu

(k) **Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo:-**
(i) abudu
(ii) fisidi

(l) **Andika katika hali ya ukubwa**
Mwanamke huyu amezaa watoto wanne.

(m) **Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigwa mstari**
(i) **Mbio** hizi hazitakufikisha mbali
(ii) Mwambie Abedi asifanye **mbio** kuhusu hiyo kazi.

(n) **Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi**
Msichana aliyeitwa alikuwa mkorofi

(o) **Eleza dhana zinazowakilishwa na viambishi awali katika sentensi zifuatazo: -**
(i) Aliitwa
(ii) Hakupata

(p) **Tunga sentensi mbili kubainisha maana tofauti ya maneno yafuatayo:-**
(i) Kuna
(ii) guna

(q) **Taja mianzo mitatu** tofauti ya ngeli ya **U-ZI**

(r) **Eleza maana ya semi hizi :**
(i) Kunja jamvi

(ii) Piga kambi

7. (a) *Andika sentensi ifuatayo bila kutumia* "**amba**":-
(i) Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali
(ii) ***Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea***:-
Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea
(b) ***Badilisha sentensi hizi hadi usemi wa taarifa:-***
(i) "Nitarudi tu ikiwa mtakubali kuomba msamaha". Juma alisema
(ii) "Elezeni vile mlivyokuja hapa na namna mtakavyokwenda." Mwalimu mkuu alisema
***(c) Fuata maagizo uliyopewa baada ya kila sentensi ili kujibu maswali haya :***
(i) Aliogopa kumwangalia simba aliyekula mzoga. (Tumia neno 'Ogofya' bila ya kubadililsha ya sentensi:-)
(ii) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ukiwa unatumia msumeno. (***Anza*** **Ni rahisi...**)
(d) **Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii** :-
Alimlilia mwanawe
(e) (i) **Kanusha sentensi hii:-**
Tungewalaki kama tungejua watakuja
(ii) **Sahihisha sentensi ifuatayo na uiweke katika wingi**:-
Ningalifanya kazi ningekuwa tajiri
(f) Tunga sentensi **nne** kuonyesha matumizi na maana nne za kijineno '**ki**'

(g) **Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi:-**
(i) Bibi yule alinunua gari ________________________(-pya)
(ii) Mti (-ingine) ________________________uliangushwa badala ya ule wa kwanza.
(h) **Unda majina mawili mawili kutoka vitenzi hivi na utumie katika sentensi ili kubainisha maana**
(i) Safiri
(ii) Zaa
(i) **Akifisha kifungu hiki**:-
Yohana na Emanueli walifunga safari wakielekea mashariki kusini na hatimaye magharibi walifikia huko novemba mwaka jana walipokuwa wakirudi walimkuta mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale
(j) ***Geuza sentensi hii hadi udogo***:-
Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi
(k) ***Andika upya sentensi hii kwa kuandika kinyume cha kila neno lilipigwa mstari***:-
Wifi **<u>alipovaa</u>** nguo na kusimama ajuza yule **<u>alikaa</u>**
(l) Sauti hizi ni za aina gani na hutamkwa wapi?
(i) **gh**
(ii) **j**
(m) Mahabusu walifyeka uwanja vizuri
**Andika sentensi hiyo upya ukimaliza kwa neno mahabusu**

**8.** (a) **Onyesha maneno yaliyokopwa toka lugha za kigeni na kuswahilishwa kwa kuyaongezea irabu** ***k.m. Bint (Kiarabu) – Binti***
Toa mifano minne
(b) *Andika sentensi ifuatayo kwa usemi halisi:*
Mwalimu alipoingia darasani aliuliza kitabu chake kilipokuwa.
(c) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi nafsi huru umoja
(d) **Kanusha sentensi hizi kwa wingi**:-
(i) Mtoto huenda shuleni kila siku
(ii) Mwalimu amemfunza mwanafunzi vizuri
(e) **Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo**
Wanafunzi waliandikiana barua
(f) **Ziandike sentensi hizi bila maneno yaliyopigiwa mstari:-**

(i) Mwanafunzi **ambaye** alituzwa ni wa shule yetu

(ii) Sikuziona nyuzi **ambazo** huzitengeneza ngoma **ambayo** huiona pale

(g) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vielelezo vya vishale:**
Kiarie ni mwanafunzi mtiifu

(h) **Bainisha ngeli za nomino hizi :-**
(i) Kisu
(ii) Nyavu
(iii) Chai

(i) **Ainisha viambishi katika neno lifuatalo** :-
Kilichokikata

(j) **Nyambua kitenzi 'oa' katika hali tatu zifuatazo: tendewa, tendwa, tendea**

(k) **Eleza matumizi manne ya nukta**

(l) **Onyesha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo**:
Kamau alimlimia mamake shamba kwa trekta

(m) **Unda nomino kutokana na vitenzi hivi**:-
(i) Chapa (ii) Goma

(n) **Tambua kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii :-**
Chakula ambacho ni muhimu, huweza kujenga au kobomoa mwili wako.

(o) **Sahihisha sentensi ifuatayo:**
Ukienda mle pao atakuweko

(p) **Andika sentensi ifuatayo katika udogo:**
Mbwa mdogo amekanyagwa na gari.

9. (a) **Andika katika usemi halisi**
Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(b) **Andika kwa umoja**
Uovu waliotuonyesha hautasahaulika

(c) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo:
(i) Pamba
(ii) Bamba

(d) Sauti zifuatazo hutamkiwa wapi?
(i) /f/
(ii) /v/

(e) Onyesha matumizi **manne** ya kistari kifupi

(f) **Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo**
(i) Nafsi ya tatu umoja
(ii) Wakati uliopita
(iii) 'O' rejeshi
(iv) kitendwa
(v) mzizi
(vi) kiishio

(g) **Tambulisha aina za vitenzi vilivyotumika katika asentensi hizi**
(i) Kazi hii **ni** nzuri.
(ii) Mazingira **yamekuwa yakihifadhiwa.**

(h) Pigia mistari chini ya viwakilishi katika sentensi zifuatazo
(i) Ambaye ni mjinga hatafaa kwa shughuli hizi
(ii) Nani anaye huzunisha?

(i) Ngeli ya LI-YA hujumulisha nomino za vitu vya aina mbalimbali. Toa mifano **minne** ambayo ni tofauti na uelezee

(j) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo na ueleze ni shamirisho ya aina gani?
Wazazi wanalipia watoto karo kwa hundi;

(k) Neno **'tikiti'** hupatikana katika **ngeli mbili** tofauti. Taja ngeli hizo na utunge sentensi

(l) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.**
Hakimu alimwadhibu kinyama.

(m) Nyambua vitenzi hivi kulingna na kauli ya kutendua na kutenda

| **Kutenda** | **Kutendua** | **Kutendama** |
|---|---|---|
| Ficha | | |
| Tanda | | |

(n) Ni nini maana ya neno kirai ?

**10 .** (a) Kati ya nomino za Kiswahili taja **ngeli mbili** ambazo nomino zake hazibadiliki katika umoja na katika wingi. Kisha utoe mfano mmoja kwa kila ngeli

(b) **Yakinisha:** Waumini wale hawaimbi wala hawaombi

c) **Andika kwa umoja**

Nguo zile uzionazo zilinunuliwa Ulaya

(d) Taja na kutolea mifano aina nne za silabi za Kiswahili

(e) **Unda nomino moja kutokana na nomino hizi**

(i) Mtu. (ii) Mhasibu..

(f**) Andika kwa ukubwa**

Kipaka hiki hakitosheki kwa maziwa haya kimezoea kipanya

(g) Onyesha shamirisho kipozi na shamirisho kidondo katika sentensi hii:-

Mama amempikia moto chakula kizuri

(h) **Tunga sentensi ya neno moja inayoonyesha sehemu zifuatazo**:-

(i) Kiambishi kikanushi nafsi
(ii) Kiambishi kiwakilishi cha hali timilifu
(iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendwa (nafsi)
(iv) Kauli
(v) Kiishio

(i) **Sahihisha sentensi hii kwa njia tatu tofauti**

Mtoto mwenye alicheza ameteguka

(j) **Andika visawe vya maneno haya**

(i) Rabsha..... (ii) Damu..

(k) Jaza mchoro ufuatao kwa irabu inayofaa




(l) Tunga sentensi ukitumia **'ni'** kama

(i) kitenzi (ii) kielezi

(m) Andika katika msemo halisi

Johana alisema kuwa angepata alama zote katika majaribu ya wiki iliyotangulia

(n) Tumia '**O'** Rejeshi ya mazoea katika sentensi ifuatayo;

Jembe ambalo lilinunuliwa limepotea

(o) Changanua ukitumia mtindo wa mishale

Mtoto anayelia sana ameadhibiwa leo asubuhi

(p) Onyesha matumizi mawili katika sentensi ya alama (**'**)

(q) Wafuatao wana ulemavu upi?

(i) Toinyo . (ii) Huntha ..

**11.** (a) Andika vinyume vya vitensi vilivyopigwa mistari

(i) **Alikashifiwa** kwa kazi aliyofanya
(ii) Kuimba **kulifurahisha** hadhira

(b) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi

(i) Abiria waliojeruhiwa sana walipelekwa hospitali haraka

(c)Eleza maana **mbilimbili** za sentensi zifuatazo ;

(i) Bibi yake amefika

(ii) Alimpigia mpira

(d) Kwa kutoa mifano, onyesha namna mbili vile kiambishi –j- hutumiwa

(e) irabu **a, i,** na **u** hutamkwa wapi kwenye ulimi?

(f) Kamilisha na kueleza maana ya methali hii

(i) Mfinyanzi -......................................

**(g) Andika usemi huu kwa usemi wa taarifa**

"Kefule! Mtoto huyu ni kaidi kama kirongwe. Hamheshimu babake!" alisema mzee Kamau.

(h) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentenzi ifuatayo

(i) Darasa lililojengwa limefunguliwa rasmi

(ii) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo;

(j) Kanusha sentensi ifuatayo kwa udogo

(i)Mbuzi wake ana manyoya mengi na harufu kali

(k) Onyesha maana **mbili** ya neno taka (ala. 2)

**(l) Andika kwa umoja** (ala. 2)

(i) Tumewaondoleeni matatizo yenu, yafaa mtushukuru

(m) Eleza maana ya misemo:- (ala. 2)

(i) Fuga mtu –

(ii) Kuwa na faragha -

(n) Panga nomino hizi katika ngeli mwafaka (ala 2)

(i) Kipofu- .

(ii) Uyoga- .

(o) Bainisha viwakilishi katika sentenzi kisha useme ni vya aina gain. (alama

i) Mimi nitaondoka kesho

(ii) Huyo alichaguliwa na wengi

12. (a) Tumia kiulizi kifaacho kukamilisha maswali yafuatayo:

(i) Waashi wale wanaishi kwa

(ii) Mtoto alitaka majina…

(iii) Wanitania hivyo

(b) Tambua mzizi katika neno:

Tuliwalimia :

(c) Andika sentensi **tatu** ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii

Pale ndiko alimoingia

(d) (i) Nini maana ya yambwa (shamirisho)

(ii) Taja aina ya yambua iliyoipigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:

**Mama amempikia baba wali kwa sufuria**

(e) Neno "**mlango**" lina maana ya "uwazi wa kuingilia nyumba." Tunga sentensi **mbili** kubainisha matumizi mawili ya neno hili

(f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya **"ndivyo**"

(g) Chai hiyo iliwavutia watahi **(*Anza* : Watahi…………..)** (al. 2)

(h) Tumia neno **"haraka**" katika sentensi kama: (al. 2)

(i) Nomino (ii) Kielezi

(i) Andika maana **mbil**i za sentensi:

(i) Nenda ukamwone mwenyewe, usiogope.

(j) Onyesha maana za '**ni**' zilizopigiwa mstari

Nihamrishe "**Tokeni darasani**"

(k) Atakapokuja atamletea mlinzi uta na upote

(l) Maneno hayo yako katika ngeli gani?

(i) Ridhaa (ii) Nanasi

(m)Andika mifano ya sauti zenye sifa zifuatazo:

(i) Kipasuo cha kaakaa laini (ii) Nazali ya ufizi

(n) Tumia neno "**ngali**" kutunga sentensi kuonyesha

(i) Kitenzi kisaidizi (ii) Kitenzi kishirikishi

(o) Tumia kirejeshi kuonyesha mazoea katika sentensi ifuatayo:

(i) Mtoto anayelia ni huyu (ii) Neno maana ya kiwakilishi?

(q) Tambulisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani?

1.Nani alikukasirisha?... 2. Huyu huwashinda wote

(r) Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano

13. (a) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi

(i) Kishirikishi kipungufu

(ii) Kikuu

(b) Akifisha

je, unaipenda hali ilivyo mwenzake alitaka kujua

(c) Eleza matumizi ya '**ka**' na '**hu'** katika sentensi zifuatazo.

(i) Nilienda kanisani nikamkuta, nikamwamkua, nikamwomba msamaha.

(ii) Baba hufika nyumbani usiku wa manane

(d) Yakinisha sentensi ifuatayo :

Mama hakutuchapa, hakutupa chakula wala maji

(e) Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti si ghuna huku ukitolea mifano miwili kwa kila aina

(f) Tunga sentensi mbili kutofautisha matumizi ya vitate hivi: Dua na tua

(g) **Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi**

Njia nyembamba ni hatari kwa usafiri wa gari

(h) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia matawi**

Mzee ambaye hukuza pamba amefaidika sana

(i) **Ainisha mofimu zinazojitokeza katika kitenzi hiki**

Waliochekeshwa

(j) **Andika sentensi zifuatazo kulingana na kauli ulizopewa katika mabano**

(i) Ugonjwa wa saratani hufanya watu **wafe** polepole. (kauli ya kutendesha)

(ii) Mkulima **alisuka** kamba ndefu. (Kauli ya kutendata)

(k) **Tunga sentensi moja inayojumulisha sehemu hizi, Ala, kipozi, kitondo na chagizo**

(l) Neno kijana linaweza kutumiwa kama kivumishi au nomino, tunga sentensi kudhihirisha***U**

(i) Kivumishi

(ii) Nomino

(m) **Sahihisha sentensi zifuatazo**

(i) Mtoto ambaye aliyekuwa anacheza ameanguka.

(ii) Vitabu hizi ambazo zimesahihishwa ni za wanafunzi.

(n) Tunga sentensi mbili ukitumia vielezi vya namna mfanano na viigizi.

(o) Bainisha maneno yafuatayo yapo katika ngeli gani kisha tunga sentensi mwafaka:

(i) Manukato (ii) Uwati

(p) Eleza maana ya methali ifuatayo:

"Avunjaye nazi ni lazima aafaidi tui.

**14.** A) **Eleza maana mbili za:**

Mwanaida alikwenda sokoni peke yake.

B) **Akifisha sentensi hizi.**

i) Hodi hapana wenyewe nini Juma alimwaka nitarudi kesho.

C) **Andika maana ya methali ifuatayo.**

Achanikaye kwenye mpini hafi na njaa.

D) **Tumia "O" rejeshi katika sentensi hii.**

Mwanafunzi ambaye hudurusu ndiye hupita mtihani.

E) **Andika sentensi ifuatayo kwa kunyambua maneno yaliyo kwenye mabano kwa usahihi.**

Dhambi za mwanadamu zilim____________ (fa) Bwana Yesu.

F) **Eleza maana ya misemo ifuatayo.**

i) Teka bakunja.

G) **Taja maana ya maneno yaliyopigwa mistari**.

Tulipogawa mkate kila mtu alipata <u>sehemu moja kwa nane</u> tu kwani tulikuwa wanane

H) **Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maelezo.**

i) Sikusoma kwa bidii ndiposa sikufaulu katika mtihani ule.
(Anza: Ningalisoma ………………………………………)

ii) Anakuja (andika katika wakati ujao hali timilifu)

I) **Eleza maana ya neno chungu kama lilivyotumiwa katika sentensi zifuatazo.**
i) Chungu yule ni mkubwa.
ii) Chungu kile ni kikubwa.

J) **Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kama vivumishi.**
i) Sote. i) Zote.

K) **Andika nomino mbili kutokana na kitenzi safari.**

L) **Tumia viunganishi mwafaka kuunganisha sentensi hizi ziwe sentensi moja.**
Alikimbia kwa nguvu zake zote. Alishindwa, kulikuwa na mtu mwenye mbio kumliko.

L) **Eleza maana ya matumizi ya "ka" katika sentensi ifuatayo**.
Aliingia ndani, akaoga, akala kisha akalala.

N) **Taja sauti mbili za ving'ong'o**

O) **Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.**
Juma ameinjika chungu mekoni.

P) **Andika sentensi ifuatayo katika wingi wa udogo.**
Mtu/ mchoyo hamfai mwingine kwa vyovyote vile.

Q) **Kanusha sentensi hii;-**
Ukionana naye mwambie aje anione.

R) **Eleza na udhibitishe kwa mfano, matumizi mawili ya tu**.

S) **Changanua sentensi ifuaatayo kwa kielelezo visandu**.
Mwanafunzi aliyeleta kitabu chake amepongezwa

T) **Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo**
Soroveya atapima wanunuzi viwanja.

U) **Nomino zifuatazo ni za ngeli gani?**
i) Insi … ii) Soksi

# Isimu Jamii

1.

| | |
|---|---|
| Saidi | : Hallo............Hallo....Huyo ni Bw. Mohamed? |
| Mohamed | : Ndio...uko wapi... |
| Saidi | : Shuleni...sasa...ulinifikishia ujumbe? |
| Mohamed | : La. Parade ilikuwa imehitimishwa |
| Saidi | : Sina credit. Nipigie tafadhali. |
| Mohamed | : Sina pia, nitatuma sms |
| Saidi | : Iwe saa hii eh? |
| Mohamed | : Baada ya dakika tano |
| Saidi | : Good day |
| Mohamed | : Welcome |

(a) Taja na uthibitishe sifa zinazojitokeza katika mazungumzo haya

(b) Eleza sababu za wazungumzaji kutumiambinu zifuatazo katika mazungumzo yao
(i) Mdokezo
(ii) Lugha mseto

2. Lugha ya kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Yataje na kuyaeleza.

3. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***

Uchunguzi uliofanywa umeonyesha kuwa anasumbuliwa na uto mwingi mwilini. Uto unaweza kudondoshwa kwa kufanya mazoezi, kupunguza ulaji wa vyakula vya wanga na hata protini. Protini iwapo nyingi mwilini hugeuzwa kuwa glukosi ambayo huhifadhiwa mwilini. Hii huwa msingi wa unene pia ambao unahatarisha afya. Jamaa yake aliyeaga dunia alikuwa mgonjwa wa bolisukari ambayo inaweza kurithishwa. Kimsingi, lazima awe na welewa bora kabisa wa lishe. Mwenzake naye aliathiriwa na **aflatoxins** zilikuwa kwenye chakula alichokula.

(a) Sajili hii inapatikana wapi? Kwa nini?
(b) Taja sifa zinazohusishwa na sajili yenyewe

4. Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa kiswahili nchini Kenya
5 (a) Ni mambo yapi yanayochangia kudidimia kwa Kiswahili nchini Kenya.
(b) Mambo haya yanaweza tatuliwa vipi?
6. a) Bainisha kwa kutoa mifano sifa **tano** za lugha ya vijana '**sheng'**
b) Fafanua changamoto **tano** zinazozuia maenezi ya haraka ya lugha ya Kiswahili

**7.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***
Niaje wasee! Ma-holiday ndizo hizo tena. Najua ma-mission ni mingi! Lakini jo, mambo imebadilika ! Ni kubaya maze. Usifikirie kila kitu unaona ni reality, ukadhani ni gold ! Hiyo siyo real life maze ! Round hii maze ni ''Ku-chill!'' Usipige ma-stunts zingine zitakuacha uki-regret later! NI POA KU- CHILL au aje maze?

a) Bainisha rejista ya mazungumzo haya
b) Kwa kurejelea kifungu andika sifa za rejista hii.
c) Kwa nini watu hutumia lugha zaidi ya moja.
d) Orodhesha hatua tatu zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha matatizo yanayokumba Kiswahili nchini.

8. ***Soma mzungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali :***
**A** : Ohh, dada Naomi
**B** : Dada Ruth (anamsogea kwa bashasha wanakumbatiana). Ahh Mungu asifiwe!
**A**: Asifiwe sana
**B**: Ehh dadangu, miezi ...mingi...sijakuona
**A**: dada wee...Nilitumwa huko kusini ...Kuwahubiria watu injili (mtuo mdogo)singeweza kukata...
**B**: Ehh, usiwe kama Yona
**A**: Habari ya siku nyingi?
**B**; Nzuri Mungu bado ameendelea kunibariki
**A**: Amen!
**B**: Nimeendelea kuiona neema yake
**A**: Amen! Asifiwe Bwana
**B**: Halleluya
**A**: Ni Mungu wa miujiza!
**B** : Amen. Hata nami nimeona neema yake
Bado niko imara katika wokovu katika siku hizi za mwisho
**A** : Amen !
**B** : Ni Mungu wa ajabu kweli !
**A** : Nilikumbana na matatizo lakini nikategemea sala
Kama Paulo na sila… Na nikashinda (anatua). Sikuweza kumpa shetani nafasi…maana ameshindwa
**B** : Ameshindwa kabisa

**<u>Maswali</u>**:-
(i) Hii ni sajili ya wapi ? Fafanua
(ii) Taja na ueleze sifa za sajili hii
(iii) Taja na ueleze mambo **mawili** muhimu yaliyosaidia katika maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki na kati

9. Bw. Mosuka : Mheshimiwa spika, naichukua fursa hii kuipinga hoja iliyowasilishwa na mbunge wa Mahira, mheshimiwa Kochaberi kuhusu suala la kuavya....
(a) Hii ni sajili gani?
(b) Eleza sifa za mazungumzo ya sajili hii

10. Eleza juhudi tano zinazotumika kukiendeleza Kiswahili

11.` (a) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha wa maabadini
(b) Matumizi ya lugha yoyote ile huthibitiwa na mambo fulani. Fafanua **matano** kati ya hayo

12. **AZIZ** : Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao kenyatta, railways!
**SHIKU** : Namba nane ngapi?
**AZIZ** : Mbao ingia, blue.
**SHIKU** : Nina hashuu.
**AZIZ** : Blue Auntie.
**SHIKU** : Sina.
**AZIZ** **:** Ingia. 46 Adams mbao, kenyatta railways gari bebabeba.
**AHENDERA** : Mimi sinako shirini. Chukuako tu kumi.
**AZIZ** : Dinga inakunywanga petrol mzee.
**AHENDERA**: Kumi mingi.
**AZIZ** : Haaya ingia twende. Driver imeshon twende.

**<u>Maswali</u>**
(i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya
(ii) Taja sifa **sita** za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya

13. ***Kifuatacho ni kifungu kifupi cha mazungumzo. Kisome kisha ujibu maswali yaliyoulizwa:-***
Mzee Oluoch :..................................................................ni kweli hayo!
Mzee Mwenda : Ndio. Huyu mtoto wangu nimemsomesha mpaka akahitimu chuo kikuu na anafanya kazi ya uhasibu.
Mzee Oluoch : Na wangu amehitimu na sasa ana shahada ya uzamili. Yeye ni mhandisi mkuu. Chukua tu mbuzi hamsini na utukubalie kujenga uhusiano wa ukwe.
Mzee Mwenda : Je, mbuzi hao ni wa ‘mfuko’ au ni .......?
Mzee Oluoch : Kuna wa mfuko ......thelathini na hao wengine ishirini.
Mzee Mwenda : Basi lete hao ulio nao. Wengine hamsini watabaki deni. Utakuwa ukinilipa polepole. Idhini yangu nimetoa ili mipango iendelee.

(a) Mazungumzo ya aina hii hutokea katika muktadha wa aina gani?
(b) Eleza sifa **nane** za lugha inayotumika katika wa aina hii

# <u>Karatasi ya tatu (102/3)</u>

## <u>RIWAYA: UTENGANO: S.A. MOHAMMED</u>

1. ‘Pesa iweke mbele, Pesa mwanzo. Sisi tuna msemo wetu. Watose. Ndio, watose, maana sisi tumeshatoswa
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(b) Eleza mawaidha **<u>mawili</u>** ambayo msemaji alimpa katika muktadha huu
(c) Eleza maana ya ‘**Sisi tumeshatoswa**” kwa kurejelea riwaya ya Utengano

2. “Maisha ya Maimuna yalitawaliwa na Majaaliwa kwa kiasi kikubwa.” Thibitisha kauli hii kwa kurejelea matukio **<u>kum</u>**i katika riwaya ya Utengano.

3. “Mkinipa mimi kura zenu nitajenga njia, nitawapa watu kazi, nitajenga skuli zaidi na maisha yenu yatakuwa katika raha.”
(a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake
(b) Msemaji ana ila gani zinazomfanya atoe ahadi hizi?
(c) Onyesha jinsi wanasiasa walivyosawiriwa katika riwaya

4. Said .A. Mohammed ameangazia migogoro na misukosuko inayosambaratisha jumuiya ya Utengano na Jamii kwa jumla. Jadili.

5. "Mama usifanye ivyo." :Ikiwa kuogopa kuvunja miiko ya nyumba hii, tusiogope. Naivunja leo hiyo miiko. Hujui utazaa vipi mama. Tutangojea idhini ya mtu asiyekuwepo, wala tusiyemtarajia kurudi saa hizi?"
   (i) Eleza muktadha wa dondoo hili
   (ii) Fafanua miiko inayorejelewa katika dondoo hili
   (iii) Eleza sifa za mhusika 'asiyetarajiwa kurudi saa hizi'

6. Ndoto na nyimbo za Maimuna ni ufundi wa kisimulizi unaojikita katika misingi ya taswira. Onyesha jinsi mwandishi anavyotumia taswira kufanikisha malengo yake ya usimulizi

7. Mkamia maji hayanywi, na akiyanywa humsakama. Kwa kurejelea wahusika wowote watano katika riwaya ya <u>Utengano</u> thibitisha ukweli wa kauli hii

8. "…mkubwa kabisa ni mwananchi. Umma ndio mkubwa kabisa, na umma umeshautenda vya kutosha……………
   (a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya
   (b) Eleza mambo aliyoutendea umma mhusika anayezungumziwa katika muktadha huu
   (c) Eleza mafunzo ambayo umma unajifunza kutokana na kisa kinachoibua mazungumza haya

9. Hapo ndipo ninapokuona mjinga **…** wewe nani hasa wakukataa ?
   (a) Eleza muktadha wa dondoo
   (b) Taja mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili
   (c) Eleza sifa nne za mzungumzaji
   (d) Fafanua maudhui mawili yanayojitokeza katika dondoo

10. Fafanua kwa mifano mwafaka aina tano za uozo wa kijamii katika riwaya hii

11. "Akakumbuka ubeti wa shairi alilolitunga karibuni katika jumla ya mashairi aliyoyakusanya katika kitabu alichokiita Kilio cha Wanyonge".
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya
   (b) Fafanua ujumbe mkuuu katika shairi linalorejelewa hapa.
   (c) Onyesha Inspekta Fadhili anavyotofautinana na kakake Maksuudi.,

12. "Mwanamke ni kikwazo na adui kwa maendeleo na ukombozi wake". Kwa kutoa mfano mwafaka kutoka kwenye riwaya ya Utengano, ifafanue kauli hii

13. "Mwanamke Mtumwa. Nani kasema utumwa umeondoka. Viumbe vya kupika na kupakua, kufua na kupiga pasi..."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili
   (b) Jadili maudhui yanayoonyesha maonevu ya wanawake katika riwaya
   (c) Je, wanawake wamejitokeza vipi katika kupigania mabadiliko katika maisha yao kwenye riwaya hii

14. "Majuto ni mjukuu" Onyesha ukweli wa uneni huu kwa kurejelea wahusika: Maksuudi na Maimuna

15. Mwandishi wa riwaya ya Utengano amefaulu kuichora picha ya mwanamke katika uhalisi wake katika jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha

16. Mimi nilidhani umepata mtoto mwenye sura na tabia zake, mtoto mwenye kwao….nimesafiri kwa mwendo wa meli mia mbili na hamsini kujanileteа kwa mtu asiye na asili wala fasili ? "
   (a) Fafanua muktadha wa maneno haya :
   (b) Kwa nini mzungumziwa anachukuliwa kuwa hana asili wala fasili ?
   (c) Fafanua mbinu zozote **tatu** za lugha katika muktadha huu
   (d) Mzungumzaji amekuja nini ?
   (e) Fafanua kwa ufupi yaliyotendeka baada ya usemi huu

17 "Leo amekomolewa na bado ataumwa na nge kwa mdomoni na mkiani."
   (a) Fafanua muktadha wa maneno hayo
   (b) Eleza kwa kutoa hoja nane jinsi anayerejelewa alivyoumwa na nge
   (c) Eleza sifa nne za mnenaji

18. Eleza jinsi **kinaya** kimetumiwa katika riwaya ya Utengano

19. Kuna mengi ambayo Kazija anayachukia. Ndiyo, anachukia……kwanza, anamchukia mwanamme. Ni sababu zipi zinazosababisha wanawake kama kazija kuwachukia wanaume?

20. Anwani "**Utengano**" inafaa katika jumuiya ya utengano. Fafanua. 21.

**Mshiba Mungu staghafiru, naye mwepesi wa kusamehe waja wake**…

(i) Eleza muktadha wa Dondoo hili

(ii) Eleza yaliyomsukuma anayezungumziwa kufikia kiwango hiki

(iii) Taja alama alizo nazo anayezungumziwa

(iv) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili

(v) Eleza jinsi maudhui ya Dini yanavyojitokeza katika riwaya ya utengano

22. Mwandishi wa riwaya ya Utengano anakashifu mambo kadhaa katika jamii . Taja na ueleze kwa kutoa mifano

23. Haloo, nani ? Aha Mr. Smith….ni wewe. Nilikutarajia . Nilikuwa nakusubiri kwa hamu. Ndiyo…Nitafanya kama ulivyoagiza.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(b) Kabla ya mazungumzo haya kujiri, kulikuwa na ushairi wa "kilio cha mnyonge". Taja ujumbe unaojitokeza katika ushairi huu

(c) Mzungumzaji katika muktadha huu alikuwa mwovu. Thibitisha

24. "Nataka nikueleze hivi darling…."

Unajua watu wakikaa pamoja kama vilivyo visahani hugongana"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(b) Eleza sifa za aliyeelekezwa maneno haya

(c) Baadhi ya mabailiko yametokea katika riwaya ya 'Utengano"

# Tamthilia

## TAMTHILIA: KIFO KISIMANI: KITHAKA WA MBERIA

1. Kwa kurejelea tamthilia ya "Kifo Kisimani", eleza jinsi utawala mbaya unavyoathiri jamii

2. Kwa kurejelea diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine, tetea kauli kwamba "Hadithi katika Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi Nyingine inamulika jamiii iliyojaa uozo wa kila aina

3. **. . .** hatuwezi kuendelea kuwa na mwiba katika mguu wa Butangi **. . .**Butangi imo safarini **. . .** imo mbioni **. . .** Inasonga mbele.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(b) Ni mbinu zipi za sanaa zilizotumika katika dondoo hili? Taja na utoe mifano

(c) Taja na ufafanue sifa zozote **tano** za anayezungumza.

(d) Taja na ueleze mfano mmoja wa maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili

4. Linganisha hulka za wahusika wafuatao. Gege na Mwelusi kisha ueleze umuhimu wa Gege katika tamthilia hii

5. (a) Eleza mchango wa wahusika wafuatao katika harakati za ukombozi katika tamthilia ya Kifo Kisimani. (al.14)

(i) Mwelusi

(ii) Raia

(iii) Nyalwe

(iv) Askari I na Kame

(b) Mbali na haki ya kuchota maji kisimani, taja mambo mengine sita ambayo Mwelusi angependa yazingatiwe katika Butangi mpya.

6. "...Njiwa na kozi ni ndege wenye maisha tofauti; Tungalikuwa sote njiwa au sote Kozi ..."

(a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya.

(b) Eleza mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili.

(c) Kando na mbinu uliyoitaja katika swali la (b), taja na kueleza mbinu nyingine za lugha **tano** zilizotumiwa katika tamthilia ya Kifo Kisimani.

(d) Ni vipi mzungumzaji ni kielezo cha wanyonge katika tamthilia ya kifo kisimani?

7. Linganisha wasifu wa wahusika wafuatao na uonyeshe umuhimu wao katika tamthilia ya

**Kifo Kisimani.**
(i) Mtemi Bokono
(ii) Mwelusi

8. "Kazi ya mikono yangu yenyewe nimeuchomoa mwiba tayari, kisu kilimpata sana tumboni. Pengine kwenye ini au wengu".
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(b) Ni yapi yaliiyomfanya msemaji kuuchomoa mwiba
(c) Fafanua yaliyofuata kauli hii na hatima ya wazungumzaji
9. Huku ukirejelea tamthilia ya **Kifo Kisimani** fafanua vile uongozi mbaya unaweza kuwa kikwazo cha maendeleo katika jamii
10. Eleza jinsi vijana walivyosawiriwa katika tamthilia ya '**Kifo Kisiamani**."
11. "Nimeshakwambia tulale hapa langoni! Tulale umati unaokuja kumtoa mfungwa gerezani utukute hapa. Watu wanatupenda sana kwa kazi nzuri ya kumzuia mfungwa gerezani. Kwa hivyo tuwasubiri waje watupake mafuta."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(b) Taja na kueleza mbinu ilivyotumika katika dondoo hili
(c) Eleza kwa kutolea mifano maovu matano yaliyotekelezwa na wahusika katika dondoo hili
12. A : Mtemi ataingia hivi punde. Na anatarajia kusikia habari nzuri …
B : Mtemi nataka kumsamehe kwa masharti gani ?
(a) Eleza muktadha wa maneno haya
(b) Taja masharti ambayo yanarejelewa hapa
(c) Jumuiya ya Butangi ililemewa na ufisadi. Eleza
13. Tamthilia Kifo Kisimani imedhihirishaje ukweli wa methali 'Kikulacho ki nguoni mwako ?
14. Butangi ni kielezo cha mojawapo wa nchi za kiafrika zianzua. Thibitisha.
15. a) Taja jazanda zilizotumika katika tamthilia ya kifo kisimani na ueleze maana yake
b) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika
i) Methali
ii) Tashhisi
iii) Kinaya
16. "**Msimamo wangu hautokani na uoga, unatokana na kuthamini maisha ya binadamu"**
a) Eleza muktadha wa maneno haya
b) Eleza sifa za anayeambiwa maneno haya
c) Taja wahusika wanne wanaoendeleza maudhui ya uzalendo katika kifo kisimani
d) Eleza msimamo wa mwandishi wa tamthilia ya Kifo Kisimani kuhusu uongozi mbaya

17. **"Ha-li Haa-ih! Nyoka ameniuma! Sumu ya nyoka!**
(i) (a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(b) Maneno haya yanaashiria nini kuhusu hali ya mnenaji?
(c) Taja mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili
(ii) Jadili mbinu alizotumia Mtemi Bokono kuudhiti utawala wake
18. Diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi imejikita katika masuala ibuka yanayofaa kushughulikiwa na jamii. Taja na uthibitishe.
19. Fafanua dhamira ya **Ken Walibora** alipoandika kisa cha **"Tuzo"**

# Ushairi

**1.** **SHAIRI 'A'.**
Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
Watoto Wakukimbia

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza Panya
Akalia kulikuwa na pala
Kichwani
Mchawi kutaka sana kutisha
Alijigeuza Simba
Akalia na risasi kichwani

Jongoo kutaka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa yatakwenda
Bwanako kumpa sumu ?
Hadija umeshika nyoka kwa mkia
Hadija umepitia nyuma ya punda

**SHAIRI 'B'**

Piteni jamani, Piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka

Vijana kwa nini hampiti ?
Kwa nini mwanicheka kisogo ?
Mzigo niliobeba haupo.

Lakini umenipinda ngongo na
Nendako
Haya piteni ! Piteni haraka ! Heei !

Mwafikiri mwaniacha nyuma !
Njia ya maisha ni moja tu.
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengi wenu
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kutazama
Ningewambia siti miaka
Mingi.

(a) Haya ni mashairi ya aina gani ? Toa saabu
(b) Washairi hawa wawili wanalalamika. Yafafanue malalamishi yao
(c) Onyesha jinsi kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili
(d) Ni vipi Hadija :-
  (i) Amekata mti mtima ?
  (ii) Amepita nyuma ya Punda (al.2)
(e) Toa mifano 2 ya uhuru wa mashairi kwa kurejelea mashairi haya
(f) Kwa kurejelea shairi '**B**' eleza maana ya:-

(i) Mzigo
(ii) Siri
(iii) Kula nimekula
(iv) Niko nyuma ya wakati

2. Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwandani.
Afya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini
Sisi tokea **azali**, twende zetu mizumuni
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu za kirijali, Mkuyati uamini
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani
Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zongo huanoni
Zabadili pia **sahali,** kwa maradhi yalo ndani
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini
Daktari k'ona mwili, tanena kensa tumboni
Visu visitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama fagili, **tumbo nyangwe** na maini
Nifuateni sipitalini, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi **dhalili**, kutenguliwa tegoni
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Wambiwa damu kaliti, ndugu msaidieni
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, Wakueleze undani.
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu thamani
Utete huku wawili, wa manjano na kijani
Matunda pia asali, vitu vyae shamoni
Nifuateni sipati, na dawa zi langoni?

**Maswali**
(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka
(b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili
(c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitalini
(d) Eleza umbo la shairi hili (al. 6
(e) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi ?
(f) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye shairi :-
(i) Dhalili –...........................................................................................................
(ii) Azali -...............................................................................................................
(iii) Sahali -...........................................................................................................
(iv) Tumbo nyanywe ..............................................................................................

3. **WAFULA KABILIANA NA KISU**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamme,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu !
Iwapo utatingiza kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu,
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,

Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa,
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri

**Maswali**

(a) Hili ni shairi la aina gani ? Thibitisha
(b) Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ?
(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume
(d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili
(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili
(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili

(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili ?
(i) Mbari
(ii) Msununu
(iii) Ngariba
(iv) Uvundo

4. **HATIMA YANGU**

1. Mke wangu wameshanipoka
Ndugu zangu, wamedai ububu
Wazazi kuzoea kunigombeza

2. Juzi mali lilimbikiza
Furaha lilitanda
Makanwa yalijaziwa
Hoi hoi ikawa desturi

3. Kilabu tulikwenda
Nyama tulichoma
Mahali tulizuru
Tuliteremsha!

4. Leo mambo yamenigeuka
Wao masahibu siwaoni
Matumbo yakaninguruma
Kama radi ya mvua

5. Nyumbani nimebaki pweke
Mke amenitoroka
Watoto wameparara
Skuli kugharamia
Imegeuka balaa belua

6. Ndipo nimeamua
Afadhali kitanzi badala ya balaa
Kumbe kupanga ndiyo maana
Maisha na waasia

(a) Eleza mambo muhimu yanayoelezwa katika shairi hili
(b) Fafanua sifa mbili za anayezungumza katika shairi
(c) Dondoa na ufafanue mbinu zozote mbili za lugha katika shairi hili
(d) Eleza maana ya:-
(i) Ndugu zangu wamedai ububu
(ii) Kumbe kupanga ndiyo maana

5. 1. Nitampa nani, sauti yangu ya dhati
Kwa kipimo gani, ingawa kiwakatiti
Amefanya nini, la kutetea umati
Kipimo ni kipi?

2. Yupi wa maani, asosita katikati

Alo na maoni, yasojua gatigati
Atazame chini, kwa kile ule wakati
Kipimo ni kipi?

3. Alo mzalendo, atambuaye shuruti
Asiye mafundo, asojua mangiriti
Anoshika pendo, hata katika mauti
Kipimo ni kipi?

4. Kipimo ni kipi, changu mimi kudhibiti
Utu uko wapi, ni wapi unapoketi
Nje kwa mkwapi, au ndani kwa buheti
Kipimo ni kipi?

**Maswali**

a) Eleza umbo la shairi hili
b) Taja na ueleze jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wa ushairi
c) Eleza ujumbe unaowasilishwa na mshairi
d) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha ya nathari
e) Taja bahari **tatu** zinazojitokeza katika shairi na utoe sababu
f) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi hili
i) Katiti
ii) Gatigati
iii) Mangiriti

6. **KIPI NIKITENDE?**

. Tayari ni sarakani, niambie yote johara,
Mosi nimpe shukrani, kanizaa bira zira,
Wapo haiko hisani, ningefaa kwa uparara,
Kipi takachokitenda, ni nene heko kwa mama?

. Miezi tisa tumboni, yote nina kajinyima,
Kanikopa uchunguni, safari ndefu kazima'
Kama kinda kiotani, kiniasa huyu mama'
Kipi takachokitenda, ninene heko mama ?

. Baba siku jana madadi, **kawa vingaito mambo,**
Kaolewa na asadi, kachalazwa kwa **wimbombo**,
Kaona – bali jadili, kuchao puani bombo,
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

. Kila kuchao zarani, kupalilia kondeni,
Kachanika mpinini, chungu povuka motoni,
Kaviyariya fingani, kinijali jikoni,
Kipi tukachokitenda , ninene heko mama?

. Wa siku hizi vijana, wakahujuru nyumbani,
Wengine wao jagina, kawa lofa mutaani,
Hali ukashiba nina, afikapo tu, "**kongoni!**"
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

. Nawe bwana siwe maya, vita hasha kiwa kombo,
Tena simfanye yaya, ya kikoa ndio mambo,
Simtende ya hizaya, siwe mwao kila jambo,
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

.

Sasa jamvi nakuja, kisa nimesakarika,
Naomba niliyotaja, tatia manani kaka,
Nenayo yasiwe ngoja, ili nipokee baraka,
Mema nitamtendea, apate futahi pia.

**Maswali**

(a) Eleza umbo la shairi hili
(b) Kwa nini msanii amshukuru mamaye ?
(c) Ni kina nani wanaokashifiwa na msanii ? Kwa nini ?
(d) Onyesha tofauti katika ujumbe iliyoko katika beti nne za kwanza na mbili zinazofuata
(e) Toa majina mengine yenye maana sawa na haya yaliyotumiwa katika shairi hili :
   (i) Mama
   (ii) Dawati
   (iii) Imara/thabiti
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika kaika shairi:
   (i) Kawa vangaito mambo
   (ii) Wimbombo
   (iii) Kongoni

7. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

**MWANAMKE**

1. Namwona yu shambani,
Na jembe mkononi,
Analima,
Mwanamama,
Mavuno si yake,
Ni ya mume wake.

2. Namwona viwandani,
Pia maofisini,
Yu kazini,
Hamkani,
Anabaguliwa,
Na anaonewa.

3. Namwona yu nyumbnai,
Mpishi wa jikoni,
Yaya yeye,
Dobi yeye,
Hakuna malipo,
Likizo haipo.

4. Namwona kitandani,
Yu uchi **maungoni.**
Ni mrembo
Kama chombo,
Chenye ushawishi,
**Mzima utashi.**

5. Namwona mkekani,
Yuwamo uzazini,
Apumua,
Augua,

Kilio cha kite,
Cha mpiga pute.

6. Kwa nini mwanamke,
Ni yeye peke yake,
Heshimaye,
Haki anakosa,
**Kwa kweli ni kosa**
***(Muhammed Seif Khatib)***

7. (a) "**Shairi hili ni la kukatisha tamaa**". Fafanua dai hili kwa kutoa mifano **minne**
(b) Eleza umbo la shairi hili
(c) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari
(d) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima utoe mifano **miwili** ya jinsi ilivyotumika
(e) Onyesha mifano miwili ya ubabadume inayojitokeza katika shairi hili
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi:
(i) mzima utashi
(ii) maungoni

8. **KIACHE KINACHONG'AA**

Katu siwe na harara, wala moyo kukupapa,
Usichukue hasira, na moyo kutapa-tapa,
Utaharibu na sura, mwishowe uende kapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Mbeleye kina madhara, kile kinachokukukwepa,
Mbele yake ni hasara, si chema kitakutupa,
Hutaipata ijara, kuchuma ama kukopa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Hicho jangwa la Sahara, si mnofu ni mfupa,
Hakina njema ishara, humtupa mwenye pupa,
Kibovu kama tambara, hupasuka kama chupa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Kitaleta ufukura, si huko wala si hapa,
Kina mengi mazingira, na mbele kitakuchapa,
Sijitie usogora, ukavimbisha mishipa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Si kazi yenye ujira, mshahara kukulipa,
Ya cheo chenye kinara, na heshima wakikupa,
Mbele haina imara, japo leo wajitapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Japo kazi ya biashara, kutwa wauza makopa,
Uwe mtu na kipara, Mwananchi ama Yuripa,
Bora uwe na busara, fedha tajaza mapipa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara
Usione kinang'ara, huku chapiga marapa,
Ukimbilie kupora, moyo wako kukuzipa,
Kitakugeuza chura, mbele yake utaapa,

Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Usitupe sarara, nyuma kisogo kuipa,
Ukaenda kwa papara, kiumbe mbele kitanepa,
Kwanza tumia fikira, uchague njema chapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Na sisemi masihara, hakika kweli nawapa
Mlio pwani na bara, wa Mufindi na wa lupa
Maneno haya kitara, muarifu na Wachepa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Tamati niliyochora, ya shikeni si kuepa
Kisha muwe na basira, na Mola kumuogopa,
Kinachokwepa si nyara, ufunge ndani ya kwapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

(a) Eleza hii ni bahari gani ya shairi
(b) Eleza dhamira ya mshairi
(c) Fafanua hasara nne zinazoletwa na tamaa - vile ving'aavyo
(d) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi
(e) Andika ubeti wa tano katika lugha ya nathari
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi
(i) Kuchuma
(ii) Kisogo kuipa

9. Alipokwenda kwao, mamaye alimwambia,
Nipa fedha au nguo, nataka kwenda tumia!
Nikosapo hivi leo, nipa kisu tajitia !
Huzunguka akilia kwa maana ya uketo

Ndipo mamaye kawaza, pamwe na kuzingatia,
Fedha zako umesoza, na leo zimekwisha,
Kisu sikukukataza, twaa upate jitia!
Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!

Ulipogeuka nondo, nguo ukazingilia,
Kakaka kwa vishindo, usisaze hata moya,
Leo wanuka uvundo, wambeja wakukimbia!
Mbele zangu n'ondokea ! Wende na ukiwa wako!
Ukijigeuza nyama, kama Simba ukilia,
Watumwa ukawaegema, ukawla wote pia,
Pasi kuona huruma, kutoa wahurumia,
Mbona hukuzingatia? Wende na ukiwa wako!

Si mimi naliokupa, **ukata** huo, sikia!
Kwamba utakuja hapa, nipate kuondolea,
Naapa thama, naapa, sina la kukutendea!
Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!

Tamati, nalikomile, ni hayo nalokwambia,
Hapahitaji kelele na kujirisha mabaya,

Na kwamba yakutukie, sema yapate n'elea!
Zidi radhi kuniwea ! Wende na ukiwa wako!

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka
(b) Ni maudhui gani yanayojitokeza katika shairi hili
(c) Taja na ueleze tabia za mnenewa katika shairi hili
(d) Mshairi ametumia uhuru wa utunzi. Taja sehemu mbili alikotumia uhuru huo
(e) Eleza umbo la shairi hili
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi :-
(i) Uketo
(ii) Ukata

10 . ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,
Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,
Husuda wameikata, hata hawasengenyani,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja

Mchwa nao nikaona, wamejenga masikani,
Wafanya bidii sana, uvivu hawatamani,
Wao husaidiana, tena hawadanganyani,
Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja

Nalo jeshi la siafu, hutandawaa njiani,
Laenda bila ya hofu, maana ajiamini,
Silaha zao dhaifu, meno, tena hawaoni
Wa kuwatadia nini ? Kwani wanao umoja.

Nao chungu wachukuzi, nyama warima njiani,
Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani,
Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,
Katu hawafarakani, wanadamu kwa umoja.

Sisi ni wana Adamu, mbona hatusikizani,
Tusitietie hamu, ukubwa kuutamani,
Wachache wataalamu, tuwasadi kwa imani,
Hii "Huyu awezani," yatuvunjia umoja

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka.
(b) Ni sifa zipi nne zinazopewa wanaozungumza.
(c) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili.
(d) Eleza muundo wa shairi hili.
(e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari.
(f) Taja mafunzo mawili unayopata kutokana na wahusika wanaozungumziwa.
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hilo.
(i) Chungu
(ii) Tuwasadi

11**.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Twamshukuru Mwenyezi. Kamwe wingi ukarimu
Alo na kiti cha enzi, Mola wetu akramu
Kutupa kitu azizi , lugha kutakalamu
Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia

Lugha mkuu mlezi , aleaye binadamu
Hata wanyama ja mbuzi, wema lugha wafahamu
Hafuguwa simulizi, izaayo tabasamu
Lugha huwa ni imamu, ujuwapo kutumia

(3) Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu
Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasama
Ikazidisha mapenzi, wapendanao kudumu
Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia

(4) Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu
Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu
Aidha hufanya kazi, ikawa mustakumu
Lugha kwayo ni timamu, ujuwapo kutumia

(5) Lugha ni mpelelezi, maovu kuwakasimu
Huwatowa palo wazi, kashuhudia kaumu
Yasifiwa na wajuzi, kuwa ni kitu adhimu
Lugha mkuu hakimu, ujuwapo kutumia

(6) Lugha huizuwa kazi, kutatiza mahakimu
Huwaacha kanwa wazi, wakili kitakalamu
Muhalifu na jambazi, wakaishinda hukumu
Urongo huwa timamu, ujuwapo kutumia

(7) Lugha iwe ni kiongozi, Kizungu au Kiamu
Iwekapo waziwazi, silabi na tarakimu
Huyakimu maongezi,yakasikizwa kwa hamu
Lugha huwa ni muhimu, ujuwapo kutumia.

(8) Lugha ni mapinduzi, wanyonge na wajukumu
Kadhalika ni jahazi, ya nahodha muhitimu
Kufa maji haiwezi, si vina si miizamu
Lugha maji zam-zamu, ujuwapo kutumia

**Maswali.**

(a) Eleza maudhui ya shairi hili
(b) Eleza muundo wa shairi hili
(c) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nadhari/ nadharia
(d) Taja huku ukitoa mifano, mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi kuwasilisha ujumbe
(e) Eleza maana ya msamiati kama ulivyotumika
    (i) Azizi
    (ii) Uhasimu
    (iii) Adimu.

12. ***Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali :-***

**SHAIRI A:**

Tunda la elimu zote, wasema wanazuoni,
Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani.
Ndipo hadhi aipate, akumbukwe duniani.

Elimu bila ukweli, haizidi asilani
Giza na nuru muhali, katu havitengamani,
Uwongo uje kwa ukweli, itue nuru moyoni.

Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani,
Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni,
Elimu njema miali, iangazayo gizani.

Mtu hachomwi na mwiba, na viatu mguuni,
Ulimwengu una miiba, tele tele majiani,
Elimu ukiishiba, U salama duniani.

Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini,
Hai ndio waulama, wapaao maangani,
Elimu jambo adhima, aso nayo maskini

Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni
Pale uitafutapo, ujira usitamani
Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni,
Wao wameongolewa, na ni taa duniani.
Kweli wanapojua, watoe bila kuhini.

Elimu bila amali, mti usio majani,
Haumtii kivuli, aukaliaye chini,
Inakuwa mushkeli, wa kushuri insani,

**SHAIRI B**

Inakera moyo
Hii anga ambayo
Huwasonya njiani
Watokao mashambani
Wa kusalimu kwa bashasha
Wanaoshinda kivulini.

Chini ya mwembe
Wa umma.

Inakera moyo
Hii sebule ambayo
Huwahini mezani
Wagotao nyundo kutwa
Wa kukabili chakula
Wanastarehe daima

Chini ya paa

La umma.

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa kila shairi la A na B
(b) Haya mashairi ni ya aina gani?
(c) Taja sifa zozote **tatu** za kishairi katika shairi B
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa :-
 (i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa saba katika shairi la A
 (ii) Katika ubeti wa nne wa shairi la B
(e) Fafanua kwa mukhtasari maudhui ya mashairi yote mawili
(f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha nathari
(g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A
(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi:-
 (i) Maulama
 (ii) Wameongolewa
 (iii) Wagotao
 (iv) Huwahini

13. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-***

**CHEMA HAKIDUMU**

Chema hakidumu, kingapendekeza,
Saa **ikitimu**, kitakuteleza,
Ukawa na hamu, kukingojeleza,
Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza.

Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,
Japo mara tumbi, kinshaniliza,
Na japo siombi, kipate n'ongeza,
Mtu haniambi, pa kujilimbikiza.

Chema mara ngapi, kinaniondoka,
Mwahanga yu wapi? Hakukaa mwaka,
Kwa muda mfupi, aliwatilika,
Ningefanya lipi, ela kumzika?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,
Alojipa tabu, kwamba anilee,
Na yakwe sababu, ni **nitengenee**,
Ilahi wahhabu, mara amtwee.

Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,
Hadi siku hini, Yu moyoni mwangu,
Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,
**Ningamtamani**, hatarudi kwangu.

**Maswali**

(a) Eleza dhamira ya mwandishi
(b) Fafanua umbo la shairi hili
(c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari
(d) Taja na kutoa mfano mmoja wa tamathali yoyote ya lugha inayojitokeza katika shairi
(e) Taja mbinu nne za uhuru wa mshairi huku ukitolea kila mbinu mfano
(f) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na vile yalivyotumika**:-
 (i) Nitengenee
 (ii) Ningamtamani

(iii) Ikitimu

14.. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-***

1. Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa wazazi

2. Ni sumu, sumu hasiri
Unahasiri watoto
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa 'moja baridi'
Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu, sumu jeruhi
Unajeruhi watoto kwa pesa,
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye madawa ya giza baridi
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi

**<u>Maswali</u>**

(a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili
(b) Fafanua maudhui ya shairi hili
(c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta?
(d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mfano
(e) Eleza umbo la shairi hili
(f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari
(g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi ;
  (i) Giza baridi
  (ii) Yanakufunga katika klabu

# Fasihi Simulizi

**1.** ***Soma kisha ujibu maswali***

Lala mtoto lala x2
Mama atakuja lala
Alienda sokoni lala
Aje na ndizi lala
Ndizi ya mtoto lala
Na maziwa ya mtoto lala
Andazi lako akirudi
Pia nyama ya kifupa
Kifupa, kwangu, wewe kinofu
Kipenzi mwana lala x2

Titi laja x2

Basi kipenzi lala
Baba atakuja lala
Aje na mkate lala
Mkate wa mtoto lala
Tanona ja ndovu lala

**Maswali**

(a) Huku ukithibitisha jibu lako eleza huu ni wimbo wa aina gani?
(b) Eleza sifa za wimbo wa aina hii
(c) Onyesha umuhimu wa wimbo huu
(d) Eleza amali kuhusu jamii zinazojitokeza katika wimbo huu
(e) Tambua mbinu zozote **mbili** za utunzi zilizotumika katika wimbo huu
(f) Taja vitendo **viwili** vinavyoambatana na uimbaji wa aina hii ya wimbo
(g) Wimbo huu una wahusika wangapi? Wataje

2. ***Soma hadithi hii halafu ujibu maswali ulivyoulizwa***

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme "wanadamu hamtakufa." Kinyonga alienda kwa mwendo wa kuduwaa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akaseme, "Mwanadamu sharti kufa." Mjusi aliunyanyua mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, "Wanadamu sharti kufa!" Akarejelea haraka kwa Mungu. Baada ya muda kinyonga naye akafika duniana na kutangaza, "Wanadamu hamtakufa!" Wanadamu wakapinga mara na kusema, "La! Tumeshapata ujumbe wa Mjusi, wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la mjusi, wanadamu hufa.

**Maswali**

(a) (i) Hadithi hii huitwaje?
(ii) Toa sababu zako
(b) Eleza **sifa tatu** zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii
(c) Kinyonga ni mhusika wa aina gani?
(d) Hadithi hii ina umuhimu gani?
(e) Taja njia zozote **nne** za kukusanya kazi za fasihi simulizi
(f) **Tambulisha vipera hivi**:-

(i) Kula hepi
(ii) Sema yako ni ya kuazima
(iii) Baba wa Taifa

3. (a) Fafanua sifa **tatu** za ushairi simulizi
(b) Wawe na kimai ni nini katika fasihi simulizi? Eleza faida zake
(c) Ainisha mambo yanayobainisha muundo wa nyimbo
(d) Jadili muundo wa kitendawili
(e) Bainisha tamathali za usemi zilizotumika katika methali zifuatazo:-
(i) Ujana ni moshi ukienda haurudi
(ii) Usipoziba ufaa utajenga ukuta
(f) Jadili kwa kina matatizo ambayo huenda yakakabili fasihi simulizi katika jamii ya kesho kisha utoe mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na hali hii

**4.** ***Soma wimbo/shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***

**MUITALIA ANAZWE**

Saa kumi alfajiri
Sote tuliamshwa
Safari tuliianza
Lazima tuimalize
Maji ukiyavulia nguo
Lazima uyaoge

Wazee kwa vijana waliimba
Muitalia lazima anazwe
Mashamba yao walilia
Uui! Jikaze wavulana
Hawataki rangi hii

Wengi wanauliza
Mwitalia alikuja lini? Na ataondoka lini?
Mnaze huyu mlowezi
Hatuchoki
Hatuchoki
Lazima yeye anazwe

Vifaranga na mbuzi
Mbavu zao zahesabika
Meee! Sauti zilihinikiza kote
Haya yote hakika, ni madhila ya Muitalia
Nguvu kweli tunayo
Simama mbele tunayo
Simama mbele uone !
Muitalia ondoka !
Au nikuondoe kwa nguvu

**Maswali**

(a) Taja madhila yaliyosababishwa na Muitalia katika makala haya.
(b) Thibitisha kuwa utungo huu ni wimbo.
(c) Eleza maana inayojitokeza katika mistari ifuatayo:-
(i) Mbavu zao zahesabika.
(ii) Haya yote hakika, ni madhilia ya Muitalia.
(d) Huu ni wimbo wa aina gain? Eleza ukitoa ushahidi
(e) Eleza kwa sentensi mbili au tatu shughuli muhimu za kiuchumi za watu wanaimba wimbo huu

(f) Taja mbinu za lugha zilizotumiwa katika wimbo huu. Toa ushahidi
(g) Taja mafunzo mawili yanayotokana na wimbo huu

5. (a) Eleza maana ya miviga kisha uonyeshe inakotumika
(b) Eleza sifa za miviga
(c) Onyesha umuhimu wa miviga

6. Ni nini maana ya wimbo ?
Ni nini maana ya nyimbo zifuatazo.
Tenzi
Kongozi
Sifo
Wawe
Tendi
(a) Eleza umuhimu wa nyimbo
(b) Eleza sifa za wimbo wa aina ya Bembelezi

7. (a) Nini maana ya khurafa/kharafa?
(b) Fafanua sifa **tano** za kharafa
(c) Elezea mbinu **nne** za kutongolea hadithi

8. (a) (i) Ngomezi ni nini katika fasihi simulizi?
(ii) Eleza sifa zozote mbili za ngomezi
(b) Onyesha tofauti kati ya vikundi hivi:
(i) **Hekaya**
**Hurafa**
(ii) **Visakale**
**Visasili**
(iii) **Ngano za mtanziko**
**Ngano za mazimwi**
(c) (i) Vitendawili ni nini?
(ii) Fafanua kwa mifano, mbinu zozote nne za lugha zinazopatikana katika vitendawili
(d) Soma kifungu hiki cha wimbo kisha ujibu maswali yafuatayo :

**Kuumeni** : (Waliimba) Tumeupata mpilipili na maua yake. Chikicha x2
**Kukeni** : (Wimbo wao kwa sauti tofauti)
Tausi waendaa x2
Tausi waenda wamuacha mama kwenye banda
**Kuumeni** : (Wakijibu wimbo) Mwacheni aendee x2
Mwacheni aende akaone mambo ya nyumba
**Kukeni** : Mama ataota nini x2
Ataota nini, hana mtu wa kumletea kuni
**Kuumeni** : Ataota moto wa magunzi, wa magunzi, wa magunzi.
Twamchukua , kisura wetu, kisura wetu, kisura wetu.
Tausi ni wetu, sasa, ni kito chema, ni kito chema ni kito chema.

**Maswali**
(i) Wimbo huu ni wa aina gani na unastahili katika hafla gani ?
(ii) Fafanua ujumbe uliojikita katika utungo huu

9. ***Soma kifungu kifuatacho kisah ujibu maswali yafuatayo :***

(vigelegele vya harusi vililia alilili ; x3)
**Kuumeni** : (waliimba) Tumeupata mpilipili na maua yake chikicha x2
**Kukeni** : (wimbo wao kwa sauti tofauti) Tausi waendaa x2
Tausi waenda wamuacha mama kwenye banda.
**Kuumeni** : (wakijibu wimbo) Mwacheni aendee x2

Mwacheni aende akaone mambo ya nyumba.

**Kukeni** : Mama ataota nini x2.

Ataota nini, hana mtu wa kumletea kuni.

**Kuumeni** : Ataota moto wa magunzi, wa magunzi wa magunzi. Twamchukua, kisura wetu, kisura wetu, kisura wetu.

Tausi ni wetu sasa, ni kito chema, ni kito chema ni kito chema.

(a) (i) Wimbo huu ni wa aina gani, na unastahili katika hafla gani ?

(ii) Bainisha wahusika Kuumeni na Kukeni

(iii) Fafanua ujumbe uliojikita katika utungo huu

(iv) Wimgo huu una umuhim;u gain hafia ulioimbiwa?

(v) Tambua mtindo uliotumika katika utungo huu

(b) Taja na ujadili aina nyingine **sita** za nyimbo

10. a) **Taja sifa za tanzu zifuatazo za fasihi simulizi**

i) Hurafa

ii) Mighairi

iii) Miviga

b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamii

c) Eleza umuhimu wa mafumbo

d) Eleza tofauti kati ya malumbano ya utani na mawaidha

11. (a) Huku ukizingatia sifa za kimuundo za methali, jadili matumizi ya tamathali za usemi sifuatazo:-

(i) Istiari/sitiari

(ii) Tashihisi

(iii) tashbihi

(b) Vitanza ndimi vina dhima gani katika jamii?

(c) Taja majukumu matatu ya nyimbo katika fasihi simulizi

(d) Eleza sifa tatu za ngano za mtanziko

(f) Eleza sifa tatu za Nyiso

(e) Fasihi simulizi ina sifa ya kuhifadhiwa akilini. Eleza udhaifu wa uhifadhi wa akilini (al. 4)

12. (i) Eleza maana ya vitanza ndimi.

(ii) Taja na ufafanue umuhimu wa vitanza ndimi katika jamii.

# Hadithi Fupi

.

## K. WAMITILA: MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINEZO

1. Ukirejelea mkusanyiko wa hadithi fupi: **Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine**, Onyesha msimamo wa mwandishi Rayya Timammy kuhusu kura na uongozi.
2. K. Wamitila anatumlikia jamii iliyojaa uozo wa kila aina. Eleza kauli hii kwa kurejelea diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.
3. "**Euphrase Kezilahabi ni mwingi wa Jazanda na Ndoto katika uandishi wake**." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi ya Mayai waziri wa maradhi.
4. "Hii ni dunia ya dua la kuku halimpati mwewe!" Alijiambia. Baada ya muda aliongeza "**anayepanda juu kipungu hafikili mbinguni**."

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili

   b) Ukirejelea hadithi ya Msamaria Mwema, onyesha vile hii dunia ni ya '**Dua la kuku**
5. ***Soma makala haya kisha ujibu maswali***

   Angeko, Angeko ee

   Angeko, Angeko ee

   Ni kilio, Kilio ee

   Ni kilio, kilio ee

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(b) Eleza mbinu ya uandishi iliyotumiwa kwenye dondoo hili.
(c)Eleza matukio ya kweli ambayo mtunzi ameyaangazia katika hadithi. “Ndimi za mauti”.

6. Kwa kurejelea hadithi ya Mkimbizi eleza madhara ya vita
7. Sote tulisimama ghafla kama tumesimikwa ardhini”. Huu mwisho wetu sasa!”
   (a) Fafanua muktadha wa maneno haya
   (b) Taja na ueleze mbinu ya lugha ambayo imetumiwa katika muktadha huu
   (c) “Nilikumbuka ile sura ya mama na ndugu zangu”. Ni kwa nini msemaji anawakumbuka mama na ndugu zake?
   (d) Eleza matatizo yaliyowakumba wakimbizi kulingana na hadithi
   (e) Eleza maudhui yanayoibuka katika muktadha
8. Jadili wahusika wafuatao na dhima yao katika hadithi ya Fumbo la mwana :
   i) Makulu
   ii) Mwalimu
   iii) Mzee Atanasi
9. (a) Kwa kurejelea hadithi za Mkimbizi na Fumbo la Mwana, eleza jinsi ambavyo mchafuko wa kisiasa na matumizi ya dawa za kulevya zinavyoweza kuzorotesha ukuaji wa jamii
   (b) Kwa kurejelea hadithi za Uteuzi wa Moyoni na Ngome ya Nafsi, eleza jinsi haki za wanawake zilivyokiukwa
10. "Unavyoona ni kama aligongwa.....basi mimi nikamkuta pale anagaragara chini. Unajua zamani nikienda kanisani.. nakumbuka kisa cha Msamaria ; kufupisha habari mimi ni Msamaria mwema niliyemwokota mzee huyu chini."
   (a) Ni nini kilikuwa kimetendeka ili dereva ayatamke haya ?
   (b) Ingawa Dereva alijiita msamaria mwema, ni yapi hakuwa tayari kufanya masamaria mwema aliyoyatenda katika Bibilia ?
   (c) Unafikiri ni ni kilichosababisha ajali ndiposa mzee huyu agongwe ?
   (d) Onyesha vitendo vya ‘**Msamaria Mwema’** vinavyoelekea kuthibitisha kwamba ndiye aliyemgonga mhasiriwa
11. Mbinu ya majazi na mbinu rejeshi hutumiwa na waandishi wengi ili kuwasilisha ujumbe wao. Huku ukitoa mifano kutoka hadithi mbalimbali thibitisha ukweli wa kauli hii
12. Utamaduni unaomkandamiza mwanamke umetamalaki katika jumuiya ya hadithi za Uteuzi moyoni na ‘Ngome ya Nafsi’. Kwa kurejelea hadithi hizi, eleza jinsi utamaduni umetumiwa kukandamiza wanawake
13. Diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi imejikita katika masuala ibuka yanayofaa kushughulikiwa na jamii. Taja na uthibitishe.
14. Fafanua dhamira ya **Ken Walibora** alipoandika kisa cha **“Tuzo”**
15. "Mara nyingi vijana hushughulikia mambo ya kibinafsi. Mara nyingi mawazo yao hufuata mkondo wa anasa za vijana tu."
   (a) Eleza muktadha wa usemi huu.
   (b) Onyesha ushahidi wowote katika tamthilia kudhihirisha ukweli wa kauli hii.
   (c) Fafanua mambo waliyofanya vijana katika tamthilia kuonyesha kuwa walipigana kwa niaba ya umma.

# MWONGOZO WA KUSAHISHA kiswahili 102/1-2-3

## Karatasi ya kwanza 102/1

1. Mahojiano
   (a) Mwanafunzi aendeleze mahojiano baina ya watu wawili
   (b) Yahusishwe maswali na majibu
   (c) Maswali yalenge mambo muhimu katika mada
   (d) Lugha iwe ya mnato, komavu na ya kuvutia
   (e) Pawe na msamiati unaohusiana na mada
   (f) Mhoji awe na utaratibu mwafaka wa kuuliza maswali katika utiririko
   (g) Insha ichukue sura ya kitamthilia
   SURA
   - Pawe na majina /cheo/vyeo vya mhoji /mhojiwa
   - Herufi kubwa au ndogo itumiwe
   - Matumizi ya hisia au masolugha yawe mabanoni (vicheko, furaha)- iandikwe kwa kifupi

   Mifano ya utovu wa uslama ni kama;
   (i) Uzembe
   (ii) Umaskini
   (iii) Ufisadi
   (iv) Ukosefu wa elimu katika jamii
   (v) Kuvunjika kwa taasisi za jamii (k.m ndoa, elimu)
   (vi) Wizi wa kimabavu
   (vii) Kuvamiwa na genge lililo mafichoni
   (viii) Vita katika nchi jirani
   (ix) Watoro kusababisha michafuko katika sehemu walikohamia
   (x) Silaha hatari bila idhini
   (xi) Ulanguzi wa madawa ya kulevya
   (xii) Ukosefu wa kazi

2. Hii ni barua rasmi
   Iwe na sura ifuatayo:
   i. Anwani mbili; ya mwandishi na mwandikiwa
   ii. Sehemu ya maamkuzi; kwa Bw/ Bi
   iii. Mtajo: KUH: YAH: (Kiini cha barua)
   iv. Mwili wa barua Sehemu ya maudhui (Hoja)
   v. Hitimisho au mwisho wa barua

   Mimi wako………
   Sahihi
   Jina
   Baadhi ya hoja za insha
   Visa
   - Wizi
   - Mauaji
   - Matumizi ya dawa ya kulevya
   - Unajisi/ubakaji
   - Magenge ya majambaz

   Mapendekezo
   - Kujenga vituo vingi vya polisi
   - Mabaraza kufanywa ili kuwashauri wananchi kuepuka maovu/ uhalifu
   - Wageni vijijini kuchunguzwa
   - Hatua kali kuchukuliwa dhidi ya wahalifu
   - Serikali ijishughulishe kumaliza umaskini – kazi kwa vijana/ mikopo ya biashara

- Kuimarisha doria wakati wa usiku n.k

Anayekosa kuzingatia sura ya barua rasmi aondolewe maki 4 baada ya kutuzwa

3.

- Hii ni insha ya mazungumzo
- Mtindo uwe wa kitamthilia. Wahusika washiriki moja kwa moja katika mazungumzo kizamu.
- Majina ya washiriki yaandikwe upande wa kushoto yakifuatwa na koloni (nukta pacha)
- Maelezo kuhusu vitendo yaweza kuonyeshwa katika mabano.
- Mtahiniwa aweza kuwapa majina halisi washiriki katika utangulizi
- Mada ya mazungumzo ni njia za kukomesha uadui unaotokana na ukabila nchini.

Baadhi ya hoja

- Kuhimiza michezo baina ya makabila
- Kazi zibuniwe ili watu wasiwe na nafasi ya kushiriki maovu k.v. vita
- Ugavi wa raslimali kwa njia ya usawa.
- Wahalifu wakamatwe na kufunguliwa mashtaka
- Nchi iwe na kura/uchaguzi wa haki na huru
- Viongozi daima wahubiri amani
- Ndoa baina ya makabila zihimizwe

(Tambua na usahihishe hoja zozote totauti zinazoafikiana na mada)

- Asiyezingatia sura ya maznungumzo aondolowe ala.4 baada ya kutuzwa
- Lazima kila mhusika ashiriki katika mazungumzo

4. Barua hii ni barua rasmi.

- Iwe na anwani ya mwandishi pembeni kulia.
- Iwe na anwani ya anayeandikiwa chini kushoto.
- Barua hii itapitia kwa mwalimu mkuu au mwelekezi wa masomo kabla ya kumfikia mlengwa hivyo itakuwa na anwani mbili.

MTINDO

[ ]

[ ]

Kupitia kwa,

[ ]

Kwa Bw/Bi,

<u>NT: MWALIKO KATIKA MJADALA</u>

I________________________________________________________________________

<u>RATIBA</u>

<u>SURA</u>

Shule ya upili ya ____________________________________________

<u>RATIBA YA MJADALA TAREHE 26/02/2010 KATIKA UKUMBI WA MKUTANO WA SHULE</u>

| SAA | MAJIRA | MATUKIO |
|---|---|---|
| 9.00 – 9.30 | Kuwasili: | Kwa wanafunzi na kuingia katika ukumbi |
| 9.30 – 9.35 | | |
| 9.35 – 10.00 | | |

- Mwanafunzi aeendeleze katika yake kwa shughuli muhimu za siku hiyo ya mjadala. Muda mwingi utengewe mjadala wenyewe.

5. (i) Insha ichukue sura ua ripoti.
(ii) Iwe na utangulizi
(iii) Njia za uchunguzi zielezwe
(iv) Sababu za ajali kama :-
- Ubovu wa barabara nyingi nchini
- Ubovu wa magari mengi nchini
- Madereva kutozingatia sheria za barabarani
- Madereva kutumia mihadarati na kunywa pombe.
- Abiria kutokuwa waangalifu wanapotumia barabara
- Madereva ambao hawajahitimu au wasio na ujuzi
- Askari wa kitengo cha trafiki kula rushwa.

(v) Watoe mapendekezo kama:
- Barabara zikarabatiwe
- Magari yakaguliwe mara kwa mara na yaliyo mabovu yasiruhusiwe kutoa huduma barabarani
- Askari trafiki kuhakikisha kuwa madereva wote wanazingatia sheria za barabarani
- Madreva walevi na wanaotumia mihadarati kuchukuliwa hatua za kisheria
- Elimu kupitia vyombo vya habari kwa abiria kuzingatia uslalama wao barabarani
- Sheria itumike dhidi ya wale wanaoendesha magari na vyombo vya usafiri bila ya leseni.
- Askari wanaochukua hongo wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu

(vi) Atoe hitimisho mwafaka
(vi) Aandike jina lake, atie sahihi na kuandika tarehe

6. Jibu la swali la kwanza
Sura ya kumbukumbu iwe na :-
(i) Mada/kichwa/anwani
(ii) Waliohudhuria
(iii) waliotoa udhuru
(iv) wasiotoa udhuru
(v) Waalikwa (si lazima)
(vi) Ajenda: 1. Kusoma na kudhibitisha
2. Maswali Ibuka
3. Ajenda 3, 4, 5 n.k ndio maudhui
(vii) Kufungua mkutano
(viii) Wasilisho la mwenye kiti
(ix) maudhui
(x) Shughuli nyinginezo
(xi) Kufunga mkutano
(xii) Thibitisho

| | | |
|---|---|---|
| Mwenyekiti | sahihi | tarehe |
| ..................... | .................... | ...................... |
| Katibu | sahihi | tarehe |
| ..................... | .................... | ...................... |

Maudhui; Ajenda zitenge:
- Vijana wapewe mikopo na serikali /benki n.k
- Vijana waelimishwe ili kuboresha maisha yao
- Waepukane na kuwa wategemezi
- Elimu ifanywe ya bure
- Vijana waelimishwe kutochagua kazi
- Waepuke uzembe/uvivu
- Vijana wafunzwe maadili katika jamii ili waepuke ulevi, ukahaba, uvivu na magonjwa kama ukimwi
- Washiriki siasa ili wahusishwe katika uamuzi na mambo
- Wamche Mungu

- Wazame katika ukulima/biashara (hoja zisipungue 5)

UMUHIMU

- Mtahiniwa ahimize urefu wa insha kuanzia kumbukumbu ya kwanza yaani:

Kumbu 01/10: KUFUNGULIWA KWA MKUTANO

- asiyetimiza urefu, aondolewe alama 2u

7. Mwanafunzi azingatie vipengele muhimu vya mahojiano kama vile:
   - Hali ya kupokezana mazungumzo kupitia kwa njia ya kuuliza maswali na kutoa majibu
   - Mzungumzaji mmoja asitawale mazungumzo
   - Lugha yenye staha/ adabu
   - Kuwe na mhojiwa (mwanafunzi/ mgonjwa) na mhojiaji (daktari)
   - Mawazo mazuri yanayofululizwa kimantiki

Mambo yafuatayo yanaweza kujitokeza
   - Maamkizi
   - Sababu za kuja hospitalini
   - Dalili za ugonjwa

8. <u>MSAMIATI</u>

Jumla ya maneno yaliyotumiwa kuafikiana na mada au kichwa kilichopendekezwa

MAUDHUI NA MSAMIATI

baada ya kusoma mtungo utafikiria maudhui na msamiati uliomo kwa jumla

USALAMA ZA KUSAHIHISHA

Hupigwa chini ya sehemu ambaya kosa la sarufi limetokeza kwa mara ya kanza tu.

Hupigwa chini ya sehemu ua neno ambako kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza.

Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno

Hutumiwa kuonyesha msamati bora.alama hii hitiwa juu ya neno lenyewe

Hutumiwa kuonyyesha msamiati usiofaa.alam hii hutuwa juu ya neno lenyewe

Maelezo mafupi kuhusu tuzo la mtahini yanahitajika .kila ukurasa uwe na alama ya _chini katikati kuonyesha kuwa mtahini amepitia ukurasa huo

MANENO

| | | | |
|---|---|---|---|
| maneno | 8 | - | ukurasa1 ¾ |
| maneno | 7 | - | kurasa 2 |
| maneno | 6 | - | kurasa 2 ¼ |
| maneno | 5 | - | kurasa 2 ¾ |
| maneno | 4 | - | kurasa3 ¾ |
| maneno | 3 | - | kurasa4 ½ |

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

<u>Muundo wa kumbukunbu</u>

i) Kichwa kiwe na mada ,mahali tarehe na saa ya mkutano na kiandikwe kwa herufi kubwa

ii) Waliohudhuria_itifaki izingatiwe km mkuuu wa wilaya/mwenyekiti.afisa mkuu wa polisi ,wilayani/katibu.

iii)waliokosa kuhudhuria

iv) Walioomba radhi/udhuru

v) Ajenda

vikufunguliwa kwa mkutano

kumbukumbu zenyewe.orodhesha kumbukumbu kwa majawapo ya mbinu zifuatazo :KUMB.1/2010

KUMB1/7/2010

KUMB.1/26/7/2010 n.k

vii) Shughuli nyinginezo

ix) Kufungwa kwa mkutano

x) Thibitisho.mojawapo ya mbinu hizi yaweza kutumiwa

mwenyekiti sahihi tarehe
katibu
au
1. ________________________ 2. _______________________
Mwenyekiti Katibu
ii) MAUDHUI
Mtahiniwa agusie mikakati iakayafanywa na kamat ya usalama wilayani kuimarisha usalama wilayani humo k.v.
a) Hatua kali za ksheria/kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya maafisa wa polisi ambao ni wazembe na wafisadi i
b) Ushirikiano kati ya umma na kikosi cha polisi uimarishwe km kuwashirikisha raia kuwatambua na kuwaripoti wahalifu
c) Nafasi za kazizibuniwe kwa vijana wilayani
d) Hatua kali zichukuliwe dhidi ya wanasiasa na vyombo vya habari vinavyo chochea wananchi
e) Zawadi zitolewe kwa raia wanaotoa habari kuhusu wahalifu sugu wanao tafutwa na polisi
f) Wahalifu kusakwa na kuchukuliwa hatua kali
g) Maombi ya magari zaidi ya polisi yafanywe kwa serikali kuu
h) Kushika doria kuimarishwe zaidi
i) Nambari za dharura za simu zitolewe kwa raia

<u>TANBIHI</u>

Mtahiniwa azingatie sura kamili ya kumbukumbu.anayekosa vipengele viwili au zaidi vya sura aondolewe 45 (4 Sura)
Mtahiniwa anayekosa kutosheleza urefu aondolewe 2u(2 urefu)
Urefu unakadiriwa kuwanzia kumbukumbu ya kwanza

9 :SURA

Hii ni Insha ya mazungumzo

- -Mtahiniwa anaweza kuandika kichwa au asiandike awashirikishe wote watatu ; mwandishi wa habari aulize maswali na mwenyekiti na Afisa wa sheria wa Tume ya kupambana na ufisadi nchini wajibu
- Azue maudhui tofauti tofauti ili kuikuza na kuifafanua mada kikiamilifu
- Atumie nafasi ya 1 na wakati uliopo
- Atumie mtindo wa kitamthilia

<u>Upungufu ufuatao uadhibiwe</u>

- Atakayeshirikisha mazungumzo ya mhusika mmoja hadi mwisho halafu wa pili aongee aondolewe alama 4s (4 sura)
- Atakayefanta mhusika mmoja tu aongee bila wa pili kuongea aondolewe 2w(2 wahusika) .
- Anayeongezea wahusika wasiokuwepo aondolewe alama 2w (2 wahusika)

ii Maudhui- Mbinu kupambana na ufisadi

- Kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya ufisadi kupitia kwa redio, magazeti, runinga n.k
- Ufishaji kupitia kwa redio,magazeti runinga nk
- Kuwaadhibu wahusika –wapelekwe mahakamani na kufungwa jela.
- Wananchi wafunzwe maadili
- Viongozi wawajibike katika kazi zao
- Sheri za kupambana na ufishadi zibuniwe na kutekelezwa
- Kubuni nafasi zaidi za kazi
- Kuimarisha elimu
- Kuongeza mishahara kwa wafanyakazi

- Tume zaidi za kukabiliana na ufisadi

10. MUUNDO WA KUMBUKUMBU
    - Kichwa
    - Kumbukumbu za mkutano
    - Tarehe na mahali
    - Kichwa kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigwe mstari
    - Waliohudhuria
    - Majina na nyadhifa
    - Wasiohudhuria
    - Wageni/ waalikwa
    - Ajenda
    - Ufunguzi
    - Mwili – maudhui
    - Umuhimu wa amani na jinsi ya kuidumisha
    - Mikutano ya mara kwa mara kati ya makabila husika
    - Kuhubiri umuhimu wa kusameheana
    - Kuhimiza ndoa za mchanganyiko
    - Viongozi kushurutishwa kutotoa matamshi ya uchochezi
    - Wahalifu kushtakiwa na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria
    - Washukiwa wakuu wa uchochezi waghasia kushtakiwa na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria
    - Raslimali kugawanya sawa n.k.
    - Shughuli nyinginezo
    - Hitimisho
    - Kufungwa kwa mkutano, saa na maombi
    - Kuthibitishwa
    - Mwenye kiti __________ Tarehe ________________
    - Katibu __________ Tarehe________________
    - Mtahiniwa azingatie muundo wa kumbukumbu. Asipozingatia sura aondolewe al. 45
    - Mtahiniwa awe ndiye mwandishi wa habari. Asipojihusisha aondolewe alama 2
    - Mada izingatiwe au asipofanya hivyo atakuwa hajajibu swali

11. Sura ni ya kitamthilia. Kiwe na kichwa, kiwe na utangulizi ukifafanue maudhui na wahusika hasa iwapo mtahiniwa atawapa majina

    Wahusika ni mwanahabari na mtahiniwa/ mwanafunzi aliyeibuka bora katika mkoa wa magharibi. Mwanahabari ndiye atamwuliza mwanafunzi bora maswali naye atamjibu

    <u>Maudhui</u>

    Miongoni mwa mengine watazungumzia
    1. Mambo yaliyochangia ufanisi wake k.m. bidii, nidhamu, ushuri wa walimu/ wazazi
    2. Himizo kwa wanafunzi wengine
    3. Changamoto alizokumbana nazo katika harakati za maandalizi ya mtihani
    4. Maoni yake kuhusu elimu ya chuo kikuu na kazi ambayo angependa kufanya

    Kutuza

    Asipojaza urefu aondolewe 24

    Akipotoak kisura (asipoandika tamthilia) aondolewe 4

    Usemi uwe halisi

    Mkwaju √ utumike kwa maudhui

12. Kumbukumbu

    Muundo/ umbo/ sura ya kumbukumbu

    a)
    1. Waliohudhuria
    2. Wasiohudhuria na udhuru
    3. Waliokosa kuhudhuria

iv. Wageni/ waalikwa

b) Agenda ya mkutano

i. Kusomwa kwa kumbukumbu za mkutanouliopita
ii. Yaliyotokana na kumbukumbu za mkutano uliopita
iii. Matokeo ya mtihani wa 2009
iv. Ulipaji wa karo
v. Uchaguzi wa waakilishi wa kidato cha kwanza
vi. Namna ya kuwaanda watahiniwa 2010
vii. Miradi ya maendeleo shuleni
viii. Shughuli nyinginezo
ix. Kufunga mkutano

13. Chanzo cha mzozo:
- ♦ Uhasama wa kikabila
- ♦ unyakuzi wa ardhi
- ♦ kuzuka kwamaabaka
- ♦ ufisadi
- ♦ wizi wa kura
- ♦ ubaguzi wa rangi n.k

(b) Hasara iliyotokana na mzozo:-
- ♦ Majumba yaliyobomolewa
- ♦ watu waliuawa
- ♦ usafiri ulikataliwa
- ♦ elimu ilizorota
- ♦ wakimbizi walitokea ikabidi wahudumiwe
- ♦ raslimali zilihabiwa
- ♦ usalama ulizorota
- ♦ uchumi ulidorora
- ♦ uhasama wa kikabila uliendelea ziaid

(c) Namna ya kutatua
- ♦ kuunda mikakati inayolenga kuwa na uswa wa kijamii
- ♦ kutoa adhabu kali kwa wanaozua hisia hasi za kikabila
- ♦ kigawana mamlaka
- ♦ kuunda tuem ya haki na maridhiano
- ♦ kuanzisha michezo ili kuwepo na mkabala mzuri bain aya jamii

Taz,.(a) Atumie mtindo wa mahojiano –watu wawili au zaidi
-Mpatanishi /msuluhishi na mwanasiasa wadhihike vizuri katika mahojiano
- Mtahiniwa anaweza kuwapa majina lakini aeleze mpatanishi ni yupi na mwanasiasa ni yupi.

14. Hii ni insha ya ripoti
Mtahiniwa azingatie sura ya ripoti
Anaweza kuwa na vijichwa vifuatavyo;
- Utangulizi
- Safari ya kwenda mashindanoni
- Mashindano yenyewe

Mbio mbalimbali- Za masafa mafupi/ marefu
Kuruka viunzi
Utupaji wa uzani
Urushaji wa mkuki n.k

Kilele- mbio za kupokezana vijiti
- Matokeo ya mashinandano hayo
- Sherehe ya kufunga mashindano-pengine hotuba mbalimbali kutoka viongozi wa michezo wilayani

- Hitimisho
- Kujitambulisha kwa mwandishi- jina na sahihi

Anaweza kuandika kwa mfululizo kiaya huku vijisehemu mbalimbali zikidhihirishwa kwa mtiririko wenye mantiki inayofaa

Mfuatano wa matukio ujitokeze kwa mtiririiriko mzuri. Anayechukua mtindo huu atakuwa sahihi pia kisura

Asitumie vitambulishi nafsi k.v. ni, tu, n.k.

Anayetumia vitambulishi nafsi atakuwa na udhaifu wa kimtindo

15. Insha izingatie mtindo wa barua rasmi
- Anwani mbili
- Mtajo (kwa mhariri)
- Mada

Utangulizi – mwanafunzi aeleze alikotoa habari

Mwili – Mwanafunzi ataje mabadiliko yoyote ya naga k.m kuenea kwa ukama
- Kuongezeka kwa joto
- Kupungua kwa mvua
- Mafuriko

Mwanafunzi aeleze athatri za mabadiliko haya k.m.
- Kukauka kwa mito
- Vifo vya wanyama
- Vifo vya binadamu
- Kuenea kwa majanga
- Kuongezeka kwa maji baharini
- Magonjwa ya ngozi
- Ukosefu wa chakula

Hitimisho
- Mwanafunzi atoe njia mwafaka za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga k.m
- Kupunguza ukataji wa miti
- Kupanda miti kwa wingi
- Kupunguza gesi hatari kutoka viwandani inayoachiliwa hewani

Mwanafunzi ahitimishe kwa kuandika:
- Jina lake
- Sahihi
- Mahali anakotoka

## <u>Insha za kawaida (KA)</u>

1. Sharti mwanafunzi amalizie kwa maneno aliyopewa
- Kisa kieleze hali ya maisha ambapo inaenda kando na matarajio ya wengi
- Insha iwe na awani iliyopigiwa msitari
- Azingatie msamiati mwafaka
- Ashughulikie kisa kinachoonyesha namna watu (marafiki) hugeuka na kusaliti walioamini.

2. Changa moto za elimu bila malipo
- Kichwa k.m chanagmoto zinazokumba elimu bila malipo
- Kichwa kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigwe mstari
- Ataje changamoto
- wanafunzi wengi shuleni
- Ukosefu wa walimu wa kutosha
- Ukosefu wa vifaa vya kutosha
- Matokeo kudidimia
- Ukosefu wa vitabu
- Dhana potofu miongoni mwa wazazi na wafadhili kutegemea serikali

- Ufisadi miongoni mwa maafisa, walimu wakuu na wafanya biashara, wanakandarasi n.k.
- Wizara na idara mingine kukosa ufadhili
- Shule za kibinafsi kuongeza karo kwa sababu ya matokeo mema
- Mbinu zisizofaa kutumika kuimarisha matokeo k.m. wizi wa mitihani, kuzuia watahiniwa dhaifu kufanya mtihani

3. Usawa masomoni
   - usawa kazini
   - Kupiga marufuku ukeketaji wa wasichana
   - Kupinga ndoa za mapema
   - Kupinga ndoa za lazima
   - Kuweka idadi maalum ya wabunge wa kike

4. Hili ni swali la maelezo
   Mtahiniwa aeleze madhara ya ajira ya watoto kwa kina
   Madhara ni kama vile:
   i. Ukosefu wa elimu
   ii. Kudhulumiwa kimapenzi
   iii. Magonjwa
   iv. Utovu wa nidhamu
   v. Malipo duni
   vi. Ulemavu
   vii. Vifo
   viii. Mapigo
   ix. Lishe duni
   x. Kukosa mavazi
   xi. Huchangia uhusiano mbaya katika jamii
   xii. Kulemaza ukuaji wa motto

5. Hii ni insha ya methali
   Maana ya nje: Mzigo uliobeba chakula hata ukiwa mzito haumchoshi
   Anayeubeba
   Maana ya ndani: jambo lililo na manufaa halimchoshi mtu
   Matumizi: Hutumiwa kumhimiza mtu anayefanya jambo lililo na manufaa kwake kwamba aendelee kujikaza licha ya ugumu anaokabiliana nao. Mtahiniwa atunge kisa au visa vinavyoonyesha ukweli wa methali hii.
   Ikiwa na visa na muumano. Arejelee pande zote mbili za methali kikamilifu
   Aonyeshe jinsi jambo husika lilivyo zigo la kuliwa na namna lisivyolemaa

i) UTAHINI
   Kisa kisipotoa maana ya methali, takuwa amejitungia swali. Atuzwe Bakshishi (BK 01 -
ii) Asiyeshughulikia pande zote mbili hajajibu swali. Atuzwe (BK 01 – 02 )

6.
   i. Hii ni insha ya mdokezo
   ii. Lazima mtahiniwa atamatishe insha yake kwa maneno haya
   iii. Atakayekosa maneno yote, au baadhi ya maneno swali. Atuzwe BK 01 02
   iv. Atakayeongeza maneno mengine, vile vile atakuwa amejitungia swali. Atuzwe KB 01 – 02
   v. Kisa kionyeshe njia za kuzuia uhalifu ambazo zitapendekezwa na mkuu wa askari au wananchi

**MBINU ZA KUZUIA UHALIFU**

i. Kuelimisha watu kuhusu madhara ya uhalifu
ii. Wahalifu kuchukuliwa hatua kali
iii. Wahusika doria wawepo kuzuia uhalifu

iv. Ajira kuwepo ili watu wapate riziki
v. Sheria ziimarishwe
vi. Wavyele wapewe mafunzo ya malezi
vii. Maadili ya kidini yahimizwe
viii. Miradi ya mapato ianzishwe
ix. Kuwe na njia za kuwatambua wahalifu
x. Kuwe na njia za kuwatuza/ kuwapongeza walioadilika

UTAHINI
i) Anayetunga kisa kisichorejelea mambo haya amejitungia swali
ii) Azingatie angalau mambo matano

7. Mwenye kovu sidhani kapoa
Hii ni insha ya methali
Mtahiniwa anaweza kufahamu methali kimaana na kimatumizi (si lazima) . Kilicho muhimu ni kisa au visa kilichoandikwa kuonyesha ukweli wa methali hii.
Mwenye kovu- Mtu aliyewahi kukumbwa na jambo Fulani baya/ lenye kuumiza/ lenye kusababisha uchungu Fulani

Sidhani kapoa- Usihukulie kuwa amesahau jambo lile na kutulia
Maana: Mtu aliyewahi kukumbwa na jamboo lenye kutia uchungu au kuumiza atabaki akilikumbuka hasa kwa hasira. Atakuwa akitafuta nafasi ya kulipiza kisasi hasa ikiwa jambo lile lilisababishwa na mtu anayemjua
Kisa kitasawiri hali ya kulipiza kisasi kwa uovu aliotendewa mtu
Anayekosa kutunga kisa atakuwa jajalijibu swali

8. Elimu/ masomo ya bure
Athari- matokeo; yaweza kuwa mazuri au mabaya
Aonyeshe pande zote mbili kwa kutoa hoja mwafaka
Mfano: Athari mbaya
- Uhaba wa vifaa
- Ushuru kuongezeka kulipia
- Miradi mengine ya serikali kuathiriwa
- Kiwango cha masomo kimezorota
- Uhaba wa walimu

Faida
- Nchi imeimarisha uwezo wa kusoma na kuandika
- Watoto kutoka jamaa maskini kuendelea na masomo
- Wazazi wamepunguziwa mzigo wa malipo ya karo n.k.
- Hakiki na utambue hoja zozote zaidi zinazoafikiana na mada

9. Hii ni insha ya madokezo
Mtahiniwa abuni kisa kitakachoafikiana na kimalizio kilichotolewa
Kisa kionyeshe majuto; mhusika kuonywa dhidi ya tabia Fulani, ayakaidi mashauri na hatimaye kukumbwa na balaa; kudhoofika kiafya kutokana na tabia yake
Kisababishi chaweza kuwa
Ugonjwa wa ukimwi
Kuathirika na dawa za kulevya n.k.
Anayekosa kumalizia kimalizio hiki achukuliwe kuwa hajajibu swali, na kuwekwa katika kiwango cha D 03

10. Uhaba wa kazi
- Mwanafunzi ajadili pande zote mbili
<u>kuunga mkono</u>

uhaba wa kazi umesababisha :-

- umaskini
- ukosefu ya usalama
- matumizi ya dawa za kulevya
- Uvunjaji wa sheria
- uhasama kati ya walio na kazi na wasio na kazi
- wizi wa mabavu

<u>Kupinga</u>

- Mtu anaweza kujiajiri
- walio na kazi huchangia katika visa vya uvunjaji wa sheria k.v. ufisadi
- Mwishoni mwa mjdala mwanafunzi atoe msimamo wake/aonyeshe msimamo wake
- Taz- ashughulikie hoja <u>tano</u> au zaidi

11. Maana : Subira ni sawa na kungojea ili jambo fulani likutokee au utendewe jambo fulani la haja.
    - Heri i sawa na matokeo mazuri/mema yanayopatikana baada ya mtu kuwa mvumilivu kwa kusubiri labda kw amuda mrefu hata ingawa kuna mambo mengine sawa sawa na yale anayoyasubiri. Lakini yanayopatikana baada ya subira huwa yenye manufaa ziaidi kuliko yanayopatikaka kwa haraka.
    - Mtahiniwa aeleze kisa au visa vinavyoafiki maana ya methali
    - Insha izingatie pande zote mbili za methali
    - Asiyeshughulikia pande zote mbili atakuwa amepungukiwa kimtindo.
    - Insha isipoafiki maana ya methali alikuea anajitungia swali. Kwa hivyo atuzwe

12. Insha iakisi hali ya kunusirika, kuponea chupuchupu, kuokoa
    - Mtahiniwa akamilishe kisa kwa kifungu cha maneno aliyopewa
    - Asiyehitimisha kwa hilodondoo atakuwa amejitungia swali – atuzwe D-02
    - Atakayeongezea maneno yasiyozidi matano ataondolewa maki 02m (maneno) kazi nzuri !

13. Namna ya kumaliza umaskini katika jami i
    1. Kuendeleza kilimo cha kisasa
    2. Kuhamasisha watu dhidi ya ufisadi
    3. Kushirikisha wafadhili katika shughuli za kielimu na kilimo
    4. Kukuza/ kuipa kipa umbele sekta ya juakali na kuongeza nafasi za kazi
    5. Serikali kuwapa mkopo wafanya biashara ndogo ndogo
    6. Kupuuza mila na desturi zilizopitwa na wakati- idadi kubwa ya mifugo wa kienyeji
    7. Ulipaji wa ushuru kuimarishwa
    8. Ugavi sawa wa raslimali za nchi
    9. Kumaliza mizozo ya kisiasa
    10. Uzembe/ ulazaji damu kumalizwa kwa kuwapa kiinua mgongo wanaofanya bidii
    11. Matumizi ya mihadharati na pombe haramu kukomeshwa
    12. Elimu ya msingi kuimarishwa ili kuondoa ujinga nchini
    13. Serikali kuwapa wakulima pembejeo kama vile mbolea, mbegu n.k

14. Mwanafunzi atunge kisa/ visa vinavyooana na maana ya methali
    - Watu wenye uwezo wanapozozozana/ kupigana/ wanaoteseka/ kuumia ni wale walio chini yao

15. Mwanafunzi atunge kisa kitakachomalizika kwa mdokezo, aliopewa na kukipa kisa hicho mada inayooana na mdokezo

16. Hii ni methali. Kisa kirejelee sehemu zote mbili. Atoe kisa/visa kinacholenga maana ya methali na matumizi yake. Mtu akizungumzia jambo Fulani huwa amelipitia na anaielewa tosha. Hasemi

tu kwa kulisikia au kulisoma vitabuni kwa mfano aliyewahi kuporwa mali, kunajisiwa au hata kupata msaada kutoka kwa mtu Fulani atampa sifa kutokana na ule usaidizi alioupata
Kutuza
Asiyelenga methali/ anayepotoka asipate zaidi ya D 03
Atakayerejelea sehemu moja ya methali asipate zaidi ya C 08
Hii ni insha ya kukadiria

17. Maudhui
Mabadiliko katika sekta ya elimu ni kama vile:

a) Kuondolewa kwa adhabu ya kiboko
b) Kutoajiriwa kwa walimu na tume ya kuwaajiri walimu. Wanafunzi ni wengi na walimu Wachache
c) Elimu ya bure imesababisha msongamano wa wanafunzi wakiwemo walio na utovu wa nidhamu
d) Masuala ya haki za watoto
e) Mtaala ulio mwema unaotokana na mfumo wa elimu wa 8-4-4 unaowalemea wanafunzi
f) Msisitizo uliotiliwa suala la kupita mtihani

Katika kupiga
Kuna masuala mengine kamam vile:

i) Uozo katika jamii kwa jumla
ii) wazazi kuwapa majukumu yao ya malezi
iii) athari za kigeni
iv) Kudorora kwa mila na desturi za kiafrika

18. Hii ni insha ya mdokezo
Mwanafunzi aandike mtungo (insha ya kubuni) utakaomalizikia kwa maneno aliyopewa
Akikosa kuyatumia atakuwa amejitungia swali lake la binafsi. Atapewa bakshishi 01
Akiongeza maneno yake ataadhibiwa kwa kuondolewa 2 (kimalizio)
Kisa chake kionyeshe mja aliye tajiri lakini asiye na utu na anavyoangamia kutokanan na uroho/ ukatili wake. Aidha aonyeshe maskini anayepata ufanisi kutokana na matendo yake mema (maadili)

19 **MAFANIKIO YA ELIMU YA BURE**

- Watoto wengi kupata elimu
- Njia ya watoto kupunguka – kiasi kikubwa
- Idadi ya watoto wanaorandaranda
- Wazazi wengi wasiojiweza wamenufaika na mpango huu n.k.
- Matatizo
- Msongamano wa wanafunzi
- Ukosefu wa vifaa – vitabu vya kutosha n.k.
- Upungufu wa walimu
- Kiwango cha elimu kuathirika
- Majengo kutoweza kutosheleza mahitaji yanahitaji upanuzi
- Walimu kulazimika kuwafunza watu wazima (Umri mkubwa)
- Uhaba wa pesa za kutosha kutosheleza mahitaji shuleni n.k.

20. Hii ni methali
Chuma – kufanya kazi na kupata faida
Janga – Balaa; shida; hatari; tabu; matatizo
Maana: Yeyote asababishaye shida, huwatia hasara watu wa nasaba yake.
Hili lina maana kuwa watu wa jamii moja hushirikiana kwa kila hali, iwe ni mbaya au nzuri
Matumizi: Huambiwa mtu aliyetia ukoo wake hasara

- Mtahiniwa ashughulikie pande zote mbili za methali yaani : kuchuma na kula
- Atakayechagua kisa aonyeshe kazi iliyofanywa na ile faida au matokeo kwa wa kwao
- Anaweza kuonyesha methali nyingine zinazoweza kuchukua maana yah ii methali

- Wakati wa kutuza, ambaye hatashughulikia pande zote mbili, awekwe katika kiwango chake kisha aondolewe alama 4 (maudhui)

Anaweza kutumia visa zaidi ya kimoja ila tu inabidi vionane

21. Mtahiniwa aandike kisa
    - Kisa kinachomhusisha yeye akitenda makosa
    - Pawe na majuto
    - Ziada
    - Asiyejihusisha amepotoka awekwe kiwango cha D – (alama 2)
    - Akikosa sehemu ya makosa au majuto aondolewe alama 2 (maudhui)
    - Asipomalizia maneno ya dondoo amepotoka apewe D – alama 2
    - Asipomalizia maneno matano (5) ya mwisho aondolewe alama 2 (Kimalizio)

    Akizidisha baada ya dondoo maneno yake, hajajibu swali

22. Insha ya methali
    - Udongo uwahi/upatilize ungali maji
    - Udongo hauwezi kusarifiwa kama umekauka lakini mtu huweza kuusarifu na kuufinyanga vizuri kama maji. Methali hii hutumiwa kutufunza kwamba tunaponuia kulifanya jambo fulani tusingojee hadi wakati uakapita, tunapaswa kuliwahi mapema. Watu wngine husema upatilize udongo uli maji au udongo ukande uli maji. Udongo uuwahi ungali maji.
    - Lazima mwanafunzi alenge swali/methali kionyeshe kuwa jambo liliwahiwa kabla halijaharibika.
    - Kisa kilenge methali hiyo.

      Mfano: Matumizi ya dawa za kulevya, uhifadhi wa mazingira, kujiingiza katika ukahaba

23. <u>Ubaya wa kuavya mimba</u>

    - Ni uhalifue
    - Huzorotesha afya ya mhusika
    - Husababisha kifo
    - Inaweza kusababisha utasa
    - kiwango cha laana/dhambi/imani
    - Hushusha heshimana hadhi ya mhusika

    <u>Uzuri wa kuavya</u>

    - Huokoa maisha ya wale walioathirika.
    - Mimba ambazo hazihitajiki mfano ubakaji, watoto wadogo, undugu

    <u>Msimamo</u>

    - Mwanafunzi atoe msimamo wake

24. Hii ni insha ya mdokezo. Kisa cha mwanafunzi kiafiki maneno hayo na asiongeze wala kubadili mpangilio wa maneno hayo.

    Mwanafunzi abuni kisa cha kusisimua kinacholenga maneno hayo.

    DOSARI

    - Uozo katika jamii
    - Ukosefu wa kazi
    - Magonjwa
    - Uchafuzi wa mazingira
    - kuvuruga maisha ya binadamu

    Mtahiniwa aonyeshe kwamba hiyo teknolojia imemwathiri

    Asipojihusisha aondolewe alama (2w) za wahusika

25. Wasifu – Kazi iwe na mpangilio au vipengele vifuatavyo:-

    Maudhui

(i) Maelezo ya kibinafsi
a) Jina
b) Tarehe ya kuzaliwa
c) Mahali pa kuzaliwa
d) Ndoa/Hadhi
e) Lugha
f) Anwani
g) Nambari Ya simu
h) Barua pepe

Vipengele hivi vitengwe kwenye mstari mmoja

(ii) Kiwango/viwango vya elimu
- Mwanafunzi aanze na kiwango cha juu cha elimu.
- Mwaka wa kusoma – Kiwango na cheti alichopata baada ya kuhitimu/kufuzu

mfano :- 1999 – 2004 – Chuo kikuu cha Kenyatta Shahada ya kwanza ya ualimu.

(iii) Tajriba ya kitaaluma

Aanze kwa kazi anayoifanya kwa sasa

(iv) Uteuzi (ikiwa upo) majukumu au nyadhIfa ulizowahi kupewa.

(v) Semina ulizo hudhuria (ikiwa zipo)

(vi) Kazi za ziada/ tuzo/ machapisho

(vii) uraibu

(viii) Wadhamini/ warejelewa ataje wawili au watatu lakini wasizidi hapo.

26. Methali

Mwongozo

MTAHINIWA ATOE MAANA YA NJE NA NDANI YA METHALI
- Pande zote mbili ya methali zishugulikiwe
- Anaweza kutumia visa au kisa kufafanua methali
- Anawaza kuonyesha maana ya ndani /yenye/kuanzia kisa au visa moja kwa moja
- Kisa/visa vionyeshe mali akisifwa kwa jambo zuri huauza kuregea ua kuharibu mambo

27.
- Insha itamatishwe kwa mdokezo uliotolewa
- Mtahiniwa asimilie kisa kinacholenga uchaguzi katika uwanja wa kisisa kisa chenyewe
- Uchaguuzi kufanyua baada ya kifo cha mbunge wa eneo bunge hilo
- Mbunge wa awali kuhusika katika wizi wa kura
- Mtahiniwa asipomaliza kwa maneno aliye atakuwa amepotoka hivyo kupewa Al:2(bakshishi)

28 - sha itamatishewe kwa mdokezo ulitolewa
- Mtahiniwa asimilie kisa kinacholenga uchaguzi katika uwanja wa kisisa kisa chenyewe
- Uchaguuzi kufanyua baada ya kifo cha mbunge wa eneo bunge hilo
- Mbunge wa awali kuhusika katika wizi wa kura
- Mtahiniwa asipomaliza kwa maneno aliye atakuwa amepotoka hivyo kupewa Al:2(bakshishi)

29. Kisa cha mwanafunzi kionyeshe ukweli wa methali hii. Anayehama kambini au pahala Fulani hawezi kunya au kuchafua pale eti kwa kuwa anatoka, la. Huenda ikatokea haja, ikabidi arudi pahali hapo. Tusidharau cha zamani kwa kuona kipya (Usiache mbachao kwa msala upitao)

30. Mwanafunzi aonyeshe
- Maana ya uavyaji wa mamba
- Madhara ya uavyaji mamba
- Kusababisha vifo vya wahusika
- Kutozaa baadaye
- Mauaji ya vilenge/ vijusi
- madhara ya kiafya kwa mama mfano maradhi ya chupa ya motto n.k
- Waweza kushtakiwa / kufungwa
- Dhambi kwa mola – kuua

Manufaa ya uavyaji

- Kuokoa maisha ya mama aliye hatarini
- Mimba ya ukooni mwa mama- mivigo, kuondoa aibu
- Mwanafunzi arudi shuleni (mama)

N.B - Katika aya ya mwiso, atoe uamuzi au maoni yake
- Aeleze upande mmoja mfano apinge kisha aunge mkono mjadala kisha atoe uamuzi

Au

- Atoe uamuzi wake, kisha atoe maoni

32. Mtahiniwa kwanza aeleze hiyo halafu atolee suluhu

Maudhui

1. Ubakaji wa watoto wadogo
   Suluhu:- Watoto wachungwe na wazazi au walezi wahusika waadhibiwe vikali
2. Watoto kuteswa na wazazi k.v. kuchapwa hadi kulemazwa au kuchomwa.
   Suluhu : Wazazi waadhibiwe mahakamani
3. Ajira ya watoto
   Suluhu:-Serikali ihakikishe kila mtoto yu shuleni kwani masomo ni ya bure na wasiopeleka hao wachukuliwe
   hatua kali
4. Kuavya mimba-
   Suluhu – wahusika wafungwe kifungo cha mda mrefu
5. Watoto wachanga kutupwa pipani
   Suluhu: Serikali ijengee watoto kama hao makao ; wahusika wachukuliwe hatua
6. Watoto kuadhibiwa na walimu kupita kiasi
   Suluhu: Walimu kama hao wafutwe kazi
7. Ukosefu wa chakula
   Suluhu Wazazi washurutishwe kuwalea watoto wao vyema; serikali itoe misaada ya chakula

(Hoja tano na zaidi zifafanuliwe vyema huku masuluhu yakitolewa )

**UMUHIMU**

Sura

- Insha iwe na kichwa kilichoandikwa kwa herufi kubwa na kupigwa mstari
- Au aanze tu kuandika insha muradi ameonyesha ni swali nambari gani.
- Urefu wa kunasa mbili au zaidi uzingatiwe ili kutimiza idadi ya maneno
- Asiyetimiza idadi ya maneno aondolewe alama 2u baada ya kukadiriwa katika kiwango chake

33. - Mtahiniwa atunge kisa kifaacho

Maana : Kitu cha anayeondoka pamoja naye.

_ Huweza kutumiwa kuipigia mfano hali ambayo imebadilikka na kuwa mbaya zaidi au kubadilika na kuwabora zaidi

- Si lazima mtahiniwa aeleze maana mwanzoni
- Si lazima aandike anwani/kichwa cha insha yake
- Anaweza kuanza moja kwa moja kisa chake
- Mtahiniwa azingatie maana kikamilifu

34. - Mwanafunzi ajaribu kuelezea wasifu wa ‘Rais Julius Nyerere

- Si lazima mwanafunzi azungumzie ukweli na kihistoria
- Mwanafunzi amekubaliwa kubuni na kumpatia Rais Nyere sifa ziada zisizo halisi

**MAUDHUI**

- Mwanafunzi aeleze jinsi mhusika huyu anavyojulikana kitaifa na kimataifa
- Kiwangochake cha elimu
- Umaarufu wake kisiasa
- Familia yake
- Alivyoendelea kuichumi
- Duri
- Marafiki zake

- Jinsi alivyopata umaarufu wake
- Maudhui yasipungue matano

**Sura**

- Maandishi ya mfululizo.
- Mwanafunzi atimize urefu unaohiajika .
- Aisyetosheleza urefu aondolewe al. 2u.

35. (i) Anaweza kuunga mkono, kupinga au kujadili pande zote mbili
(ii) Akishughulikia pande mbili atoe uamuzi katika hitimisho

**Kuunga mkono**

- Kuavya mimba ni kinyume cha amri ya Mungu isemayo usiue. (Maadili ya Kidini)
- Mtoto anayeaviwa ni kiumbe ambaye ana haki ya kuishi
- Ni kwenda kinyume cha utu wa mwanadamu
- Kuavya kukiruhusiwa ni kuchochea kuporomoka kwa maadili
- Ni sawa na kuhalalisha mauaji
- Huhatarisha maisha ya mama
- Ni hatari kwa afya ya mama (magonjwa)
- itachangia utasa katika jamii
- huweza kusababisha kuwepo kwa mayatima
- Ni hasata katika uchumi wa taifa kwani mama akifa mchango wake utakosekana

**Kupinga**

- Kuavya kuruhusiwe ikiwa afya ya mama iko hatarini
- Kuavya kuruhusiwe ikiwa mimba ilitokana na ubakaji
- Wanaosaidia kuavya mimba watakuwa ni madaktari waliohitimu na hivyo hamna wasiwasi wa kutokea maafa.
- Kutazuia vifo vingi kwa sababu kuharamisha kutawazwa wasichana na wanawake kuavya kwa siri na madaktari bandia/hasi/matapeli.
- Kuruhusiwe kwa sababu maisha huanza baada ya mtoto kuzaliwa.
- Kuruhusiwe ikiwa wahusika wote ni wachanga na hawajawajibiki
- Kutusaidia kupanga uzazi
- Ili kupunguza mayatima kwa sababu mama aweza kufa anapokuwa akizaa
- Yaweza kuwapa wahusika muda wa kujiandaa katika ndoa halali
- Ili kuepusha wanaharamu katika jamii

36. (i) Mtahiniwa aeleze maana na matumizi ya methali
(ii) Atoe kisa kinahcoafikiana na methali

<u>Maana</u> :- Mtu awapo na tatizo lolote halafu mtatuzi au masaidizi akionyesha nia ya kumsaidia, kumwacha mwenye tatizo na matumaini/matarajio.

<u>Matumizi :</u> Hutumiwa kuwahimiza watu kuwa wanapoendewa ili kuombwa msaada au ushauri, wasioneshe nia ya kutojali kwani kufanya hivyo huwakatiza wahasiriwa tamaa.

37. (i) Lazima amalizie maneno ya mdokezo
(ii) Asipomalizia maneno hayo atakuwa amepotoka
(iii) Akiongezea zaidi maneno matatu (3) atolewe alama mbili
(iv) Yakizidi kwa maneno matano, amepotoka.

**38. Bandu Bandu Huishia Gogo**

Mwanfunzi atunge kisa kinacho dhihirisha ukweli wa hiyo methali (juhudi za kidogo kidogo hatimaye huleta ufanisi katika shughuli).
- Si lazima mwanafunzi kufafanua maana. Mwanafunzi aweza kuanza kwa masimulizi yake moja kwa moja. Hata hivyo aliyefafanua methali vilivyo asiadhibiwe.
- Kisa kimoja kirefu au visa vidogo vidogo vinavyioafikia methali vitafaa.
- Kisa cha mwanafunzi kisiishilie kupinga methali.

39. **MATATIZO**

1) Ukosefu wa ajira kwa vijana.
2) Ufisadi uliokithiri.
3) Raslimali kuliandikiwa wachache.

4) Uongozi mbaya – Taasisi za serikali kuingiliwa na serikali kuu.
5) Ukosefu wa usalama.
6) Ukabila.

KUUNGA

SULUHU

Katiba iweze kuweka mikakati ya

KUPINGA

40. - Mwanafunzi atunge kisa kinachoaibisha.
- Asiongeze maneno yake katika kile kifungu cha kuishilia.
- Utaratibu wa kuhakiki insha uzingatiwe katika utuzaji na utozaji wa alama.

41. Hii ni insha ya methali

Mchumia – chuma – tafuta riziki

Juani – kustahimili ugumu/ kwa shida

Mtu anayeshughulikia jambo fulani kwa dhati na kwa kuvumilia ugumu wowote hatimaye hufanikiwa na kustareheka.

Mtahiniwa aweza kutoa ufafanuzi wa maana na matumizi ya methali

Atoe kisa/visa vinavyooana na maana ya methali

Asiyetoa kisa achukuliwe kuwa hajajibu swali na kuingizwa katika kiwango cha D.

42. Sababu zinazochangia uhalifu

(i) Umaskini
(ii) Kuimarika kwa teknolojia k.m. rununu
(iii) Ukosefu wa ajira
(iv) Uhasama baina ya makabila
(v) Siasa duni – k.m viongozi kuchochea uhasama baina ya makabila
(vi) Ulanguzi wa silaha hatari
(vii) Ulegevu wa maafisa walinda usalama
(viii) Ufisadi
(ix) Matumizi ya dawa za kulevya

Njia za kukomesha

(i) Walinda usalama walegevu waachishwe kazi
(ii) Hatua kali kuchukuliwa dhidi ya walanguzi na watumizi wa dawa za kulevya
(iii) Ajira zibuniwe
(iv) Vijana kusaidiwa kuanzisha miradi ya maendelo k.m. mikopo.
(v) Vituo vingi vya polisi kujengwa
(vi) Vituo vya urekebishaji tabia vijengwe
(vii) Hatua kali zichukuliwe dhidi ya wavunjaji wa sheria

43. Hii ni insha ya mdokezo

- Ni insha iliyo na kimalizio
- Mhusika ajipate katika hali ya huzuni. Mkasa k.m. wa moto kuzuka na kuichoma nyumba yake – likaonekana jivu tu palipokuwa nyumba yake
- Lazima mtahiniwa amalizie maneno ya kimalizio
- Anayepunguza au kupunguza maneno hadi manne ya kimalizio aondolewe maki 2m baada ya kutuzwa.
- Anayekosa sehemu ya kimalizio aondolewe maki 4mk baada ya kutuzwa.

44. Jitihada haiondoi kuduru

Maana: Bidii za mja haziwezi kubadilisha majaliwa au mpango wa Mungu.

Matumizi: Hutumiwa kuwatia moyo na kuwahimiza watu ambao huenda bidii wanazotia katika shughuli zao zisifanikiwe kuwapa wanachotarajia. Wanachopata ni kile Mungu aliwapangaia.

- Mwanafunzi atunge kisa/visa kadhaa vinavyolenga mada ya methali
- Insha ionyoshe ukomavu wa mtiririko kilugha na kimsamiati
- Mtahiniwa ashughulikie sehemu zote mbili za methali.
- Tanbihi: Anayeshughulikia sehemu moja atakuwa amepotoka

45. **<u>MADHARA YA RUNUNU</u>**

(i) Kuchangia kuongezeka kwa visa vya ajali barabarani
(ii) Kuchangia katika kuzoroteka kwa maadili ya jamii/zina filamu potofu.
(iii) Visa vingi vya uhalifu vimefanikiwa kupitia rununu
(iv) Familia/ndoa zimevunjika – kukosana kutokana na rununu.
(v) Wanafunzi wameshindwa kujimudu kilugha kwa sababu ya rununu – wamezoea lugha ya mkato na isiyo sahihi kisarufi na msamiati.
(vi) Zinaathiri mbegu za uzazi iwapo zinawekwa kwenye mfuko wa nguo kwa muda mrefu.
(vii) Ni ghali kutumia kwa vile huhitaji kununua kadi ili kuwasiliana

**<u>FAIDA YA RUNUNU</u>**

(i) Kuwezesha kufanikiwa kwa mawasiliano wakati wowote.
(ii) Husaidia katika kuweka ujumbe (siri muhimu)
(iii) Ni nyepesi / hubebeka kwa urahisi

46. - Ni insha ya kubuni
- Mwanafunzi azingatie sehemu zote k.m. utangulizi, mwili na hitimisho
- Mtahiniwa atunge kisa kinachomalizia kifungu kilichotolewa

Tanbihi :- Mwanafunzi ambaye atashindwa kumaliza insha na kimalizio hiki achukuliwe amejitungia swali na atuzwe D- (01-02)

47. Hili ni swali la kutoa hoja na kuzifafanua

Baadhi ya hoja:

- Masomo kuimarishwa
- Kubuni nafasi nyingi za ajira
- Serikali iimarishe sera k.v kazi kwa vijana
- Riba ya mikopo ipunguzwe
- Mashauri kupitia kwa mikutano ya hadhara na mabaraza kuhusu kukinga ugonjwa wa ukimwi – ukimwi husababisha utegemezi mkubwa na hivyo umaskini
- Watu kuhimizwa kushiriki kazi, wasizembee
- Usambazaji wa nguvu za umeme katika sehemu za mashambani
- Kilimo kipewe kipaumbele

48. Samaki mkunje angali mbichi

Hili ni swali la methali

Mtahiniwa aweza kufafanua maana na matumizi (si lazima)

Maana: Jambo linapoharibika lirekebishwe mapema kabla halijakuwa gumu kulirekebisha. Rekebisha jambo likiwa bado laweza kurekebika. Likiachwa likitiri hufikia kiwango kisichoweza kurekebishwa

Mtahiniwa atunge kisa/ visa vinavyoonyesha ukweli wa methali hii

Aweza kuchukua mtazamo wa:

i. Hali iliyoharibika na hatua za haraka kuchukuliwa na hivyo hali nzuri kurejeshwa
ii. Hali Fulani kuonyeshwa kuharibika na kuachwa hadi ikawa vigumu kuirekebisha

Kisa kinachobuniwa kiweze kuoana na moja kwa moja na methali.

Kisa kikikosa kuhusiana na methali mtahiniwa achukuliwe kuwa amepotoka na kuingizwa katika kiwango cha D (03)

Ikiwa mtahini hatatunga kisa achukuliwe kuwa hajajibu swali na kuwekwa katika kiwango cha D (02)

49. Hili ni swali la mdokezo

Mtahiniwa amepewa kianzio cha insha

Lazima ayatumie maneno yale yote mwanzo wa insha

Kisa kionyeshe kwanini siku hiyo ilisubiriwa kwa hamu; ilikuwa na umuhimu na gani?

Mtahiniwa adhihirishe bayana tukio/ shughuli/ jambo muhimu ambalo lingetokea siku hiyo

Atumie nafsi ya kwanza katika masimulizi yale.

## Karatasi ya pili 102/2

## **Ufahamu**

1. MAHOJIANO
Mtindo – kichwa
Mada
Muundo wa tamthilia huzingatiwa
Alama za uakifishaji ziziznngatiwe ila alama za usemi
Mahojiano yapokezanwe
Lugha rasmi itumike
Mahojiano yasipite mpaka
Mwanafunzi ajieleze kulingana na;
    - Maelezo ya kibinafsi
    - Elimu
    - Tajriba ya kazi
    - Changamoto ya kazi

2.
a) Mashaka ya kilimo cha mahindi.
b) Shilingi elfu saba na mia tatu.
c) i) Tisho la korogo na vidiri kufukua mbegu.
   ii) Kiangazi.
   iii) Mvua ya barafu.
   iv) Gharama kubwa.
d) i) Haikua vizuri kufurahia faida kabla kuuza mahindi.
   ii) Mungu anao uwezo wa kuleta barafu na kuangalia kustawisha mimea.
e) i) Kiwango cha chini cha mvua.
   ii) Kushuka kwa bei
f) Mahindi aliyodhani yameangamizwa na kiangazi au barafu yalinawiri tena.
g) i) Malipo ya kustaafu.
   ii) Wataalamu wa kilimo.

3. (a) – malezi
  - Wajibu wa wazazi katika malezi
  - Jawabu lolote linalogusia juu ya malezi ( 1x1=al. 1)
(b) (i) – Baba kuona kuwa wajibu wake ni kulea watoto wa kiume tu
  (ii) – Watoto wa kiume kuonyesha kuwa wao ni tofauti na watoto wa kike (al.2)
(c) Kwa kuhofia kuwa stamfunza tabia za kike (hoja 1x2=al. 2)
(d) (i) Palikuwa na ugawaji wa kazi ya malezi
  (ii) Watoto walifunzwa sifa kama vile uvumilivu, bidii , utii n.k.
  (iii) Watoto wa kike walifunzwa upishi, ukulima , usafi n.k. (hoja 2x1=al. 2)
(e) Palipotokea jambo ambalo kwa kulipima <u>mama</u> aliona linampita kimo, alimwita <u>baba</u> kuingilia naye alimwagiza <u>dadake</u> aje atoe suluhisho. (3x1=al. 3)

(f) Sifa- (i) Ushujaa
  (ii) uvumilivu (1x2=al.2)
(g) (i) Chanzo cha chemichemi – kitovu cha maisha/asili
  (ii) Akishachuchuka – ongeza kimo /kua
  (iii) Hulka – tabia/mwenendo/sifa (3x1= al. 3)

4. (a) – Sera ya elimu na athari zake
  -Sera ya kusimamia elimu iwepo

-Mfumo hasi wa elimu
-Masomo ya ziada
*Mada ilenge Elimu ;maneno yasizidi 6

(b) -Ina dosari/dosari
-Haiwapi wanafunzi muda wa kutosha wa kula,kucheza,kupumzika na hata kuchunguza afya na usalama wao

(c) -Watoto kukosa maadili mema `
-Watoto kukosa furaha na kuchanganyikiwa akili .
-Watoto kukosa nafasi ya kucheza na kutangamana hivyo kuathiri viungo vya miili yao kama moyo,mapafu na akili.
-Watoto kuwa wategemezi wasioweza kujipangia na kutekeleza mambo kivyao.
-Wazazi kutotekeleza majukumu yao ya kuwalea na kuwaelekeza watoto kwani mfumo huu huwaondolea mzigo wa malezi na gharama ya kuwaajiri walezi.

(d) -Wanapaswa kutekeleza majukumu yao ya kuwalea na kuwaelekeza wanao jinsi wanavyotaka wawe.
-Wawashinikize wanao wahudhurie shule maana kutawafanya wawe wategemezi wasioweza kujipangia na kutekeleza mambo kivyao.

(e) (i)Tashhisi-kufukuza ratiba.
(ii )Msemo –Wakiunga mkono
-Kupiga marufuku
(iii)Takriri –Kazi nzito nzito 2*2

(f) (i) Huwindwa kitandani
-Kuondolewa kitandani/usingizini bila ana yeondolewa kupenda
-Kulazimishwa kuamka
ii) Maadili- Tabia njema /matendo mema
iii) Kuwashinikiza - Kuwalazimisha /kuwashurutisha
iv) Wakembe-Wadogo/wachanga

5. 1. Wizi wa wa mali ya umma

- Vyeo na madaraka kutolewa hivi hivi tu
- Uuzaji wa stakabadhi za serikali
- Kuiba madawa
- Kuhonga ili kupata nafasi za kusoma
- Kuhonga au kutumia undugu ili kupata kazi
- Kutowajibika kikazi
- Kuiba madawa

2. - Kufilisisha serikali
- Kunyima wagonjwa matibabu
- Kuzorotesha maendeleo na huduma muhimu
- Kuelimika watu wasiohitimu na kuacha walio werevu
- Kupandisha vyeo watu wasiostahili
- Kazi kufanywa vibaya bila uajibikaji

3. - Kuunda tume na kamati za kuchunguza visa vya ufisadi
- Kurudisha mali iliyoibiwa
- Kuwashtaki wahalifu

4. - Uhaba wa kazi
- Uozo wa maadhili katika jamii

- Kuongezeka kwa umaskini
- Tamaa ya anasa na starehe
- Uongozi mbaya wa kitaifa
- Kukosa huruma na uajibikaji
- Kukosa uzalendo

5. Hongo/ kuzunguka mbuyu/ chai/kadhongo
6. Kazi walizopewa √
   a) Ufunuo wa siri ya jambo la aibu√
   b) Kuenea kwa jambo au habari√
   c) Ona wivu√
   d) Waliodhuriwa/ walioumizwa√
      Umeshikilia √

6. (a) Ufisadi (al.1 x 1=al.)
   (b) (i) Ajali za barabarani zinasababishwa na kuendesha gari kwa kasi sana
   (ii) Kung'olewa kwa vidhibiti mwendo kinyume na masharti ya uchukuzu na mawasiliano.
   (iii) Kuwepo kwa magari mabovu barabarani ambayo hayakutimiza masharti ya ukaguzi.
   (iv) Ufisadi wa maafisa wa usalama
   (v) Barabara mbovu zenye mashimo
   (vi) Matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa madereva wa malori na matrela *EZ*
   (c) (i) Wananchi wafahamishwe ya kwamba wana jukumu la kuwaeleza walinda usalalam endapo gari linapelekwa kwa kasi kupita kiasi.
   (ii) Wananchi waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo yamejaa kupita kiasi
   (d) (i) Kuwekwa kwa vidhibiti mwendo kwenye magari ya abiria
   (ii) Kuwachukulia hatua wale wanaotoa na kuchukua hongo
   (iii) Kurekebisha baadhi ya barabara mbovu
   (iv) Kuwekwa kwa mikanda ya usalama kwenye magari
   (e) (i) Kung'olewa kwa vidhibiti mwendo
   (ii) Kutokuweko kwa mikanda ya usalama
   (iii) Gari kwenda kwa kasi zaidi kutokana na kurekebishwa kwa vidhibiti mwendo ( 2 x 1)
   (f) (i) Shida ambayo imedumu muda mrefu bila suluhisho kuliko kiwango kilichokubaliwa
   (ii) Mashimo yaliyoachwa baada ya madini kutolewa
   (iii) Vifaa vya gari kwenda kwa kasi kuliko kiwango kilichokubaliwa
   (iv) Urekebishaji
   (v) Kuchukua au kutoa mlungula/rushwa
   (vi) Tia hamu ya kufanya jambo (6 x ½ =al. 3 )

7. a) -Ubakaji wa watoto wa kike
   - Kupigwa kwa wanawake na waume zao
   - Kuchomwa kwa wanawake na waume zao
   - Hutukanwa na kubezwa anapojiunga na siasa
   - Huchukuliwa kuwa kinyago cha mzaha na wanavitimbi/ waigizaji

   b) - Hutekeleza wajibu kama mama – kulea familia/ kutayarisha chakula
   - Hufanya kazi ya ofisi ambapo anakabiliwa na migogoro mingi ya kusuluhisha
   - Hurejea nyumbani kutayarisha chajio, kushughulikia kazi za shule za watoto na kuchangamsha familia3x1= 3

   c) - Kulinda mazingira
   - Ongezeko kubwa la uzalishaji wa chakula
   - Kutoa ajira ya kibinafsi
   - Kuongezeka kwa pato la ndani

d) Wawe watu wa vitendo sio kupayuka
e) Kinyago - sanamu
Mabeza – madharau
(f) i) Mbalagha – Utashangaa mja huyu atayabeba vipi?
ii) Uhuishi – mara watupwe mabezo ya kila aina

8. i) Umakinifu wa watu binafsi, vyombo vya habari, sera na utayarifu wa serikali katika kugharamia shughuli hii (4x1=ala.4)
ii) Si lugha dhaifu. Hii ni kwa sababu hakuna lugha hata moja ulimwenguni inayoweza kujitisheleza bila kukopa. Hivyo, Kiswahili kinapokopa, hali hiyo haipaswi kuchukuliwa kuwa ni lugha dhaifu (ala 3)
iii) - Istilahi zinazokopwa zinafaa zichukuliwe zilivyo katika umbo lao asili na kufanyiwa marekebisho machache tu
- pale ambapo istlahi ya asili haiwezi kukopwa, lugha husika ijaribu kubuni msamiati ufaao
- kiswahili kisikope kiasi cha ku[poteza upekee wake
- uundaji wa istahili uzingatie mafologia ya kawaida ya lugha (3x1=al 3)

iv) Uundaji wa istilahi katika Kiswahili n.k. ala 10
v) a) Dhana – Fikira inayoeleza ambo fulani
b) Takriban – Neno linaloonyesha ukaribiano wa vitu kwa hali au idadi
c) Istilahi – Neno linalowakilisha dhana Fulani katika uwanja maalum wa maarifa k.v. siasa, uchumi au hisabati
d) mafologia – Tawi la isimu linaloshughulikia uchambuzi wa maneno (4x1=al.4)

9. (a) - Haki za wanawake
- Taasubi ya kiume
(b -Mwanamke kuumbwa kutokana na ubavu tu wa mwanaume
(c) - Ya mawazo akilini, kujinyenyekeza na kujidunisha mbele ya mwanamume
- Ni mwiko kudhihirisha tabia za kimabavu
- Hutarajiwa kujilinda heshima kimwili kwa kuhifadhi ubikira wake
- Mahali pake ni jikoni, hasikiki bali aonekanalo
(d) – Kuhifadhi ubikira mpaka aolewe
- Mwanamke huolewa haoi
- Ndiye mkosaji kila mara
- Nyumbani aonekana tu, asisikike
(e) - Wana uhuru wa kutembea na wanawake ovyo
-Wana uhuru wa kujitetea na kupigana
- Mwanamume ndiye huoa
- Yeye hahesabiwi makosa ila mkewe tu kila wakati hulaumiwa kutuze ufahamu

1. Ondoa nusu moja ( ½ ) kwa kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza.
Usiondoe zaidi ya nusu za alama alizotunwa mwanafunzi
Tahajia
Ondoa nusu alama (½) kwa kila kosa la hijai (h) litokeapo mara ya kwanza kwa swali la ufahamu hadi makosa 6 (yaani alama 3)

(f) – Twawashtumu wengine ilhali sisi twabaguana kimaumbile
- Akasemwa vibaya mtaani
- Hupigwa /hushutumiwa
- Wajitolee

10. Ufahamu
- Mwanafunzi aliyeambukizwa Ukimwi
- Ukimwi vyoni
- Hofu ya kuambukizwa Ukimwi (yeyote moja =al. 1)

2. Kuwaambukiza wanafunzi wenzake mia moja na ishirini na wanne virusi vya Ukimwi al.2

3. Aliambukizwa Ukimwi na mwanfunzi wa chuo hicho ambaye alikuwa akifanya majaribio

ya ualimu shuleni mwao

4. _ Apewe adhabu ya kifo
- Atiwe nguvuni maramoja
- Tayari amekiri kosa lake na hivyo kumfanya awe na hatia (zozote mbili al. 4)

5. Maadili hayapo tena katika vyuo vikuu nchini

6. - Kupoteza tumaini kabisa/kuwa katika taharuki kuu
- Daima dawamu/ kwa vyovyote vile
- Kutumia watu wengine kuwatia adhabu kwa kosa lake mwenyewe (1x3=al.3)

11. 1. Nyimbo za jadi zilizokuwa zikiimbwana Manju, Wangoi au waimbaji stadi wa tangu walipojumuika katika matukio na hafla mbalimbali kama za jando, arusi, matanga, noma n ashangwe zao za maishani (al 2)

2. - Mawaidha√1
- Taathira au jadhba kutokana na sauti tamu ya manju√1
- Burudani√1 (al 3)

3. - Uzito wa mawazo maadilifu √1
- Mizani ya sauti ya manju kulingana na lahami, pumzi zake pamoja na madoido katika uimbaji √

4. - Lugha √1
- Umbo √1

5. Haijaenea na kupamba moto

6. - Kongamano – mjadala juu ya jambo fulani unaofanywa na mkusanyiko wa watu √1
- Jadhba – Hisia au taathira ya mawazo inayomfanya mtu ajisahau nafsi yake √1
- Farka – tofauti √1
- Awali – Asili, mwanzo √1 (tazama makosa ya hijai/ sarufi – adhibu ½ )

12. (a) Madhila ya Chamkosi/masaibu ya Chamkosi/shida za Chamkosi
(b) – Husabasiha kifo
- Hufuja mali katika kutibu/umaskini
- Kuacha mayatima
- Kuporomoka kwa ndoa/familia (zozote 2x1=al. 2)
(c) Uasherati; madharau/mapuuza kwa ushauri (3x1 = al. 3)
(d) (i)

| Baba | Mama |
|---|---|
| - Alikuwa baba dume/katili<br>- Mreda/sherati/mkware | - Mshauri mwema<br>- Mpole kwa bwanake<br>- Mtiifu kwa bwanake<br>- Mlezi mwema |

(e) Alikata shauri kusomea taaluma ya uelekezi na ushauri ili kusaidia wengine
Maoni; - Uamuzi huu ulikuwa mzuri kwani ungezuia madhara zaidi. ( Dhana alama 2 maoni al. 1)
(f) (i) Kutumbulia macho – kuangalia bila la kufanya/kukodoa macho.
(ii) Ameumwa na mbuzi – kuugua ugonjwa wa Ukimwi

13 .
i. Uhai unavyoanza
ii. Hatua ya kwanza katika uhai wa binadamu
iii. Kioja cha mwanzo wa uhai n.k.

2. Ana maana ya kujamiana ambapo mamba hutungwa
3. Imani inayokita mizizi ni kwamba mungu huwatumia mume na mke kumwanzishia binadamu maisha ya duniani

4. Kromosomu humkadiria inadamu

i. Rangi ya ngozi yake
ii. Aina ya nywele
iii. Jinsia- kama atakuwa mume au mke
iv. Kiasi cha werevu
v. Aina ya damu
vi. Utu wake katika maisha ya usoni

5. Kwa sababu elimu kutoka kwa jamii na mazingara, pekee haifai kitu, lazima ijenge juu ya msingi wa kromosomu

6.- Kunyonya au kutegemea
-Mamlaka
Hana uhusiano na mama yake

14. (a) Uhusiano wa Ukimwi na kifua kikuu
(b) Kuchipuka kwa viini vya ukimwi kulikosababisha kudhoofika kwa kinga mwili
(c) Hupunguza uwezo wa mwili wa mgonjwa kupigana na vijidudu vya maambukizi magonjwa, kutodhibiti maambukizi ya magonjwa mbalimbali
- Huwa na nafasi ya kinga mwilini
(d) Katika baadhi ya nchi maambukizi ya kifua kikuu hufanyika mapema katika umri mchanga maishani. Hivyo basi kutokea kwa ugonjwa huu mara nyingi husababishwa kuwepo kwa ukimwi
(e) Ukosefu wa kinga mwilini
(f) Mmoja kati ya watu wawili au watu wenye virusi vya ukimwi hupata kifua kikuu
- Asilimia 50-60 ya wagonjwa wa kifua kikuu wameambukizwa ukimwi
(g) Maambukizi ya kifua kikuu hufanyika mapema katika umri mchanga
- Maambukizi mara nyingi hayasababishi ugonjwa huu kwa kuwa kinga za mwili zasitiri maambukizi haya.
- Baadaye viini vyaweza kuwa hai tena na kusababisha ugonjwa
(h) (i) Kukinga
(ii) Kipindi cha miaka kumi
(iii) Shughuli/jambo la muhimu/haraka
(iv) Chembe chembe zinazosababisha ukimwi

15. a)– Elimu na teknologia
- Umuhimu wa elimu ya teknolojia
b) Hali ya kuhuzunisha ni taasisi ya elimu kukosa kutoa wafanyakazi wenye ujuzi tosha, hasa wa teknologia za kisasa kama kutumia kompyuta kutenda kazi mbalimbali
c) - Akipata atajiunga na chuo kikuu ambako ataendeleza ujuzi huo wake
- Akikosa nafasi katika chuo kikuu aweza kuendelea na elimu kupitia elimu mtandao
- Mwanafunzi aweza kufanya utafiti wa kina kupitia intaneti

d) Vizingiti

- Mitambo na vifaa vya kompyuta ni ghali
- Kuna ukosefu wa walimu waliohitimu wa somo la kompyuta katika shule nyingi
- Tatizo la ukosefu wa nguvu za umeme katika maeneo ya mashambani
- Wanafunzi na wazazi kutoka vijijini huona somo la kompyuta kama gumu na linalofaa kwa wanafunzi wa mjini pekee

e) Manufaa ya kompyuta kwa walimu
Kufunza madarasa kadhaa kwa kipindi kimoja bila kuhudhuria darasani
Kufanya utafiti wa hali ya juu kupitia mtandao wa intaneti

f) Kompyuta- tarakilishi
Intaneti- Mtandao wa mawasiliano wa tarakilishi

# Ufupisho

1. (a)

i. Ukosefu wa elimu
ii. Kulaza damu/ uzembe
iii. Ufuaji
iv. Umaskini pia huletwa na majanga ya kimaumbile Kama vile:-
    - Mitetemeko ya ardhi
    - Maradhi hatari
    - Moto
    - Ukame
    - Mafuriko

b)
- Kupunguza mwanya mkubwa uliopo kati ya matajiri na maskini
- Kupandisha viwango vya kodi inayotozwa wenye mshahara mnono na wafanya biashara wenye pato kubwa
- Huduma za burudani kutozwa kodi ya kiwango cha juu
- Elimu tekelezi isisitizwe
- Kupunguza ushuru kwa bidhaa zinazoagizwa
- Kuwapa wahitaji mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo
- Kusambaza huduma za umeme na maji sehemu za mashambani

Utiririko

TAZAMA

i. Kwa kila kosa la sarufi mtahiniwa huadhibiwa ½ alama hadi jumla ya makosa 10
ii. Kwa kila kosa la tahajia mtahiniwa huadhibiwa ½ alama hadi jumla ya makosa 6
iii. Kwa kila ziada ya maneno kumi, mtahiniwa huadhibiwa alama 1 na kwa kila mengine matano --huadhibiwa ½ alama

2. a) - Kuzuia uharibifu

Kuhakikisha meno yetu ni mazuri

Kuhakikisha meno yetu yanadumu na kuendelea kutufaidi

- Kuondoa mabaki ya chakula ambayo ni chanzo cha viini zozote 4x1=4

Mtiririko 1x1=1

b) Tunapokula meno yetu huvunja chakula
Vimegenye hukifanyia chakula kazi
Meno ya binadamu ni ya meno nne
Kazi ya meno ni kutafuna na kusaga chakula
Idadi ya meno ya mtu mzima ni 32
Ni vyema kudumisha afya nzuri ya meno
Lazima tuyapige mswaki meno ili koundoa mabaki ya chakula
Tuhakikishe kuwa hatuaharibu ufizi wa meno
Afya ya meno ni muhimu ili kuhakikisha kuwa meno yetu yanadumu na kuendelea kutufaidi katika uhai wetu zozote 8x1=8 Mtiririko 2=2 Jumla =10

3. Ufupisho

a) Inawezesha nchi kupata bidhaa ambazo haitengenezi

- Husaidia kuwepo na uhusiano kati ya nchi mbalimbali
- Nchi hupata bidhaa kwa bei rahisi kuliko ambavyo ingekuwa kama zingetengenezwa kwao
- Husaidia wakati nchi imekumbwa na dharura au majanga kwani itasaidiwa na nchi nyingine
- Huchochea upatikanaji wa nafasi za kazi kwa wengi
- Nchi inawezesha kupata pesa za kigeni na kuuza bigdhaa za ziada (6x1=al.6)

b) Kuna matatizo yanayozikumbuka nchi za kiafrika katika biashara hii

- Hutatiza viwanda vichanga katika nchi zinazoedelea kwa ushindani usio sawa huku nchi zilizoendelea zikitumia biashara hii ‘kutupa’ bidhaa za hali ya chini
- Nchi zinaweka mikakati ya kulinda viwanda vichanga
- Kuwekwa kwa ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa

- Kupunguzia viwango vyao ushuru
- Kuvipa viwanda vyao mikopo
- Kuhakikisha usafirishaji nafuu wa bidhaa kwa viwanda vyao
- Kuweka viwango vya bidhaaa zinazoweza kuagizwa kutoka nje kwa kipindi Fulani (6x1=ala.6)

4. (a) -Punda na ngamia wanaweza kwenda mwendo mrefu bila kunywa maji.
- Ngamia naye ana kwato nzuri zinazomwezesha kusafiri kwa urahisi jangwani
- Ngamia anaweza kwenda mwendo mrefu bila chakula

(b) –Zamani watu walisafiri kwa miguu, watu hao pia walitumia wanyama kusafiria.
- Kinyume na ilivyokuwa zamani, usafiri kwa motokaa, gari la moshi na hata ndege.
- Biandamu leo amepiga hatua kubwa kwani anaweza kuruka kwa ndege na kwenda anga za mbali (3x2=al.6) (utiririko al.2)

5. a)
- Inapasa vijana wa Kenya kufanya kazi kwa bidii ili kupata ufanisi na kuinua nchi yetu
- Sharti tutilie maanani elimu ya vijana, watu wazima, kilimo uchumi na amani katika nchi yetu
- Bila elimu itakuwa vigumu kutekeleza mipango ya maendeleo
- Lazima tuzidishe mazao mashambani kwani idadi ya watu inaongezeka
- Pia tujishughulishe na biashara kwani wengi wana mawazo kuwa lazima kila mtu aajiriwe
- Tujitahidi kuweka uchumi kwa mikono ya wananchi badala ya kuwaachia wageni

8X1 = 8 utiririko 2

b) Lazima vijana wayashughulikie na kutatua matatizo yanchi.
- Vijana wawe na nidhamu shuleni na nyumbani

Wawe na ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendelo
- Wachague viongozi watakaoleta ufanisi , sio wale wanaotoka kwa nasaba kubwa au ya utajiri 4x1 = 4 utiririko 1

a) 08
b) 04
<u>03</u>

6. A. Binadamu ni sawa kimaumbile ukilinganisha na wanyama
Binadamu hutofautiana kwa fikra, tabia kimo, uwezo na mahitaji.
Wakufunzi na wazazi wawape wanao widhaa mapema ili wachague kazi watakayoifanya
Wazazi huwasomesha watoto ili wajitafutie kazi itakayowapa pesa za shughuli
Tangu uhuru watu wa wakiajiriwa kulingna na viwango vya masomo
Kazi zilikuwepo wakati wa uhuru ziliwachwa na wageni walioacha nchini
Siku hizi wanafunzi wanaokomea viwango vya chini hadi kidato cha nne hawapati kazi au kupata za madarakawanaotawasiri masomoni wakifuata taaluma fulani ndiyo hupata kazi

Hoja zozote 9x1=al. 9) Mtiriko (al. 2)

B.
- Serikali imewatusilia wananchi kuwa wakati wa kuania kazi za utanashati umekamilika
- Huu ni wakati wa kufanya kazi yoyote kwani uchaguzi wa kazi kimasomo ni dhana ya kibwanyenye ambayo haipo.
- Usemapo kuna kazi nzuri au mbaya unaanzisha maswali mengi
- Kuna kazi ya kuajiriwa na ya kuajiri
- Ijapo kazi ya kujiajiri ni ngumu na ina matatizo mwanzoni, pato lake ni kubwa, ukishapata msingi imara.
- Ujasiri wahitajika ili kujenga msingi imara
- Ardhi ni thawabu tunu kwani matumizi mazuri ya ardhi yataondoa umaskini

(Kila hoja alama 1x7 = al.7 Mtiririko ala. 2)
Namna ya kutuzwa
makosa ya sarufi (s)

Ondoa nusu alama (½) kwa kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza hadi makosa 10 yaani jumla alama 5

Makosa ya hijai (h)

Ondoa nusus alama (½) kwa kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza, hadi makosa 6 yaani alama 3

Idadi ya maneno Akiandika chiini ya idadi iliyopewa amejiadhibu mwenyewe kwa hoja chache

Akizidisha kwa maneno kumi (10) ya mwanzo uondolewe alama 1 (moja), kila matano yanayofuatana aondolewe alama moja moja (1).

Akiorodhesha tu hoja asipewe alamaza mtiririko

7. (a) – Ni nyenzo mwafaka ya kufundishia.
- Huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani kote
- Huauni katika kukuza stadi ya kujifundisha au kujielimisha
- Hutumbuiza na kuchangamsha
- Hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii

(b) – Hujumuisha ujumbe usio na maadili kama matumizi ya mabavu, ngono za kiholela, lugha chafu .
-Kuwafanya vijana kuingilia ulevi na afyuni na kuvaa vibaya
-Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia.
-Mawasiliano yakikosa, familia hutengana.
-Haichangii uhusiano bora
-Hukuza ubinafsi
-Huendeleza hulka ya kuhadaa na mengine mabaya

8. a) Vyakula vyenye vitamini B, vyenye amino asidi na vile vyenye madini ya chuma kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
- Vyakula vyenye glukosi husaidia kuendesha viungu vya mwili na ubongo. Lakini mtu anatakiwa kutahadhari asizidishe kiwango cha sukari mwilini, kwani kinaweza kuthiri uwezo huu.
- Ni muhimi kutotumia vileo na vyakula vyenye nikotini kwani huzorotesha uwezo wa kukumbuka (Kila hoja na maelezo al. 2 na mbili za mtiririko).

b) Ni muhimu kuepuka woga na kuvurugika akili kulikozidi haya huathiri uwezo wa kukumbuka. Halikadhalika, lazima mtu awe na ratiba kuonyesha viungo. Hili ni kwa kuwa unyooshaji wa viungo huimarisha ubongo pamoja na uwezo huu. Uimarishaji wa uweza huu ni muhimu kwa maendeleo ya jamii na unahitaji mchango wa kila mmoja kila wakati.

9. (a) – Ndio wakati mtu anaulia peke yake
-Anajisakaknakijiuliza mema mangapi amyatenda siku hiyo
- Maovu mangapi amayatenda
_ Iwapo siku hiyo ilikuwa ya manufaa au la(Hoja 4x1=al. 4) – (al. 1 ya utiririko)

(b) - Hukusanyika katika makundi na kucheza kamari
- Hukusanyika kwa madhumuni ya kupiga gumzo
- Wengine huenda vilabuni kujiliwaza na kujiburudisha kwa vileso (hoja 3x2=al.6)

c) – Wazazi watoe maongozi bora
- Wawe vielelezo bora kwa wana wao (hoja 2 x 1= al. 2) (al. 1 aya utiririko)

M
a = 4
b = 6
c = 2
ut. = 3
15

10. Mwongozo wa kusahihsisha muhtasari

(a)Ili kujiondoa kutoka umaskini ni lazima tuthamini kilimo/tukipe kilimo umuhimu
- Mamilioni ya wakenya/zaidi ya wakenya milioni kumi wanaweza kufa njaa/kwa sababu ya njaa

- Sababu ya njaa ni kupuuzwa kwa kilimo
- Wakenya asilimia sabini na tano hutegemea kilimo kwa chakula na fedha
- Kilimo hutoa nafasi za kazi
- Huletea serikali robo ya mapato yake (kila hoja al. 1 x 6 = 6)

. (b) Serikali za Afrika na wanaoopanga masuala ya uchumi kujitahidi ili kumaliza njaa na umaskini

- Wafunze wakulima wa mashamba madogo kukuza na kuzalisha matunda na mboga na kufuga wanyama na ndege
- Kuanzisha nafasi za kazi
- Serikali kufadhili kilimo
- Kupunguza gharama za pembejeo
- Kuweka sera zinazodhibiti kilimo
- Kuongeza sehemu ya bajeti ya kilimo
- Tusipofanya hivyo tatuzidi kuomba misaada kutoka mataifa (al 6- kila hoja moja 1x6=al 6)

M
a - 06
b - 06
ut - 03

- Makosa ya sarufi; Kila kosa linapojitokeza, huadhibiwa kwa kuondoa ½ alama hadi makosa 6 x ½ = alama 3. Mtahiniwa akipata 0 makosa ya sarufi huondolewa.
- Makosa ya hijai/tahajia huondolewa hadi makosa 6 x ½ = ala. 03
- Mtahiniwa akizidisha kwa maneno 10 aondolewe alama 1, baadaye akizidisha kwa 5 ondoa ½
- Mwanafunzi asipotiririsha kazi yake asituzwe alama za utiririko hasa akiorodhesha hoja au aandike vistari kabla ya hoja, atuzwe 0 katika sehemu ya utiririko.

11 . (i)Viwanda hutoa moshi unaosambaa na kuchafuka hewa.
(ii)Uchafu unaotupwa ovyo huhatarisha afya ya binadamu
(iii)Maji machafu huchafua maji mitoni,maziwani na baharini
(iv)Wanyama wengi huharibu misitu,nyasi na vichaka
(v)Barabara zaidi zinapojengwa miti hukatwa zinapopitia
(vi)Magari hutoa moshi unaoharibuhewa
(vii) Ongezeko la watu huharibu misitu ya asili kwa kujiongezea ardhi ya makaazi

(b) (i) Kukomesha ujenzi wa viwanda mijini penye watu wengi
(ii) Takataka na maji taka kutupwa bila kudhuru afya ya binadamu
(iii)Upangaji wa uzazi usisitizwe kuzuia ongezeko la watu
(iv) Raia waelimishwe kuhusu madhara ya uharibifu wa mazingira
(v)Wahimizwe kupanda miti mingi utiririko alalma 3 jumla (alama 5)

12. (i) Hoja muhimu
- Vijana ni waasi na hawawajibiki vyovyote
- Vijana wamependekezwa na wana ubinafsi sana
- Vijana wamekataa uongozi wa wazee na wamepuuza imani na itikadi zao. Mfano; wanaoweka nywele Kama za wendawazimu.
- Wanawaona vijana kama wavivu na wasio na nidhamu
- Vijana hupenda kuzurura ovyo ovyo.
- Vijana wanapenda anasa na raha za dunia

.- Hoja muhimu
- Huwafuati utamaduni wa kutii wazazi wao
- Hawafanyi kazi na kuonyesha nidhamu
- Vijana hawathamini sherehe za jadi kama kutoa kafara
- Hawajinasibishi na watu na koo au tamaduni zao wala ngoma zao badala yake wanapenda kuhudhuria

dansi na sinema za kileo pamoja na karamu.

13. a) Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo shughuli zote za kiuchumi ghairi zile za lazima <u>kwa serikali</u> huwa huria kwa <u>watu binafsi</u>

b)

i. Soko huru huwawezesha watu hatima yao
ii. Swala ibuka ni kule kuwekwa mipaka bainifu baina ya shughuli za kijekali na zile zinazoachwa huria kwa watu binafsi
iii. Haki za kuishi na kulindwa dhidi ya shambulizi haziwezi kuachiwa mtu binafsi
iv. Huduma za kimsingi za afya haziwezi kubinafsishwa
v. Huduma hizo zikiachwa huru zitaishia kuwa istihaki ya watu wa kipato cha juu
vi. Udhibiti wa serikali hutokea kuyalinda mazingira dhidi ya uchafuzi
vii. Pia udhibiti huo hutokea kulinda haki za watu binafsi

14 1.- Kutumikia taifa kwa moyo wetu wote
- Tuwe shupavu, wenye busara, adabu njema na ari ya kutenda kazi
- Ni muhimu kulinda, kutumika na kuendeleza taifa
- Inatupasa tuelewe ujamaa wetu na jinsi ya kupambana na ukoloni mamboleo
- Tutumie elimu kuelewa meme na mabaya maishani mwetu
- Tutambue usawa wa kibinadamu

2.
- Ni staha vijana wetu kukosa nidhamu
- Wasitumikie taifa kwa mioyo yao yote
- wasiwe shupavu na wenye busara na ari ya kutenda kazi
- Pasiwepo ujamaa na jinsi ya kupambana na ukoloni mamboleo
- Tusiweze kutambua usawa wa kibinadamu
- Pawepo na uongozi nbaya, kutokuwa na bidii, ushirikiano na kutofuata sheria katika uchaguzi wa viongozi (tazama makosa ya hijai/ sarufu. Adhibu ½ )

## Matumizi ya lugha

1.

a) Mtoto aliaye huchapwa
b) Wavulana watatu wanatoka darasani pole pole (hakuna kinyume cha nomino)
c) i)Kule ndiko alikoingia
ii) Pale ndipo alipoingia
iii) mle ndimo alimoingia
d) amewahi- kitenzi kisaidizi
Kupika
e) i) hali ya umaskini mkubwa
ii) Vumilia shida/ taabu
f) i) Funza
ii) Enea
g) i)Sentensi sahihi- mfano; mama anapika jikoni (kitenzi kimoja)
ii)Sentensi ambatano- mfano mama anapika jikoni na baba anasoma gazeti
iii) Sentensi changamano – mfano mwanafunzi aliyechelewa aliadhibiwa (vishazi viwili) tegemezi na huru)
h) S____ KN+KT
KN_____N+ V+V
V_________Huyu
V_________ Mzuri
KT________ T+E
T_________ Anafundisha

E__________ Darasani

i) i Mama alifanya kwa niaba ya mwanawe
ii) Mama alilima shamba ili mwana afaidike
j) "Ah huu ndio upuzi aliotuitia?" mmoja akaropoka
k) Anakula kifisi
Kitausi
Kinyama nk
l) "Mimi nimeonewa kwa kuwa sijashiriki ulevi kutoka mwaka jana".
Mshtakiwa alijitetea
m) TU- Nafsi ya kwanza uwingi (watendaji)
LI- Wakati uliopita
WA- Nafsi ya tatu uwingi (Watendewa)
LIM- Mzizi wa kitenzi
I- kauli ya kutendewa
a-Kiishio/ kimalizio
n) Mzizi wa mbaruti huu haukumponya mtu ambaye alikuwa na shida kama hii yako
o) i) vile vitauzwa
ii) Vitu vile vitauzwa
iii) Viti huuzwa vile meza huuzwa
p)
i. KU- kiambishi kanushi cha wakati uliopita
ii. KU- kurejesha nafsi ya pili umoja
iii. JI- binafsi yenye mwenyewe
iv. JI – uzoefu wa kutenda jambo
q) jibwa langu si kali sana

2. (a) (i) Chota - chovya (al.1)
(ii) Lewa – levya (al. 1)
(b) (i) King'ong'o – m, n, ny, ng' (yoyore 1x1 =al.1)
(ii) Kiyeyusho – y,w (yoyote 1x1=al.1)

(c) Kwa mfano:-
Kivumishi : Askari <u>shujaa</u> ametuzwa (1x1= al. 1)
Kielezi: Askari yule alipigana <u>kishujaa</u> (1x1=al. 1)
(Hakiki jibu la mwanafunzi)
(d) Vitenzi – tulkwisha, kutambua, alikuwa ndiye (hoja 4 x ½ = al. 2)
(e) Ma(ji) chinjio haya ualikarabatiwa kwa ma(ji) pesa mengi (al. 2)
(f) (i) Jambazi lililoiba linaishi dukkani (al. 1)
(ii) Jambazi linaloishi dukani ndilo liliiba (al.1)
(iii) Jambazi liliiba punde tu baada ya kutoka dukani (al.1)
(iv) Jambazi liliiba vitu kutoka kwenye duka (al. 1)
(g) (i) Uvichanganue (al. 1)
(ii) Kulizibua (al. 1)
(h) Wavu uliookatika ni wao (al. 1)
(i) –(i) Lengo /nia k.m. Nipe pesa nikanunue kitabu
- (ii) Kitendo cha pili (matokeo ya kitendo cha kwana k.m. Alianguka akaumia.
(k) "Harakisheni mrudi leo, la sivyo mtakosa tuzo" mama alisema
Mama alisema "Harakisheni mrudi leo, la sivyo mtakosa tuzo".
(l) "Sijaona kitabu kizuri kama "Mayai waziri wa Maradhi," Utaniazima siku ngapi?" Bashiri alimwuliza Rita.
(m) Mama anapika na baba akisoma gazeti. (al. 4)

| | |
|---|---|
| S ⟶ $S_1 + U + S_2$ | $S_2$ ⟶ KN + KT |

| | |
|---|---|
| S1 → KN + KT<br>KN → N<br>N → Mama<br>KT → T<br>T → anapika<br>U → na | KN → N<br>N → baba<br>KT → T+N<br>T → akisoma<br>N → gazeti |

(n) Hakiki jibu la mwanafunzi.
k.m. Ziada alimfagilia mama nyumba kwa ufagio
Nyumba – kipozi, mama-kitondo- ufagio – ala/kitumizi

(o) (i) Fa (mazoea) k.m. watu hufa kwa maradhi mbalimbali
(ii) La(kutendeka) k.m. Chakula hiki hulika upesi.
(iii) Pa(kutendea ) k.m Alinipea mtoto maziwa nilipochelewa kazini (kwa niaba yangu )

(p) – Wanafunzi waliofanya vyema – kishazi tegemezi
- Walituzwa jana- kishazi huru(al. 2)

(q) wa – nafsi
li – wakati
wa – nafsi (mtendewa)
pend – mzizi .shina
eze- kauli/kinyambuzi
a – kiishio 6x ½ = 3)

3. a) i) U- nafsi tegemezi
ii) hicho- Kiwakilishi kionyeshi
kutaja alama ½ maelezo alama ½

b) i) Sentensi iwe na maana bila ya, pasipo, ghairi ya n.k Mfano wanafunzi walisafiri mighairi ya shida
ii) Wala – sentensi ileta maana ya kulinganisha na kupinga. Mfano sitaenda kazini wala kuhudhuria mkutano

c) Chakula kinapikika vizuri

d) i) Hatujui alikotorokea
ii) Wangekuwa na pete, wangewapatia
Wasingekuwa na pete wasingewapatia

e) Tamina- Shamirisho kitondo
Kasri- Shamirisho kipozi
Kwa matofali- shamirisho ala/ kitunzi

f) S______S1+U+S2
S1_____KN1=KT1
KN1____ N1+V
N1_____Watoto
V______Wote
KT1____T+E
T_______Wameamka
E_______Mapema
U_______na
S2______KN2+KT2
KN2____N2
N2_____Wazazi
KT2_____T2
T2______Wanatayarisha
KN3____N3
N3_____Staftahi

g) Shuku- mshukukiwa/ kushuku/ ushukiwa
vumilia- uvumilivy/ mvumilivu/ kuvumilia
Shona- Mshono/ mshoni/ mshonaji/ ushonaji/ kushona
Lia- mlio/ kilio/ kulia

h) i) jinsi- Imetumika kuonyesha jinsi ya kutekeleza jambo
ii) Jinsi- Imetumiwa kuonyesha mwenendo

i) Uhodari- nomino dhaharia
Wanariadha- nomino ya kawaida
Kenya- nomino ya pekee

j) i) Choyo kama nomino
Mfano Uchoyo wa kocho ni wa kupita kiasi
ii) kama kivumishi
Mfano Mtoto mchoyo hapendwi na wenzake
iii) Kama kiwakilishi
Mfano Mchoyo aliyeninyima chakula ameshikwa na polisi
k) i) Mstari ________
Hutumika a) kutilia neon au fungu la maneno msisitizo
Mfano Ukienda dukani uninunulie <u>daftari la hesabu</u>
b) Kuonyesha anwani ya vitabu, vichwa vya habari au majina ya machapisho kama Mjarida
Mfano Tamthilia ya <u>kifo kisimani</u> imesifika
ii) Parandesi [ ]
a) Kufungia maneno yatoayo maelezo zaidi kuhusu maneno yanayotangulia
Mfano Alipoenda katika maabara [chumba cha sayansi] hakufuata maagizo ya mwalimu
b) kubainisha nambari au herufi katika orodha
Mfano [a] [b] [c]
c) kutoa maelezo na maelekezo kwa waigizaji katika mchezo wa kuigiza
Mfano Bokono: [Akiashiria kwa kidole] tukutane pale kwa haraka!
l) i) Fundi ameharibu saa
ii) umeonewa mgeni?
m) Kigari cha mzee Maritu kimekigonga kigombe cha jirani wake

4. Matumizi ya lugha
a) i) e – Irabu ya mbele – hutamkwa kutumia sehemu ya mbele ya ulimi
- Irabu ya midomo – hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa
ii) n – sauti ya ufizi
- Nazali
b) i) Kiimbo – Ni upandaji na ushukaji wa sauti unaofanyika wakati mtu anapozungumza
Shadda – Ni mkazo katika nenoau maneno
c) i) U – U – Nomino za dhaharia zitumiwe
ii) Pokomo/ Pakumu k.m Mahali humu ndimo alimoingia
d) Tubu
e) - Kudhihirisha vitenzi vya silabi moja – kula, kuja n.k
- Mwanzo wa vitenzi
- Wakati wa ukanusho k.m haku, hatuku……
- Kuonyesha mahali k.m kuliko na miti
- Kiwakilishi cha nafsi k.m anakuita
f) Mfano: Msichana yule anasoma barabara
g) Ng’ombe aliyeletwa juzi ameuzwa leo jioni

h) a) Mshangao

- Kuonyesha hisia
- Kuamrisha
- Kutahadharisha/ kuonya

b) Mshazari

- Katika uandishi wa kumbu 2
- Kuonyesha maneno Fulani yana maana sawa
- Kuonyesha 'au'

i) Mfano: majirani waliwiana radhi baada ya utesi wa siku nyingi
j) Kijdama cha kijigombe kile kimeuzwa
k) i) Dhamani – mwezi wa mwisho wa kusi (demani)
ii) Thamani – Gharama / ubora wa kitu/ bei
l) Tusingalikuwa na pesa tuingalinunua magari

m) Mchezaji – kipozi
mwenzake – kitondo
kwa mguu- ala
n) Sahihi – sentensi ya wazo moja/ kitenzi kimoja
Ambatani – sentensi mbili au zaidi zilizounganishwa
o) Ni- e- tamati
ta- awali a - ji-
p) Mwalimu alimwambia mwanafunzi kuwa wangeaza masshindano kesho yake/ siku itakayofuata
q) – Njia
- Vizuri/ mwafaka/ sawasawa
r) Mofimu huru
Mofimu tegemezi

5. a) (i) Mkwezi, ukweaji, mkweaji
(ii) Uhimarishaji, kuimarisha
b) (i) Muundo wa irabu pekee; mfano, a, e, i , o, u
(ii) Muundo wa konsonanti na irabu, mfano; pa, ma, to
(iii) Muundo wa konsonanti, konsonanti na irabu, mfano; kwa, cho, twa
(c) Mungu ndiye aliye na uwezo wa kuumba na kuumbua
(d) Meza zizi hizi ndizo zilizotumiwa kulia
(e) (i) chiwa
(ii) nywewa
(f) a nafsi ½
Ta wakati ½
Ku mtendwa ½
- Ajiri kiini/mzizi ½
(g Japo tu wafisaidi tunajua sheria.
h) (i) darasani – kielezi cha mahali
(ii) kisabuni – namna mfanano



j) /z/ hutamkiwa kwa ufizi
- ni sauti ghuna
/k/ - hutamkiwa kwa kaakaa gumu
- ni sauti hafifu

(k) – kuonyesha ukubwa
- Jia la kuingia ikulu limefungwa
- Kiambishi cha kurejelea mtenda
- Rehema anajitahidi sana.

(l) Vigaari vyote vilivyobakia vitauzwa na kizee kile chembamba (vitahiniwa 7-2;vitahiniwa

m) (i) Kila mwanafunzi alipewa andazi a yai moja.
(ii) Nipe huo mkoba nitoe ndani vitabu vyangu.

(n) (i) Darasa <u>lako</u> ni safi.
(ii) <u>Chako</u> kinapendeza sana.
(iii) Watoto <u>wako</u> uwanjani

(o) Shamba lile kubwa – kishazi tegemezi
- Litauzwa kesho – kishazi huru.

(p) Musa alimkaribisha Rahma na kumsihi akae.
- Rahma alishukuru na kumuuliza habari za pale

q) Somo la kiswahili lilikamilika vizuri
- Rita ni somo yangu kwa sababu tunaitwa jina moja.

6. (A) O na U

(B) Ng'oa kisiki hiki haraka!"Askari akaamrisha mahabusu.

(C) (i)Si vizuri wanafunzi kuibiana pesa.
(ii)Mchuzi huu uliharibika kwa kuongezwa chumvi vyingi.
PO-ya pili-mahali

(E) Naibu wa Chansela chuo kikuu <u>aliwaambia</u> mahafala kuwa wasichana <u>wakichumishwa</u> <u>wangeweza</u> kuiwa zaidi masomoni kuliko wavulana.

(F) Mtoto wetu mdogo amepotea. (Mwalimu akadirie) .

(G) Lina<u>lo</u>semwa silo lina<u>lo</u>kuwa.

(H) Ukiwa mwenye bidii utayapata mafanikio maishani

(I)

| | |
|---|---|
| $S \rightarrow S^1+U+S^2$ | $S^2 \rightarrow KN+K$ |
| $S^1 \rightarrow KN+KT$ | $KN \rightarrow N$ |
| $KN \rightarrow W$ | $N \rightarrow$ Mwenda |
| $W \rightarrow$ MIMI | $KT \rightarrow T$ |
| $KT \rightarrow T$ | $T \rightarrow$ Hakumwona |
| $T \rightarrow$ sikumwona | |
| $U \rightarrow$ wala | |

(J) (i)Hitilafiana /kosana/pigana
(ii)Kashifu (Mwalimu akadirie

(K) Ibaada
Maabadi
Ufisadi
Mfisadi

(L) Janajike hi<u>li</u> limezaa <u>ma</u>toto <u>ma</u>nne.

(M) (i)Mbio –Nomino
(ii)Mbio-Kielezi

(N) Msichana aliyeitwa - tegemezi
alikuwa mkorofi-huru

(O) A-nafsi

| | |
|---|---|
| (i)Aliitwa | (ii)Ha-Kikanushi |
| A-nafasi | Ku-Nafsi ya tatu |
| Li-Wakati | Wakati uliopita kikanushi |

(P)(i)Kuna- kukwaruza kutumia kitu chenye meno mf-Kukuna nazi. Dhana ya-Kuwa na kitu
Guna-Kukataa
mf-Mwanafunzi aliguna alipotaka kuchapwa

(Q) Huanza na U halafu hudondoa u
mf Uzi-Nyuzi
U-Mb
Wa-Nya nk (alama 3)

(R) (i) Kuhama
(ii)Kukaa mahali

7. (a) (i) Jitu linalotusumbua sharti liadhiwe vikali
(ii) Mmea upendwao/ambao hupandwa katika msimu wa masika humea

(b) (i) Juma alisema ya kuwa /kuwa/ ya kwamba / kwamba angerudi tu ikiwa/ kama wangekubali kuomba msamaha
(ii) Mwalimu Mkuu aliwataka /aliwaambia waeleze vile Walivyoenda hapo na namna wangeenda watakavyoenda

(c) (i) Simba aliyekula mzoga alimuogofya kwa hivyo hakumwangalia
(ii) Ni rahisi kukata mti wa zambarau ikiwa unatumia musumeno

(d) (i) Alilia kwa sababu ya mwanawe
(ii) Alimnyenyekea mwanawe ili ampe msaada

(e) (i) Hatungewalaki kama hatungejua hawaji
(ii) Tungalifanya kazi tungalikuwa matajiri au Tungefanya kazi tungekuwa tajiri

(f)
- ki ya masharti
- ki ya udogo
- ki ya lugha kwa mfano kikamba
- ki ya ngeli ya ki-vi
- ki ya jinsi / namna kwa mfano tembea kijeshi n.k

(g) (i) Jipya
(ii) Mwingine

(h) (i) Safari/msafara/usafiri
(ii) Mzazi/mzaliwa/uzazi

(i) Yohana na Emanueli walifunga safari wakielekea Mashariki, kusini na hatimaye MagharibiWalifika huko Novemba mwaka jana . Walipokuwa wakirudi, walimkuta Mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale.

(j) Kijoka kile kirefu kilifukuzwa na vijitu vingi

(k) (i) Alipovua
(ii) Alisimama

(l) (i) gh – Kikwamizo /kaakaa laini
(ii) j - kikwamuzo /kaakaa gumu

(m) Uwanja ulifyekwa vizuri na mahabusu

8. (a)
(i) Kiosk (Kiingereza) – Kioski
(ii) Hundir (Kihindi) – hundi
(iii) Lakh (Kihindi) – Laki
(iv) Shukran (Kiarabu) – Shukurani
(v) Shirt (Kiingereza) – Shati
(vi) Rushn (Kiajemi) – roshani
(vii) Kod (Kiajemi) – Kodi
(viii) Duvin (Kifaransa) – divai
(ix) Court (Kiingereza ) – Korti zozote 4 x ½ = al. 2)

(b) "Kitabu changu kipo wapi?"Mwaimu laiuliza alipoingia darasani ( ½X 4 (vitahiniwa)

(c) (i) Mimi

(ii) Wewe
(iii) Yeye
Mtahini ahakiki sentensi za watahiniwa sentensi (tuza al. 1)
Viwakilishi tuza al. 1)

(d) (i) Watoto hawaendi shuleni kila siku
(ii) Walimu hawajafunza wanafunzi vizuri (2x1=al. 2)

(e) (i) Kila mmoja aliandika kwa niaba ya mwenzake
(ii) Kila mwanafunzi alimpelekea mwenzake barua (2x1=al.2)

(f) (i) Mwanfunzi aliyetuzwa ni wa shule yetu
(ii) Sikuziona nyuzi zitengenezwazo ngoma tuzionazo pale (2x1=al.2 )

(g) Sentensi sahili

S – KN +KT
KN – N
N – Kiarie
KT – t + KN
t – ni
KN – N + V
N – mwanfunzi
V – Mtiifu

(h) (i) Kisu – Ki-Vi
(ii) nyavu – U-Zi
(iii) Chai –I-I

(i) KI - Kiambishii awali kiwakilishi nomino (nafsi)
LI - Kiambishi awali – wakati
CHO – Kiambishi awali kirejeshi
KI - Kiambishi awali –kitendwa
KAT - Mzizi
A - Kiishio

(j) (i) Olewa
(ii) Ozwa
(iii) Olea

(k) – Kukamilisha sentensi
- Kuandika vifupi
- Kuonyesha tarehe
- Kuonyesha desmali

(l) (i) Shamirisho kipozi – Shamba
(ii) Shamirisho ktiondo – mamake
(iii) Shamirisho ala – kwa trakta

(m) (i) Cahapa – uchapishajiii, machapishi, mchapishaji, kichapo, kuchapa
(ii) Goma – mgomo, migomo, mgomaji, ugomaji, kugoma

(n) (i) Kishazi huru – Chakula huweza kujenga au kubomoa
(ii) Kishazi tegemezi – ambacho ni muhimu

(o) (i) Ukienda mle mwao atakuwemo
(ii) Ukienda pale pao atakuwepo
(iii) Ukienda kule kwao atakuweko

(p) Kijibwa kidogo kimekanyagwa na kigari

9. a) "Mrudi leo, la sivyo mtakosa tuzo," mama alihimiza √
b) Uovu aliotuonyesha hautasahaulika
c) i) Mkulima alipanda <u>Pamba</u> shambani ( Mmea)
Au
Msichana yule <u>alijipamb</u>a vizuri (kujipodoa)
ii) Jambazi yule <u>alimbamba</u> askari (Kamata kwa nguvu)

Au
Gari lake liliharibiwa <u>bamba</u> (Sehemu ya gari)

d) - Mdomo/ meno
- Mdomo/ meno

e) i) Kuonyesha neno linaendelea katika mstari wa pili k.m tulikwenda uwanjani kuji - onea mchezo wa kandanda
ii) Kuonyesha silabi za maneno k.m ba – ba
iii) Kutenganisha maneno ambatano k.m elimu – viumbe, isimu – jamii
iv ) Kuonyesha kipindi cha muda Fulani 1950 - 1960, 1970 – 1983
v) kuonyesha aina za maneno yaliyoandikwa kwa vitengo; kwa mfano:-
- Nyanya amepanda ndizi za aina ya mkono - wa – tembo!
vi) Kudumisha sauti k.m masala – a – a – le!

f) Aliyepiga

g) i) ni – kitenzi kishirikishi kikamilifu √1
ii) yamekuwa – kitenzi kisaidizi √1
- yakihifadhiwa – kitenzi kikuu √1

h) Ambaye – kiwakilishi kirejeshi √1
nani- kiwakilishi kiulizi √1

i) Kuonyesha ukubwa wa nomino
Jitu <u>li</u>mekufa
Majitu <u>ya</u>mekufa
ii) Kuonyesha nomino ambazo hazina umoja na wingu
Tikiti <u>li</u>lilonunuliwa
Tikiti <u>ya</u>liyonununliwa
iii) Kuonyesha vitu visivyo na uhai
Jiko <u>li</u>livunjika
Meko <u>ya</u>livunjika
iv) Kuonyesha vitu dhahaima
Shetani <u>li</u>lifukuzwa
Mashetani <u>ya</u>lofukuzwa

j) - Karo – SH kipozi
- Watoto – SH kitondo
- Kwa hundi – SH Ala/ kitumizi

k) I – ZI – Tikiti ienunuliwa
Tikiti zimenunuliwa
Li – ya – Tikiti lilinunuliwa
Tikiti yalinunuliwa

l)
S ⟶ KN + KT √1
KN ⟶ N √1

N ⟶ Hakimu √1

KT ⟶ T + E √1

T ⟶ alimwadhibu √1
E ⟶ kinyama √1 (al 4)

m)

| Kutenda | Kutendua | Kutendama |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| Ficha<br>Tanda | Fichua √1<br>Tandua √1 | Fichama √1<br>Tandama √1 |

n) Kivai – Ni tungo ambalo huundwa kwa maneno aghalabu mawili na huwekwa pamoja kuwasilisha kitu kimoja (al 1)

10. (j) Rabsha – fujo, ghasia
Damu- ngeu

(k) 


(l) Kijani ni mrefu
Nendeni shambani
(m) Johana alisema; Ni<u>ta</u>pata alama zote katika majaribu wa jana
(n) Jembe linunuliwalo hupotea

(o)

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KJ | | |
| N | J | T | E | E |
| Mtoto | anayelia sana | ameadhibiwa | leo | asubuhi |

(p) Kibainishi (')
Fupisha neno 'taondoka
Ving'ong'o ng'ombe
Kuonyesha tarakimu iliyodondolewa '95
Hakikisha majibu ya mwanafunzi
(q) Toinyo- mtu aliyekatwa sikio moja
Huntha – mtu aliye na sehemu mbili za siri

11. (a) (i) Alisifiwa
(ii) Kuliridhi
(b) Abiria waliojeruhiwa sana walipelekwa hospitali haraka




(c) (i) - Nyanya yake amewasili
- Mke wake amewasili

(ii) - Alimrudi kwa sababu ya mpira
- Alimpiga kwa kutumia mpira

(d) - Kuonyesha hali ya ukubwa, mfano; jitu, jisu, jiji n.k.
- Ikiwa mwishoni mwa kitensi jina ili kuunda nomino yenye maana ya kazi ya mazoea.
Kwa mfano; msemaji, mwimbaji, mchoraji n.k.
- Kama kiambishi cha kuonyesha dharau au kudumisha mfano jivulana, jisichana, n.k.
- Kiambishi rejeshi kinachotambulisha kama mtendaji amejifanyia kitendo yeye mwenyewe au anajionyesha kuwa mtu wa tabia au matendo fulani .

mfano; - Mavitu ali<u>ji</u>tia kitanzi
- Amejiwekea akiba ya kutosha n.k

(e) a – Karibu na kati, chini ya ulimi
i – Juu mbele ya ulimi
u – Juu nyuma ya ulimi

f) (i) – Mfinyanzi hulia gaeni
Kigae- Kipande cha kitu
Mfinyanzi – Mtu anayetengeneza vyungu
-Ina maana kuwa mtu anaweza kutengeneza kitu kama chungu na badala ya kufaidika na maarifa yake kwa kutumia kile chungu hubakia kutumia kitu cha hali duni (kigae). Ni wengine ndio wanafaidika na maarifa yake

(g) Mzee Kamau alishangaaa na kusema kuwa mtoto huyo alikuwa mkaidi kama kirongwe hasa kwa kutoheshimu babake.

(h) – Kishazi huru – Limefunguliwa rasmi
- Kishazi tegemezi darasa lililojengwa

(i) - Shamirisho kitondo – watoto
- Shamirisho kipozi – karo
- Shamirisho ala – kua hundi

(j) <u>Ki</u>buzi/ki<u>ji</u>buzi chake <u>hakina</u> vijinyoya/vinyoya <u>vingi</u> wala <u>kiha</u>rufu/kijiharufu <u>ki</u>kali

(k) – Kuhitaji
- Uchafu
- Kuwa na nia ya kufanya jambo fulani

(l) <u>Nime</u>kuondolea <u>tatizo</u> lako yafaa unishukuru

m. (i) Nyima mtu uhuru unaohitajika
(ii) Kuwa na siri

n) (i) A – WA
(ii) U – U

(O) (i) Mimi – cha nafsi
(ii) Huyo – kiwakilishi kiashiria

12. a) i) nani? √
ii) Yapi? √
iii) Mbona? √

b) LIM √ 1

c) i) Pale ndipo alipoingia√1
ii) Kule ndiko alikoingia √ 1
iii) Mle ndimo alimoingia √ 1

d) i) Ni nomino inayopokea athari ya kitenzi √ 2
ii) Wali – shamirisho kipozi √ 1
Baba – shamirisho kitondo √ 1
Kwa sufuria – shamirisho ala √1

e) i) Ukoo/ nasaha – hawa ni watu wa mlango/ wa samba
ii) Kifungu katika Biblia – Kitabu cha Yohana mlango wa 3 mstari wa 4

f) i) Hivi ndivyo alivyofanya kazi (kielelezi cha namna) √ 1
ii) Viatu hivyo ndivyo tulivyonunua (kisisitizi) √ 1

g) Watalii walivutiwa na chai hiyo
h) i) Haraka zake zilimwumiza √ 1
ii) Tembea haraka ili usichelewe √ 1
i) (i) Yeye mwenyewe aende asitumie mtu mwingine √ 1
(ii) Mtu anayemiliki ktu atembelewe √
j) NI – nafsi ya kwanza umoja√1
- uwingi wa wahusika√1
- undani wa mahala √ 1
k) Watakapokuja watawaletea walinzi nyuta na pole
l) (i) I – ZI √ 1
(ii) LI – YA √
m)- k/g √1
-N √1
n) (i) Mama angali anapika jikoni (kitenzi kisaidizi)
(ii) Mama angali ji koni (kitenzi kishirikishi)
o) Mtoto aliaye ni huyu
p)- Nani- kiwakilishi kiulizi √1
- Huyu – kiwakilishi kionyeshi √1

13. a) (i) Sisi tu wanafunzi
(ni, ki, u, zi, li, yu, ndisi, ndimi)
(ii) Mwalimu alikuwa <u>anafundisha</u> .
(Tathmini jibu ya mwanafunzi)
(b) "Je, unaipenda hali ilivyo ?' Mwenzake alitaka kujua . alama za mtajo ½
Kuanza kwa herufi kubwa ½ (Je)
kama ½
Alama ya kiulizi ½
Mwenzake kuanza kwa herufi kubwa ½
Kituo mwishoni mwa sentensi (.) ½
(c) Ka – Inaonyesha mfululizo/mfuatano wa matukio/vitendo
hu – Kuonyesha hali ya mazoea
(d) Mama alituchapa, akatupa chakula na maji.
(e) - Ghuna – zinasababisha mtetemeko wa nyuzi za sauti;
/b,/d/,/v/, /z/, /g/, /gh/ /l/,/r/, /m/, /n/, /ng/, /ny/, /w/, /dh/.
- Si ghuna – Hazisababishi mtetemeko wa nyuzi za sauti; /h/, /th/, /ch/, /t/, /p/, /f/, /s/, /k/, /sh/
maana
mifano miwili kila aina

(f) Dua – maombi – Marehemu aliombewa dua na kasisi
Tua-shusha – Ndege ilitua kiwanjani abiria wakashuka
(g) Vijia vyembamba ni hatari kwa usafiri wa vigari
(h)




***Mzee ambaye hukuza pamba amefaidika sana***

(i) Wa – Mofimu ya nafsi (tatu wingi) /ngeli (A-WA)
Li – Mofimu ya wakati (uliopita)
O- Mofimu ya 'O' rejeshi
Chek- mofimu ya mzizi/shina la kitenzi

eshw – mofimu ya kauli /mnyambuliko
a = kiishio (mofimu)

(j) - Ugonjwa wa saratani hufisha watu polepole
- Mkulima alisokota kamba ndefu

(k) Ongancha alimjengea babake nyumba kwa matofali mazuri sana
babake – kitondo
nyumba – kipozi
kwa matofali – ala
sana – chagizo
Kitondo- mtendewa/kitendewa
Kipozi – kilichotendwa
Ala – kilichotumika kitenda
Chagizo – Kielezi, jinsi kilivyotendwa

(l) Mchezaji kijana alifunga bao- kivumishi
Kijana yule alifunga bao – Nomino
(Tathimini majibu ya mwanafunzi)

(m) – Mtoto ambaye alikuwa anacheza ameanguka au
- Mtoto aliyekuwa anacheza ameanguka
- Vitabu hivi ambavyo vimesahihishwa ni vya wanafunzi

(n) – Msichana yule alitembea kitausi – kielezi namna mfanano
- Mbwa alibweka bwe! – kilezi nmana kiigizi (1x1=al.1)
(Tathmini majibu ya mwanafunzi)

(o) Manukato – YA-YA: Manukato – manukato
- Manukato yananukia
- Manukato yananukia
uwati – U-Zi: Uwati – mbati
- Uwati uliotumiwa kujenga nyumba umevunjika
- - Mbati zilizotumiwa kujenga nyumba zimevunjika

(p) Tui ni maji meupe yanayopatikana katika nazi iliyokunwa
- Mtu anayevunja nazi lazima afaidi tui lake
- Yeyote anayeifanya kazi ngumu lazima afaidi matunda ya kazi yake.
- Anayehusika na shughuki yoyote yenye tija atafaidika (jibu lolote moja al. 1)

14. A) Mwandishi hakuwa na mtu mwingine yeyote alipoenda sokoni. (al. 2)
Mwandishi hakwenda mahali pengine ila sokoni.

B) “Hodi! Hapana wenyewe nini?” Jinani alimaka. Nitarudi kesho. (al. 4)

D) Mwanafunzi adurusuye ndiye apitaye mtihani. (al. 1)

E) Dhambi za mwandamu zilifisha Bwana Yesu. (al.1)

F) Kumchukulia kuwa mjinga (kumdhalilisha/dudisha mtu) (al. 1)

G) Thumni. (al. 1)

H) i) Ningalisoma kwa bidii ningalifaulu katika mtihani ule .
ii) Atakuwa amekuja.

I) i) Chungu – Mdudu
ii) Chungu - Chombo cha kupikia.

J) i) Sisi sote tuna soma (Nafsi ya kwanza wingi)
ii) Kuni zote zimewaka moto ya ‘U-zi’ wingi.

K) Msafiri - safari
Kwafiri – msafara usafiri.

L) Alikimbia kwa nguvu zake zote lakini (ijapokuwa, ingawa) alishindwa kwa vile/madhali/ kwa sababu kulikuwa na mwenye mbio kumliko.

M) Kutokesakwa vitendo mtawalia (Kimoja mara tu baada ya kingine)

N) M n ny ng’

O) Ameepua/ Amedeua/Ametegua chungu mekoni.

P) Vijitu vichoyo havifai kwa vyovyote vile. (al. 2)

Q) Ukionana naye mwambie asije kuniona. (al. 2)

R) i) Kama kiambishi kiwakilishi cha nafsi yakwanza wingi (sisi). (al. 1)
Tutasafiri kesho kutwa)

ii) Kuonyesha kuwa hakuna ziada ya kilichotajwa. (Mkutano ulihudhuriwa na wanachama watano tu). (al. 1)

S)

| KN | | KJ | |
|---|---|---|---|
| N | S | T | E (CH) |
| Mwanafunzi | Aliyeleta kitabu | amepongezwa | sana |
| | | | |
| | | | |

T) Wanunuzi <u>viwanja </u>(al.2)
SH Kitondo SH Kipozi

U) i) a-wa
ii) i-zi

# ISIMU JAMII

1. (a) - Lugha elezi imeumika
- lugha takriri
-Lugha mseto hutumika
- Serntensi fupi fupi hutumika
-Kanuni za lugha hazizingatiwi
- Huendesha kwa malumbano na ngonjera (hoja 6x1=al. 6)

(b) (i) Mazungumzo hulipiwa – kupunguza gharama kupoteza mda (hoja 2x1=al. 2)
(ii) Uhusiano wao wa kielimu
- Athari ya asili ya kifaa cha mawasiliano
- Kuonyesha ubwana
- Mazingira ya mazungumzo (hoja 2x1 = 2
- Kwa kuwa wanajua zaidi ya lugha moja

2. Ushindani kutoka lugha nyingine kama kiingereza
- Hadhi – Kiswahili kimedumisha
- Athari za lugha ya mama
- Mitazamo hasi kuhusu Kiswahili
- Kutokuwepo kwa sera mwafaka kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa muda mrefu
- Kuhusishwa kwa lugha ya Kiswahili na dini ya kiislamu/ eneo la pwani
- Wamishenari walieneza dini zao kwa lugha ya kiingereza
- Kutokouwa na vitabu vya kutosha vilivyoandikwa kwa Kiswahili
- Uchache wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili
- Mkazo wa ufundishaji wa lugha za kikabila katika shule za msingi
- Kuwepo kwa sheria katika shule kuwa Kiswahili kizungumzwe siku moja kwa juma
Lugha imetengwa katika matumizi ofisini za kiserikali

3. a) hospitalini/ uwanja kisayansi
b) Sifa za sajili ya hospitalini Matumizi ya msamiati maalum
Matumizi ya vifupisho ambavyo vinaeleweka na wanaohusika na uwanja wenyewe
Kuwepo kwa maelezo yanayoambatanishwa na michoro kujaliza maelezo yanayotolewa
Matumizi ya alama zinazohusishwa na taaluma ya hisabati hasa katika maagizo ya kutumia dawa
Huweza kuwepo na matumizi ya maneno ya kilatini yanayohusishwa kwa kiasi kikubwa

na taaluma hii
Huweza kutumia neno mgonjwa kumweelezea mtu badala ya jina k.m yule mgonjwa wa homa ameruhusiwa kwenda nyumbani
Utohozi wa maneno hutumika
Kuna kuchanganya ndimi
Lugha hii ni ya heshima hasa upande wa mgonjwa
Sarufi huzingatiwa Zozote 7x1=7 Mahojiano kati ya mgonjwa na daktari

4. Mikakati inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya
   i) Sera madhubuti – hii itaelekeza hatua za kupanga na kuendeleza lugha. Pia itabainisha nyanja na maeneo ya matumizi ya Kiswahili
   ii) Kuimrisha Kiswahili – kitumiwe kama lugha ya kufundisha baadhi ya masomo, somo la lazima n.k
   iii) Ufadhili wa miradi ya utafiti
   iv) Maandalizi mema ya walimu na wataalamu wa Kiswahili
   v) Kubuni vyombo vya kukuza Kiswahili
   vi) Kusisotiza matumizi ya lugha sanifu
   vii) Serikali kufadhili uandishi na uchapishaji wa vitabu vya sarufi
   viii) Kuingiza Kiswahili kwenye kompyuta
   ix) Kuunda jopo la kitaifa la wataalamu – lengo leo ni kutoa mwongozo kuhusu Kiswahili na maendeleo yake

5. (a)- Matumizi ya sheng' katika lugha ya Kiswahili
   - Kushushwa hadhi ya Kiswahili – Kiswahili kimepewa nafasi finyu ukilinganisha na Kiingereza
   - Vyombo vya habari – vinatumia lugha ya Kiswahili ovyo ovyo bila kuzingatia usanifu wake.
   - Ushindani mkubwa ambao Kiswahili kinapata kutoka lugha nyingine k.m. kifaransa, kingereza.
   - Kutokuwepo kwa mwongozo na taasisi inayokuza na kuendeleza msamiati na istilahi za Kiswahili.
   - Kutokuwepo kwa waandishi wa kutosha wanaoandika katika lugha ya Kiswahili sanifuUGU*
   - Ukosefu wa ufadhili wa kufanya utafiti katika lugha ya Kiswahili
   - Kutokuwepo kwa sera madhubuti au imara kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu
   - Kasumba ya kikoloni miongoni mwa watu

   (b) kutilia mkazo ufundishaji ufaao wa kiswahili katika shule na taasisi zote
   - Kupitishwa kwa sera nzuri kuhusu Kiswahili, kuhimiza kuwepo kwa idara za Kiswahili katika taasisi nchini
   - Kubuniwa kwa vyombo vya kukiendelza Kiswahili kukisambaza na kuhimiza matumizi yake
   - Wachapishaji kuhimizwa kuchapisha kazi za Kiswahili sanifu ili wananchi na wanajamii kwa jumla kufaidika.
   - Kuwepo kwa vipind vya redio na runinga ambavyo vihinamiza matumizi sanifu ya lugha ya Kiswahili.
   - Serikali kutenga fedha kila mwaka ambazo zitachangia katika utafiti na maendeleo ya Kiswahili
   - Kuanzishwa kwa tuzo zitakazopewa waandishi wanaoandika kazi nzuri zinazosaidia ukuzaji wa kiswahili.
   - Kuhimiza uchapishaji wa magazeti mengi ya Kiswahili

6. (a) huchanganya lugha hasa kiswahili na kingereza k.m. <u>utado</u>, anani <u>enjoy</u>.
   - Hufupisha maneno k.m. mtoi, tao, Nai , Kach
   - Hutumia misimbo k.m. keja, ocha, ndae
   - Lugha fiche k.m. ganja (bangi), mapai (polisi)
   (b) Mashindano na lugha zingine kama Kingereza.
   - Kasumba kwamba lugha ya kiswahili ni duni/ya watu wasiosoma.
   -Sura mbov za serikali

-Ukosefu wa taasisis maalum za kuendeleza kiswahili.
-Matumizi ya 'sheng' yanadidimiza kiswahili (zozote 5x1=al.5)

7. (a)Lugha ya vijana

(b) •Kubadilisha msimbo –usifikirie kila kitu unaona ni reality.
•Si lugha sanifu-Najua ma-mission ni nyingi lakini jo, mambo imebadilika
•Matumizi ya sheng- Ma-mission
Ku-chill
Uki-regret
•Matumizi ya sentensi fupi- Ni kibaya maze
Ni poa kuchill
•Kuchanganya msimo-Kuchill ;Ukiregret ;Ma-mission.
Tuza ½ kwa kila sifa inayotolewa na ½ alama kwa mfano (Jumla al.4)

(c)•Ukosefu wa msamiati.
•Kukubalika katika kikundi fulani.
•Kujitambulisha na lugha fulani au kuonyesha umahiri katika lugha zote mbili

(d)•Kutilia mkazo ufundishaji ufaao wa Kiswahili.
•Kupitishwa kwa sera nzuri inayoweka wazi malengo ya serikali kuhusu lugha hii.
•Kuhimiza kuwepo kwa idara za Kiswahili katika taasisi za juu ili kuendeleza utafiti.
•Raia kukumbushwa kuionea fahari lugha hii.
•Wachapishaji kuhimizwa kuchapisha machapisho ya Kiswahili.
•Vipindi vya redio na runinga viwepo vya kuhimiza matumizi fasaha ya Kiswahili.
•Kiswahili kuwa msingi muhimu katika taasisi za elimu. k.m.Daktari asiweze kuwa daktari bila kuonyesha uwezo mzuri wa lugha ya Kiswahili.

8. (i) Sehemu za kuabudu/ ibada / mzungumzo ya Kristo
(ii)(a) Matumizi ya lugha iliyojaa upole/ unyenyekevu
(b) Msamiati maalum unaohusiana na dini Fulani. Kwa mfano ‚Yesu" okoka, , Mungu asifiwe' , Halleluya, , Amen' dini ya kikikristo
(c) Huweza kuwapo matumizi ya maneo au makuu kutoka kwa Bibilia m.f. usiwe kama Yona, Paulo na Sila. .
(d) Huwepo matumizi ya msamiati ambao unaeleweka tu katika muktadha huo wa mazingira yanayohusika tu. Mungu anaendelea kunibariki. ‚Amen"
(e) Lugha haina matumizi ya misimu au hata lugha inayoonekana kama isiyozingatia adabu; huwa lugha yenye tasfida.
(f) Majina yanayofungamana na ibada inayohusika, injili, sala, Mungu, Bwana asifiwe
(g) Matamshi au lafudhi ya utamkaji wa maneno kutegemea mazingira fulani ya ki-ibada
(i) Dini
(ii) Biashara

9. (a) Sajili ya bungeni
(b) Sifa
- Msamiati na istilahi huhusiana na bungeni k.m. vikao vya bunge, spika, mesi, karani n.k.
- Hurejelea sheria za nchi au katiba katika kutetea hoja fulani inayojadliwa
- Lugha ya heshima katika mawasiliano na majadiliano-Mheshimiwa spika
- Kuchanganya ndimi katika mijadala, ili kujieleza vyema
- Wabunge hutaja msamiati unaorejelea sheria na kanuni za bunge wanapojadiliana kuhusiana na maswala mbali mbali, hasa shughuli za kinidhamu (zozote 4 x 2= al. 8)

10.
(i) Kuwepo kwa vipindi vya redio na runinga ambavyo huhimiza matumizi ya lugha sanifu
(ii) Uchapishaji wa vitabu vya kisarufi
(iii) Ufundishaji wa Kiswahili kuwa somo la lazima shuleni

(iv) Kiswahili kinaendelezwa kitaaluma katika vyuo vikuu
(v) Mashirika mbalimbali yanayoshughulikia uimarishaji wa lugha ya Kiswahili kwa mfano Chakita, Chakike
(vi) Mashindano ya uandishi
(vii) Kukariri mashairi katika tamasha mbalimbalIi
(viii) Kuandaliwa kwa semina na warsha mbalimbali zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili
Kilitangazwa kuwa mojawapo ya lugha za bunge

11 (a) – Kurejelea sura au aya za maandishi matakatifu kama Bibilia, kurani n.k.
- Kuna msamiati maalum kama kasisi, shehe, kadhi, hekalu, jehanamu n.k.
- Matumizi ya ishara za mwili hutamalaki. Haya hulenga kuwanasa wasikilizaji wa kudunisha hali ya kusikiliza. s
- Matumizi ya lugha huhusisha kubadilikabadilika kwa sauti kutegemea madhumuni na matakwa ya msemaji.
- Ni lugha ya upole na kunyenyekea.
- Kuwa na hali ya kuzungumza kwa pamoja hasa katika maombi
- Lugha inayotumiwa huwa ya wastani, isiyo ngumu kueleweka au nyepesi.
- Ni lugha ambayo mtu hapewi fursa ya kuuliza swali
- Ni lugha ya unyonge na hutumiwa sana wakati mtu/watu wamefikwa na msiba

(b) - Muktadha wa matumizi au mazungumzo
- Wahusika na uhusiano wao
- Umri wa wahusika
- vyeo vya wahusika wa mazungumzo
- Tabaka au nafasi ya kijamii ya wahusika wa mazungumzo
- Madhumuni ya mawasiliano au mazungumzo
- Mada zinazozungumziwa
- Jinsia ya wahusika wa mazungumzo
- Lugha aizungumzayo mzungumzaji

12. i) - Hii ni sajili ya magari ya uchukuzi
- Inatokea katika kituo cha matatu au barabarani gari linaposimama kubeba abiria
- Kuna utingo anayetangaza kiasi cah nauli kwa wasafiri wanaotaka kulipa malipo nafuu

ii) - Kuna matumizi ya lugha maalum kama 46, ingia twende shona
- Kuna kutaja vituo mbalimbali ambako gari litapitia
- Ni lugha ya kuchanganya ndimi kama vile "driver" n.k
- Inatumia misimu au simi k.m hashuu, dinga n.k
- Haizingatii sarufi sanifu k.m inakunywanga, sinako n.k
- Sentensi ni fupi fupi
- Ina ucheshi mwingi

<u>TAZAMA</u>

i. Kwa kila kosa la sarufi mtahiniwa huadhibiwa nusu alama
ii. Mtahiniwa haadhibiwi zaidi ya nusu ya alama alizozipata katika kila swali
iii. Kwa kila kosa la tahaja, mtahiniwa huadhibiwa nusu alama hadi jumla ya makosa sita

13. a) Muktadha wa ndoa/ arusi/ kuzungumza juu ya mahari

b)
i. Lugha ya kujibizana
ii. Kukatana kalmia/ kauli
iii. Sentensi fupifupi- lugh ya mkato
iv. Kuna matumizi ya udokezo mfano au ni………………..
v. Lugha ya kupatana/ kuelewana mfano basi lete hao ulio nao…
vi. Lugha ya kujisifu mfano huyu motto wangu nimemsomesha
vii. Lugha ya ahadi

viii. Lugha ya istiara mfano je mbuzi hao ni wa mfuko au………

ix. Lugha yenye misemo- kujenga ukwe

TAZAMA sarufi/ isimu jamii

1. Kwa kila kosa la hijai mtahiniwa huadhibiwa ½ alama hadi jumla ya makosa sita
2. Kwa kila kosa la sarufi mtahiniwa huadhibiwa ½ alama
3. Mtahiniwa asiadhibiwe zaidi ya nusu ya alama alizozipata katika kila swali.

# Karatasi ya tatu 102/3

## RIWAYA: UTENGANO: S.A. MOHAMMED

1. a) - Msemaji ni mama Jeni.
   - Msemewa ni maimuna.
   - Mahali - mkahawa wa Café Afrique.
   - Trikio – Baada ya ziara ya kumnunulia maimuna mavazi katika duka la baniani Mama Jeni alitaka kumpa Maimuna kuzozana na James, baharia aliyetaka kufanya mapenzi na maimuna. ( 4x1) ala.4

   b) i) Watu wanapoishi pamoja hawana bud kuzozana hivyo basi ilibidi pawe na sheria au makabiliano ya kuongoza maingiliano yao.

   ii) Ingebidi Maimuna Kumgawia mama Jeni sehemu ya pesa alizopata kutoka kwa wateja wake.

   iii) Alimhakikishia kwamba angeyazoea maisha yale baada ya muda. ( zozote 2x2) ala. 4

   c) i) Wasichana hakupewa elimu kama vile Maimuna ilhali waume walipata elimu (Mussa).

   ii) Maksuudi alimtawisha mkewe Tamima na bintiye.

   iii)Wanaume walikuwa wazinifu ku maksuudi na shoka bila kujali wake zao.

   iv) Maksuudi alihini Mwanasuru mali yake na kusababisha kifo chake.

   v) Wanawake walipigwa bila sababu muhimu.

   vi) Wanawake walipewa talaka na wanaume bila sababu muhimu

   vii) Pesa za mkewe Japu ziliwa na Mksundi alipofika amwekee sahihi.

   viii) Nchi zilizostawi zuilinyanyasa nchi maskini (zozote 6X2) ala. 12

2. Majaaliwa ni mambo yatokanayo na rehema za Mungu, Kindura, mambo amabyo binandamu hana mamlaka nayo.
   - Maimuna alipata fursa ya kutoroka kwao siku ambayo mamake alijifungua.
   - Ni majaliwa kuwa siku ambayo Maimuna alitoroka nyumbani Bw. Maksuudi hakuwa nyumbani, alikuwa kwa kazija.
   - Mkutano wa Maimuna na Maulidi ni ya kimajaaliwa. Alikuwa akiimab huku akiosha vyombo ndiposa akapata kazi ya kuimba huko Kumbalola Hoteli.
   - Maimun a aliposingiziwa kwamba ameiba kwa mama Jeni alisaidiwa na Dora kwenda kwa Biti surur.
   - Ndoa yake kwa kabi ilimbadili nia na akajisameha na pia kusamehe babake.
   - Uchechefu wa chakula ulimleka kuzuru upwa alipokutana na Kabi – wakawa wachumba.
   - Matatizo yaliyomkumba maishani hatimaye yalimzindua akawa msomaji wa magazeti na mwanaharakati wa ukombozi wa wanawake.
   - Alipata shida nyingi kujikimu huko Futoni. Hili lilimfanya awe alghaina kusababisha kupata mali kwa Bwana Ashuru.
   - Anapotoroha kwa Biti suru ndipo anapopata fursa ya kwenda Futoni na kuanza maisha mapya. (zozote 10X2) ala. 20

3. a) Muktadhaa wa dondoo
   - Haya ni maneno ya Zanga, mmojawapo wa wagombeaji kiti cha ubunge
   - Alikuwa akihutubia umati wakati wa kampeini
   - Alikuwa katika uwanja wa Uhuru
   - Alitaka maswali yaulizwe na umma lakini watu wakanyamaza kama ishara ya kutoridhika

- (Zozote 4x1=4)

- b) Ila za msemaji (Zanga)

- Zanga hawajibiki katika kutumikia umma
- Anawadharau na kupuuza waliomchagua
- Anajilimbikizia mali bila kuwajali waliomchagua k.m. magari matatu na nyumba tatu
- Hapatikani kazini
- Anabagua watu maskini na kupendelea matajiri
- Ana kiburi na majivuno mengi
- Hakutimiza ahadi za awali alizoahidi kabla ya kuwa mbunge (zozote 3x2=6)

c) Jinsi wanasiasa walivyosawiriwa

- Wanasiasa ni pamoja na waasi wa chama, Zanga, Maksudi, Siwa na wakoloni wakongwe waliotawala nchi
- Maksudi ni kiongozi asiyetimiza ahadi yake
- Wanajilimbikizia mali k.m. Maksudi ana kasri na amejiwekea akaunti huko nje naye Zanga ana nyumba tatu na magari matatu
- Wanadhulumu umma kwa mfano Maksudi anatwaa ardhi ya umma
- Wafisadi k.m Maksudi anajaribu kumhonga inspekta Fadhili
- Wanajihusisha na magendo k.m Maksudi
- Wakoloni wakongwe walijipenda na kumiliki majumba makubwa makubwa
- Wakoloni wakongwe walikuwa wabaguzi, waliwabagua watu wa tabaka la chini na kuita mtaa wao mtaa wa 'walatope'
- Waliwadhaulumu wapigania uhuru
- Siwa ni mwaminifu, anatoa hotuba fupi bila kutia chumvi kama Zanga na Maksudi katika uwanja wa Uhuru
- Siwa ana mienendo mizuri na anakabiliwa na umma

Kutaja wanasiasa alama 2 ; Hoja zozote 8x1=alama 8; Jumla (c) alama 10

4. Migogoro/ misuko suko – (haya mawili yajadiliwe sambamba)

(i) Ufafanuzi- migogoro- hali ya kutoafikiana baina ya pande mbili au zaidi- fujo- kusiko na utulivu, ugomvi/ sokomoko. Misukosuko- hali ya kutowepo na utulivu au Amani ghasia , machafuko/ migogoro

(ii) Familia ya Bwana Maksudi Kambe. Anawatisha/ anafungia binti na mkwewe Tamima wana Huzuni, wana sosononeka kwa kufungiwa kama watumwa. Maimuna anaamua kutoroka, naye Tamina baada ya kuzalishwa apewa talaka. Familia ya Maksudi inapitia misukosuko na migogoro unayosababisha isambaratike kabisa. alama 3

(iii)Bwana Maksudi, Mussa na Kazija. Hawa wanapita migogoro wanapokutana kwa karija. Wote wawili wamevutiwa na urembo wake wanataka penzi. Wanapokutana, kuna vita, fujo- nusura kuuana. Vita hivi vinasabibisha uhusiano kati ya baba na mwanawe kusambaratika- hawaonani tena Mussa atokomea kwenye giza. alama 2

(iv) Bi. Farashuu- Ana kisasi na Bwana Maksudi kwasababu huyu wa pili alimwoa bintiye akamtesa, akamnyan'ganya urithi/ mali kisha akamtaliki na kusababisha kifo chake.

Farashuu anadhamiria kusambaratisha uhusiano kati ya baba na mwanawe kusambaratisha familia ya Maksudi. Anafaulu vilivyo kwa kutumia binti Kocho, Bi. Kazija na hata yeye mwenyewe kuingia nyumbani mwa hasimu wake na kusababisha talaka. alama 3

(v)(Umma na Maksudi- Katika mkutano wa kisiasa, Maksudi anapoomba kura, anakumbushwa
uovu wake, kama kiongozi mfano kujilimbikizia mali, kunyanyasa maskini, kusahau alikotoka.

Bi kazija kkwa niaba ya umma anampasulia mbarika. Maksudi anaaibika umma wataka kumwangamiza mabo yanasambaratika- anakamtwa na kufungwa jela. alama 3

(vi) Zanga na umma- Katika mkutano wa kisiasa- Anapojitetea mbele ya umati unapuuza, Kazija tena anakumbusha umma, kuwa Zanga amejilimbikizia mali, ana maringo- hajali raia wa kawaida.

Ni mjeuri. Mambo yanamharibikia. Raia wako tayari kulipiza kisasi. Naye pia awekwe pingu na

kupelekwa na askari alama 3

(v) Migogoro ya Danguriko kwa mama Jeni- Fujo kati ya Maimuna na James, fujo ya Maimuna na wasichana wengine waliomwonea gere/ uwivu hadi kumsingizia wizi. Mambo yanasambaratika Maimuna ahamia Bobea. alama 3

(vi) Danguroni kwa inti Sururu- fujo ya ulevi, uasherati, ugomvi kati ya Maimuna na kijakazi. Ulevi wa Shoka na uasherati unasambaratisha familia yake. Mkewe alalama. Ugomvi waleta vita, majeraha, kovu kwa Maimuna. Ni picha kamili ya jamii iliyosambaratika. alama 3

(vii) Hotelini Rumbalola- Maksudi ajaribu kumfikia Maimuna lakini anamkosa, anapigwa vibaya na mashabiki- anaishia kwenye hospitali nusu maiti. Maimuna anatoweka bila ilani-afutwa kazi na mwenye hoteli- Balaa na fujo tupu- mambo yamesambaratika. alama 3

(viii) Bobea kwa Binti Sururu- Maksudi kwa mara ya pili aandamana na Mussa na Rashid kumtafuta Maimuna, wanampata Maimuna katika hali ya kutisha wanajaribu kumpata lakini awaonya "Tokeni mbele nyie--------- nirejee kwao----------- sahau uk 145" mambo yanasambaratika. alama 3

(ix) Kuna matumaini- Maimuna abadilisha maisha- aolewa na Kahi na kujenga jamii mpya. Maksuudi aaga dunia, Mussa na Tamina wanaungana tena katika ujenzi za jamii mpya Isiyosambaratika. alama 1

Kutuza Alama
Maelezo:Alama 1
Matumaini: Alama 1
Hoja- Kutaja aina ya migogoro (Alama 1)
Maelezo alama 2=2
Jumla 3x6=18+2= Jumla 20

5. (i) - Hapa ni nyumbani mwa Bw. Maksuudi
- Anayezungumza ni maimuna bintiye Maksuudi na anamzungumzia Tamina mamake
- Bi Tamina alikuwa mja mzito na siku hiyo alianza kupiga kite kwa kuhisi kujifungua
- Maksuudi alikuwa nyumbani na hiyo ilimaanisha kuwa hangeeza kupelekwa hospitali na mtu mwingine ila Maksuudi. Wala hangeweza kuagiza mkunga wa kienyeji kuja kumzalisha pale nyumbani
- Maimuna alimwonea mamake huruma na ulimwelekeza kumsihi mamake wavunje miiko/ sheria ya Bw. Maksudi. Hapa ilikuwa baada ya kuzungumza na kushawishiwa na Binti Kocho mmja wa watumishi wa Bw. Maksudi

(ii) - Bi Tamina na Bintiye Maimuna walikuwa wakitawishiwa na Bw. Maksudi
- Hawakuwa na ruhusa ya kutoka nje bila idhini yake
- Maimuna na mamake hawakuwa na uhuru wa kujiamulia lolote walilotaka hata kama maisha yao yalikuwa hatarini Zozote 3x2=6

iii) <u>SIFA ZA MAKSUUDI</u>
- Ni katili- k.m kumchapa mkewe Bi tamina
- Ni fisadi- k.m alipata utajiri wake kwa kujilimbikizia mali kwa njia isiyofaa
- Mnafiki- Husema aneanda kwa kaburi la shehe kumbe huenda kwa kazija
- Mzinifu- Ana mpenzi nje ya ndoa –Kazija
- Mbinafsi- Hajali maslahi ya watu wengine
- Maksudi ni mwongo na ni mwenye kutoa ahadi za uongo- wakati wa kufanya kampeini zozote

6.
- Ndoto ni mbinu anayoitumia mwandishi
- Mbinu hii kwa kiasi kikubwa hutegemea hisia za msomaji ili kumchochea hisia za uoni, usikizi, ugusaji na uonaji
- Mwandishi ametumia ndoto na nyimbo za Maimuna kujenga picha kadha wa kadha akilini mwa msomaji
- Maimuna anaota ndoto mbili, ndoto ambazo ni ruya na jinamizi kwa sababu zinatisha na kuogofya
- Ndoto ya kwanza ni juu ya nyama kubwa, ndumakuwili labda linalommeza Maimuna
- Mwandishi ametumia ndoto zote mbili kama utangulizi pale Maksuudi anapotoka kwenda kumtafuta bintiye Maimuna

- Ndoto hizi zinatumika kuashiria maandaizi ya mikosi na maafa yatakayomsibu Maksudi
- Maksudi katika ndoto zote anawasilishwa na kuthibitishwa kwa mifano ya kutisha. Kwanza kam nyama la kutisha lisilotambulikana
- Ndoto ya pili imechukua taswirahiyo hiyo ya nyama la kutisha isipokuwa mara hii ni chatu, joka la kutisha
- Jambo hili la Maaksudi kujitokeza katika mifano ya wanyama wa kutisha na ambao wajibu wao ni kuua
- Maimuna aliwahi kushuhudia unyama aliotendewa, kutawishwa na kunyimwa uhuru
- Si ajabu basi kwamba kila Maksudi alipojitokeza katika ndoto za Maimuna alijitokeza kama nyama mla mtu
- Nyimbo za Maimuna nazo zina umuhimu unaokaribiana na ule wa ndoto, nyimbo hizi pia zinatanguliapale Maksudi anapojitokeza kumtafuta bintiye
- Wimbo anaotumia Maimuna una simango na sumbulio inayochora picha nzima ya maovu ambayo jamii imemtendea
- Maneno ya Maimuna katika nyimbo yanamsimanga na kumsuta Maksuudi kwasababu alimtia Maimuna kovu na dosari inayomkosesha na kumwondolea ukamilifu wa utu
- Dosari alizonazo, madhila aliyo nayo na kovu alilo nalo ni matokeo ya tabia ya maingiliano na babake
- Ndoto na nyimbo hizi zinaonyesha ukwasi wa kiumbuji wa mwandishi
- Anazitumia ndoto hizi na nyimbo kifani na kiufundi , kama utangulizi na ubanishaji dhahiri wa mambo Fulani muhimu katika kazi
- Ndoto na nyimbo zinazomwandaa msomaji na kumtangulizia na mikasa ielekeayo kutokea
- Zinatumika pia kama mbinu rejeshi
- Ndoto na nyimbo hizi pia zinatekeleza jukumu na kuwa kama vituo vya mapumziko katika mtiririko wa muumano wa masimulizi
- Ndoto na nyimbo hizi ni mbinu ambayo mwandishi anaitumia kuivisha hadithi na masimulizi kwa jumla kutoka daraja moja hadi nyingine, kutoka hatua moja hadi nyingine zozote 21x1=20

7. Mkamia maji hayanywi, na akiyanywa humsakama (al. 2)

Ithibati - Maana – Akusudiaye kwa hamu kubwa kupata kitu fulani hukumbwa na pingamizi kiasi cha kukosa na hata kupata hasara.

mifano

(a) Bwana Maksundi

Kukamia

(i) Kutaka mali
- Alimfilisi mwanasururu
- Alikuwa akiitisha pesa kutia sahihi stakabadhi kwa mfano kutoka kwa mzee Japu
- Alipora mali ya umma
- Alishiriki biashara haramu/magendo
- Alitwaa ardhi ya via sera isivyo halali
- Alitaka kuwa mbunge

(ii) Kutaka anasa na starehe
- Kwenda kwa kazija Juma la mwisho wa kila mwezi
- Pamba kasri lake kwa fenicha za thamani kuu
- Kushiriki ulevi

Sakama

(i) Kisasi na chuki kutoka kwa Bi. Farashuu,Biti Kocho na Kazija
(ii) Ndoa yake kuvurugika na kuvunjika.
(iii) Kutoroshwa kwa mwanawe Maimuna.
(iv) Kufumanishwa na mwanawe Mussa
(v) Alimtaliki mwanasururu na Bi. Tamima
(vi) Kesi ya jinai na kifungo jela cha miaka miwili

(vii) Siri zake kufichuliwa hadharani na kazija
(viii) Upweke na ukiwa baada ya kutorokwa na jamaa.
(ix) Ugonjwa
(x) Kifo (kukamia 3, sakama -3 = al.6)

(b) Maimuna (al. 4)
Kukamia
(i) Kutafuta uhuru/kuvunja utawa
(ii) Kukubali kutoroshwa nyumbani na Biti kocho na Bi. Farashuu

Sakama
(i) Kutumiwa na wanaume na kutupwa
(ii) Kusingiziwa kuwa mwizi kwa mama Jeni kuchukiwa na kufukuzwa
(iii) Kupigania mwanamume (shoka) na kijakazi na kujeruhiwa vibaya.
(iv) Kuzoroteka ki-afya na wanaume kwa mfano kushiriki ukahaba na James, na shoke (kamia al.2 , sakama al. 2= 04)

(c) Bwana Zanga (al. 04)
Kamia
(i) Mali na utajiri – magari matatu, nyumba tatu
(ii) (ii) Alitaka uongozi – ubunge

sakama
(i) Wananchi wanamsuta kwa kutojali maslahi yao
(ii) Anashikwa na askari na kushtakiwa kwa kosa la jinai
(iii) Anakataliwa na wananchi katika uwanja wa uhuru
(iv) Siri zake kufichuliwa hadharani na Kazija (kamia al.2 , sakama al. 2= al 4)

(d) Mussa (al.2)’
Kamia
(i) Starehe na Anasa kwa Kazija
Sakama
(i) Fumanizwa na babaake Bwana Maksundi kwa Kazija na kuaibika
(ii) Kabwa koo, kunyongwa nusura afe
(iii) Kutoroka nyumbani na kutengana na familia yake (kamia al. 1, sakama al 1=al.2)

(e) Bi Farashuu (al. 4)
Kamia
(i) Kulipiza kisasi dhidi ya Bw. Maksundi
(ii) Kumtorosha Maimuna hadi kwa waendesha madanguro – Mama Jeni – pumziko
(iii) Tenganisha Bi Tamima na Bw. Maksundi
(iv) Tnganisha Bw. Maksundi na Bi Maimuna
(v) Fumanisha Bi. Maksundi na Maimuna
(vi) Kujaribu kuvunja ndoa kati ya Maimuna na Kabi

Sakama
(i) Maimuna alimharibu kuolewa na mjukuu wake –Kabi
(ii) Familia ya Bw. maksundi aliyeichukia kuungana na yake kupitia ndoa kati ya Kabi (mjukuye) na Maimuna bintiye Bw. Maksundi
(iii) Alisikitika kwa kumsababishia Bwana Maksundi kifo chake
(Kamia al.2, Sakama al. 2= al. 4

8. (a) Muktadha
(i) Msemaji ni Inspekta Fadhili
(ii) Alikuwa anaelezea Bw. Maksundi

(iii) Wamo katika “kasri la watawa” nyumba ya Bwana Maksundi
(iv) Inspekta Fadhili alikuwa amekataa kuhongwa ili kuficha ushahidi wa kesi ya magendo dhidi ya Bw. Maksuudi.
(v) Bw. Maksundi alimweleza kuwa Inspekata Fadhili ana wakubwa wake (zozote 4 x1=ala.4)

(b) <u>Maovu ya Bw. Maksundi</u>

(i) Unyang’anyi – alihalifu via Sera kutoka kwa Rembani kijana wa kihadharami.
- Alihalifu shamba, ng’ombe, pesa, na vyombo vya dhahabu kutoka kwa Mwanasururu

(ii) Ukatili:- Alizoea kupiga Mwanasururu na hata Bi. Tamima
- -Alimfukuza Bi. Tamima kando ya mapigo bila kujali hali yake. Alikuwa ndio amejifungua mtoto
- Bi Tamima alifukuzwa bila mtoto wa siku moja tu

(iii) Hongo- alichukuwa shilingi 200/= kutoka kwa mzee Japu
- o Anakubaliana na wafidiwa nusu bin nusu ili kuwapa fidia licha ya kutokuwa halali

(iv) Unafiki
- Alidai kutetea haki za akina mama nawatoto wasichana dhidi ya kutawishwa. alitawisha Mwanasururu, Bi Tamima na Maimuna.
- Ni muumini wa dini ya Kiislamu/shehe, lakini anamwendea mkewe/Bi. Tamima kinyume. ana vipusa nje/kazija.
- Aliendeleza biashara za magendo na kuficha pesa nje ya nchi licha ya kudai kuwa mzalendo.

(v) Amejaa ubinafsi
- Alijitenga na wananchi na kujali wenye pesa pekee- Smith
- Hakuruhusu mtu kuingia au kutoka kwake bila idhini yake
- Alimfukuza nduguye Fadhii alipokataa kushirikiana naye kwa manufaa yake-ubunge
- Alidhalisha wanawake kwa kuwaita paka, mbwa, maskini, viumbe vya kuliwa n.k

(zozote 5x2 = al.10) (kutaja -1, maelezo/mfano -1 = ala. 2)

(c) Mafunzo ambayo Umma unajifunza kutokana na kisa kinachoza mazungumzo haya ni (alama6)

(i) Mabadidliko yanahitaji ujasisir. Inspekta Fadhili anakataa kushiriki katika uhalifu na nduguye Bw. maksundi
- Alikataa kuhongwa kuficha ushahidi wa uhalifu/kesi ya jinai dhidi ya Bw. Maksundi

(ii) Uwajibikaji kazini – Inspekta Fadhili alimkataza ndeugye Bw. Maksundi dhidi ya kujilimbikia mali ambazo si za halali.
- Alihoji chanzo utajiri wa Maksundi akitilia Maanani mshahara wake
- Alikataa kuchukua hongo kama wafanyavyo wakubwa wake katika madai ya Maksundi

(c) - Utiifu na mazingatio ya sheria na kanuni za kazi
- Alimtia mbaroni Bw. Maksundi (nduguye) na Zanga

(d) Kuwa na msimamo thabiti
- Inspekta Fadhili alidumisha msimamo wake wa siasa za ujamaa kutetea wanyonge kutoka wakati wa ukoloni hadi sasa licha ya vishawishi vya pesa.
- Bw. Maksundi na Zanga walibadilika na kuwa mabepari makabaila

9 . (a) Anayesema ni Bw. Maksundi
Akimwambia Inspekta kadhili
Wakiwa nyumbani kwa Bw. Maksundi.
Fadhili alikuwa amepata mwaliko kutoka kwa kakake

(b) Mbinu
Balagha – wewe nani hasa wakukutaa ?
Mdokezo – Hapo ndipo ninapokuona mjinga … (2x1=2)

(c) Sifa nne za mzungumzaji – maksundi
(i) Mkatili
- Anampokonya Mwanasururu mali na kumtaliki

Kumtawisha mkewe na bintiye

-Kumchapa mkewe na kumetenganisha na kitoto chake

(ii) Mwepesi wa hasira

Hasira zinampanda kwa haraka pale anapokuta kwake bado kwawaka taa usiku wa manane

(iii) Mzinifu/mkware

- Yeye ni mteja wa Kazija ambaye ni kahaba

(iv) Mfisadi

- Anakabiliwa na shtaka la ufisadi na kufungwa jela
- Mazungumzo yake na Mr. Smith yanalenga ufisadi
- Ametajirika kwa haraka

(v) mbinafsi

(vi) Mnafiki- Anapoenda kwa kazija ingawa anajulisha kwake kwamba anaenda kufanya maombi kwa kaburi la shehe wake

(vii) Mpenda anasa - Kila mwezi anajipa wiki nzima ya kwenda kujistarehesha kwa kazija

(d) Maudhui mawili yanayojitokeza katika dondoo

(i) ufisadi - Maksuudi alitaka kumhonga Inspekta Fadhili afiche habari kuhusu kesi ya ufisadi iliyokuwa ikimkabili

(ii) Uongozi mbaya - Maksundi alitrajia kugombea kiti cha ubunge, kwa hivyo alitaka kesi ya ufisadi iliyomkabili isijulikane na wananchi. Kwani huenda ikamharibia nafasi ya kuibuka mshindi

(iii)Kutoajibika - Maksuudi alitaka kutumia mamlaka na uwezo wake kuficha uozo alio nao

10. UOZO

Ukahaba

– Kazija alishiriki ukahaba pale kwake
– Aliwakaribisha wanaume na hata kuwalewesha k.m. Musa, Maksuudi
– Mama Jeni na Biti Sururu wanashiriki na kukuza madanguro. Wanatumia wasichana wadogo kama vitega uchumi vyao
– Wanawanasa wanaume kama James na Shoka ili kuwapoka pesa na wakati huo huo kuwaharibu wasichana na kuwakosesha maadili
– Biti Sururu ameendeleza ukahaba, anampokea Maimuna, anawazungusha wanaume walevi kana kwamba anamnadi Shoka anaendeleza ukahaba kwa kuwa na macho ya nje

(ii) ULEVI

- Musa ni kijana mdogo, anajizamisha kwenye anasa ya ulevi. Katika hali hiyo anafoka kijinga na kumtusi Kazija
- -Shoka alishiriki ulevi na kumaliza pesa zake na kuisahau jamaa yake
- Maimuna anazidi kujidhuru afya yake kwa ulevi wa pombe kali. Ilimfanya akapoteza urembo wake
- Mamake Kabi (Mwanasururu) katika hali ya ulevi wake anajaribu kumshurutisha mwanawe kutenda ‘maovu’
- Walevi ni kama Manda walioshiriki kwa Biti Surru. Badala ya kuwakanya na kuwatenganisha kijakazi na Maimuna waliwachochea wapigane zaidi

(iii) KISASI

- Hali ya kulipiza ubaya uliofanyiwa mtu mwingine. Wanaoshiriki ni Kazija, Maksundi – kutenganisha familia yake
- - Kazija amepanga njama ya kumfumanisha Bwana Maksundi na manaye Musa wote wakija kwa shughuli za ukahaba
- Bi Farashuu na Biti Kocho wanafaulu kutenganisha familia ya Bwana Maksundi zaidi kwa kumtorosha Maimuna nyumbani kwao

- Bi Kazija kumwangusha Maksundi kisiasa pale uwanjani wa Uhuru. Anapopata kusema, anamchambua Bw. Maksundi kama mtu ovyo aliyeshindwa kuendesha nyumba yake, mnyang'anyi, na aliyesababisha kifo cha mke wake wa kwanza.
- Katka uwanja wa Uhuru, umati unataka kulipiza kisasi dhidi ya Bwana Maksundi ingawa mpango huu unatibuliwa na Inspekta Fadhili anapowaka moto na kupelekwa kortini

(iv) UFISADI
- Ni kitendo cha kupokea hongo ili kumtendea mtu jambo fulani
- Baada ya uhuru, Bwana Maksuudi alipata cheo cha mkuu wa wilaya alitumia kujitajirisha .
- Pia alipokuwa mkurugenzi wa shirika la bima la Taifa
- Bw. Maksuudi alimtaliki, Mwanasururu ili apate fursa ya kupora mali yake aliyoachiwa kama urithi na babake
- Mazungumzo ya Bw. Maksuundi na Mr.smith inaonyesha dhahiri kuwa wanazungumzia swala la ufisadi ambako wangawana pesa nusu bin nusu
- - Ushawishi wa Bw. Maksuudi kwa Inspekta Fadhili ili afiche vitendo vyake vya kifisadi

(vi) UNYANYASAJI WA WANAWAKE (UKATILI)
- Bi Tamima na Maimuna wanatawishwa nyumbani na Bw. Maksuudi
Bi Tamima anachapwa akiwa angali na tumbo bichi/bado tu ya kujifungua
Biti Kocho na Bi Farashuu wanamtorosha Maimuna nyumbani kwao wakifahamu tosha kuwa nia yao ni kumkaribia maisha
Mwanasururu kwa kuteswa na kuchapwa, na kunyang'anywa urithi alioachiwa na babake na Bw. Maksuudi
Bi. Selume anadhulumiwa na mumewe Shoka kwa kuachiwa aikimu familia yao pekee. – Mumewe pia anatembea na wanawake wengine nje ya ndoa k.m Maimuna na Kijakazi.

(v) UONEVU WA KITABAKA
- Wenye mali waliishi katika mita ya kifahari yenye taa na barabara nzuri kama Liwanzoni na Pumziko
Tabaka la chini liliishi katika vibanda vibovu penye mitaro michafu, mavumbi, bila taa, wala barabara k.m. alikoishi Biti Sururu

(vii) UONEVU WA KISIASA
- Wakolon wajerumani waliwatesa wapigania ukombozi mfano ; Sakamu ya wazalendo inaonyesha viungo vilivyokatwa katikati
- Baada ya uhuru uonevu huu unaendelezwa na Maksuudi na Zanga. Wanajilimbikizia mali, majumba , magari na fedha (zozote 5x4=20)

11 Akakumbuka ubeti wa shairi alilotunga karibuni katika jumla ya mashairi aliyoyakusanya katika kitabu alichokiita kilio cha wanyonge

a) Muktadha
i. Haya ni maneno ya mwandishi
ii. Anaeleza yalimpitikia inspekta Fadhili mawazoni
iii. Inspekta Fadhili yumo ukumbini mwa kakake Maksudi ambamo Maksudi amemwalika
iv. Fadhili aliwasili na akamkuta Maksudi akijizoeza kutoa hotuba, na Fadhili akashangazwa na zana zilizokuwa pale nyumbani
v. Ndipo akakumbuka ubeti wa shairi alilotunga Zozote 4x1=4

b) Ujumbe katika shairi
i. Wanyonge wanalima lakini hawapati mavuno ya kazi yao
ii. Wafanya kazi walifanya kazi sana lakini walilala njaa
iii. Wanyonge na wafanya kazi walikumbwa na maradhi
iv. Walikosa elimu wakabaki ujingani
v. Waliahidiwa shibe, matibabu na elimu na watetezi wa uhuru
vi. Lakini uhuru ulipopatikana hali yao haikubadilika

vii. Ukoloni uliondoka Afrika lakini kuacha ukolono mamboleoTUZA Zozote 6x1=6

Onyesha Inspekta Fadhili anavyotofautiana na kakae maksudi

i. Maksudi ni mfisadi anayejitajirisha na mali ya uma- Fadhili ni mwadhilifu na anapigana na ufisadi
ii. Maksudi anaonelea kuwa tofauti zao ni za kisiasa- Fadhili anashikilia kuwa hawafai kuwa na siasa tofauti kwasababu siasa ya nchi yao ni moja
iii. Maksudi anataka fadhili amfichilie zile habari za kesi ya magendo aliyo nayo isitoke na kumharibia kura. Fadhili anakataa kudidimisha kesi hii kwa madai kuwa yeye ni mtumishi wa umma aliyeaminiwa kulinda uhuru, haki na usalama
iv. Maksudi ana ubinafsi wa kujilimbikizia mali- Fadhili hapendezewi na ubinafsi huu ni mtumishi wa umma
v. Maksudi anajaribu kumhonga Fadhili ili afiche habari ya kesi ya magendo – fadhili anakataa hongo yake
vi. Maksudi anamwona Fadhili kuwa mjinga kwa kukataa hongo ilhali polisi wengine wanaichukua – Fadhili anashikilia kuikataa hongo
vii. Maksudi anaamini kuwa atashinda kiti cha ubunge anachogombania- Fadhili anamweleza kuwa hawezi kushinda kwasababu watu wamechoka kudanganywa na wanafiki kama yeye
viii. Maksudi ni mnafiki- alijifanya mzuri, mcha Mungu na mtetezi wa wanyonge ili apewe cheo kisha ajitajirishe
ix. Fadhili ni mkweli na mpenda usawa na ndio sababu alipendwa na umma aliyoifanyia kazi
x. Maksudi alichukuliwa na watu kwasababu alizingatia haki na usawa Zozote 10x1=10

12. Mwanamke kama kikwazo cha ukombozi wake

i. Bi Farashuu anataka kulipiza kisasi kwa kifo cha bintiye (mwanasururu) kwa Bw. Maksudi. Badala ya kukabiliana na Maksudi mwenyewe, anawaharibia Maimuna na mamke maisha yao
ii. Binti Kocho, kwa ushirika na Bi Farashuu, anamchochea maimuna kutoroka kwao huku akiwa na nia ya kumharibia maisha
iii. Maimuna anapotorokea kwa Bi.Farashuu, badala ya Farashuu kumsaisia, anamsafirisha hadi kwa mama Jeni akiwa na nia ya kumwingiza katika maisha ya ukahaba
iv. Badala ya mama Jeni kama mwanamke aliyekomaa kumpa malezi mema, Maimuna ambaye yungali mchanga, anamtafutia wanaume wa kufanya naye mapenzi huku yeye mwenyewe akinufaika kwa malipo anayopewa
v. Mama Jeni anawatumia wasichana wengine wachanga kama vile Dora kuwashirikisha ukahaba
vi. Maimuna anapotorokea kwa binti Sururu hapati afueni. Licha ya binti sururu kuendeleza ukahaba, anamfanya Maimuna kuanza kutumia pombe ambayo inamwathiri hata zaidi
vii. Kijakazi kumwonea wivu Maimuna na kumsengenya badala ya kumwona kama mwenzake katika maisha magumu ya ukahaba. Baadaye wanapigana na kuumizana vibaya
viii. Kabi anapotaka kumuoa Maimuna, Bi. Farashuu anapinga wazo hili licha ya kuwa ndiye aliyemfanya maimuna kuwa kahaba
ix. Bi. Tamima hatetei haki yake nay a bintiye. Anakubali kudhibitiwa na mumewe bila pingamizi na hata kufikia kiwango cha kumpigia magoti na kuomba msamaha licha ya kuwa hajatenda kosa lolote
x. Bi. Kazija anakubali kutumiwa na Bi. Farashuu kulipiza kisasi kwa Bw. Maksudi. Licha ya kuwa anachukia wanaume, angetumia njia nyingine ya kujipatia pato badala ya kufanya ukahaba
xi. Selume hasaidiwi na mumewe Shoka kuikimu familia yao. Selume anafanya juu chini kutafuta chakula. Wakigombana, Shoka hutoweka nyumbani kwa muda wa wiki nzima hadi Selume amtafute. Selume angejikomboa kutokana na ndoa iliyoegemea upande mmoja

Kazija kumchukua maksudi ilhali anajua kuwa ana bibi na watoto. Anamharibia maisha ya familia yake

13. (a) - Yalisemwa na Kazija.
- Anamwambia Musa.
- Musa alikuwa mlevi huku akiropokwa kuhusu wanawake ndipo Kazija akamjibu kwa hasira.
- Kazija alikuwa amepanga njama ya kuwakutanisha Musa na babake. (4 x 1= al. 4)

(b) - Mwanamke hutumika kukidhi matakwa ya wanaume kama Kazija.

- Kupigwa vibaya kama Bi. Tamima na Mwanasururu walivyopigwa na Maksuudi
- Mwanamke kutalikiwa vivi hivi bila sababu k.m. Tamima na Mwanasururu.
- Wanawake kutawishwa na kunyimwa uhuru k.m. Tamima na Maimuna.
- Mwanamke kutumikishwa kikahaba k.m. Maimuna na wengine.
- Kuhiniwa mali kwa mwanasururu na Farashuu.
- Kubaguliwa hata baada ya uhuru – kuendelea kunyimwa usawa hasa ile sanamu ya mashujaa.
- Wasichana wa Farashuu kuoka mikate hadi usiku wa manane. (Hoja zozote 4x2= al.

(c)- Kazija achukua hatua ya kulipiza kisasi dhidi ya maksuudi.
- Anamweleza maksuudi uovu wake na kumuonya.
- Biti Kocho aonyesha kwamba umoja wao utawaangusha waovu kama Maksuudi ili wajikomboe.
- Maimuna ajijasirisha na kutoka nje ya kasri.
- Maimuna aamua kuachana na ukahaba.
- Biti Sururu anajihusisha na uuzaji wa vileo kuibadilisha hali yake ya kiuchumi.
- Farashuu akazania ulipizaji kisasi kwa ajili ya mali yake ili kumkomesha maksuudi.
- Farashuu anashughulika na uokaji wa mikate ya kuuza.
- Biti Kocho ana mpango wa kupata kiwanja na kujenga /anakataa utumwa wa maksuudi.
- Mke wa japu anaenda kwa mkuu wa Wilaya kupata hati ya umiliki wa ardhi.
- Selume ang'ang'ania kuwakimu watoto na anamsuta mumewe shoka kwe uzohali.

14. (a) MAKSUUDI

- Anajutia kumfukuza bibiye Tamima
- Ajutia unyama aliomtendea Mwanasururu
- Ajutia kumtawisha Maimuna na Tamima
- Ajutia unyang'anyi alioutendea Umma
- Ajutia alivyotengana na mwanawe Musa
- Ajutia kujilimbukizia mali
- Ajutia kushiriki ufisadi
- Ajutia mateso ya jela yaliyomponza hata akawa kilema
- Ajutia kupoteza muda katika jela
- Ajutia hali ya upweke/ukiwa
- Ajutia kupoteza mali yake
- Ajutia kuwadhulumu watu wengine (zozote 5x2=al. 10)

(b) MAIMUNA anajutia;-

- Kutoroka kwao
- Hali yake ya ukahaba
- Kutengana na aila yake
- Kupapia uhuru ambao umemuumiza
- Kifo cha babake kabla ya kutangamana naye
- Mateso ya mamake
- Kitendo cha kuolewa na Kabi (zozote 5x2=al. 10)

15. – Mwanamke anatawaliwa na mwanaume aghalabu hupigwa na kunyanyswa mf. Bi Tamima na Mwanasururu.
- Mwanamke kama pambo na chombo cha starehe. mf. Kazija na wasichana wengine.
- Mwanamke hana sauti ndani ya familia, m.f. Bi Tamima.
- Mwanamke anatengwa na jamii katika masuala ya kisiasa na uongozi
- Mwanamke hapewi fursa ya kustosha katika masuala ya elimu mf. Maimuna
- Wasichana hawana ujasiri wa kuwashirikisha wazazi katika masuala yanayowahusu hasa ya kimapenzi k.mf Maimuna anashindwa kumweleza Tamima hamu yake ya kutoka nje.
-Mwanamke anawajibika katika kuikimu familia hasa watoto kwa mfano zingatia Selume

anavyojitahidi kwa kila njia kutunza familia yake.
- Wanawake ndio wanafanya kazi zote za nyumbani : Rejelea kwa watumishi wa Tamima na wasichana waokaji wa mikate kwa Farashuu

16. (a) Maneno haya anayasema Bi farashuu na anamwambia mjukuu wake Kati. alikuwa nyumbani kwa Kabi.

(b) - Anayezugumzia ni mchumba wa mjukuu wake, anaitwa maimuna .
- Babake alimtesa mtoto wa Bi. Farashuu
- Farashuu ana hasira na familia ya Maksundi akiwemo Maimuna
- Hakutaka aonekane kwake akiwa salama.
- Maimuna alikuwa chakaramu – asiyestahili kuolewa na mjukuu wake.
- Familia ya Masuudi ilikwisha hathirika na kusambaritika

(c) – Takriri – neno mtoto
- Mdokezo ....
- Msemo – Hana siri wala fasiri
- Swali la balagha – dondoo lenyewe

(d) Amekuja kutambulishwa kwa mchumba wa mjukuwe Kabi

(e) - Kabi alitoka kuwaacha nynanyake na Maimuna
- Maimuna na Farashuu walibishana kuhusu matendo yake
- Baadaye wakatambua mkosa yao kisha wakasameheana
- Farashuu akawabariki Kabi na wakasameheana
- Ndoa ikafungwa ya Kabi na Maimuna Wakahama

17. (a) (i) Maneno ya Bi Farashuu
(ii) Anamwambia Biti Kocho
(iii) Ni nyumbani kwa Bi Farashuu – Madingo poromoko
(iv) Farashuu alishangaa sababu ya Biti Kocho kuenda kumchukua ili akamsaidie mke wa tajiri wao
(v) Biti Kocho alimwambia haya ni kati ya njama ya kutaka kumtorosha Maimuna
(vi) Farashuu alifurahi alipotambua kuwa lengo la Biti Kocho ni kumsaidia kulipiza kisasi Maksundi.
(vii) Kwa uchungu mwingi alieleza maovu ya Maksundi na unafiki wake ndipo akasema maneno haya (8 x 1= al. 8)

(b) (i) Kazija alifanya njama ya kumfumanisha Mussa na babake.
(ii) Alimpa Mussa miadi ya kufika saa tatu na maksundi akaambiwa afike saa sita.
(iii) Maksundi alipokutana na Mussa alimpiga nusura amwue.
(iv) Mussa alilazimika kuchopeka vidole vyake kwenye macho ya babake na akafaulu kutoroka.
(v) Alipoachiliwa hakuonekana tena nyumbani kwao a hata kwa Kazija – alitengana na babake.
(vi) Alizomewa na Kazija na akalazimika kurudi nyumbani usiku wa manane kwa miguu.
(vii) Haya yote yalipangwa na Farashuu ili kukamilisha kisasi cha mateso aliyofanyiwa Mwanasururu na Maksundi.
(viii) Usiku huo huo Maimuna alitoroka kwao na kwenda kumtafutia mamake mkunga (anakaidi amri ya kutoka nje)
(ix) Kisha baada ya kurudi nyumbani usiku huo, alitoroka kwao ili kutafuta uhuru baada ya kuonja uhuru wa siku moja.
(x) Maksundi anaporudi anamlaumu Tamina na kumpiga sana kisha kumtaliki.
(xi) Hatimaye Kazija anamfedhehesha katika uwanja wa uhuru
(xii) Baadaye anamtumikia kufungocha miaka miwili baada ya kupatikana na makosa ya jinai

(c) (i) Mwenye bidii
(ii) Mwenye kisasi
(iii) Katili
(iv) Mnafiki

(v) Mkarimu
(vi) Mshirikina
(vii) Msiri
(viii) Msamehevu
(ix) Mpole/Mtulivu
(x) Mwenye majuto
(xi) Mwenye huruma (4x1= 4)

18. (i) Kazija kuchukia wanaume ilhali anajipamba kwa sababu yao.
(ii) Maksundi alipofika kwake na kusikia sauti ya kitoto anakasirika badala ya kufurahi
(iii) Biti Kocho anamwambia maimuna "mjukuu wangu, dunia furahi" usemi huu ni kinyume na nia yake iliyokuwa kumtia Maimuna matatani.
(iv) Azimio la Farashuu kuenda kumtafuta Tamina ili ashiriki katika poso ya Maimuna ni Kinaya.
Hapoawali Farashuu alimpeleka Maimuna pumziko ili wawili hawa wasiweze kukutana
(v) Matokeo ya Maksundi huku Rumbalola ni kinyume na matarajio yake. Alitaka kumuona Maimuna lakini badala yake anapigwa vibaya.
(vi) Kinaya kwa Mama Jeni anapomhoji Maimuna na kudai kutojua kilichokuwa kikiendelea. Yeye ndiye aliyemfungia kwa chumba kimoja na James.
(vii) Kinaya kwa Maksundi na Zanga kuomba kura na kuwaambia kuwa wanahitaji viongozi kama wao na wao ni fisadi wadhalimu.
(viii) Kinaya Maimuna anapopewa chumba kibovu chenye mazingira mabaya na atarajiwe apate usingizi mzito.
(ix) Kinaya Maksundi anapojihusisha na matendo mabaya ilhali yeye ni mtu wa dini.
(x) Kinaya Farashuu anaposema kuwa atampeleka Maimuna pumziko akapumzike. Hatumwoni akipumzika na badala yake masabiu yake yanazidi.
(xi) Taswira ya shoka haipendezi lakini mwandishi asema " juu ya urembo huu kupambwa"
(xii) Maimuna anapotoroka anatarajia maisha ya furaha na uhuru. Badala yake anaishi maisha duni
(xiii) Maimuna kulalamika wanakandamizwa ilhali wao wenywe wanakandamiza wenzao.
(xiv) Maimuna alikuwa akichukiwa sana na Bi Farashuu mwishoni anaolewa na mjukuu wake Kabi.
(xv) Maimuna huishi uwazoni na mamake lakini hawapati liwazo lolote kutokana na dhuluma za Bw. Maksundi.
(xvi) Maimuna maksundi kupigania uhuru kwa dhati lakini nia yake ni kupata cheo baadaye ili ajinufaishe.
(xvii) Maksundi ni shehe lakini vitendo vyake ni vya uzinzi, ufisadi na dhuluma (al.10 x2= 20)

19.
- Wanaume wanapenda sana kujiweka mbele katika mambo ya elimu na kuwabagua wanawake
- Kazi yote ya nyumbani inaachiwa mwanamke k.v. kupiga pasi, kupika, kuosha n.k. Mwanaume hasaidii kwa vyovyot
- Mwanamke hushika mamba au huza, lakini mwanaume hazai
- Mwanamke hapati kazi nzuri kama ile inayofanywa na mwanaume
- Mwanaume aghalabu hutoa ahadi za uongo mfano Bwana maksudi kutochaguliwa na wanawake katika auchaguzi
- Mwanaume ni fisadi mfano maksudi na washirika wake
- Mwanaume kuwa na kasumba ya kuwa ukahaba hutendwa na wanawake lakini sivyo kwani hutendwa na wote – wake kwa waume
- Mwanaume ni mlaghai mfano maksudi alimlaghai Bi. Sururu mali yake
- Mwanaume hawajibiki ipasavyo mfano shoka
- Mwanaume ni katili Hoja 10x2=20

20.
- Utengano wa kifamilia – Maksudi atengana na familia yake.

- Utengano wa kijinsia – wanawake wametengana na wanaume kupitia taasubi ya kiume
- Utengano wa watawala na watawaliwa – Bwana Maksudi ametengana sana na watu anaowatawala mfano akiwa mkuu wa wilaya
- Utengano wa kitabaka – mtajiri kwa maskini
- Utengano unaotokana na kifo – Bi Tamina na kitoto chake kichanga
- Utengano wa kimaadili – Mama Jeni anafanya biashara ya danguro Zozote 5x4=20

21. a) - Haya ni maneno ya mwandishi
- Alikuwa akieleza kuhusu Bwana Maksudi alivyombadilika
- Alikuwa anamcha Mungu sasa

b) - Mke na watoto wake walikuwa wametoroka
- Alikuwa mgonjwa
- Alikuwa mpweke
- Hakujua cha kufanyia mali yake
- Hakuweza kufikia mali yake
- Alikuwa amefungwa jela
- Hakuwa na rafiki

c) - Alikuwa mfisadi
- Ni katili
- Alishiriki ngono na wanawake wengi
- Alikuwa muuaji

d) Tashhisi – Mshibe Mungu
Kutaja alama 1 Mifano alama 1

22. Mambo anayoyakashifu mwandishi
- Ufisadi
- Ukahaba
- Ulevi
- Ukatili
- Ubaguzi wa kitabaka
- Utawishaji
- Ulipizaji wa kisasi
- Taasubi ya kiume
- Dhuluma
- Kutowajibika

23. a) Muktadha
i. Anayezungumza ni Bwana Maksudi
ii. Anazungumza na Mr. Smith kwa simu
iii. Mr.Smith ni mshirika wa Bwana Maksudi kibiashara
iv. Mazungumzo haya ya simu yanatokea nyumbani mwa Bwana Maksudi
v. Inspekta Fadhili alikuwa amengojea sebuleni (Alama 4x1=4)

b) Ujumbe wa shairi la "Kilio cha mnyonge"
i. Wakulima walilima lakini hawakuona faida yao
ii. Wafanyikazi walijibidisha kazini lakini walilala njaa
iii. Wao walikumbwa na magonjwa ya kila aina
iv. Watu walikumbwa na ujinga wa kila aina
v. Ubaguzi ulikuwepo
vi. Bara la Afrika bado linatawaliwa kupitia mlango wa nyuma
vii. Ukoloni mamboleo wa kutoka nje na ndani (Uk 71 – 72) (Alama 6x1=6)

c) Uovu wa mzungumzaji

i. Fisadi – mazumgumzo baina ya Maksudi na Smith alichukua shillingi mia 200 kutoka kwa mkewe mzee Japu. Nyumba na shamba kwa mpango wa siri
ii. Mnyang'anyi – alimdanganya mwanasururu
iii. Mwenye tama mali/ ubinafsi – hakujali yeyote haswa kama kiongozi. Alitumia cheo chake ili kujitajirisha
iv. Mnafiki – Alipigania uhuru akiwa na nia ya kuchukua nafasi hiyo kujirundikia mali
v. Katili – Alimpiga mwanasururu na kumtaliki, Alimpiga Bi. Tamina akiwa na uchungu wa uzazi, Alimpiga Mussa nusura kumuua
vi. Msherati – Alikuwa na uhusiano wa nje na Kazija
vii. Kuwatisha – Aliwafungia Tamina na maimuna
viii. Msaliti – Alisaliti imani ya wananchi kwake. Aliwasaliti wanawake aliowaoa
ix. Mwenye dharau – Alidharau wanawake/ alidharauwanawake/ alidharau watu wa tabaka la chini
x. Mwenye taasubi ya kiume/ ubabedume, Aliamini mwanamke ni mwepesi ni mwepesi wa kuliwa , kuwatisha wanawake, kuwapiga wanawake
xi. Mwenye kiburi/ dharau
xii. Mgomvi – aligombana na Tamina, Mwanasururu, Mussa na Fadhili Zozote 10x1=10

24. a) Muktadha

i. Msemaji ni mama Jeni
ii. Akimwambia maimuna
iii. Walikuwa kwenye mkahawa wa café Afrique
iv. Walikuwa wameenda pumziko ili Maimuna anunuliwe nguo 4x1= 4

b) Sifa za aliyeelekezwa maneno

i. Mwenye kisasi – ana kisasi kwa babake kwa kumtawisha
ii. Mwepesi wa hamaki – anakasirishwa na maneno ya kijakazi, pia anamsimanga James
iii. Mpenda anasa (Uroda) Anaishi maisha ya anasa
iv. Mkosa tahadhari – hajali hatari inayoweza kumkabili baada ya kutoroka nyumbani kwao
v. Msamehevu – anamsamehe babke na Farashuu Zozote 4x2=8

c) Mabadiliko yaliyotokea

i. Familia ya Maksudi inabadilika baada ya usiku wa fumanizi
ii. Maksudi anapanda cheo, anakuwa mwanasiasa, anafungwa jela, afya yake inadhoofika
iii. Kiburi cha maksudi kinayeyuka, utajiri unamkwepa kisha anathamini utu
iv. Anawathamini watoto na mke wake kasha kuanza kuwatafuta
v. Mussa anawacha tabia ya ukware anazingatia masomo na kuwa daktari
vi. Uhasama wa Mussa dhidi ya babake unaisha kasha anamhudumia hospitalini
vii. Mussa anamuoa Sihaba kinyume cha matakwa ya babke
viii. Mwanasururu ananyang'anywa mali yote na kutalikiwa akiwa mlevi, mwendawazimu na akafa
ix. Maimuna anatoroka nyumba kubwa na kuwa kahaba na kujiingiza na ulevi
x. Maimuna anakuwa mwimbaji hodari wa nyimbo na hataki
xi. Kuna mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kimazingira n.k Zozote 8x1=8

## TAMTHILIA: KIFO KISIMANI: KITHAKA WA MBERIA

1. Athari za utawala mbaya kwa jamii

- Dhuluma- unyanyasaji- usaliti
- Wanajamii kutiwa kizuizini kwa kuchongwa makosa- Mwelusi
- Wanajamii kulazimishwa kuhudhuria mikutano ya kisiasa
- Makabila kuchochewa/ kushambuliwaili kueneza hofu- Wanabatuitui na Wabausi
- Wanajamii kuteswa kwa kuuawabila sababu maalum- Askari wa pili na mshukiwa- Mwelusi

- Mwelusi kuteswa na baadaye kuuwawa
- Ukosefu wa chakula kusababisha njaa
- Uharibifu wa mazingira na viongozi kunyakua misitu kujifaidi
- Unyakuzi wa ardhi ya umma- uwanja wa kuchezea watoto
- Wananchi kunyimwa haki za kutumia raslimali za jamii- maji ya kisima
- Jamii kugawika katika matabaka mbalimbali viongozi na vibaraka wao kisha wananchi
- Mauaji ya wazalendo wanaopinga utawala mbaya
- Mizozoz katika familia- Nyalwe anazozana na mumewe Bokono kwa kuupinga utawala mbaya
- Gege anazozana na mamake kwa kuwa kikaragosi wa kutumikia utawala mbaya
- Gege anazozana na hatimaye kumuua nduguye Mwelusi kwa kudanganywa
- Ufisadi- Watu kuajiriwa bila kuzingatia uwezo/ elimu au tajriba- motto wa Kaloo
- Unyanyasaji wa kijinsia- Andua kupapaswa

2. Jamii ilivyojaa uozo katika mayai Waziri wa maradhi na hadithi nyingine

UTEZI WA MOYONI

- Wanawake kutopewa elimu ya kuwawezesha kujikimu
- Wanawake wanaozwa wangali wachanga wala hawana hiari ya kujichagulia waume
- Taasubi za kiume k.m Ali alivyomdhibiti Zena na wanawake kulaumiwa kwa kukosa kuzaa
- Wanawake kuchukuliwa kama vyombo vya wanaume na kupigwapigwa bila sababu
- Wananchi kuuza kura zao badala ya kushiriki katika kujagua wabunge watakaotetea haki zao

SIKU ZA MGANGA

- Watu kumwendea mganga mganga ili kupata cheo
- Mganga kumpatia Asteria mume wa mke mwingine kwa kutumia uganga
- Mganga Mwaibale kuwaibia wateja kwa kudai alinunua jembe kila wakati
- Uzinifu- Asteria na mazungumzo yake na rafikiye kuhusu kiruka njia

KACHUKUA HATUA NYINGINE

- Uongozi mbaya unaokubali mauaji ya wapinzani k.m. Kala nduguye Sakina
- Chifu kuuza chakula cha bure kilichotolewa kwa watu maskini
- Jirani kumtunga motto wa Mavitu mamba
- Mavitu kunyang'anywa kipande cha ardhi na jirani na deni lake kuongezwa

PWAGUZI

- Shehe kijuba kujihusisha na upigaji ramli
- Salimu kuwaibia watoto 2500/= na Shehe 10,000/=
- Tamaa ya shehe kumfanya amkaribishe Salimu kwake akamfungie vijana ili aendelee kupiga bao
- Shehe Kijuba alikuwa mnafiki aliyejifanya kuelewa mambo ya dini lakini wapi

TUZO

- Ufisadi unamfanya profesa Dzoro umtangaza Salome Dzoro kama mshindi kwa kuwa alikuwa amu yake
- Unafiki- Salome kumdanganya Kibwani kuwa alikuwa mshindi akijua vizuri kuwa ilikuwa uongo
- Ubaguzi- Profesa Dzoro kuwabagua washindani wengine na kuchagua aliyekuwa naye na uhusiano wa kidamu

Hakiki majibu ya wanafunzi na kuutuza hoja yoyote nyingine iliyo sahihi

Zozote 10x2 alama 20

3. (i) Anayezungumza ni Bokono
(ii) Anazungmza na washauri wake Batuzigu na Kame
(iii) Wako katika ukumbi wa utawala wa Mtemi Bokono
(iv) Washauri walikuwa wakingoja Bokono aliyetaka kujua hatua watakazochukua kua(washauri) kumkomesha Mwelusi (1x4=al.4)

(c) Sifa za msemaji

(i) Mkatili

- Anashiriki katika kuwatesa wansnchi anaowatawala, pia anaamrisha aksari kuwa wale wote wanaokosoa viongozi wateswe kwa kupwa gerezani

(ii) Ni mwenye kiburi

- Anaonyesha kiburi kwa mkewe anapomkosoa
- Hamsikilizi mama Agoro anayekuja kulalamika kwa kwake kuhusu kunyakuliwa kwa kiwanja

(iii) Mfisadi

- Yeye pamoja na viongozi wengine wanashirikiana kupoa mali ya wanachi kama vile ardhi, kisima cha Mkomani n.k

(iv) Ni Mkware

- Ana tamaa ya wanawake
- Anafanya mapenzi haramu na hawara Fulani aliyepigwa na mkewe. Anamnyemelea Kaloo

(v) Mbinafsi

- Utawala wake unalengo la kumnufaisha yeye kwani anautumia kukilimbukizia mali

(vi) Mnafiki – Amejua hapendwi lakini anajifanya anapendwa

(vii) Mwenye majivuno – Nadai kuwa uongozi wake ni bora kuliko wa watu wote

(viii) Ni mwoga – Alihofu sana pale alipohisi kuwa angeweza kung'atuliwa (zozote 5x2=al.10)

(c). Mbinu za Sanaa

- Jazanda/Istiari - Mwiba –kumnyelea mweluso
- Uhuishi / Tashhisi – Butangi iko safarini – Butangi imo mbioni (2x2=al.4)

(d). Maudhu

Udhalimu/Unyanyasaji – Vitendo vya kutoa mwiba mguuni ili Butangi kendelee (kumuua Mwelusi)

AU

4. (I) Gege na Mwelusi

(a) Mwelusi ni mjasiri – anaamua kukabiliana na utawala wa Mtemi Bokono. Haogopi kuteswa na askari. Gege ni mwoga anaogopa kuwakasirisha viongozi, anapitwa an aMweke anatetemeka,

(b) Mwelusi ni mwerevu- anauelimisha umma wa Butangi kuhusu uovu wa utawala wa Butangi na namana wangewa kujikwamua kutokana na uongozi huo-mbaya. Anatumiwa kumuua nduguye

(c) Mwelusi ni mwadilifu – Anashiriki na wanawake katika vita vya ukombozi lakini mapenzi nao (Atega). Gege ni mnafiki /mwongo. Anadanganya mamake

(d) Mwelusis ni mzalendo- anapenda nchi yake ndiposa anajitolea mhanga kupigania mabadiliko. Gege ni mbinafsi – hataki kushughulikia mambo yaw engine

(e) Mwelusi ni mvumilivu – anavumilia mateso ya askari huko gerezani. Gege ni mbishi anabishana na Mwelusi kuhusu utawala wa Butangi, Anabishana hata na mamake Mwelusi anamsimamo thabiti- anashikilia msimamo ule ule wa kupigania haki za wanabutangi hadi mwishoni. Anakataa vishawishi vya Bokono. Gege ni msaliti , anamsaliti ndugu yake pale anapotumiwa na utawala wa Bokono. (zozote 4x4=al.16)

5. Mchango wa wahusika

Mwelusi

(i) Alitambua chanzo cha matatizo/shida za wanabutangi

(ii) Mwelusi na wenzake wajiitao « Nuru ya Butangi » waliwazindua raia kupitia elimu kuhusu haki zao. Gege anathibitisha hayo.

(iii) Mwelusi aliwaongoza raia kupigania haki zao kwa kuvunja kanuni/sheria potovu na basi kuleta mabadiliko.

(iv) Alijitolea kuteseka na hata kuuwawa kwa ajili ya mabadiliko (Zozote 4x1=4)

(b) Raia (Tanya, Atega, Andua) au umma.

(i) Raia walisusia mkutano ambao ulifaa kuhutubiwa na mtemi Bokono

(ii) Raia kama vile Andua waliandamana na kutetea haki zao kama kuchota maji kisimani – mkomani.

Andua alimkabili zigu kijasiri akidai haki ya kutumia maji ya kisimani.

(iii) Raia kama vile Tanya walianza kupinga washauri wa Mtemi Bokono. Tanya alimpinga Batu na kufichua uovu wa serikali ambayo kupitia kwa Batu inatumia askari wa kukodi kuwashambulia raia ili kulazimisha uzalendo.

(iv) Raia walisaidia mfungwa (Mwelusi) kutoroka kutoka gerezani. Atega alimpelekea Mwelusi tupa aliyoitumia kukata minyoro huku askari wakiwa walevi.

(v) Raia walifanya mapinduzi na kuwatega nyara viongozi chini ya Atega (zozote 5x1=al.5)

(c) NYALWE

(i) Aliwasilisha malalamishi ya mama Agoro kwa Mtemi Bokono kuhusu unyakuzi wa ardhi-kiwanja cha watoto kuchezea.

(ii) Alifichue unafiki wa washauri wakuu wa Mtemi Bokono kuwa raia hawampendi Mtemi Bokono na utawala wake.

(iii) Alimshutumu/kumkashifu mumewe kwa vitendo vya kuwadhulumu raia.

(iv) Alimshauri mumewe abadilishe uongozi wake ambao ulikuwa unawaumiza raia (zozote

(d) Askari I na Kame

<u>Askari I</u>

(i) Alipinga kanuni za kidhalimu za gerezani za kumtenga mfungwa na jamaa yake

(ii) Alipigania haki za watuhumiwa dhidi ya madai kuwa ni waharibifu na pia kupata chakula mfano Mwelusi

(iii) Alishirikiana na raia (wapinzani) katika kuung'oa utawala dhalimu wa Mtemi Bokono)

(iv) Alikusanya ushahidi wa mauaji ya mtuhumiwa 'jiwe' kutoka kwa askari II (zozote 2x1=2)

<u>Kame</u>

(i) Alipinga kumtenganisha mfungwwa (Mwelusi) na uhai/maisha

(ii) Alishirikianana na raia katika kuung'oa utawala dhalimu wa Mtemi Bokono

(iii) Anaunga mkono kutoroka kwa Mwelusi na kuwaondolea lawama askari jela kuhusu kutoroka kwa mwelusi (yoyote 1x1=1)

(b) Mabadiliko ayatakayo Mwelusi.

(i) Butangi iliyo na uslama kwa wananchi wote

(ii) Butangi yenye shibe/isiyo na njaa.

(iii) Butangi itakayochukulia sawa watu wote bila kujali kijiji au ukoo.

(iv) Butangi inayozingatia haki na heshima kwa watu wote

(v) Butangi ambayo haibagui mtoto wala wazee/mwanamke na mwanamume

(vi) Butangi iliyo na usawa, haki na maendeleo (zozote 6x1=6

6. (a) Muktadha

(i) Msemaji ni Tanya

(ii) Anamweleza Batu

(iii) Wako uani kwa Tanya

(iv) Batu yuko hapa katika harakati za kumsaka ili amtie kufika kwake kwa Batu ambaye anamlinganisha na kozi naye njiwa (zozote 4x1=al.4)

. (b) Mbinu ya lugha

- Sitiari
- Batu mwenye nguvu na katili ni kozi
- Tanya mnyonge na mnyanyaswa ni njiwa (ala.2) (kutaja mbinu 1, maelezo 1= al. 2)

(c) Mbinu za uandishi katika tamthilia ya kifo kisimani (ala. 10)

Jazanda

- Pembe na nyati au kifaru – njia za mauti
- Mwiba katika mguu wa Butangi- Mwelusi kuwa kikwazo kwa utawala dhalimu wa Mtemi Bokono

- Njiwa, kazi na vifaranga – tofauti za kitabaka k.v. Tanya ni njiwa, Batu ni kozi, na watoto wa Tanya (Mwelusi, Andua) ni vifaranga.
- Minyororo – hali ya watu kufungwa
- Kisima – Chanzo cha uhai wa watu n.k

Tashihisi
- Mawazo yakanishika miguu – hakuendelea kutembea kwa sababu alikuwa akifikiri.
- Usipoondoka, utatembelewa na kofi – askari alitisha kumpiga Andua
- Ulimi wako utakufisha umeme – onyo la askari III kwa askari I kwani alikuwa anatisha madai yake kuwa Mwelusi ni mharibifu.
- Dunia haipendi wenye kukata tamaa-Azena anamweleza Tanya kuwa duniani hakuna nafasi kwa wanaokufa moyo/kata tamaa

Semi Misemo/nahau)
- Hunikoroga nyongo – hunikasirisha sana.
- Kukata tamaa- kupoteza matumaini
- Nikupe nikupe – hongo/hakuna cha bure
- kilichomtoa kanga manyoya – kumta adabu

Tashbihi
- Viuno vitatingishwa mpaka viyeyuke kama mafuta karibu na moto- maelezo jinsi wanawake watakavyomkatikia Bokono
- Ni wazalendo thabiti kama majabali
- Ukweli huuma kama nge
- Bahati kama mtende
- Mara nyingi uhalisi huonekana kama ndoto
- Utakuwa kama ndege anayeishi juu ya mbuyu
- Moyo wangu wangalikuwa mzito kama jiwe

Taswira
- Pale ambapo Mwelusi yuko uwanjani, mahali pa mkutano kupitia kwa mawazo yake tanaiona picha ya pale – mapambo
- Kipigo na kuingizwa kizuizini kwa Mwelusi
- Vifo vya wale waliopigania ukombozi – Askari wa II alieleza jinsi walivyomuua mtu waliyekuwa wakimhoji.
- Vita vya kikabila – Mashambulizi ya askari wa kukodi waliwaacha wengi wakiwa wamefariki, wengine kujeruhiwa na mali nyingi kuharibiwa.

Istiari
- Alikuwa jiwe – hakukubali mashtaka yake
- Ni gogo la mti – Tanya anaeleza hisia za Gege aliyekuwa amekataa kumtembelea kakaake
- Wana mawe vifuani – hawana utu
- Askari ni wanyama – hawana utu- wamejaa ukatili

Methali
- Sikio la kufa, halisikii dawa- Bokono alikuwa anapotoshwa na hakutaka kurekebishwa
- Hasira hasara – askari wa II anawaeleza aksari I na wa III wanapotaka kupigana

(zozote 5x2=al.10))(kutaja =1, kueleza/mfano =1 = 02x5=ala. 10)

(d) Umuhimu wa mzungumzaji – Tanya (ala.4)
- Ananyimwa nafasi ya kumwona mwanawe gerezani ambaye ni Mwelusi.
- Anaandaa chakula kwa lengo la kumfikia mwanawe Mwelusi gerezani lakini kinaliwa na askari II na III.
- Anakosewa heshima na askari II na III anaposisitiza kumwona mwanawe gerezani.
- Askari III anamwangusha Tanya kule kwake uani/nyumbani katika harakati za kumsaka kutoka kizuizini na Mtemi kuamrisha akamatwe.
- Ni mmoja wao wanaonyimwa haki mfano kuchota maji kisimani. (zozote 4x1=al.4)

7. (i) MTEMI BOKONO - WASIFU

i. Mwenye tama ya uongozi- anasema ataongoza Butangi kwa miaka mia moja

ii. Kiongozi dhalimu – anatesa wake k.m. Mwelusi
iii. Mwepesi wa kushawishika – anaamini vile Batu anamdanganya kuwa watu wa Butangi wanampenda
iv. Mtawala wa kiimla/ kidikteta/ mabavu – anawatisha washauri wake kuwa angetafuna mifupa yao wasipofaulu kumkamata Mwelusi kwa siku nne
v. Hataki upinzani wowote kwa utawala wake
vi. Mwenye hasira – anapandwa na hasira wakati watu wanasusia mkutano wake pia anakasirika anapopashwa habari kuwa Mwelusi ametoroka kizuizini
vii. Ni mwoga mwenye wasiwasi mwingi, ana wasiwasi kuhusu kunyang'anywa uongozi.Anaota akizikwa akiwa hai
viii. Katili – anaunga mkono utesaji na mauaji kwa wapinzani wake k.v Mwelusi na mtoto wa Chendeke
ix. Mwenye mapuuza – anapuuza Nyalwe na mama Agoro kuhusiana na uongozi wake mbaya na pia kuhusu unyakuzi wa kiwanja cha watoto kuchezea
x. Ni fisadi- Anawapa ardhi watu kama askari mkuu kupitia kwa mgawa ardhi. Pia motto wa Kaloo kupewa kazi, kukataza matumizi ya kisima na bonde la ilangi kwa manufaa yake na marafiki zake

(ii) UMUHIMU WA BOKONO

i. Ni kielelezo cha viongozi ambao huongozwa na tama baada ya kuingia mamlakani
ii. Anawakilisha viongozi wanaodhulumu wapinzani wao k.m Mwelusi
iii. Anaendeleza ujinga wa viongozi wanaoshauriwa na wapambe wao laghai
iv. Ni kielelezo cha viongozi wanaowasaidia marafiki zao wanaounga mkono tawala – zao ili kuimarisha kudumisha utawala potovu – k.m. mgawa ardhi kumpa askari mkuu ardhi
v. Ni kielelezo cha viongozi ambo hupuuza maoni ya wananchi- anakataa kusikiza maoni ya Nyalwe na Agoro eti kwa sababu ni wanawake
vi. Anawakilisha viongozi waliokosa kuadilika katika jamii k.m. kukosa heshima katika asasi ya ndoa yake
vii. Ametumika kuonyesha jinsi viongozi wengine hutumia utesaji na mauaji kama nyenzo za kuimarisha na kudumisha uongozi wao
viii. Anawakilisha viongozi ambao wanatafuta kila mbinu kama vile mauaji ili kuyalinda mamlaka yao wanayohofia kunyang'anywa
ix. Ni kielelezo cha uongozi ambao huhasirika na huhasiri nchi zao baada ya kutawaliwa na hasira
x. Ametumiwa kuonyesha jinsi udikteta unavyoweza kutenga maendeleo kwa kuwakandamiza na kuwanyamazisha wanaojaribu kupinga uongozi mbaya

(iii) <u>MWELUSI - WASIFU</u>

i. Ni mzalendo wa kweli- anaongoza harakati za kukomboa Butangi kutokana na uongozi mbaya
ii. Jasiri- anakashifu uongozi wa Butangi bila uoga – anajasiri kutoroka gerezani na hata kuongoza watu kukivamia kisima
iii. Mwanaharakati- anatak kuleta mabadiliko ya uongozi
iv. Mwenye msimamo thabiti- licha ya kuteswa gerezani habadilishi msimamo wake
v. Mwenye busara- anajaribu kuwazindua wanabutangi (amezinduka kimawazo)
vi. Mwenye maarifa – anatumia maarifa kutoroka kizuizini kwa kukereza minyororo kwa tupa
vii. Ni mwerevu- akiwa kisimani, baada ya kutoroka kizuizini, anamkuta Zigu na kumweleza kuwa Mwelusi hajatoroka bali kajificha momo humo gerezani
viii. Ni mbishi- anabishana na Zigu pale kisimani kuhusu matumizi ya kisima

(iv) <u>UMUHIMU WA MWELUSI</u>

i. Ni mhusika kielelezo cha wazalendo wanaodhihirisha apenzi ya dhati kwa nchi yake
ii. Anawakilisha vijana wanaopenda nchi yao na hata kuyatoa maisha yao kwa manufaa ya jamii
iii. Anasaidia kubainisha ujinga wa viongozi wasiowajua raia wanaowaongoza- Zigu
iv. Anaonyesha kuwa juhudi za ukombozi zinahitaji uvumilivu na subira
v. Anatumiwa kuonyesha malezi mema ya Tanya

vi. Ndiye mhusika muhimu zaidi anayeendeleza na kuthibitisha anwani ya kifo kisimani anapouawa karibu na kisima cha mkomani
vii. Ni kielelezo cha jinsi wanaharakati wanavyofaa kutetea haki na kupima bila kukubali yote waambiwayo
viii. Ni kielelezo cha jinsi wanaharakati wanavyoweza kutumia maarifa yao kujikomboa na kukomboa jamii kutokana na uongozi dhalimu
ix. Ametumiwa kuelimisha wanabutangi kuhusu uovu unaotokana na utawala mbaya. Anawaonyesha jinsi ya kujikomboa kutokana na uongozi huo
x. Ametumiwa kuhimiza wanaharakati kutokata tama licha ya kupitia mateso au changamoto mbalimbali hadi wafikie lengo lao
xi. Anatumiwa kuonyesha matatizo yanayowasibu viongozi na wanaharakati (wanamapinduzi) katika jamii ambao aghalabu huteswa hata kupoteza maisha yao

Kutuza: wasifu, zozote Bokono tano, Mwelusi tano Jumla 10

Umuhimu zozote Bokono tano, Mwelusi tano , jumla 10 Jumla 20

8. "Kazi ya mikono yangu yenyewe"

a) i) Msemaji ni Gege
ii) Wakiwa kwenye majengo (ukumbi) ya utawala ya Butangi
iii) Anazungumza na Bokono akiwepo Batu na Mweke
iv) Anaripoti jinsi alivyomuua nduguye Mwelusi plae kisimani kwenye chemba 4x1=4

b) Yaliyomfanya msemaji kuuchomea mwiba

i. Alikuwa ameahidiwa Alida bintiye Bokono
ii. Aliahidiwa ardhi kubwa yenye rotuba
iii. Aliahidiwa mitumbwi ya kuvulia samaki
iv. Angepata mashamba ya minazi na miembe
v. Aliahidiwa mashamba yam tama na migomba
vi. Atavua samaki kwa majahazi makubwa na
vii. Kuwa tajiri mwenye mali nyingi na jina kubwa

c) Yaliyofuata kauli hii na hatima ya mzungumzaji

i. Alipewa jina la mkuki wa Almasi – baada ya kuuchomoa mwiba. Yaani kumuua Mwelusi
ii. Kulikuwa na mapinduzi – waliokuwa namakani waling'olewa k.m. Bokono na kundi lake la washauri
iii. Gege alitiwa mbaroni baada ya kupigwa na wanamapinduzi
iv. Bokono, Batu, Mweke, Zigu na Tahu walifungwa na kutupwa gerezani wakingojea kufunguliwa mashtaka
v. Baraza la hukumu liliundwa upya ili kutoa hukumu kwa Mtemi, Bokono na washauri wake
vi. Gege alipigwa kofi kali na kufurushwa nje na Mweke baada ya Gege kudinda kuondoka ukumbini akidai zawadi yake kuu – Alida
vii. Gege hakupata ardhi kubwa alioahidiwa kwa sababu mapinduzi yalitokea kabla hajaonyeshwa pamoja na zawadi zingine mali
viii. Utawala wa kiimla wa Bokono ulifikia mwisho
ix. Nyalwe alibahatika kukwepa hasira kali za wanabutalangi kwasababu alikuwa akisaidia kumshauri Bokono japo alitia masikioni
x. Mitumbwi ya kuvulia samaki, mashamba makubwa ya migomba na miembe aliyokuwa ameahidiwa Gege hakuipata

9. UONGOZI MBAYA

- Mauaji ya Mweluzi yameipokonya jamii kiongozi mwenye maendeleo.
- Kukata miti ovyo ovyo kumesababisha ukame/jangwa na njaa.
- Kuendeleza ufisadi ni chanzo cha umaskini.
- maandamano na misukosuko husababisha uhasama na ukosefu wa amani/utulivu.
- Husababisha vibaraka/vikaragosi ambao ni wasaliti waletao madhila kwa wananchi.
- Vijana kukoasa ajira.
- Uozo wa kijamii k.m. Kaloo.

- Hukuza matabaka.
- Hukuza unyanyasaji (Mbutwe kunyimwa haki yake (malipo).
- Uhasama wa kikabila.
- Kusetiri uhalifu, k.m. mfungwa kuuawa kisiri. (10 x 2 = al. 20

10. - Vijana wamesawiriwa katika makundi mawili:

(i) Wazalendo

- Mwelusi
- Askari
- Andua
- Atega
- Kame
- Mgezi

(ii) Wasaliti

Gege
- Askari II
- Askari III
- Makacheto (Mweke, Talui)

Kila mhusika (al. 1) , maelzo ya aliyesawiriwa (al. 1)

Wazalendo – (Wahusika watano – (al. 5)

( Maelezo matano – (al. 5)

Wasaliti – (wahusika watano – (al. 5) (Maelezo matano – al

11 (a) -Msemaji ni askari wa pili

-Anamsemesha askari wa tatu

-Wako nje ya gereza

-Askari wa pili aligundua kuwa Mwelusi alikuwa amekata pingu na umati wa watu wenye hasira ulikuwa unawajia

b) i) Kinaya- maneno yaliyo kinyume cha ukweli

ii)Askari alisema watu waliwapenda ilhali waliwachukia

- Alidai walifanya kazi vizuri ya kumzuia mfungwa gerezani ilhali walimtesa na kula chake
- Mfungwa alitoroka
- Askari hawangepakwa mafuta bali wangepigwa

c) -Waliwaua watu k.m mtu jiwe

- Walikula chakula cha wafungwa k.v askari II na III walikula chakula cha Mwelusi
- Walikosa heshima na adabu kwa watu wote wa rika zote k.m Tanya aliambiwa asitoe hotuba ya uzazi, kumgusa adua kifuani
- Askari waiwatesa washukiwa kwa njia mbali mbali ili wawape habari walizotaka k.m kung'oa kucha n.k
- Kuwapiga wanabutangi k.m majeraha ya andua, motto wa chendeke aling'olewa meno

12. a)Batu $^{\surd 1}$ anazungumza na washauri$^{\surd 1}$ wengine wa Bokono$^{\surd 1}$ wakiwa wakiwa katiak ukumbi$^{\surd 1}$ wa
utawala wa Butangi.

b) Masharti yalikuwa ikiwa amekata msamaha basi ashirikiane na Batu Kwa:

- Mwelusi awataje vijana wanochochea chuki dhidi ya utawala wa Bokono.
- Apelekwe vijini awatangazie watu kwamba ameacha uchochezi
- Aseme umuhimu wa kuungana pamoja chini ya uongozi wa hekima wa Bokono
- Aseme uchochezi katika Butangi umepangwa na majirani ambao wanaonea wivu amani na maendeleo ya Butangi.

c) Ufisadi:

- Kisima cha Mkomani: kinabina fsishwa – watu wanakatazwa kutummia maji eti yanahifadhiwa kwa siku zijazo.
- Wananchi wasikanyage Bonde la Ilangi,kumbe limetengewa Bokono na marafiki zake.
- Ardhi kunyakuliwa
- Wasaliti kuahidiwa ardhi.
- Mali ya Butangi ilikuwa ya wachache.
- Batu hakuwa tayari kumlipa Mbutwe pesa za viti.
- Botono alibinafsisha bahari/ziwa – alikuwa na sehemu yake ya kuuna samaki.
- Bokono alikuwa na mali nje ya Butangi – Macheleni.
- Mtoto wa Kaloo kupewa kazi kwa 'mapendeleo.
- Watu kupata vyeo kwa sababu ya uhusiano wa kifamilia na Bokono.
- Uharibifu wa Kufichwa.
- Motto wa mteni ku chafua maji ya bwawa. (hoja 12X1 ) ala 12

13. Maana – kinachokuathiri ama kitakachokuangamiza daima kimekundama; u nacho kila wakati

- Kame – ana uhusiano wa kiukoo na Bokono, lakini anawatetea wachochezi na kuungana nao katika harakati za kumpindua Bokono
- Mgezi – anahudumu nyumbani mwa Bokono na huwapelekea wanabutangi habari kuhusu yanayoendelea katika nyumba ya utawala
- Askari I – mwana mapinduzi ingawa yuko serikalini. Huenda alishiriki katika njama ya kuingia tupa gerezani
- Gege – anamsaliti nduguye na kummua kwa kisu
- Wanabutangi – wametangana wao kwa wao kutokana na ubinafsi na woga wao

  Kutaja mhusika – al 1
  Maelezo – ala 3
  Hoja 5x4

14.

- Hakuna maendeleo yoyote k.v. askari kutumia mapanga na mikuki kulinda usalama na nchi
- Hakuna utumizi maalumwa pesa bidhaa hubadilishwa mfano Mbutwe kudai malipo ya mbuzi wawili
- Wanachi hawajakua kiakili kuhusu siasa, waijue haki yao. Gege haoni uovu unaoendelezwa na utawala wa Bokono
- Hakuna mfumo wa kuajiri na kufuta kazi. Bokono anatoa amri k/v. mtoto wa Kaloo. Ujira pia huendelezwa kwa misingi ya kiakbila
- Serikali ya Butangi haijajitajirisha kwa majanga yanayoweza kutokea wakati wowote k.v. askari kukosa mikuki ya kutosha hinvyo basi hawawezi kukabiliana na umati uliokwenda gerezani kumnasua Mwelusi
- Butangi haina mfumo maalum na sheria – Mtemi ndiye bunge – anatunga sheria za kiubinafsi k.v. utumiaji wa kisima
- Hakuna demokrasia – wananchi hawachangii katika ujenzi wa taifa lao
- Kiongozi yuko juu ya sheria – anatenda lolote alitakalo bila hoja wakati wowote
- Hakuna vikundi vya kutetea haki ya mwananchi. Vilivyoko vimeundwa na serikali sio kuwatetea bali kuwaonyesha kuwa malalamiko yao yanashughulikiwa
- Kuna utawala wa nyumba kuu- inayohusiana na Mtemi kama dadke ameolewa na kakake Mtemi. Wana wa Mtemi ndio wanaosimamia kandarasi n.k. familia ya Mtemi ina mamlaka zaidi- kawaida katika nchi zinazokua

15. a)Jazanda

  i. Bafe – wapinzani wanaomshambulia Bokono
  ii. Mamba – Bokono na uwezo wake unaowadhuru watu
  iii. Nyati/ kifaru- matumizi ya silaha kuwaua wapinzani

iv. Fisi – ulafi wa askari II na III
v. Chui – Bokono na ukali wake, mkewe Bokono na ukali wake
vi. Zimwi – Bokono na washauri wake
vii. Njiwa – watawala wanaonyanyaswa
viii. Kozi – Ndege mwenye uwezo – Bokono anatumia uwezo wake kuwaangamiza watawala
ix. Mwiba katika mguu – Mwelusi – kikwazo kikuu katika utawala wa Bokono Zozote 5x2=10

b) i) Tashhisi
- Mawazo yakashika miguu – Mwelusi hakuendelea kutembea kwasababu alikuwa anafikiria
- Usipoondoka utatembelewa na kofi – vitisho
- Ndoto zimekifanya kichwa changu kuwa uwanja wa kuchezea . Tanya anaota kila wakati

Zozote 2x2= 4

- Dunia haipendi wenye kukata tama- Azena anamshauri tanga
- Pombe haipendi tumbotupu
- Huzuni imejenga nyumba moyoni mwangu - Tanya anahuzunika daima mtoto wake kizuizini, mume wake alikufa
- Jua lilimchekelea akiwa papo hapo kwa muda mrefu Zozote 3x1=3

ii) Methali
- Sikio l aa kufa halisikii dawa
- Bandu bandu huisha gogo
- Udongo uwahi ungali maji
- Dawa ya moto ni moto
- Maziwa yakimwagika hayazoleki
- Uerevu mwingi huondoa maarifa Zozote 3x1=3

iii) Kinaya
- Bokono anasema kwamba nia yake ni kuongoza Butangi kwa busara ilihali wananchi wa Butangi wanateseka
- Batu anasema kwamba ataongoza Butangi kwa manufaa ya wanabutangi wote wote ukweli ni kwamba ni wachache wanaonufaika

16. a) Msemaji ni kame alimwambia Batu katika ukumbi wa utawala wa Bulangi batu alipendekeza Mwlusi auwawe kama anapinga 4x1=4

b)
- mwongo
- Katili
- Mnafiki
- Mchochezi
- Kigeugeu
- Kibaraka
- Mbinafsi 5x1=5

c)- Mwelusi
- Andua
- Atege
- Askari 1
- Tanya
- Nyalwe
- kame

Kutaja mhusika 1
Kutoa mifano 1

17. (a) Maneno haya yalisemwa na Mtemi Bokono
- Anajisemesha mwenyewe
- Alikuwa katika makao ya utawala

-Alikuwa na wasiwasi

(b) (i) Mwenye wasiwasi na uwoga

(ii) Anahofia huenda uongozi wake ukaanguka

(iii) Hadhibiti tena uongozi wa Butangi

(iv) Kuumwa na nyoka ni ishara ya kufa/kushindwa na adui hivyo uongozi wake waelekea kwisha.

(c) Nidaa- hai

(ii) Jazanda – Sumu ya nyoka ni nguvu za upinzani

(iii) Taashira – Nyoka kumuona ni ishara ya kuanguka kwa uongozi wake.

(iv) Mchezo ndani ya mchezo (2x1= 2)

**(d)** (i) Tenga utawale – aliwatenganisha watu ili kuvunja umoja wao na aweze kutawala kwa urahisi mfano; Gege na Mwelusi.

(ii) kuwatia jela na kuwatesa wapinzani wake mf. Mwelusi

(iii) Kuwaua wapinzani wake mf. Mwelusi

(iv) Kuwatenga wapinzani wake na jamaa, marafiki mf. Hakuna anayeruhusiwa kumwona mwelusi kizuizini.

(v) Kuwatumia askari kushambulia wapinzani wake kisha kusingizia majirani. M.f. wabalusi kushambulia batuitui

(vi) Kuwatunza wazalendo na wafanyikazi watiifu kwa mfano Gege, Kaloo na askari mkuu

(vii) Kuunda tume za uchunguzi kuuliza raia kila kulipozuka swala nyeti (malalamiko)

(viii) Kueneza propaganda kuwa Bokono amepewa utawala na Mungu ili watu waache kumpinga na wamtii

(ix) Vitisho – anawatisha washauri wake kuwa angekula mifupa yao kwa siku tatu kama hawangemsaka na kumrejesha

(x) Kuzorotesha uchumi ili raia wasiweze kujitegemea na ili atawale kwa urahisi- kuwanyima maji, kuwanyima ardhi

(xi) Kuwanunua/kuwahadaa wapinzani wake. Mwelusi anahadaiwa kuwa akiacha uchochezi angefanywa
kuwa kiongozi wa vijana angepewa ardhi na ng'ombe.

(xii) Kutumia washauri kutawala na kupata habari kwa mfano Batu na Kame.

(xiii) Kuunda Baraza la hukumu kwa lengo la kunyamazisha wapinzani wake (10x1=al. 1))

18. Masuala Ibuka

i) Ukimwi - siku ya mganga
- Mwaibale anausambaza kwa wembe
- wagonjwa/ wateja wamekondeana na kudhoofika kiafya

ii) Haki za watoto i) Kuchukua hatua nyingine
- watoto kukosa sare, karo, chakula na kwenda shuleni
- Ajira ya watoto
- Mtoto kupachikwa mamba

ii) Fumbo la mwana
- dawa za kulevya

iii) Ngome ya nafsi
- Watoto kuozwa mapema

iv) Uteuzi wa moyoni
- Ndoa za mapema
- wasichana kukosa elimu

iii) Ufisadi – Mayai waziri, waziri fisadi, wizara ya mlungula
- Msamaria mwema – Bw. Kizito Kibambo
- Uteuzi wa moyoni – wapiga kura kuuza kadi zao
- Ngome ya nafasi – Chifu alihongwa, kuficha wahalifu

iv) - Matumizi ya dawa za kulevya/ mihadarati na madhara yake kwa vijana
- Fumbo la mwana
- Nanda anatumia dawa za kulevya

- Anazorota kimasomo, mchafu n.k

v) Ndoa za mapema kwa wasichana
- Zena aliozwa mapea – uteuzi wa moyoni
- Ngome ya nafsi – Naseko anaozwa kwa mzee

vi) Migogoro shuleni
- Ndimi za mauti – Wanafunzi kuchoma wenzao bwenini
- Mayai waziri – Migomo ya walimu

vii) Vita vya kikabila na suala la wakimbizi
- Mkimbizi

ix) Uongozi mbaya – Kuchukua hatua nyingine
- Uhalifu wakati wa kura
- Viongozi walikosa uwajibikaji
- Chifu kuuza chakula kilichotolewa bure wakati wa ukame
- Serikali ilifutilia mbali elimu ya bure na kusababisha maskini
- Mayai waziri wa maradhi
- Waziri mayai
- Viongozi walafi

x) Uhalifu katika jamii
- Pwaguzi
- Salim ni tapeli na mizi mkuu
- Kuchukua hatua nyuingine
- Ngome ya nafsi

xi) Umaskini
- kuchukua hatua nyingine
- fumbo la mwana
- msamaria mwema
- mayai waziri wa maradhi

xii) Haki za wanawake katika jamii
- Uteuzi wa moyoni
- Ngome ya nafsi
- Kuchukua hatua nyingine
- Mayai waziri wa maradhi
- Mayai haishi na mkewe

19. Dhamira ni lengo/ nia ya mwandishi wa 'Tuzo'

i) . Anaashiria kauli kuwa yote yaweza yakatokea hata yasiyotarajiwa k.m. Salome na kibwana hawana mkabala mzuri lakini Salome anakuja na kumletea habari. Mwandishi aonyesha kuwa hafla ama matukio huleta wengi pamoja hata wasiosemezana wala kuamkuana

ii) Anaonyesha kuwa mapeni ni msingi wa mengi. Nia ya kibwana unapokataliwa inakuwa chanzo cha kutosemezana kwao tena

iii) Anaonyesha kuwa kunao, wakaao pamoja na kufanya kazi pamoja lakini hawana mkabal mzuri, wao husemezana tu kwa sababu ya kikazi walakini wakitoka nje wanakuwa mjamba miwili isiyoamba. Salome na kibwana wanasemezana wakati wa kazi

iv) Pia anatuonyesha kuwa kuna wenye vitendo vizuri vyenye sifa. Vitendo vyao vinajulikana wazi wazi (kama saui zao)lakini wenyewe hawajui vitendo vinaweza kumtambulisha mtu.

v) Kuna haja ya kumtuza aliyefanya vizuri wanahabari wanatuzwa akiwemo Salome Dzoro

vi) Hamu ya kutuzwa huwa hasa katika sherehe ambayo mtuzwa hajatengezwa hadharani. Tunaiona hamu aliyonayo kibwana

vii) Pia anasisitiza umuhimu wa kauli tahadhari kabla ya athari na kuwa mwangalifu
Anaonyesha umuhimu wa kuwaza kabla ya kutenda
Kibwana angalichunguza kwa makini hangeaibika machoni pake vile.
Tunaelewa alichanganyikiwa hadi katika choo cha wanawake

viii) Anathibitisha ukweli wa methali mzaha

Mzaha hutubga usaha

Mzaha wa Salome wa kumtania kibwana unamletea aibu na kuvurugika akili

ix) Anaonyesha jinsi kutaniana na kuchezeana shere kamwe hakufai. Hii huweza kuleta vita namna kibwana alitaka walakini akajizuia

x) Anataka kuonyesha jinsi furaha huathiri akili. Kibwana alizidiwa na furaha na kusahau kuwa anaweza kutaniwa. Mwandishi anaonyesha kuwa kuna kilio au aibu inayoweza kutokana na futahi hiyo

xi) Anataka kuashiria kuwa vita sio suluhisho kwa kosa ulilotendewa. Kibwana alifumbata konzi kutaka kuirusha walakini anajizuia. Hili ni funzo dhabiti kuwa haitupasi kusuluhisha kwa vita

xii) Ni kawaida kuoa anayetuzwa akiringa ama akitembea kwa madaha. Tunaambiwa kuwa Salome alitembea kwa ndweo kwenda kuitwa zawadi yake. Zozote 10x2=20

# Ushairi

1. a) (i) Mashairi huru (2X1)ala. 2

ii) Hayazingatii arudhi za betu,vina, mishororo, mizani na kibwagizo (2x1)ala. 2

b) i) SHAIRI A – Anamlalamikia Hadija kwa kumuuwa mumewe kwa kumpa sumu.

ii) SHAIRI B – Anawalalamikia vijana ambao wanamcheka eti amezeeka na kupitwa na wakati Wanamramba Kisogo (2x2)ala 4

c) i) Katika SHAIRI 'A' - Hadija alidhani kumuua mewe angepata suluhisho lakini badala yake amejiletea matatizo zaidi. Watu sasa wamemsuta kwa kitendo chake na watoto wanamsumbua.

ii) Katika SHAIRI 'B' – Mshairi anawakejeli vijana ambao wnamramba mzee kisogo bila kujua kwamba hawataki kupita. (2x2) ala.4

d)i) Amemuua mumewe – Mti mkuu au kichwa cha nyumba.

ii) Anapata shida za Kujitakia – matatizo yamefurika ngyumbani kama mto (ukupita nyuma ya punda atakutega au kukupiga teke) (2x2)ala.2

e) Inkisari – Nendako – Niendako

- Mwendako – Mnakoenda
- Bwanako – Bwna yako (1x2)ala.2

f) <u>Mzigo</u> – uzee/umri.

<u>Jiri</u> – Tajriba /Waarifa / Elimu ya maisha.

Kula nimekula - Ameishi miaka mingi

Niko nyuma ya wakati - Amebaki nyuma ne usasa (4x1)ala.4

2. a) – Matibabu ya kiasili | Dawa za asili| dawa za Kisasa.

b) kuonyesha kuwa dawa asili zinafaa kwa matibabu kuliko za Kisasa. Watu wazirejele.

c) Ana matibau ya kiasili

Hosptiali kuna operasheni ya visu.

Kuna dawa za asili zisizopatikana hospitali. (4X1) ala 4.

d) Beti Sita.

- Takhmisa| mishoro mitano.
- Mtiririko – vina bvya ukwapi na utao vinafanana katika beti zote.
- Mathnawi – vipande viwili.
- Mizani ni 8,8
- Lina kiisho – mshoro wa mwisho unarudiwa beti hadi beti katika beti zote. ( 6x1) ala.6

e) kupata idai ya mizani inayotakikana

f) i) Dhalili – Kudharauliwa,nyonge, maskini,dhaifu.

ii)Azali – zamani.

iii)Sahali – Urahisi/ wepesi.

iv)Tumbo nyangwe

3. (a) - Shairi huru
- Halijazingatia kanunu za utunzi wa mashairi wa kuzingatia arudhi

(b) - Anayeimba ni mjomba
- Anayeimbiwa ni mpwa wake

(c) – Anaambiwa uoga ukimtikia huenda ni wa akina mamaye
- Alichinjiwa fahali ili awe mwanaume

(d) – Chuku – wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo
- Takriri – kikali
- Asitiari – upweke ni uvundo
- Tashhisi – uoga ukifikia

(e) - Wakulima – Atapewa shamba la mahindi
- Wafugaji – Atapewa mbuzi

(f) – Tabdila – aamushwe – aamshwe
- Inkisari – Mme – mwanamme
- Kuboronga sarufi – Fahali tulichinja tulichinja fahali

(g) - Mbari Ukoo ; kikundi fulani
- Msurruu – Anayenuna
- Ngariba – Mtahirishaji
- Uvundo – Harufu mbaya

4. (a) (i) Amenyang'anywa mkewe
(ii) Wazazi wake wanamgombeza
(iii) Alipokuwa na mali marafiki walikuwa wengi. Alikuwa akiwapeleka marafiki klabu na walifurahia pamoja wakichoma nyama.
(iv) Mqwandishi hawaoni tena marafiki wote; wameshatoroka. Ana njaa na matatizo mengi sana.
(v) Amebaki pweke, mke ametoroka na watoto wameparara. Mwandishi hawezi kulipa karo. Sasa ameamua kujitia kitanzi (4x1= al.4)

(b) (i) Mbadhirifu –a alitumia mali vibaya
(ii) Mpweke – Ndugu hawamsemezi anaishi upweke
(iii) Mpenda anasa =- Alikuwa akinywa pombe na kukaa sana klabuni (al. 2 x 3= 6)

(c) (i) Msemo – Balaa belua
(ii) Jazanda – "Juzi" ni wakati uliopita ilhali 'leo" ni sasa au wakati huu
(iii) Tashbihi – kama radi ya mvua (2 x 3= al. 6)

(d) (i) Ndugu zangu wamedai ubub – Ndugu zangu wamekataa kusema nami yaani hawanisemezi kwa hali yangu mpya.

(ii) Kumbe kupanga ndiyo maana- Amegundua kuwa angepanga maisha yake tangu awali atumie vizuri raslimali alizokuwa nazo badala ya kuzifuja (2x1= al.2)

5. a) - Beti nne
- Mishororo mine katika kila ubet (tarbia)
- Mshororo wa nne mfupi (msuko)
- Mizani 6:8 mshororo wa 1-3 kikai
6 mshororo wa mwisho

b) Inkisari – Anoshika
- Alo
- Asosita

Lafudhi – Katiti
- mangiriti

Kutaja 2 mifano 1

c) - Anataka asikike (mawazo yake yasikika)
- Anatafuta atakayoeleza ujumbe wake

- anashindwa atatumia kipimo kipi
- Mtu huyo lazima awe mzalendo aliye jasiri
- Lazima awe anayetambua utu

d) Lugha ya natahria
Aliye mzalendo na alambuaye haya mtu asiye mwoga, aliyejawa na upendo hata wakati wa hatari, Ni kipimo kipi cha kumtambua mtu kama huyu

e) tarbia – Mishororo mine kila ubeti
Kikai – Mizani isiyozidi 15
Msuko – Kibwagizo kifupi

f) i) katili – Kidogo
Gati gati – Ubaguzi
Mangiriti - mambo ya upipi

6. a)
- Beti saba
- Tarbia – mishororo mine
- Vina vya ndani na vya nje hubadilika badilika
- Pande mbili – ukwapi na utao
- Mizani 8, 8 jumla 16 katika kila mshororo
- Kibwagizo kipo – kipi titakachotenda, ninene huko mama

b)
Kwa kumza bila zira (chuki)
Kumpenda na kutomuua
Kujinyima yote mazuri kwa niaba yake
Kumtunza mfano wa ndege na makinda wake
Kumtafutia riziki – kufanya kazi (kulima) ili asitaabike
Kumjali
Kutojali visiki katika ulezi wake kama vile baba yake mkali Zozote 5x1=5

c)
- Vijana ambao baada ya kulelewa na kunenepa hawajali wazazi wao (mama zao)
- Akina baba wanaowapiga wake wao kwa makosa madogo madogo
- Pia akina baba wanaowatesa wake wao. Huwafanya yay nyumabni mwao Zozote 2x1=2

d) katika beti nne za kwanza mshairi anaangazia mema aliyotendewa na mama yake ilihali katika beti mbili zinazofuata anawakashifu wanaowatendea akina mama wao mabaya
Alama 3

e) Mama – nina (Ubeti wa 2)
Dawati – saraka (Ubeti wa 1)
Imara/ thabiti – jahidi (ubeti wa 3)

f) i) Mambo yakavurugika
ii) Wimbombo – Kipande cha miti cha kupekecha moto. Chuma cha kupuliziz moto
iii) Kongoni – Jina la kumkaribisha mtu

7. a) Linakatisha tamaa kwa sababu
i. Mwanamke anapolima, hafaidiki na mavuno bali yote huchukuliwa na bwanake
ii. Mwanamke hubaguliwa na kuonewa ofisini
iii. Mahali pake ni jikoni, ujakazi n.k lakini halipwi na tena hapewi likizo (hapumziki)
iv. Hutumiwa kama chombo cha mapenzi kukidhia uchuu wa mwanamke
v. Hamna anayemheshimiwa kwa chochote eti kwa sababu ni mke Zozote 4 X 1 = 4

b) UMBO
i. Beti sita

ii. Mishororo sita kwa kila ubeti
iii. Vina vya wisho vya mishororo ya kwanza miwili (mwanzo na mloto) ni –ni- isipokuwa ubeti wa sita (mwisho)
iv. Kila ubeti hususan wa kwanza hadi wa tano umeanza kwa neno Nomwona isipokuwa ubeti wa sita – kupelekea shairi hili kuwa kikwamba
v. Kila ubeti una kituo tofauti Zozote 5X1= 5

c) Lugha Nathari
Mwanamke hushinda katika boma akipika, akilea, na hata kufua nguo. Licha ya hayo halipwi na tena hapewi nafasi ya kupumzika Tuza 4. Tathmini matumizi ya lugha nathari

d) Tamathali iliyotawala
i) Taswira – hali ya kumwona mke nyumbani na kwingineko katika shughuli mbalimbali
k.m - akiwa nyumbani akipika
- akiwa kitandani uchi
- akiwa mkekani katika utungu wa kujifungua n.k.

Kutuza : Kutaja mbinu 1 Mifano 2X1= 2 Jumla 3

e) Mifano ya taasubi ya kiume
i. Katika ubeti wa kwanza, mume anayachukua mavuno kutoka kwa mkewe
ii. Wanaume katika ubeti wa pili wna ubaguzi na kuonea wanawake

f) Msamiati- Mzima utashi
i) Mwenye udiu/ tama kubwa Maungoni
ii)- maumbo, viungo vya mwili vinaonekana wazi

8. (a) - Pindu, kipande cha kiitikio ndicho kianzio cha ubeti unaofuata
- Tarbia, mishororo minne minne kila ubeti
- Mtiririko, Vina, vya pande zote vinakeketa- tangia ubeti wa kwanza hadi mwisho(yoyote al. 2)

(b) – Kile ulichojaribu kukifanya hakiwezekani usilazimishe, labda ni mapenz ya Mola.
- Si vyote ving'aavyo ni vyema, kabla ya kufanya jambo, fikiria/ tumia busara (2x2=al.4)

(c) – Kuharibika sura
- Humtupa mwenye pupa
- Mbeleni utachapwa
- Huleta hasara
-Kitakugeuza kuwa kitu kingine kisicho na utu (zozote 4x1=al. 4)

(d) – Istiari – jangwa la Sahara
- Semi – Kuvimbisha mifupa, kukipa kisogo (2x2=al. 2)]

(e) Hata ukilipwa mshahara mnono na cheo kikubwa ikiwa mbele kuna majuto kwa sababu ya majitapo yako, hutafaidi chochote kwa vile mbele utapata madhara (4x1=al. 4)

(f) (i) Kuchuma – kupata
(ii) Kisogo kuipa – Kuikataa/kuiacha (1x2=al. 2)

9. (a) Uketo/uhitaji/ukata/ufukara/umaskini (2x1=al. 2)
(b) – Umaskini
- Upweke
- Uwezo
- Uozo wa jamii
- Utovu wa nidhamu
- Ukatili/udhalimu (zozote 4x1= al.4)

(c) – Mbadhirifu
- Mwasherati
- Mlalamishi

- Kitatange
- Asiyesikia makanyo
- Mkata
- Mtovu wa heshima (Kutaja -1, kueleza -1 = al. 2) (2x2=al. 4)

(d) – Kufupisha maneno (inkisari) nikosapo, nondokea
- Ritifaa k.m n'eelea
- Tashbihi k.m. Kama simba
- Tanakali za sauti k.m. kkka
- Sitiari k.m. ulipogeuka nondo (1x4=al. 4)

(e) - Beti sita
Mishororo minne minne
Mizani nane nane
Vipande viwili viwili
Mtiririko wa vina vya mwisho, vya kati vikibadilika badilika
Kipokeo (1x4=al. 4)

(f) (i) Umaskini
(ii) Umaskini (1x2=al. 2)

10. (a) Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
(i) Umoja
(ii) ushirikiano (yoyote moja = al. 2)

(b) (i) Nyuki wanafanya kazi kwa umoja- Hawasengenyani
(ii) Mchwa wana bidii/ hawana uvivu
Mchwa husaidiana na hawadanganyani
(iii) Chungu hawafarakani
(iv) Siafu hujiamini (zozte nne ; 4x1=al.4)

(c) (i) Kubanaga sarufi/ kubananga lugha mfano :-
- Uvivu hawatamani – hawatamani uvivu
- Ukubwa kuutamani – kutamani ukubwa
(ii) Inkisari/ufupisho wa maneno
mf. awezani – anaweza nini
(kutaja alama 1 ; mfano alama 1 = ala. 2)

(d) tarbia/nne – mishororo minne katika kila ubeti
Ukaraguni – vina vinavyotofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine
- Kiishio ambacho hakifanani kutoka ubeti hadi ubeti
- Liona beti tano
- Ni la mathnawi – vipande viwili, ukwapi na utao
- Mizani 16 katika kila mchororo, 8,8, (al. 4)

(e) Mwandishi wa shairi anauliza kwa nini sisi ni wanadamu lakini hatusikizani.
Huwa tunatamani ukubwa kwa hamu.
Hata wale wachache ambao ni wataalamu hatuwaamini. Huwa tunasema kwamba hawawezi chochote. Mshairi anamalizia kwa kusema kwamaba dharau itatuvunjia umoja
(Tathmini majibu ya mwanafunzi al. 4)

(f) – Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu
- Bidii ni ushirikiano kazini
- Kujiamini katika yale tuyatendayo maishani (zozote 2x1= ala. 2)

(g) (i) Chungu – Wadudu wadogo weusi watambao
(ii) Tuwasadi – tuwasadiki, tuwaamini, tuwakubali.

11. (a) Umuhimu wa lugha:

- Lugha nikitu (azizi) cha muhimu
- Lugha hufungua simulizi na kuleta anwani
Lugha hukuza mapenzi
- N timamu katika nyanja mbalimbali za kazi
Huokoa katika kesi
Huvuta usikilizaji ikitumiwa vizuri (zozote 5x1=al.5)

(b) Mishororoinne kila ubeti – tarbia
imegawika katika vipande viwili – mathinawi
- Mizani ni 16 kila mshoro/ukwapi 8, utao 8
- Vina zi, mu
zi mu
zi-mu
mu-a
ukara vya mwisho vinatiririka
- beti ni 8
- Kituo – ukwapi – nitofauti
Kibwagizo – utao – una keketo (Bahari)

(c) Lugha hufanya kazi ngumu kama mpagazi. Isitoshe hutumiwa kupana ya siku za usoni/zijazo
bila kudhulumu.Hufana mambo yakanyooka nakwa hivyo ni nzuri unapofahamu na kwa hivyo
ni nzuri unapoifahamu

(d) Jazanda – Lugha mkuu mlezi – ni mpelekezi
- Lugha ni imamu – ni hakimu mkuu
Mashairi - Lugha hodari mkwezi – ni jahazi
- Huyeyusha sumu – maji zamu
- Ndiye mpagazi – zamu
Tashibihi – hata wanyama ja mbuzi
Misemo – huzifyeka pingamizi, huwaaxcha mkamwe
Tashhisi – Izaayo tabasamu
tabaini – Si vina ci milizamu (zozot 3 = 1x3=al.3)

(e) Azizi – kitu cha thamani
Uhasimu – Uadui, uhasama, hali ya kufarakana
Adimu – Tukufu/ushujaa/jasiri (al. 3)

12.

| SHAIRI LA A | SHAIRI LA B |
|---|---|
| a) Elimu/ elimu ni muhimu | Kero moyoni (alama 2) |
| b) Tathlitha/ utatu/ ukara | Shairi huru (alama 2) |
| c)- Lina beti nne<br>- Idadi ya mishororo hutofautiana katika kila ubeti<br>- Hakuna urari wa vina<br>- Hakuna kibwagizo<br>- Hakuna migao<br>Hoja 3 = alama 3 | |
| d) i) Tashhisi/ uhaishaji | ii) Istiara (chini ya paa la umma) yaani starehe alizonazo mwenye mali zinazotokana na jasho la wahitaji |
| e) Maudhui- umuhimu wa elimu sulubu hawaheshimiwa | Dhuluma dhidi ya wafanyakazi za sulubu k.m. wanapuuza, hawaheshimiwi (alama 4) |
| f) Mathari | |

| | |
|---|---|
| - Elimu isiyo na vitendo ni sawa na mti ambao hauna majani<br>- Haumpumzishi yeyote anayekaa chini ya kivuli chake<br>- Ni taabu tupu udanganyifu kwa watu | (alama 3) |
| g) i) Maulama- Wasomi<br>ii) Wameongelewa- Wametukuzwa, wamesifiwa<br>(Alama 2) | i) Wagatao- wagongao<br>ii) Huwahini- Nyima Kataza<br>(alama 2) |

13. Dhamira ya mwandishi ni kuwa chema hakidumu.
-Shairi lina beti 5
-Kilau beti una mishoro 4 yenye vipande 2.
-kila mshororo una mizani 6, yaani (6 kwa 6) jumla mizani 12 kila mshororo.
-Shairi limetungwa kutumia bahari ya KIKAI na pia bahari ya UKARAGUNI. (Zozote 4x1 =4)

c)Kitu chema hakidumu hata kama kinapendeza ,saa yake ikifika kwa kuponyoka ukawachwa na hamu ya kukirejea lakini wapi.Ni vigumu kwani hauwezekani. (Alama 4)
d)Mfano mmoja wowote wa tamathali uliojitokeza katika shairi ni ule wa Balagha/ Istiari/Uhaishaji (alama 2)
e)-Vina vina badilika badilika.
-Idadi ya mizani katika kila mishororo ya ubeti wa shairi hili imepunguzwa kutoka 8 hadi 6.
-Mshororo wa kwanza katika kila ubeti wa shairi hili ni kama kibwagizo au mkarara.
-Neno chema limetumiwa kubainisha maana tofauti.
-Aina ya tarbia lakini limetengeka kikai. (zozote 4x1 = 4)

f) (i)Nitengenee, Niweadilifu / niwe mwema / niwe sawa.
(ii)Ningamtamani – Ningemthamini
(iii)Ikitimu – ikifika (1x3 = 3

14. a) Kichwa
Kielelezo kibaya
Tabia mbovu kwa watoto
Wazazi wabaya/ walegevu

b) Maudhui ya shairi
Mshairi anasema kuwa wazazi wanahasiri watoto kwa pupa yao ya kulewa kila wakati na kuwa kielelzo kibaya
Wazazi kukaa vilabuni mpaka usiku wa manane bila kufahamiana na watoto wao ni vibaya
Wazazi kuwapa watoto pesa nyingi ni tabia potovu kwani wanazitumia dawa za kulevya
Wazazi wanatafuta utajiri na kukosa wakati wa kuwashauri/ kuwafunza maadili mema

c) Kinachojenga ukuta
Hapana mazungumzo ya kishauri baina ya watoto na wazazi nah ii hujenga ukuta baina ya watoto na wazazi
Kulewa kila wakati na kukaa kilabuni kwa mpaka usiku wa manane hujenga ukuta kwa kuwa mzazi huwa hapati wakati wa kuzungumza na mtoto 2x1=2

d) Tamatahli za usemi
i. Takriri – ni sumu, sumu
ii. Tashihisi – ndoto zinajenga ukuta/ yanakufunga katika klabu
iii. Istiara – ni sumu Kutaja – 1, Mfano – 1

e) Umbo la shairi
Lina beti nne
Kila mshororo una mishororo tisa isipokuwa ubeti wa mwisho
Ni shairi huru kwa kuwa halizingatii arudhi

f) Lugha nathari- ubeti wa nne

i. Mshairi anasema kuwa wazazi wanaumiza watoto kwa kuwapa pesa
ii. Ni vibaya kuliwaza watoto kwa kuwapa pesa
iii. Kwani huwaingiza katika maovu ya kuvuta sigara na ulevi na mihadarati
iv. Hali hii inaishia upotofu wa watoto/ huwaingiza katika hali mbaya/ kifo

g) Maana ya vifungu

i. Giza baridi – hali mbaya/ kifo

Yanakufunga katika klabu – kuwa na mazoea mabaya ya kukaa kilabuni kulewa mpaka usiku wa manane

## Fasihi simulizi

1. Uongozi wa kusahihisha 102/3 (Fasihi)

a) Bembelezi (lal mtoto). Wimbo unambembeleza motto alalye alama 2

b) Sifa za wimbo
- Huimbwa na walezi wa motto
- Huimbiwa watoto wachanga
- Huimbwa kwa sauti nyororo
- Huonyesha hisia za mlezi
- Maneno hurudiwa rudiwa
- Mdundo na taratibu
- Vifungu vifupi vifupi hutumiwa
- Huambatana na kumpapasa papasa motto kwa upole
- Huhusisha watoto wazazi
- Humpatia motto matumaini ya kumwona motto

c) Umuhimu wa wimbo huu
- Hufunza utamaduni
- Hufunza lugha ya ulezi/ mama
- Huliwaza motto mama akiwa mbali
- Hubembeleza motto alale
- Hufunza kuhusu amali ya jamii k.m chakula n.k.
- Mlezi hutoa malalamiko yake
- Hufunza motto mahusiano ya watu

d) Amali za jamii zinazojitokeza
- Vyakula k.v nyama, mkate, ndizi n.k
- Biashara, sokoni
- Ukulima wa ngano (mkate), mgomba (ndizi) Zozote 2x1=2

e) Mbinu zilizotumika
- Kiashiri
- Takriri
- ufafanuzi-1

f) Vitendo ambatano
- Kupapasa motto
- Mlezi hutembea tembea
- Tikisa motto
- Beba motto mgongoni/ begani/ kifuani

g) Wahusika
- Wawili
- Mtoto wa mlezi

2. . a) i)Kisasili

ii) Inaeleza jinsi kifo kilivyoingia duniani

- Asili ya kifo alama 2

b) Sifa za ngano
- Mwanzo maalum (fomula) hapo zamani za……..
- Wahusika wanyama mfano mjusi na kinyonga
- Wanyama kuwasilisha tabia na hisia za binadamu mfano kuongea, kujibizana n.k.
- Tanakali za sauti m.f pu! Zozote 3x1=3

c) Kinyonga ni
- Mvivu/ mzembe/mlegevu
- Si mzingativu- anachelewesha ujunmbe
- Mtiifu- mwishowe alifikisha ujumbe zozote 3x1=3

d) Umuhimu wa hadithi
- Kuelezea asili ya binadamu
- Asili ya kifo
- Huipa jamii melekeo
- Hukumbusha jamii
- Huburudisha/ huliwaza
- Ni historian a utamaduni wa jamii
- Huonya/ huadhibu zozote 4x1=4

e) Njia za kusanya fasihi simulizi
- Mahojiano yaliyopangwa na mtafuti na wahojiwa wake
- Kutumia vinasa sauti
- Kutumia video
- Kwa kuandika data au kazi husika zozote 4x1=4

f) Tambulisha vipera
- Kula hepi- msimu(kuwa na haraka)
- Sema yako ni ya kuazima- msemo (mtu asiringe)
- Baba wa taifa – lajabu (kiongozi wan chi)

3 a) - Huiwasilishwa kwa njia ya mdomo.
- Huhitahi uwepo hadhira
- Huweza kubadilishwa kulingana na hadhira/mahitaji
- Huandama na matendo
- Unaweza kuamba tanishwa na (3X1) ala. 3

b) - Wawe: nyimbo za kilimo (ala. 1)
Kimai: Nyimbo zinazohusiana na shughuli za uvuvi (ala. 1)
Faida:
Kuhimiza bidii.
Shukura kwa mavuno.
Beza uzembe.
Kuchapua utendakazi. ( zozote 2x1 ala. 2)

c) - Huwa na Mdundo| Mahadhi.
-Hupangwa kibeti.
-Hutumia lugha ya mkato.
-Matumizi mengi ya istiari. (zozote 3x1 ala 3.)

d) - Huwa ni fumbo|swali
-Humuia lugha iliyojaa sitiari.
-Ina fomula ya uwasilishaji.

-Huhusisha makundi mawili| watu wawili. (zozote 3x1 ala 3.)

e) i) Istiari
i) Jazanda |Nasiha (ala.1)

f) Matatizo
Watu wanaendelea kuhamia mijini
Dini zinakashifu baadhi ya tamaduni.
Wazee waliohifadhi kumbukumbu hizi wanaendelea knadimika.
Mapendekezo (3x1) ala.3

- Kuborehs zaidi mashidnano katika tamasha za muziki za shule.
- Kuhifadhi kwenye kanda
- Tuwe na makazazi inayoshughul;ikia tamaduni ( 3X1) ala. 3

4. (a)Madhila ya Muitalia (al. 4) ”.
- Yeye aliwanyang’anya mashamba wenyeji”.
- Walikuwa wabaguzi wa rangi
- Mwafrika alidunishwa
- Mlowezi alikuja mika mingi na amekataa kuondoka katika nchi ya mwafrika”.
- Mifugo ya wenyeji inateseka kwa njaa na imekonda mno. Vifaranga, mbuzi n.k”.
(b) Sifa za wimbo ”.
- Urari katika vina haupo
- Mizani katika mishororo haina urari
- Mishororo katika kila ubeti haijagawanywa kwa ukwapi na utao
- Katika ubeti wa pili wanasema wazee kwa vijana waliimba

(c) Maana ya vifungu (al.4)
(i) Mbavu zao zahesabika
- Mifugo wamekonda mno
- Wamekosa malisho (al. 2)
(ii) - Haya yote hakika, ni madhila ya Muitalia.
- Haya ni mateso/masaibu/matatizo yanayotokana na mlowezi Muitalai ”.
(d) - Aina ya wimbo (al.2)
- Wimbo wa ukombozi/uzalendo
- Wenyeji wanaimba na kuonyesha cheche za kutaka kujikomboa kutokana na dhuluma madhila ya walowezi (Waitalia) (kutaja al.1, maelezo al. 1= al.2
(e) Shughuli za kiuchumi (al.2)
(i) Ni wakulima wa mifugo
- Hufuga kuku na mbuzi
(ii) Ni wakulima wa mimea
- Mashamba ambayo wako nayo wanayatumia kwa kilimo cha mimea mbalimbal 2x1=al.2)
(f) Mbinu za lugha (al.2)
(i) Methali- Maji ukiyavulia nguo, ni lazima uyaoge
(ii) Tanakali ya sauti/uidaa/siyahi
Meee !
uui !
Maswali ya balagha /mubalagha
Muitalia alikuja lini ?
Na ataondoka lini ?
a. Takriri – Hatuchoki
(g) Mafunzo katika wimbo
-Mkoloni/ mlowezi, muitalia alipokuja vbarani Afrika aliwakandamiza waafrika kwa mengi
- Umoja wa mwafrika ndio uilioweza kumwondolea dhuluma dhidi ya wanyanyasaji

- Dhuluma in mwanzo na mwisho wake

(viii) Majengo yasiyozingatia viwango vya usalama;
- Bweni la wanafunzi lilikuwa limekomelewa kwa nje
- Madirisha ya bweni yalikuwa yamewambwa kwa vyuma/nyaya kwa madai ya usalama wa wanafunzi
- Shule na hasa bweni kukosa vifaa vya kupambana na moto".
-

5. a) Maana ya mivigo na inakotumika

Mivigo ni sherehe au/ bada zinazofuata utaratibu Fulani wa kisanaa za maonyesho ya fasihi simulizi Al. 1

Inakotumiwa

i. Katika matanga miviga hutumiwa kuliwaza waliofiwa
ii. Katika jando na unyago, makunguni, maghariba na manyakanga hutumia miviga kufunza wavi, nasaha na mazingira yao
iii. Katika mavuno miviga hutumiwa kutoa shukrani
iv. Baada ya vita – hutumiwa kuongoa na kuwatolea shukrani mashujaa waliotoka vitani
v. Motto anapozaliwa au kupewa jina, miviga ya kumkaribisha ilifanywa
vi. Wakati wa arusi
vii. Matambiko ya kutakasa n.k. k.m. aliyemuua mtu
viii. Kutawaza kwa viongozi

b) Sifa za Miviga

Hulenga kundi maalum katika jamii
Hutoa mawaidha
Hukusanya wanaotoa mawaidha na wanaotolewa hayo mawaidha
Hutokea kwa misimu
Kila tukio (jambo) huwa na mivigo yake
Hutumia pesa katika

c) Onyesha umuhimu wa Miviga

Hudumisha mila na utamaduni wa jamii
Huwawezesha vijana kuwa na kumbukumbu za kila sherehe ilivyofanywa, wakati na maana yake
Huelimisha vijana
Hutahadharisha kuhusu maovu
Huwezesha vijana kuelewa au kufahamu desturi zake
Huleta umoja na ushirikiano katika jamii
Huburudisha
Hufundisha unyumba na malezi
Uhimiza bidii ya kufanya kazi na kujitegemea
Huleta maendeleo

6. (a) Ni tungo zilizoundwa kwa mpangilio wa maneno au sauti zilizoteuliwa na msani na zenye utaratibu za kimuziki zinazopanda na kushuka (al. 2)

(b) (i)Tenzi – nyimbo za kutoa mawaidha
(ii) Kongozi – ziliimbwa wakati wa kuaga mwaka
(iii) Sifu – zinaotoa sifa kwa wahusika kutokana na umaarufu
(iv) Wawe – zinazoimbwa na wakulima wakiwa shambani
(v) Tendi – Za masimulizi ya mashujkaa (al.5)

(c)- Huhifadhi matukio muhimu ya kihistoria
- Chombo cha kupitisha utamaduni
- Ni burudani inayotumbuiza waimbaji / hadhira
- Huliwaza na kufariji wenye majonzi
-Huhamasisha watu kushiriki katika kutenda mambo fulani
- Ni njia ya kujipatia kipato

- Hudumisha/huwasilisha usanii wa tamaduni za jamii mbalimbali
- Huelimisha, huonya, husimanga (zozote 5)

(d) BEMBELEZI

- Ziliimbiwa watoto ili watulie/wanyamaze
- Ziliimbwa na walezi /wazazi hasa mama
- Sauti ni ya kubembeleza
- Hutoa ahadi mbalimbali kwa mtoto
- Huwa fupi / hurudiwa –rudiwa
- Ziliburudisha watoto (zozote 5 =al. 5)

7. (a) – Hizi ni hadithi zinazotumia wanyama kama wahusika (mnyama anaweza kusemezana na binadamu)

(b) – Huwezesha fanani na hadhira yake kusema mambo ambayo kwa kawaida ingekuwa mahali/aibu kuyatamka hadharani (kusema kitasifida)

- Ni njia ya pekee ya kufunzia maadili na amali za jamii (kuyapigia mambo chuku)
- Kutahadharisha hadhira dhidi ya watu waovu katika jamii (Sungura na Fisi ujanja wao ni sawa na matapeli)
- Hufurahisha . Hii ni kwa sababu, nyingi ya hadithi hizi huchekesha na kuleta huruma kwa wengine (Sungura kupigana na Ndovu na kumshinda ni kichekesho)

(c) – Watu wazima kuwasimulia watoto
- Watoto kusimuliana hadithi wenyewe kwa wenyewe
- Watu wazima kusimulia mseto wa watu wazima na watoto
- Watoto kusimulia hadhira ya mseto wa watu wazima na watoto

8. (a)(i) Fasihi ya ngoma

(ii) Matumizi ya ala

Hakuna sauti ya binadamu
Mdundo hotoa ujumbe fulani
Hutumiwa kw anjia ya mawasilinao
Saiuti ni ya kupasha ujumbe (zozote 2x1=al. 2)
Wapigaji ngoma na ala zingine
ni watu teule katika jamii

(b) (i) Hurafa- Wahusika ni wanyama
Hekaya- ujanja, ucheshi , werevu an ushindi hujitokeza al.2)

(ii) Visasili /ngano za zuli – hutoa maelezo kuhusu asili ya hali fulani
- Hujibu swali kwa nin kitu fulani kiko jinsi kilivyo
- Visakale – visa vya kale vya mashujaa /majagina (migani)

(iii) Mtanziko – Ngano zinazomwacha msomaji/ mhusika katika hali ya kutojua achague lipi.
- Ni msimulizi huuliza swali
Mazimwi – Hadithi za majitu za kuogofya
- Kiumbe cha kufikirika akilini

(c) (i) Vitendawili – tungo fupi inayotoa maelezo yanayoishia kwenye swali

(ii) Mbinu – Takriri
- Istiara\- Ukinzani
_ Tanakali ya sauti (zozote 4x1= al. 4)

9. a) i)
- Tumbuizo – wimbo wa kuburudisha katika hafla ya arusi
- Wimbo wa kitamaduni

ii) Kuumeni – wanaume
Kukeni – wanawake
Wanaume wanawakilisha wakwe na Tausi (anayeolewa) na wanawake wanawakilisha wazazi wa Tausi

iii) - Watu wa kukeni wana moyo wa kisebusebu na roho kipapo. Walipenda mtoto wao aolewe lakini awaondokeapo na kwenda kwa mumewe waliona uchungu, kwani walijua huduma alizokuwa akiwapa tausi, zingekoma mara moja

- Upande wa kuumeni walifurahi kwani walijua Tausi angeongezea huduma upande wao

iv) – Unaburudisha waliofika kwenye sherehe ya arusi

- Unaleta ushirikiano baina ya pande mbili
- Unatoa ujumbe kuwa kuondoka kwa mtu mliyezoena huwa ni wakati mgumu sana

v) takriri – Kurudia maneno kwa madhumuni ya kusisistiza mfano kisura wetu,

b)

- Mbolezi – nyimbo za matanga
- Bembelezi – kunarai watoto walale
- Hodiya/ kazi – wakati wa kazi
- Nyimbo za kitaifa – kuonyesha uzalendo kwa taifa
- Nyimbo za kisiasa – kumsifu au kumkejeli kiongozi wa kisiasa
- Nyimbo za kidini – katika ibada
- Vichapuzi – nyimbo zinazoandamana na usimulizi

10. a) i) Sifa za Hurafa

- Ni hadithi
- Wahusika aghalabu huwa wanyama
- Hupewa sifa na matendo ya binadamu
- Huwa na mafumbo — Zozote 2x1=2

ii) Sifa za Mighani

- Ni hadithi za mashujaa
- Ni hadithi za kihistoria
- Wahusika huwa mashujaa
- Hupigania haki za wanyonge — Zozote 2x1=2

iii) Sifa za Miviga

- Hujumuisha vitendo maalum k.v. kuimba, kuruka, kucheza ngoma
- Huhusisha maombi
- Aghalabu wahusika hutoa sadaka
- Wahusika huweka ahadi (kiapo)
- Kuna matumizi ya vifaa, mavazi na mapambo maalum — Zozote 2x1=2

b) Umuhimu wa Ngomezi

- Hutoa taarifa kwa njia nyepesi na kuwafahamisha wanajamii kuhusu matukio Fulani k.v. sherehe, mkutano
- Hutumika kutahadharisha watu
- Hutumika kutoa matangazo rasmi
- Ni njia ya kudumisha utamaduni
- Ni njia ya kudhihirisha ufundi wa jamii — 5x1=5

Umuhimu wa mafumbo

- Huburudisha
- Huonya na kutoa mawaidha
- Huimarisha uwezo wa kiakili
- Hufikirisha
- Huimarisha usikivu na uwezo wa kukumbuka
- Hukuza lugha — Zozote 5x1=5

Tofauti kati ya malumbano ya utani na mawaidha

| Mawaidha | Malumbano ya utani |
|---|---|
| i) Hutolewa na watu maalum katika jamii<br>ii) Hutolewa na wakubwa kwa wadogo<br>iii) Mawaidha hutumia lugha ya kipekee ya kuathiri na kuvuta nadhari | i) Wahusika hukubaliana kufanyiana utani<br>ii) Hutokea kwa njia ya malumbano au kujibizana<br>iii) Mtani hutumia lugha ya ucheshi na upigaji chuku Zozote 2x2=4 |

12. i) Maana ya vitanza ndimi

Ni maneno ambayo hutatanisha wakati wa kutamka kwa sauti ambazo zinafanana

ii) Kumzoesha anayetamka ufasaha wa kuyatamka maneno
Kueneza maarifa kuihusu lugha Fulani
Kufikirisha hasa kuielewa maana ya kitanza ulimi kinachohusika
Kuujenga uwezo wa kuongea au kuzungumza bila ya shida
Kuendeleza utamaduni kwa kurithishana maarifa ya sanaa folklore
Kuwanoa wanajamii ambao baadaye watakuwa na ugwiji wa ulumbi alama 8

# Hadithi fupi

## K. WAMITILA: MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINEZO

1.
- Mwandishi namtunia mhusika wake mku Zena kuonyesha maonevu ya kijinsia yanayoendezwa katika maswla ya mpigaji kura na uongozi.
- Anatuonyesha jamii ambayo mwanamke anachukuliwa kuwa hawezi kuongoza. Ndiyo sababu hata katika elimu watoto wengi wa kike wananyimwa.
- Kutokana na mwandshi,uzindushi wa kielimu na uongozi aliopata zena kutoka kwa rafiye carol, ulimfanya Zena kuwa mkakamavu kiasi kwao. Hili ni jambo ambalo halijawahi kuonekana katkika jamii hii.
- Anatuchorea jamii iliyojengeka katika tasubi za kiume. Ajabu ni kwammba hali imewaingia hata wanawake wenzake.
- Anaonyesha namna jamii hii ilivyo mbali kuukubali uongozi wa mwanamke.
- Uongozi hutawaliwa na kiasi cha fedha alichonacho mtu. Maskini Zena hangeweza kuwaleta wapiga kura kutoka mabli na kuwalionga wampigie kura.
- Umma usiomjua wajibu wao katika kutena viongozi
- Umma hauoni uwezo wa kwa wa kubadilisha maisha yao bali wako tayri kuuza kura zao.
- Anaonyesha ilivyo vigumu kwa mwanamke kupata nafasi ya uongozi.
- Mwandishi ana matumaini kuwa hali inawez kubadilika kutokana na majuto ya badhi ya wakaazi wanaoonekana kujiuma vidole wakijuta (zozote 10X2) ala. 20

2.
- Zena kunyimwa haki ya kuendelea na masomo
- Zena kuozwa mapema
- Zena kupigwa na Ali.
- Zena kutusiwa [ Iteuzi]

- Kuumia wembe mmoja kuchanjia wateja wengi – ulaghai.
- Uasherati [ siku ya Mganga]

- Bintiye Mavitu kutungwa momba na jirani.
- Mavitu kunya ng'unywa kijishamba na jirani.
- (Kachukwa hatua Nyingine)
- Ulagahi wa salim _ (pwagu)
- Mawaziri kukojoa ndani yam to.
- Hongo na mirungura. [ Mayai Waziri……..]

- Tanbihi:
- Lazima mtahiminwa ataje hoja kasha atambue hadithi. (zozote 10x2) ala. 20

3 Ni kweli kuwa kezilahabu ametumia jazanda nyingi na ndoto katika uandishi wake
i) jazanda/ ndoto
Watoto kumi waliodhoofika afya yao
Wanadhihirisha umaskini na shida hata ya miaka ya uhuru
Katika ile ajali, dereva na mama hawakufa ilhali ukombozi alikufa, dereva anasimamia kiongozi wa nchi na mama ni nchi yenyewe
Kipofu anayepiga ngoma kumi inasimamia viongozi wasiokuwa na mwelekeo au maneno mema kwa taifa
Ile lama ya "X" iliyoandikwa na ukombozi kwenye picha za viongozi wa baraza la mawaziri inaonyesha viongozi hawa ni wabaya, hawajahudumia nchi ipasavyo
Kifo cha ukombozi ni jazanda inayoashiria kuwa wananchi hawakupata ukombozi waliotarajia baada ya uhuru. Waliendelea kuzama katika madhila umaskin na shida

Katika ndoto moja, tunaonyeshwa watoto waliodhoofika na wanapewa chakula na ukombozi wanakula na kukimaliza; ishara ya njaa nchini
Katika ndoto ya pili ukombozi anatumia vitabu vya wenzake kupandia juu ili kufikia picha za mawaziri na kuziwekea alama ya "X" kudhihirisha hawajafanya kazi ya ipasavyo zozote 4x5=20

4. a) Anayesema maneno haya ni likono
Anajisema yeye mwenyewe (tashtiti)
Yuko katika hospitali ya Kenyatta alikopelekwa na mwuguzi Fulani baada ya kugongwa na gari kasha kupelekwa hospitali amabko hangeweza kugharamia malipo ya matibabu
Bwana aliyemgonga alipotelea mbali hakumshughulkia kwa vyovyote zozote 4x1=4

b) Ni kweli hii ni dunia ya dua la kuku halimpati mwewe, maanake wanyonge wananyanyaswa na kudhulumiwa na matajiri kama ifuatavyo:
- Kizito hakutaka kumpleka likono hospitali licha ya kwamba yeye ndiye aliyekuwa na makosa alipomgonga
Aidha kizito alidhihirisha madharau kwa kuwaita watu "wajinga wa pira"
Kizito alitoka garini polepole kwa tahadhari asikanyage maji ilhali Likoni alikuwa amelala mle majini.
Kizito hakufurahi Likono alipowekwa katika gari lake kwani aliona angelichafua.Haonyeshi huruma kwa Likoni.
Kizito alimpeleka Likono katika hospitali ya Gipfu na kumwacha huko bila kumlipia gharama ya matibabu.
Dhuluma vilevile inadhihirika pale ambapo daktari Gipfu anataka malipo kabla ya kumhudumia Likono.
Aidha daktari wa Gipfu alipendekeza upasuaji wa Likono ilhali mgonjwa hakuhitaji huduma za aina hiyo.
Dhuluma vilevile inaendelezwa na mwajiri wa Likono anapomwachisha kazi ilhali alielewa fika kuwa likono alikuwa mgonjwa. zozote (8x2=16 halimpati Mwewe'

5. "Ndimi za mauti" na Arege
(a) Muktadha (al. 4)
(i) Ni sauti akilini mwa Mbunda
(ii) Yeye na wenzake Kamalina na Musesi walichoma bweni ili kumwadhibu mwalimu mkuu.
(iii) Wanafunzi wenzao walichomeka ndani wakiwemo rafiki zao
(iv) Watu walilaani waliotekeleza kitendo hicho
(v) Mbunda aliamua kujisalimisha kwa askari (zozote 4x1=al.4)

(b) Mbinu za uandishi (al. 2)
(i) Ushairi/wmbo
(ii) Takriri
(iii) Sauti (zozote 2x1=al. 2)
(h) Uhalisia katika 'Ndimi za mauti' (al. 4)
(i) Malezi mabaya ya watoto
- Mbunda anasema ya kwamba hajawahi kugombezwa na hata kuadhibiwa na babake
(ii) Adhabu ambazo zimepita mipaka/katili /zza kinyama
- Mwalimu mkuu kuwaadhibu wanafunzi na kuwakasirisha hadi kuchukua hatua ya kuchoma bweni
(iii) Kanuni/sheria za shule ambazo zinawanyima wanafunzi uhuru ;kamaliza anadai kuwa wao ni mahabusu wa mwalimu mkuu shuleni
(iv) Mapuuza ya wale wenye mamlaka
Tume inaandaliwa kuchunguza uongozi wa mwalimu mkuu baada ya wanafunzi kuchoma bweni na wanafunzi wenzao

Viranja na walinzi kukosa kutambua njama ya wanafunzi kuchoma bweni na kuzuia kutokea kwa tendo hilo

Wazima moto kufika kama wamechelewa shule kukosa vifaa vya kushughulikia mikasa ya dharura kama vile moto shuleni

(v) Majuto kama mjukuu

- Kamaliza na Mbunda kujutia uchomaji shule na kujisalimisha kwa vyombo vya usalama/ askari

(vi) Uchomaji wa shule kama njia ya kuwaadhibu viongozi wa shule

- Kamaliza anasema kuwa uchomaji wa bweni ni njia ya 'kumshutua' mwalimu mkuu kwa kuwaheshimu/kuwakazia.

(vii) Uteuzi wa Tume za kuchunguza majanga na uhalifu baada ya tukio/hasara kutotendeka

- Uchunguzi ulianzishwa kuchunguza uongozi wa mwalimu mkuuu wa shule baada ya bweni kuchomwa
- Askari wanaanza kutafuta aliyehusika katika uchomaji wa bweni baada ya bweni kuchomwa

(viii) Majengo yasiyozingatia viwango vya usalama

- Bweni la wanfunzi lilikuwa limekomelewa kwa nje

Madirisha yalikuwa yamewambwa kwa vyuma /nyaya kwa madai ya usalama wa wanafunzi

6. (II) Umuhimu wa Gege

(a)- Ametumiwa kuonyesha madhara ya tamaa. Tamaa huwafanya watu kutenda maovu. (Gege anakubali kumuuwa nduguye ili apate mali)

(b)- Ujinga ni kizingiti cha mabadidliko ya kweli katika jamii

(c) - Ukatili haulip chochote. Gege hakufurahia vitu alivyovikamia

II. MKIMBIZI – MWONGOZO

- Vifo – watu wengi walikufa
- Nyumba zilichomwa moto
- Kutengana kifamilia
- Ukosefu wa chakula
- Ukimbizi
- Kusafiri kwa mwendo mrefu- uchovu
- Tisho la kuuwawa
- Masomo kukatizwa
- Mazingira mabaya – kulala kwenye baridi
- ukosefu wa usalama
- Kuathiriwa kisaikolojia – baada ya kuona miili ya waliokufa
- Maradhi/magonjwa ya kuambukizwa
- Uharibifu wa mali
- Uhitaji wa habari kutokana na ukosefu wa vyombo vya mawasiliano

7. a) <u>Muktadha</u>

i. Anayezungumza ni (msimulizi) ambaye ni mhusika mkuu/ mkimbizi
ii. Wako njiani wakitorokea nchi jirani
iii. Alikuwa na wakimbizi wenzake wakitoroka vita walipotishwa na askari na kuwafanya wasimame ghafla kwa uoga na hofu
iv. Ni katika hofu hiyo iliyomtia kuyatamka maneno haya kuhusu askari waliokuwa mbele yao

<u>b) Mbinu</u>

i. Taswira – jinsi walivyosimama …………….. ardhini
ii. ii) Tashbihi- kama tumesimikwa

c) Kwa nini akakumbuka mama na ndugu zake

Aliona miili ya wafu (maiti) iliokuwa imetapakaa kila mahali

d) <u>Matatizo ya wakimbizi</u>

i. Maradhi k.v. kipindupindu na kifua kikuu
ii. Uhaba wa hakula
iii. Vifo njiani k.m. Jesse
iv. Ukosefu wa usalama wa wakimbizi
v. Ukosefu wa maji safi ya matumizi
vi. Tatizo la kuvuka mto baluke ulipokuwa umefurika

e) <u>Maudhui yanayoibuka:</u>

i. Vita – watu kupigana kusababisha ukimbizi
ii. Ukabila – kati ya walutu na watutsi
iii. Vifo – kutokana na vita pia magonjwa
iv. Utengano – familia zilitenhana
v. Hofu/ woga – ilioletwa na vita, watu kuuawa

8. (i) MAKULU

Mtu aliye na nafasi. Anampa Nanda kibarua na kumplipa. Ni muhimu kwa kuwa anawasaidia wakazi wa eneo lile pale wanapokuwa hawana hela.

Ni Mkarimu – kuwapa watu bidhaa ili kuwakopesha kama Nanda kuuza mihadarati.

- Anawaajiri watoto wadogo. Mfano ni Nanda ambaye anaajiriwa na kupewa zawadi na pesa.
- Ni mkosa maadili - kule kuwatumia watoto wadogo kulangua mihadarati
- Ni msiri kwa kuwa anayafanya haya yote bila kumwambia yeyote
- Ni mwenye bidii- Aendesha duka kwa bidii. Analima mashamba yake
- Ni mnafiki kwa kuwa anajifanya rafiki mkubwa wa Mzee Atanasi huku akimharibu mwanaye.
- Ni mwongo kwani Mzee Atanasi aliwahi kumweleza kuhusu mabadiliko ya Nanda na akasema yeye hana habari na mabadiliko hayo.

<u>Umuhimu wake:-</u>

- Anatusaidia kufahamu kuwa sio vyote ving'aavyo ni dhahabu
- Ni kielelezo kuwa matajiri wengi hawakutajirika vivi hivi
- Tunajifunza kutowaamini watu wengi hadi kuwapa watoto wetu kuwafanyia kazi

(ii) MWALIMU

- Anaielewa taaluma yake. Anafuatilia maendeleo ya mwanafunzi wake Nanda
- Anawajibika . Ndio sababu amwita babake Nanda ili wajadiliane juu ya mabadiliko ya Nanda
- Ni mshauri mwema. anamshauri Mzee Atanasi la kufanya ili kumwokoa mwanaye
- Anajua kuweka miadi. Alimwalika Atanasi afike mapema naye amesubiri
- Ni mtu makini sana. Ndio sababu ametambua mabadiliko ya Nanda miongoni mwa wanafunzi wengi

<u>Umuhimu wake</u>

- Kielelezo cha umuhimu wa kuwajibika kwa walezi wa kila nui
- Ni kielelezo cha ulezi bora

- Anatuonyesha umuhimu wa kuwa makini kazini

(iii) MZEE ATANASI

- Si makini- mwanaye anaonyesha mabadiliko naye hana habari.
- Ana mapuuza. Yale mabadiliko anayoyaona katika maisha ya Nanda anayapuuza na kuchukulia tu kuwa mtoto anakua
- Ni mshirikina . Akiambiwa kuwa mwanaye kabadilika anachukulia kuwa amerogwa na jirani yake Andanda.
- Ni Mzembe. Amezembea jukumu la kumlea Nanda

<u>Umuhimu wake</u>

- Kielelezo cha wazazi wasiowajibika
- Kielelezo cha hasara inayoweza kutokana na kuamini mambo ya ushirikina
- Ni kielelezo cha urafiki wa chati
- Ni kielelezo cha hasara inayotokana na ukwepaji wa majukumu

(Makulu – al. 7, Mwalimu al. 7 Atanasi – al. 6 = al. 20)

9. (a) (al. 5) - Mkimbizi

- Kukatizwa kwa masomo
- mauaji
- uharibifu wa ali
- uhasma miongoni mwa makabila
- magonjwa/maradhi
- kutamauka(kukata tamaa)
- kugura maeneo
- njaa na kukosa malezi
- kukabilia nahatari (hoja zozote 5x 1= al. 5)

– Fumbo la mwana

Kuzorota kwa masomo

kuzorota kwa afya

kuzorota kwa usafi

uvunjaji wa uhusiano

kutowajibika (zozote 5x1 = al. 5)

(b) Uteuzi wa moyoni

-Kukatizwa kwa masomo kwa wanawake

- Udhalimu dhidi ya wanawake
- Kunyimwa nafasi katika mambo ya siasa
- Chombo cha mapenzi

-Kutukanwa na kuteswa

- Kutokuwa na suti (zozote 5x1=al. 5)

Ngome ya nafasi

- Ndoa ya lazima
- - Kukatizwa kwa masomo
- - Hawana uamuzi
- Hawana sauti
- - Kudhulumiwa
- udhalimu kutoka kw awanawake wengine
- kukandamizwa na sheria (zozote 5x1= al. 5)

10. a)

- Dereva alimgonga Likono kwa gari lake
- Alitaka kutoroka lakini alimlazimisha kumpeleka hospitalini
- Alitaka kuficha ukweli kuwa hakuhusika katika ile ajali ila tu alijitokeza kama mwokozi

b)

- Msamaria mwema halisi (katika biblia) alimpa huduma ya kwanza mgonjwa wake jambo ambalo Dereva hakufanya
- Alimbeba bila kumshurutisha na yeyote
- Aligharamia mahitaji yote jambo ambalo Dereva hakufanya

c) Dereva si mzingatifu

Aliendesha gari huku akiongea katika rununu yake

Barabara mbovu mfano Vidimbwi vya maji machafu

Utovu wa utu na kuthamini sana gari lake – angeweza kumgonga binadamu kwani hana thamani yoyote ukilinganishwa na gari lake 'Toyota Prado'

Likono pengine alizama katika mawazo sana kuhusu masaibu yaliyomkumba, na ghafla kugongwa Zozote 3x2=6

d)

- Anapoulizwa kilichotendeka, alisitasita dhihirisho la uongo- alipanga atakayosema mfano alijikohoza kikohozi cha bandia kabla ya kusema
- Usamaria wema wake hungefika tu plae yaani kumleta hospitalini bali angemshughikia zaidi
- Dereva na mwenye gari wanatoroka wakidai kwenda kutafuta pesa
- Mwenye gari anafika mwanzo wanaenda chumba 'Nzengwe'. Wanaongea huku wakitupa macho ya kuibaiba – Ishara ya kupanga watakayosema

- Dereva na mwenye gari wanajaribu kumchanganya Likono kimawazo ati kagongwa na ile "Nissan Prado' ilihali alijua visuri gari yake ni Toyota Prado Zozote 4x2=8

11. A. Mbinu ya majazi

i) kachukua hatua nyingine – mavitu – mwenye mali /mambo mengi

- Shemeji – mke wa ndugu

ii) Msamaria mwema – Kzito – uwezo/ tajiri

iii) Pwaguzi – Shehe – kiongozi wa dini ya kiislamu

iv) Tuzo – Kibwana – mtu anayejiona mkuu bila ukuu

v) mayai waziri wa maradhi – Ukombozi

- Mayai mtu ovyo
- Dr. Pondamali

B. Mbinu rejeshi

i) kachukua hatua nyingine

- Sakira kukumbu jinsi nduguye alivyomsaidia
- Sakira anakumbuka alivyoacha kazi na kujuta

ii) Fumbo la mwana

iii) Mkimbizi – Anakumbuka walivyouawa wazazi

- Anakumbuka alivyokufa jesee n amzee savalanga

iv) Anakumbuka wosia wa mzee savalanga

12. (a) Uteuzi wa moyoni

(i) Wanawake wanapigwa na wanaume zao

(ii) Ndoa za lazima

(iii) Kufanyishwa kazi nyingi za nyumbani

(iv) Kupewa elimu duni – darasa la nne, tano

(v) Kuitwa Malaya

(vi) Kuadhibiwa na waume zao

(vii) Lawama za kutopata watoto ziliwekewa wao

(viii) Kutofaulu kwa ndoa walilaumiwa wao

(ix) Mwanamke anajukumu la kumfurahisha mwanaume

(x) Kuozwa kwa mabinti mapema

(xi) Mabinti kuachishwa masomo ili waolewe (10x1=10)

(b) Ng'ombe ya nafsi

(i) Mabinti kuozwa mapema

(ii) Kuachishwa shule ili kuolewa

(iii) Kuozwa kwa lazima

(iv) Wanawake kupigwa

(v) Wanawake kuunga mkono utamaduni unaonyanyasa

(vi) Wanawake kutishiwa talaka

(vii) Utamaduni ulikubali ubakaji wa wanawake

(viii) Wanawake kulaumiwa kwa kutopata watoto

(ix) Msichana kutumiwa kuchumia mali

(x) Wanawake kutopewa nafasi ya kuchangia maswala ya ndoa (10x1=10)

13. Masuala Ibuka

i) Ukimwi - siku ya mganga
- Mwaibale anausambaza kwa wembe
- wagonjwa/ wateja wamekondeana na kudhoofika kiafya

ii) Haki za watoto i) Kuchukua hatua nyingine
- watoto kukosa sare, karo, chakula na kwenda shuleni
- Ajira ya watoto
- Mtoto kupachikwa mamba

ii) Fumbo la mwana
- dawa za kulevya

iii) Ngome ya nafsi
- Watoto kuozwa mapema

iv) Uteuzi wa moyoni
- Ndoa za mapema
- wasichana kukosa elimu

iii) Ufisadi – Mayai waziri, waziri fisadi, wizara ya mlungula
- Msamaria mwema – Bw. Kizito Kibambo
- Uteuzi wa moyoni – wapiga kura kuuza kadi zao
- Ngome ya nafasi – Chifu alihongwa, kuficha wahalifu

iv) - Matumizi ya dawa za kulevya/ mihadarati na madhara yake kwa vijana

Fumbo la mwana

Nanda anatumia dawa za kulevya

Anazorota kimasomo, mchafu n.k

v) Ndoa za mapema kwa wasichana
- Zena aliozwa mapea – uteuzi wa moyoni
- Ngome ya nafsi – Naseko anaozwa kwa mzee

vi) Migogoro shuleni

Ndimi za mauti – Wanafunzi kuchoma wenzao bwenini

Mayai waziri – Migomo ya walimu

vii) Vita vya kikabila na suala la wakimbizi

Mkimbizi

ix) Uongozi mbaya – Kuchukua hatua nyingine

Uhalifu wakati wa kura

Viongozi walikosa uwajibikaji

Chifu kuuza chakula kilichotolewa bure wakati wa ukame

Serikali ilifutilia mbali elimu ya bure na kusababisha maskini

Mayai waziri wa maradhi

Waziri mayai

Viongozi walafi

x) Uhalifu katika jamii
- Pwaguzi
- Salim ni tapeli na mizi mkuu
- Kuchukua hatua nyuingine
- Ngome ya nafsi

xi) Umaskini

kuchukua hatua nyingine
fumbo la mwana
msamaria mwema
mayai waziri wa maradhi

xii) Haki za wanawake katika jamii
Uteuzi wa moyoni
Ngome ya nafsi
Kuchukua hatua nyingine
Mayai waziri wa maradhi
Mayai haishi na mkewe

14. Dhamira ni lengo/ nia ya mwandishi wa 'Tuzo'

i) . Anaashiria kauli kuwa yote yaweza yakatokea hata yasiyotarajiwa k.m. Salome na kibwana hawana mkabala mzuri lakini Salome anakuja na kumletea habari. Mwandishi aonyesha kuwa hafla ama matukio huleta wengi pamoja hata wasiosemezana wala kuamkuana

ii) Anaonyesha kuwa mapeni ni msingi wa mengi. Nia ya kibwana unapokataliwa inakuwa chanzo cha kutosemezana kwao tena

iii) Anaonyesha kuwa kunao, wakaao pamoja na kufanya kazi pamoja lakini hawana mkabal mzuri, wao husemezana tu kwa sababu ya kikazi walakini wakitoka nje wanakuwa mjamba miwili isiyoamba. Salome na kibwana wanasemezana wakati wa kazi

iv) Pia anatuonyesha kuwa kuna wenye vitendo vizuri vyenye sifa. Vitendo vyao vinajulikana wazi wazi (kama saui zao)lakini wenyewe hawajui vitendo vinaweza kumtambulisha mtu.

v) Kuna haja ya kumtuza aliyefanya vizuri wanahabari wanatuzwa akiwemo Salome Dzoro

vi) Hamu ya kutuzwa huwa hasa katika sherehe ambayo mtuzwa hajatengezwa hadharani. Tunaiona hamu aliyonayo kibwana

vii) Pia anasisitiza umuhimu wa kauli tahadhari kabla ya athari na kuwa mwangalifu
Anaonyesha umuhimu wa kuwaza kabla ya kutenda

Kibwana angalichunguza kwa makini hangeaibika machoni pake vile.

Tunaelewa alichanganyikiwa hadi katika choo cha wanawake

viii) Anathibitisha ukweli wa methali mzaha

Mzaha hutubga usaha

Mzaha wa Salome wa kumtania kibwana unamletea aibu na kuvurugika akili

ix) Anaonyesha jinsi kutaniana na kuchezeana shere kamwe hakufai. Hii huweza kuleta vita namna kibwana alitaka walakini akajizuia

x) Anataka kuonyesha jinsi furaha huathiri akili. Kibwana alizidiwa na furaha na kusahau kuwa anaweza kutaniwa. Mwandishi anaonyesha kuwa kuna kilio au aibu inayoweza kutokana na futahi hiyo

xi) Anataka kuashiria kuwa vita sio suluhisho kwa kosa ulilotendewa. Kibwana alifumbata konzi kutaka kuirusha walakini anajizuia. Hili ni funzo dhabiti kuwa haitupasi kusuluhisha kwa vita

xii) Ni kawaida kuoa anayetuzwa akiringa ama akitembea kwa madaha. Tunaambiwa kuwa Salome alitembea kwa ndweo kwenda kuitwa zawadi yake. Zozote 10x2=20

15. a) Muktadha

i. Msemaji ni Kaloo
ii. Anamwambia Mwelusi
iii. Kaloo alikuwa anaanda uwanja kwa mkutano wa kiongozi alipomwona Mwelusi
iv. Anapomwuliza anachofikiria anajibu kuwa anafikiria misha ya wananchi wote.(Al 4x1=4)

b) Ushahidi wa kudhihirisha kauli hii

i. Gege nduguye Mwelusi anapenda kucheza ala ya muziki
ii. Yuko tayari kumsaliti nduguye kwa ahadi kuwa ataozwa binti wa Bokono Alida
iii. Muda wake anautumia kuzurura tu na kushiriki katika starehe na anasa
iv. Yeye hajali wala hashiriki katika shughuli za ukombozi wa Butangi (Zozote 3x2=6)

c) Mchango wa vijana

i. Kuwaza kuhusu maisha ya umma
ii. Wanapigania ukweli na amani – Azena, Mwelusi, Andua
iii. Wanapinga mateso, Mwelusi
iv. Wanatetea uhuru, haki na heshima kwa kila mwanabutangi – Mwelusi
v. Wanataka kutatua matatizo ya raia
vi. Wanawafahamisha wananchi kuhusu haja ya utawala wenye msingi wa haki – Mwelusi
vii. Wanahimiza maendeleo kwa wote
viii. Wanatumia maarifa kuondoa dhuluma k.m Ategа kutumia mkate wa wishwa na tupa
ix. Wanaasi utawala usiofaa m.f Andua kuteka maji katika kisima cha mkomani

(Alama zozote 10 x1 = 10)